Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Nne - Tarehe 28 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilisha mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Chuo Kikuu Mzumbe kwa Mwaka 2001/2002 *(The Annual Report and Accounts of the Mzumbe University for the Year 2001/2002).*

Taarifa ya Mwaka ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa mwaka 2001/2002 *(The Annual Report of Activities and Audited Accounts of Sokoine University of Agriculture for the Year 2001/2002).*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo na Chakula kwa Mwaka 2004/2005.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH (MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo na Ardhi kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 129

**Vivutio kwa Wawekezaji Vijijini**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa vivutio gani kwa wawekezaji ambao wangependa kuwekeza Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU k.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 *(Tanzania Investment Act, 1997)* haitoi vivutio tofauti kati ya wawekezaji wa maeneo ya vijijini na maeneo mengine ya nchini.

Hata hivyo sheria hiyo ya uwekezaji chini ya kifungu cha 20, inampa mamlaka Waziri anayeshughulikia uwekezaji kwa kushauriana na Waziri wa Fedha, kuidhinisha vivutio vya ziada kwa wawekezaji muhimu kwa uchumi wa Taifa *(strategic or major investors)* juu ya vile vinavyoelezwa chini ya kifungu cha 19 cha sheria hiyo kutegemeana na maombi maalum ya mwekezaji huyo. Baadhi ya wawekezaji walionufaika na kifungu hiki ni makapuni yanayolima miwa na kusindika sukari ambayo ni wazi yamewekeza maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inaafiki wazo la kutoa vivutio maalum katika uwekezaji vijijini. Wizara yangu inakaribisha maoni kutoka kwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ili kuboresha vivutio vya uwekezaji katika maeneo ya vijijini. Serikali itajenga uzoefu kutoka kwa baadhi ya nchi zilizofanikiwa kuweka vivutio vya ziada kama Msumbiji, ambapo baadhi ya vivutio hivyo vinalenga katika kupunguza viwango vya kodi.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa inaonekana wazi kwamba hadi sasa hakuna vivutio maalum kwa wawekezaji vijijini na kwa kwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali ikoa tayari kupokea maoni, je, yuko tayari kutoa utaratibu maalum ambao utatumika ili kuharakisha kuchukua hatua za haraka na za makusudi kuhakikisha tunaweka vivutio maalum kwa wawekezaji vijijini?

(b) Kwa kuwa siku zilizopita Serikali ilitoa sera ya maendeleo vijijini, je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza akalieleza Bunge hili kama sera hiyo iliandaliwa mkakati wa maendeleo vijijini na kama upo ni chombo kipi kinasimamia na wamesaidiaje kuvutia wawekezaji vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU k.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba hakuna ubaguzi kwa wawekezaji walioko vijijini na walioko mijini. Utaratibu kama nilivyoeleza katika jibu la msingi ni kwamba siyo kwamba itakuwa kwa kila mtu, kila sehemu kutegemeana na mwekezaji na aina ya uwekezaji anaotaka kufanya nchini, atatoa maombi maalum na kuona kwamba je, yale anayoyahitaji yana msingi kupewa kipaumbele katika kuondoa kodi au katika kuhakikisha kwamba yeye anapewa utaratibu maalum wa kuendesha hivyo.

Mheshimiwa Spika, sera ya maendeleo vijijini ipo na mkakati wake umeelezwa. Hivi karibuni tu wakati Waziri Mkuu anawasilisha hotuba yake ya Bajeti, ametoa kitabu ambacho kinaonyesha sera zote zilizokwishatolewa na Serikali. Kwa hiyo, kwenye sera hiyo utaona inavyoelezea vipi mkakati huu uweze kuendelea kwa maendeleo ya vijijini.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa wapo wawekezaji wa Tanzania wazuri ambao wameanza kuwekeza vijijini na kwa kuwa wameshindwa kuendeleza vizuri uwekezaji kwa sababu ya kukosa mitaji, mfano kwenye mashamba ya chai kule Dabaga, je, Serikali inawasaidiaje ili Watanzania hao waweze kuwa wawekezaji wazuri na kuwasaidia wananchi wa vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU k.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu juu ya kupata mitaji kwa mwekezaji yeyote ni kuandika mchanganuo wa mradi aliokuwa nao na kupeleka katika benki yoyote ile ambayo anahisi anaweza kupata mtaji huo. Pale anapokuwa na matatizo sisi Wizara ya Fedha au Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji wako tayari kumwongoza yule anayehusika kuweza kupata mtaji katika benki yoyote ile. Kuna benki mbalimbali ambazo zinatoa mitaji hiyo.

Na. 130

**Madai ya Wafanyakazi wa Shamba la Mpira Kihuhwi**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa mkodishaji wa kwanza wa shamba la mpira la Kihuhwi - Muheza alikuwa sio raia wa Tanzania ametorokea nchini Kenya huku akiacha madeni ya mafao ya wafanyakazi ambao walishinda kesi yao zaidi ya miaka kumi sasa na kwa kuwa Serikali ndiyo iliyoingia mkataba na mkodishaji huyo aliyewatoroka wananchi wa Tanzania.

(a) Je, kwa muda wote ambao Serikali inajua kwamba mkodishaji huyo ametoweka na kuacha madeni makubwa ya mafao ya wafanyakazi, ni hatua gani zimechukuliwa kumrejesha nchini ili atekeleze amri ya Mahakama?

(b) Je, ni kwa nini Serikali isichukue jukumu la kusaidia kuwalipa wafanyakazi hao mafao yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikodisha mashamba ya Mpira ya Kihuhwi, Wilayani Muheza Mkoani Tanga na Kalungwa lililopo Kilombero Mkoani Morogoro kwa *Merchantile Freighters Company Limited* ya nchini Kenya tarehe 3 Agosti, 1996.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba wa ukodishaji, mkodishaji alitakiwa kuendeleza ajira ya wafanyakazi wote waliokuwepo wakati huo kwa kuzingatia sheria za nchi. Hata hivyo, kwa sababu mbalimbali mkodishaji alishindwa kuendesha mashamba hayo na hatimaye aliondoka na kuyatelekeza bila kufuata taratibu zinazotakiwa. Kufuatia hatua hii wafanyakazi walipeleka shauri lao Mahakamani na hukumu ilitolewa kwa kuwapa tuzo dhidi ya mkodishaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi huo wa Mahakama wote wanaoguswa na hukumu hiyo ikiwa ni pamoja na Serikali na wafanyakazi wanapaswa kuzingatia hivyo. Serikali inafanya juhudi kupitia vyombo husika ili kuhakikisha mkodishaji aliyetoroka anarejeshwa nchini ili aweze kutekeleza hukumu ya Mahakama kwa mujibu wa sheria zilizopo. Endapo juhudi hizo zitashindikana Serikali itatafuta utaratibu muafaka wa kuweza kuwasaidia wafanyakazi wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa shamba hili sasa limekodishwa kwa mwekezaji kwa mkataba wa miaka kumi kuanzia tarehe 4 Januari, 2001. Baadhi ya wafanyakazi wanaendelea na ajira zao chini ya mkodishaji huyo mpya.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi ambao wapo kwa huyu mkodishaji mpya wengi wao siyo wale wafanyakazi ambao walikuwepo hapo awali na kwa hiyo, bado wengi wa wafanyakazi wale bado hawajalipwa mafao yao na kwa kuwa ni wajibu wa Serikali Kikatiba kulinda haki za wafanyakazi pamoja na mali zao na kwa kuwa muda mrefu sasa umepita, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kuwalipa wafanyakazi hao ili kuondoa matatizo hayo yanayowakabili? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa zao la Mpira limeteuliwa kuwa zao la biashara katika Wilaya ya Muheza na kwamba wafanyakazi wengi sasa hawependi kufanya kazi kule kutokana na historia hii ya wawekezaji kuwatelekeza wafanyakazi, ili kuwashawishi wawekezaji, je, Serikali sasa haioni ipo haja ya kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanalipwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya mawili ya Mheshimiwa Herbert Mntangi, kwa pamoja kwa sababu yanafana kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu swali la msingi, Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanalipwa. Katika kufanya hivyo vile vile itachukua kila juhudi kuhakikisha kwamba hili zao la Mpira linakuwa ni zao ambalo linanyanyuliwa kuhakikisha kwamba ni zao linaloleta tija katika nchi yetu vile vile. Kwa hiyo, kama nilivyosema watalipwa, tutaangalia, kama imeshindikana kumrejesha hapa itafanya kila njia kwa sababu Serikali ina wajibu wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, napenda kuuliza kwamba kwa kuwa Mpira wa Muheza umethibitishwa Kimataifa kuwa na viwango bora na kwamba ungeweza kusaidia kupunguza gharama za uingizaji wa mpira kwa ajili ya Kiwanda cha Matairi cha Arusha na kwa kuwa huyu mkodishwaji wa sasa hivi hapendi kuuza mpira huo kwa Kiwanda cha Arusha bali anauza nje, je, si wakati mzuri wa kuangalia uzalendo zaidi pale na kutoa shamba hili kwa umoja wa wakulima wa Muheza ili iweze kutumika kwa faida zaidi hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bila shaka yeye aliyeuziwa hili shamba na yeye anaangalia maslahi yake kibiashara. Pengine kuuza nje ya nchi inamletea faida zaidi kuliko kuuza hapa ndani ya nchi. Kwa hiyo, unashauri kwamba tungewapa wananchi, nimeeleza kwamba kuna mkataba wa miaka kumi kuanzia tarehe 4 Januari, 2001 mpaka tarehe 3

Januari 2011 mkataba wake utakapokwisha kama hakulitelekeza, kama alivyotelekeza mwenzake ndiyo hapo pengine tunaweza kuja kushauri kwamba tuwape wananchi. Lakini kwa sasa hivi hatuwezi kwa sababu kuna mkataba, lazima tuheshimu mkataba. *(Makofi)*

Na. 131

***Kilombero Sugar Company***

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM** alikuwa:-

Kwa kuwa *Kilombero Sugar Company* inabinafsishwa kwa kuuza hiza asilimia 75 kwa *M/S ED & F Man* ya Uingereza mwaka 1998 na kwa kuwa kampuni hiyo imefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana katika utekelezaji wa mpango wake kwani uzalishaji umefikia tani 126,000 katika msimu wa 2003/2004.

Je, Serikali imejipatia fedha kiasi gani tangu kampuni hiyo ilipobinafsishwa mwaka 1998 hadi Juni, 2004?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tangu Kampuni ya Sukari ya Kilombero ilipobinafsishwa mwaka 1998 imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa mpango wake wa uwekezaji. Uzalishaji wa sukari umeongezeka kutoka tani 42,063 zilizozalishwa mwaka 1998 na kufikia tani 126,743 msimu wa mwaka 2003/2004. Kutokana na mafanikio ya kampuni hiyo, kuanzia mwaka 1998 hadi mwezi Mei, 2004 Serikali ilikuwa imekwishajipatia shilingi 19,495,795,990/= kutokana na vyanzo mbalimbali vya kodi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kodi ya ongezeko la thamani shilingi 13,267,136,692/=, kodi ya mapato 1,956,356,357,232/=, kodi ya zuio shilingi 3,074,066,689, tozo la mafunzo ya ufundi stadi, 1,182,665,399/= na kodi ya maendeleo shilingi 15,569,981/=.

Aidha, Kampuni ya Sukari ya Kilombero imeingiza 21,490,910,000 fedha za kigeni kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1998 hadi mwezi Mei, 2004. *(Makofi)*

Na. 132

**Usafirishaji wa Chai Toka Vijijini**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH (k.n.y. MHE. BENITO W. MALANGALILA)** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha zao la chai kinastawi katika maeneo yenye milima na mvua nyingi na kwa kuwa nchi yetu imepata misaada mingi toka nje kwa lengo la kuboresha sekta ya kilimo ukiwemo Mfuko wa *STABEX* na kadhalika na kwa kuwa hata nafuu ambayo Serikali imepata tangu utaratibu wa *HIPC* uanze ni kusaidia sekta ya kilimo.

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa kuna shida kubwa ya kusafirisha chai katika vijiji vya Igoda, Ikaning'ombe, Luhuga, Mbonge, Kisanga, Ikwega na Mkalala vilivyopo Mufindi kutokana na ubovu wa barabara, hali inayosababisha baadhi ya chai kutupwa kutokana na kukwama kwa magari yanayosomba chai hiyo?

(b) Kwa kuwa miaka iliyopita kulikuwa na mradi maalum wa kutengeneza barabara za chai kama kule Lupembe, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mpango huo katika maeneo ya mazao muhimu?

(c) Je, ni nini ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo katika maeneo hayo yanayolima chai?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inalifahamu tatizo la ubovu wa barabara katika vijiji vya Igoda, Ikaning'ombe, Luhunga, Mbonge, Kasanga Ikwega na Mkalala vilivyopo katika Wilaya ya Mufindi. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inatekeleza yafuatayo:-

(i) Kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara *(Road Fund),* Serikali inaifanyia matengenezo ya dharura *Spot Improvement* barabara ya Mtwango hadi Iyegeya inayoviunganisha vijiji vya Sawala, *Lupembe Estate,* Mbonge, Luhunga, Igoda, Ikaning'ombe yenye urefu wa kilometa 38.8 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2004. Matengenezo hayo yametengewa jumla ya shilingi milioni 15.58.

Aidha Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Denmark *(DANIDA)* imekamilisha maandalizi ya mpango wa kuifanyia matengenezo makubwa sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 19.8, kutoka Kijiji cha Ikaning'ombe kupitia Vijiji vya Igoda, Luhunga hadi Mbonge. Matengenezo hayo yatafanyika katika mwaka 2004/2005 kwa gharama ya shilingi milioni 136.

(ii) Katika mwaka 2003/2004 barabara ya Mninga hadi Ikwega yenye urefu wa kilometa 6.2 imefanyiwa matengenezo ya dharura kwa gharama ya shilingi milioni 17.28. Aidha, barabara ya kutoka Ikwega hadi Kasanga yenye urefu wa kilometa 9.4 inatarajiwa kufanyiwa matengenezo ya dharura mwaka 2004/2005 na imetengewa shilingi milioni 12 kutoka kwenye Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kurejea utaratibu uliokuwepo katika miaka ya 1972 hadi 1980 na kukarabati barabara katika maeneo yanayolima chai kwa wingi nchini. Badala yake Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya, inatekeleza mpango endelevu wa ukarabati wa barabara za vijijini kwa kutumia Mfuko wa Barabara *(Road Fund).*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kutumia mfuko huo chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya husika, utatoa ufumbuzi endelevu wa tatizo la barabara za vijijini kutopitika kwa mwaka mzima. Kwa kuwa mpango huo unatekelezwa nchi nzima, maeneo yale yanayozalisha mazao muhimu yatahusihwa. Aidha, kwa kuwa mpango huo unasimamiwa na Halmashauri za Wilaya ni wajibu wa Halmashauri husika kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa zinaelekezwa katika kujenga na kukarabati barabara muhimu kwa maendeleo ya Halmashauri husika.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kutokana na majibu yake ya msingi inaonekana dhahiri kwamba pesa zinazopelekwa katika Halmashauri za Wilaya, hazitoshelezi kabisa kukidhi haja ya barabara zilizopo katika maeneo haya nchi nzima. Je, Serikali haioni kwamba inabidi ifanye mikakati maalum ya kuongeza fedha hasa katika yale maeneo ya uzalishaji ili kukuza kipato cha wananchi pamoja na Serikali kwa ujumla? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa taarifa rasmi hazipo zinazoonyesha kuwa fedha za *Road Fund* ambazo zinatoka kwenye Wizara ya Ujenzi 30% kufika huko hazitoshi. Katika maeneo yale ambayo wanawaisha mipango yao kwa mamlaka husika kwa kawaida zinapata. Fedha hizi si peke yake tu ambazo zinatumika kwa barabara zingine katika Wilaya ni za Mkoa, ziko zingine za Kitaifa, ni mifuko mbalimbali na mingine inatumika. Vile vile tusisahau unapotengeneza miradi ya *DADPs* mambo haya ikihusisha na kilimo yanafaa vile vile.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la Mheshimiwa Mbunge lilikuwa linazungumzia fedha za *Road Fund* kwamba zinatakiwa kuongezwa. Kupitia sheria namba mbili ya mwaka 1998 ambayo ilipitishwa hapa Bungeni ilianzisha Mfuko wa *Road Fund* na katika sheria hiyo, shilingi 100 za kila lita ya mafuta huwa zinakusanywa kwa ajili ya matumizi ya fedha na kwamba fedha zile zinapopatikana huwa zinapelekwa asilimia 30 Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, asilimia 70 inapelekwa Wizara ya Ujenzi pamoja na *TANROADS* kwa ajili ya matengenezo ya barabara tu. Katika hali halisi kupitia Mfuko wa *Road Fund* kwa sasa hivi kuna hatua mbalimbali zinafanywa ili kuangalia vyanzo vingine ambavyo vitaweza kuboresha huu mfuko ili fedha nyingi ziweze kupatikana kwa

ajili ya matengenezo ya barabara. Kazi hizi zinafanyiwa kazi na mfuko wa *Road Fund* na mapendekezo yake yataletwa Serikalini na baadaye yataletwa Bungeni. *(Makofi)*

Na. 133

**Gharama za Kujiunga na Elimu ya Sekondari**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa gharama za kujiunga na elimu ya sekondari ni kubwa sana na watoto waliofaulu mitihani ya kujiunga na kidato cha kwanza wanashindwa kwa sababu ya umaskini wa wazazi wao na kwa kuwa ukubwa wa gharama hizo unasababishwa na ada, chakula, majengo, madawati, tahadhari, mitihani ya shule na sare za shule.

(a) Je, Serikali iko tayari kupunguza ada ya elimu ya sekondari katika shule zake kutoka shilingi 40,000/= kwa sasa kufikia shilingi 15,000/= kwa mwaka?

(b) Je, Serikali itapokea maombi ya wazazi nchini kote kuwa jukumu la ujenzi wote wa shule na kutengeneza madawati liwe jukumu la wananchi wote kama shule za msingi badala ya jukumu la wazazi peke yao?

(c) Je, Serikali iko tayari kuchukua jukumu la kulipia mitihani yote ya shule na zile za Baraza la Mitihani la Taifa kwa vidato vya II, IV na VI kwa shule zote za Serikali?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009) au *(SEDEP)* Serikali imedhamiria kupunguza ada kwa shule sekondari kuanzia mwaka 2005, jambo hili nitalifafanua zaidi katika hotuba yangu ya Bajeti ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005 tarehe 8 Julai, 2004. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 1995 jukumu la ujenzi wa shule hadi kukamilisha ikiwa ni pamoja na kutengeneza madawati ni la jumuia nzima mwenye shule ile na siyo wazazi wa wanafunzi peke yao. Shule inajengwa kwa ajili ya watoto wa sasa na wa baadaye wakiwemo wajukuu na vitukuu. Kwa hiyo, jukumu la ujenzi wa shule ni la jamii nzima ya sasa na Serikali yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali inakataza kabisa uendeshaji wa michango yoyote ya wazazi peke yao. Kamati yoyote ya shule itakayochangisha wazazi wa wanafunzi peke yao itafukuzwa na Mwalimu Mkuu ataondolewa madarakani kwa kuishauri vibaya yeye kama Afisa Elimu wa Jamii ile anayemwakilisha Afisa Elimu Kiongozi. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu mitihani, Serikali inagharamia mitihani ya pale shuleni yaani *School Based Examination* kupitia ruzuku ya uendeshaji wa shule. Wazazi wanachangia sehemu ndogo ya mitihani ya Kitaifa ya kidato cha Pili, kidato cha Nne na Kidato cha Sita. Sehemu kubwa ya gharama za Baraza la Mitihani Tanzania kama vile mishahara na Bajeti ya Maendeleo hutokana na Bajeti ya Serikali. Hata hivyo, Serikali imeamua kupunguza mzigo kwa mzazi kwa kupunguza ada kama itakavyofafanuliwa katika hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, lakini ni muhimu ieleweke kuwa Elimu ya Sekondari inayo faida ya kiuchumi kubwa zaidi kwa mpokeaji wa elimu hiyo kuliko kwa jamii. Kwa hiyo, ni halali kabisa kila kaya husika kulipia angalau sehemu ndogo ya gharama ya elimu hiyo. Hata hivyo, Bajeti ya mwaka huu imeongeza maradufu Bajeti ya kusaidia kaya zisizo na uwezo kabisa kutoka watoto 6,000 hadi watoto 12,000 kwa mwaka kwa kutenga jumla ya shilingi 2,160,000,000/= kwa ajili ya ruzuku hiyo. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri sana na nategemea kwamba wazazi wa Tanzania watakuwa wamepokea jibu hili vizuri. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa watoto wanaoshindwa kulipia ada za mitihani ya Taifa ya Kidato cha Pili, cha Nne na cha Sita ni wale ambao wazazi wao ni maskini sana, Serikali iko tayari kuwatambua wanafunzi hawa wakati wakiwa shuleni ili wawasaidie kulipia ada hizo na kuwawezesha watoto hawa kupata vyeti vyao wanapohitimu elimu husika? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa tunaingia katika mpango wa *SEDEP* kuanzia Julai, 2004, Serikali itachangia kwa kiasi gani ujenzi wa Shule za Sekondari zinazojengwa na wananchi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuwatambua wale ambao wanashindwa kulipia mitihani waweze kupata vyeti vyao, jambo hili ni gumu ndio maana tumeweka utaratibu wa kuwatambua watoto wanaotoka katika familia maskini kuanzia ngazi ya Kijiji. Utaratibu unaanza pale Kijijini ambapo watu wanafahamiana vizuri. Kwa hiyo, ni Serikali ya Kijiji, Kamati ya Shule, ni uongozi wa pale Kijijini ndio unaoanza kutoa mapendekezo. Tunaona ukipeleka zaidi ya hapo kwa watu wasiowafahamu unaweza ukajitokeza udanganyifu mwingi.

Kwa hiyo, tunashauri kwamba tufuate utaratibu huu na waendelee kujitahidi kupata vyeti vyao wale ambao tayari wako shuleni. Sioni namna ambayo Serikali inaweza ikaingilia katikati jambo hili. Lakini kama Mheshimiwa atakuwa na ushauri zaidi nitafurahi kubadilishana mawazo.

Pili, kuhusu Serikali itachangia kwa namna gani katika kuwasaidia wananchi wanaojenga Sekondari, kama nitakavyofafanua nitakapowasilisha Bajeti hapa hiyo tarehe 8 Julai, 2004 inaanzishwa katika ngazi ya Elimu ya Serikali. Tumechota uzoefu kutoka

kwenye MMEM, tunaanzisha utaratibu wa ruzuku ya maendeleo ambayo itatolewa kwa ujenzi wa majengo ya Sekondari, shilingi milioni saba kwa kujenga darasa na shilingi milioni tisa kwa kujenga nyumba ya Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumegundua kuwa katika ngazi ya Sekondari yako majengo ambayo wananchi yanawapa taabu sana kuyajenga kwa sababu yanahitaji ujuzi maalum. Jengo kama la Maabara na jengo kama la Maktaba na *Assembly Hall* kwa sababu ya *span* kubwa inayohitajika, majengo hayo Serikali inatarajia kutumia Bajeti ya Serikali kwa zabuni zitakazotolewa Wilayani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado nina maswali matano ya msingi na nina dakika 25 tu. Kwa hiyo, naomba tuendelee ili yapate majibu. Mheshimiwa Janet Kahama, swali linalofuata.

Na.134

**Shule kwa Watoto Wenye Mtindio wa Ubongo**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi vikiwemo vikundi mbalimbali kama kile cha *Mental Retarded Support Group* cha wanawake wachache wa Mkoa wa Dar es Salaam wamehamasika na kujitolea kuchangia kwa hali na mali katika ujenzi wa madarasa kwa watoto wenye mtindio wa ubongo:-

(a) Je, Serikali imeshajenga shule ngapi au madarasa mangapi katika Mikoa yote kwa ajili ya watoto wenye tatizo hilo?

(b) Je, Serikali imeweza kutoa mafunzo maalum kwa Walimu wangapi nchini ambao wataweza kuwasaidia na kuwaelimisha watoto hao?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa sasa jamii ya Watanzania wengi imeanza kuonesha kuhamasika katika kuwapatia elimu watoto wenye aina mbalimbali za ulemavu. Hali hii imetokana na harakati za Taasisi mbalimbali za kuhudumia wenye ulemavu kwa kushirikiana na Serikali kutambua haki za walemavu.

Aidha, Vyombo vya Habari vikiwemo Luninga, Redio na Magazeti vimesaidia sana katika kufafanua wajibu wa Serikali na jamii katika kuwahudumia wenye ulemavu kwa kuwapatia elimu.

Napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi na vikundi mbalimbali kama kile cha *Mental Retarded Support Group* cha wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam na

vingine nchini kote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusaidiana na Serikali kuwapatia watoto wenye ulemavu elimu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Janet Kahama, kwa sababu yeye ni miongoni mwa uongozi wa kikundi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo napenda sasa kujibu sehemu (a) na (b) ya swali kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imefungua na kuendesha vitengo vya wenye ulemavu wa akili katika shule 105 za msingi hapa nchini. Aidha, katika kuunga mkono jitihada zinazofanywa na vikundi mbalimbali vya wananchi kama kile cha Dar es Salaam cha *Mental Retarded Support Group,* Serikali inasaidia kugharamia shughuli za uendeshaji wa Shule Maalum tano za wenye ulemavu wa akili za Sinza katika Wilaya ya Kinondoni, Mtoni katika Wilaya ya Temeke, Bethlehem katika Wilaya ya Kilombero, Miuji katika Wilaya ya Dodoma na Lulindi katika Wilaya ya Ludewa.

(b) Mheshimiwa Spika, sambamba na ufunguaji wa shule maalum na vitengo vya kuhudumia watoto wenye ulemavu, Serikali inacho Chuo cha Ualimu, Elimu Maalum cha Patandi ambacho kinaandaa walimu wataalam wa kufundisha watoto hao. Hadi kufikia Agosti, 2003 jumla ya walimu wataalam 1,033 walikuwa wameandaliwa, kati yao 266 ni wataalam wa kuhudumia au kufundisha watoto wenye ulemavu wa akili.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri na pia nampongeza sana kwa kuwa vituo vimeongezeka nchini, bado nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa watoto wenye mtindio wa ubongo wanahudumiwa na Wizara tatu, Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Afya na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, nilikuwa nataka kujua, je, Wizara hii ya Elimu na Utamaduni inashirikianaje pamoja na Wizara zile nyingine mbili katika kuleta huduma ya watoto na pia Wizara hii inafikiria lini itaendeleza huduma hii katika Shule za Sekondari? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu ushirikiano kati ya Wizara hizi tatu, Elimu na Utamaduni, Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ninachoweza kusema ni kwamba tutajitahidi kuimarisha ushirikiano na kama kuna maeneo Mheshimiwa Janet Kahama, anaona yana upungufu tuko tayari kushauriana tuone namna ya kuimarisha ushirikiano huo.

Kuhusu tutafanya nini katika kuendeleza juhudi hii katika ngazi ya Sekondari, baada ya kulifikiria sana jambo hili Serikalini tumefanya uamuzi kwamba kazi hii ya Elimu na Utamaduni kwa Walemavu, kwa kweli Serikali pamoja na jitihada zote inazozifanya hatuifanyi kwa ukamilifu. Wako wengine wanaojitokeza wanaweza kufanya vizuri zaidi. Kwa hiyo, katika maelezo nitakayoyatoa wakati nawasilisha Bajeti, Serikali inaanzisha ruzuku maalum ya maendeleo na uendeshaji kwa Taasisi na vyombo visivyo vya kiserikali wanaoweza kuifanya kazi hii vizuri zaidi ili Serikali isaidie kuwapa uwezo.

**SPIKA:** Waziri ameahidi kwamba kuna maelezo zaidi yanakuja. Kwa hiyo, tuendelee na maswali kwa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Mheshimiwa John Shango, hayupo, Mheshimiwa Mgana Msindai, kwa jina la utani Mheshimiwa *CRDB* uliza kwa niaba yake. *(Kicheko/Makofi)*

Na.135

**Miswada Kuandikwa Kiingereza**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. LEONARD M. SHANGO)** aliuliza:-

Kwa kuwa lugha ya Taifa la Tanzania ni ya Kiswahili:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazofanya Miswada ya Sheria inayoletwa mbele ya Bunge ili kujadiliwa na kupitishwa inaandikwa kwa lugha ya kigeni yaani Kiingereza?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kwa kuendelea kuchapisha Miswada hiyo kwa lugha ya Kiingereza kunawanyima wananchi walio wengi fursa ya kuelewa na kutoa mchango wao wa mawazo ya kuboresha Miswada kabla haijapitishwa na Bunge kuwa Sheria kwa sababu pale inapobidi inafikishwa kwao kama rasimu kwa lugha ya Kiingereza?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutafsiri na kuchapisha kwa lugha ya Kiswahili na kuzisambaza kwa wananchi wote sheria zilizojadiliwa na kupitishwa na Bunge kwa ajili ya kuongeza uelewa na utii wa sheria za nchi kwa wananchi walio wengi ambao hawaelewi lugha ya Kiingereza?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Miswada inayoletwa mbele ya Bunge ili kujadiliwa na kupitishwa huandikwa kwa Kiingereza kutokana na mazoea yaani *convention* ya muda mrefu. Aidha, Kanuni za Bunge ambazo chimbuko lake ni Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinaelekeza kwamba shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kuandika Miswada ya Sheria katika lugha ya Kiingereza unatumiwa na nchi nyingi za Jumuiya ya Madola ambayo Tanzania ni mwanachama. Matumizi ya lugha ya Kiingereza katika nyanja mbalimbali pamoja na uandishi wa sheria yanarahisisha mawasiliano na ushirikiano baina ya nchi yetu na Mataifa mengi ulimwenguni hasa tukitambua kwamba Kiingereza ni Kiswahili cha dunia.

(b) Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba kuendelea kuchapisha Miswada kwa lugha ya Kiingereza kunawanyima wananchi walio wengi fursa ya kuelewa na kutoa michango yao ya mawazo ili kuboresha miswada hiyo kabla haijapitishwa na Bunge kuwa Sheria. Ukweli ni kwamba, ingawa Miswada huandikwa kwa lugha ya Kiingereza, majadiliano ya sheria hizo Bungeni hufanywa kwa lugha ya Kiswahili.

Aidha, kila Muswada wa Sheria huambatana na tafsiri ya lugha ya Kiswahili kuhusu madhumuni na sababu ya Muswada wenyewe. Utaratibu huu wa Bunge kujadili Miswada kwa Kiswahili kunawapa fursa kubwa wananchi kuelewa kile kinachokusudiwa katika kila Muswada hasa wakati huu kutokana na vyombo vya habari kama vile redio, *television,* magazeti na kadhalika kuwa vingi hapa nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo umuhimu mkubwa wa kutafsiri na kuchapisha sheria katika lugha ya Kiswahili na kuzisambaza kwa wananchi pindi zinapopitishwa na Bunge lako Tukufu. Wizara yangu hivi sasa imeweka mikakati ya kukiimarisha Kitengo cha Tafsiri kilichopo kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sheria kadhaa zimeanza kutafsiriwa kwa Kiswahili kwa mfano Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999, Sheria ya Hakimiliki ya mwaka 1999 na Kanuni mbalimbali na sheria ndogo ndogo zinazotumiwa na Serikali za Mitaa. Utaratibu huu utazidi kuimarika kulingana na upatikanaji wa tafsiri, stadi, wataalam na vitendea kazi. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema ni mazoea tu yanafanya waandike Miswada na mambo mengine ya Serikali kwa lugha ya Kiingereza na kwa kuwa amesema kwamba sasa hivi wanatafsiri kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili Miswada mingi na sheria, yeye haoni kwamba haya mazoea sasa imefika muda wa kuondokana nayo ili ichapishe moja kwa moja kwa Kiswahili ili wananchi wetu waweze kupata haya mambo kwa Kiswahili? *(Makofi)*

Pili, kutokana na kuandika kwa Kiingereza, sasa hivi mimi ni wiki ya tatu nimekwenda kwenye duka la Serikali kutaka nipate Katiba nakala ishirini kwa ajili ya wananchi wa Iramba Mashariki zilizoandikwa Kiswahili na mpaka sasa hawana, haoni Serikali inawakosesha haki wananchi wa Tanzania kujua mambo yao kwa undani? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA):** Mheshimiwa Spika, mazoea kwa maana ya lugha ya Kiingereza ni *convention* yana maana pana kwa maana kwamba yanakuwa ni kama sheria, maana umeishi nayo kwa miaka yote hiyo na ndiyo maana katika maelezo ya jibu hili tumesema huo ndio msingi wake kuanzia huko nyuma. Sasa tumeendelea kusema katika jibu la msingi kwamba ni vyema kwa kutambua kwamba Kiingereza ni Kiswahili cha dunia, Tanzania tusiishi kama kisiwa, lakini kwa kutambua umuhimu kwamba wananchi wengi wa nchi yetu wanapaswa wazipate sheria hizi katika lugha ambayo wanaielewa, ndio maana Serikali inafanya juhudi kubwa sasa hivi kuhakikisha kwamba pindi Bunge lako Tukufu linapopitisha Sheria, sheria hizo zianze kutafsiriwa katika lugha

ya Kiswahili na hiyo ni vizuri tukafanya hivyo kwa sababu tutawawezesha wananchi wetu kuzipata sheria hizo.

Kuhusu upatikanaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama alivyoomba Mheshimiwa Mgana Msindai, ni kweli kuna tatizo hilo lakini sidhani kama ni kubwa kiasi hicho kwa sababu Dar es Salaam tunafahamu zipo nakala za kutosha ambazo zinaweza kusambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge kwa matumizi ya wananchi kama watu wanazihitaji. Nadhani tuwasiliane tuone jinsi tunavyoweza kulitatua tatizo hilo kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wanahitaji kupata nakala za kutosha za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inampa haki kila raia kuweza kuchagua na kuchaguliwa (kuchukua nafasi yoyote) na kwa kuwa Bunge hili sasa linakwenda na msingi wa utandawazi na mambo ya *globalization,* je, isingekuwa muda muafaka kwa Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha Katiba ili viongozi wanaochaguliwa kuingia katika chombo kama cha Bunge waweze kuwa na sifa zaidi ya kujua kusoma na kuandika tu? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, liletwe kwa njia za kawaida. Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa katika swali la msingi kipengele cha (b) muuliza swali alitaka Miswada hiyo ichapishwe kwa Kiswahili waisome kabla hatujaijadili Bungeni na kwa kuwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yeye anasema wanaisikia tunapoijadili hapa kwa Kiswahili, je, haoni kwamba amelipotosha Bunge na kuwadanganya Watanzania kwa kutokujibu swali lilivyo? *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA):** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba kupitia jibu hili tumepotosha Watanzania. Wote tunaona sasa hivi nchi nzima inaona kinachoendelea Bungeni hapa kwa wale ambao wana bahati ya kuwa na *television* nyumbani kwao. Lakini hapa niseme viongozi wa wananchi, wawakilishi wa wananchi ambao ndio Wabunge, tunafahamu kabisa wanamudu vizuri sana Kiingereza na ndio maana Miswada inapochapishwa tunataka wao kama viongozi waende wakapate maoni kutoka kwa wananchi kuhusiana na hayo maudhui yaliyomo katika Miswada inayopendekezwa na Serikali na wao wana uwezo wa kuelezea kwa lugha nyepesi yale ambayo yanapendekezwa katika Miswada hiyo. Ukiweza unaweza kusema hata Kisukuma, hata Kihaya ili wananchi waweze kuelewa.

Mheshimiwa Spika, lakini humu Bungeni kwa sababu kanuni zinataka tutumie lugha hizo mbili Kiswahili na Kiingereza, michango yote tunafahamu inafanyika katika lugha ya Kiswahili na wananchi wetu wanayafaidi sana hayo ambayo yanasemwa na wawakilishi wao katika Bunge lako Tukufu.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

Na. 136

**Vifo Vinavyotokana na Ajali, Kupigwa Mapanga au Kwa Bunduki**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi kesi za mauaji zinatokana na kugongwa na gari, kukatwa mapanga au kufyatuliwa risasi zikipelekwa Mahakamani mara nyingi wahusika walioua hujitetea kwa kudai wameua bila kukusudia, wakati mauaji mengine hutokea kutokana na mtu kuchukua panga au bunduki na kumfuatilia mwenzake kwa lengo la kumuua:-

(a) Je, ni mauaji ya aina gani yenye kuashiria kuwa mtu ameua bila kukusudia?

(b) Je, ni mauaji ya aina gani yenye kuashiria kwamba mtu ameua kwa kukusudia?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Vifo vinavyoashiria kuwa mtu ameua bila kukusudia ni vile vifo vinavyotokana na tendo la mshitakiwa ambalo wakati analitenda halikuambatana na kusudio la uovu la kusababisha kifo, kwa lugha ya Kiingereza ni *malice aforethought.* Vifo vya aina hiyo ni kama vile vifo vinavyotokana na ugomvi wa kawaida, kujihami yaani *self defense,* kulinda mali au watu, kukamata wahalifu, ulevi, hasira inayotokana na maudhi yaani *provocation* na kudhania kimakosa kwamba anayeshambuliwa mathalani ni mnyama kumbe ni binadamu yaani *mistake of fact* na kadhalika.

(b) Vifo vinavyoashiria kuwa mtu ameua kwa kukusudia ni vile vifo vinavyotokana na tendo la mshtakiwa ambalo limeambatana na kusudio la uovu la kutaka kuua. Kwa mfano, kwa kutegemeana na mazingira ya ushahidi wa tukio la mauaji, mtu anayechukua silaha na kumfuatilia mwenzake kwa ajili ya kumwua anaweza kuchukuliwa kuwa ana kusudio la uovu. Kwa hiyo, akisababisha kifo cha mwenzake atachukuliwa kuwa ameua kwa kukusudia na hivyo hushitakiwa kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, vigezo hivi vinavyotofautisha makosa ya kuua bila kukusudia na makosa ya kuua kwa kukusudia hutegemea mazingira ya tukio lenyewe pamoja na ushahidi uliokusanywa. Kwa hiyo, hata pale mshitakiwa anapodai kuwa aliua bila kukusudia lakini ushahidi ukawa unaonesha vinginevyo sio lazima upande wa mashitaka na Mahakama wakubaliane naye.

**SPIKA:** Yuko wapi mwuliza swali la msingi?

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Nipo mwenyewe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tendo la kuua kwa makusudi mara nyingi hubatilishwa na kupoteza ushahidi kwa kutoa taarifa ya kuua bila kukusudia, je, hali kama hii haoni kwamba ndani yake hujitokeza rushwa?

Pili, kwa kuwa kitendo halisi cha mauaji huonekana na kushuhudiwa na kwa kuwa baada ya kufikishwa Mahakamani huambiwa ushahidi haujakamilika, je, ushahidi gani zaidi ya kutafutwa dhidi ya kitendo chenyewe halisi kilichojitokeza?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI (k.n.y. WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA):** Mheshimiwa Spika, tukio la mauaji au mtu anapotuhumiwa kwamba ameua kama tulivyoeleza katika jibu la msingi ni kwamba lazima uchunguzi kwanza ufanyike. Polisi wanafanya uchunguzi kubaini mazingira ambapo tukio limetokea na katika kufanya hivyo wanakusanya ushahidi kwa kupata statement, maelezo ya wahusika ambao wanadhani wanalifahamu tukio hilo. Sasa maelezo hayo ndio inakuwa ni sehemu ya jalada la Polisi na ndio mtuhumiwa yeyote kwa sababu mtuhumiwa mwenyewe atatoa maelezo yake na wale mashahidi wanatoa maelezo yao na kila anayetoa maelezo inatakiwa kwa taratibu zetu za kisheria za nchi hii asomewe aeleze yote aliyoyasema kama kweli yameandikwa.

Mheshimiwa Spika, pale inapoonekana ushahidi umekamilika na jalada limekamalika basi, mhusika atafikishwa Mahakamani. Sasa yeye kama anaamini kwamba ushahidi uliomo katika jalada hilo sio wa kweli, yeye atajibu ataeleza kwa nini anasema hivyo.

Kuhusu swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kwamba mara nyingi Polisi wanasema bado hawajakamilisha upelelezi au uchunguzi wao, ni kweli kwa masuala ya mauaji mara nyingi kuna sababu mbalimbali. Inawezekana tukio limetokea eneo hili la Dodoma Mjini, lakini watu ambao wanaweza wakasaidia waliokuwepo kwenye tukio hilo unakuta wameshahama, lazima mkawatafute mahali.

Kwa hiyo, mara nyingine inachukua muda lakini sasa hivi tunajaribu kuona uwezekano wa kuiangalia tena sheria kuhusiana na eneo hili hasa kwa makosa ya mauaji tuone ni kiasi gani tunaweza tukaharakisha pale ambapo tukio limetokea kwa kipindi tuseme ndani ya miezi sita na Polisi bado wanasema uchunguzi unaendelea, pawepo na fursa itakayoruhusiwa na sheria kwamba ni heri huyo mtu, basi aweze akaachiwa wakati Polisi wanaendelea na uchunguzi wao. Hayo ni mapendekezo ambayo Serikali imeangalia tuone jinsi gani tunaweza kupunguza malalamiko ambayo yapo hasa katika haya ya kubambikiza wananchi makosa mazito kama ya mauaji.

**SPIKA:** Bado nina maswali mawili, kwa hiyo, bora yapate nafasi, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, swali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Na.137

**Maombi ya Uhamisho kwa Askari**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Askari Polisi kama wafanyakazi wengine huomba uhamisho hasa pale wanapopata matatizo:-

(a) Je, kwa nini maombi ya Askari Polisi ya uhamisho yanachelewa kutolewa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kubadilisha utaratibu wake wa sasa kuhusiana na uhamisho wa Askari Polisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi, Jeshi la Polisi *(PGO)* Na. 60 askari hastahili kufanya kazi katika kituo kimoja zaidi ya miaka sita mfululizo. Katika kipindi hiki anatakiwa awe amehamishwa. Hata hivyo kwa vile uhamisho una gharama kubwa kifedha, uhamisho wa askari polisi hivi sasa unafanyika pale Bajeti inaporuhusu. Pamoja na utaratibu huu wa uhamisho, upo pia utaratibu wa askari kuomba uhamisho iwapo anazo sababu za msingi, anayeomba hutuma maombi yake akiambatanisha vielelezo vya kushawishi kukubaliwa maombi yake, kwa mfano barua ya daktari.

Maombi haya hupitishwa kwa kuzingatia ngazi za Utawala tangu ngazi ya chini yaani kwa Mkuu wa Kituo, Kamanda wa Polisi wa Wilaya, Kamanda wa Polisi wa Mkoa na uamuzi wa mwisho hutolewa na Inspekta Jeneral wa Polisi. Kwa askari wanaohama ndani ya Zanzibar uamuzi wa mwisho hutolewa na Kamishna wa Polisi wa Zanzibar. Maombi ambayo yanakataliwa wahusika huelezwa sababu za kukataliwa kwa maombi yao.Utaratibu huu haucheweshi uhamisho wa askari wanaoomba kuhama, bali unasaidia katika kujenga nidhamu ya askari Jeshini, na hivyo kwa sasa Serikali haioni haja ya kubadilisha utaratibu wa uhamisho wa askari.

Na. 138

**Kukamatwa kwa wananchi wa Kigoma**

**MHE. KILONTSI M.M. MPOROGOMYI** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni umetokea msako wa kuwakamata wananchi hasa wa Mkoa wa Kigoma katika Mikoa ya Kigoma na Dar es Salaam na kuwatuhumu kuwa si raia wa Tanzania na kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakiandikiwa maelezo ya uongo kama vile kuingia nchini Tanzania kuwatafuta mama zao na kwa kuwa wengi

wamewekwa rumande muda mrefu na hivi sasa wanaendelea kwenda Mahakamani jambo ambalo limekuwa kero sana kwao na familia zao na kesi hizo zimekuwa zikiahirishwa kwa visingizio mbalimbali:-

(a) Je, kwa nini wanapokamatwa hawaruhusiwi kusikilizwa maelezo yao na badala yake Polisi au Uhamiaji wanawaandikia *charges* za uongo?

(b) Je, Serikali haina utaratibu wa kuwafuatilia na kujiridhisha kuwa wanaowakamata ni raia au sio raia wakati wale ambao si raia wengi wao wanavinjari Vijijini na katika mitaa mingi ya mijini wala hawasumbuliwi na kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kigoma kama ilivyo Mikoa mingine ya mipakani umeathiriwa na maingiliano na nchi jirani. Mkoa wa Kigoma umeathirika zaidi kutokana na machafuko ya kisiasa katika nchi za Kongo *(DRC)* na Burundi ambapo wimbi kubwa la wahamiaji hukimbilia nchini kwetu kupitia Kigoma, miongoni mwao wakiwa Wakimbizi wanaoishi makambini na wengine wahamiaji haramu wanaoingia nchini na kuzagaa Vijijini na Mijini.

Ili kuwadhibiti wahamiaji haramu, Serikali, kupitia Idara ya Uhamiaji huendesha misako ya mara kwa mara na kuwakamata wahamiaji haramu ambapo hatimaye huwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995. Chini ya Kifungu Na. 30 cha sheria hiyo, anayetuhumiwa kuwa mhamiaji haramu sharti ahojiwe na maelezo kuandikwa. Mtuhumiwa hupewa nafasi ya kupitia maelezo hayo na kusaini ikiwa anakubaliana na maelezo yaliyoandikwa na ndipo anaporejeshwa nchini kwao, kama anakubaliana na hayo mashtaka. Ikiwa hakubaliani na hayo mashitaka shauri hili hupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mbunge wa Kasulu Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si kweli kuwa watuhumiwa wanapokamatwa hawapewi nafasi ya kusikilizwa na kwamba Maafisa wa Uhamiaji wanawabandikia tuhuma za uongo. Hata hivyo kama Mheshimiwa Mbunge au mwananchi mwingine yeyote ana ushahidi wa jambo la namna hii kufanywa na Maafisa wa Idara ya Uhamiaji, alete taarifa itakayotusaidia kuwabaini hawa Maafisa na hatimaye kuwachukulia hatia zipasazo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina utaratibu wa uhakika wa kufuatilia na kujiridhisha kuwa inaowakamata ni wale tu ambao zipo sababu za kutosha za kuwatuhumu kuwa si raia. Kwa mujibu wa utaratibu wa sheria uliopo Kifungu cha 30 cha Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995, jukumu la kuthibitisha uraia kwa

mtuhumiwa liko kwa mtuhumiwa mwenyewe wakati anapohojiwa. Maelezo anayoyatoa mtuhumiwa pamoja na vielelezo atakavyowasilisha ndivyo vitakavyobainisha ukweli kuhusu uraia wake. Wakati wa kuchunguza uraia wa mtuhumiwa, Serikali huwashirikisha raia wema anaoishi nao hivyo si rahisi kuwakamata na kuwafukuza nchini wale ambao ni raia halali wa nchi hii kwa sababu hawatapokelewa nchi wanakopelekwa.

Watuhumiwa wanaolalamika ni wale raia wa nje waliojipenyeza kinyemela na kuishi hapa nchini kwa muda mrefu bila kufuata taratibu na sasa wanajihesabu kuwa raia wa nchi hii wakati Kisheria sio raia.

Aidha nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa bado wapo wahamiaji haramu katika Mkoa wa Kigoma. Hawa tunaendelea kuwasaka ili tuwarejeshe makwao. Tunaomba Mheshimiwa Mbunge kwa vile inaelekea baadhi anawafahamu, atupatie taarifa zao ili sheria ichukue mkondo wake. Ombi hili pia ni kwa mwananchi mwingine yeyote anayewajua wahamiaji haramu wanaovinjari Vijijini na Mijini.

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tatizo hili limekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma na kwa kuwa Serikali ilikwishaahidi kuwa itatoa vitambulisho kwa wananchi wa nchi nzima ya Tanzania, lakini kumejitokeza pengine matatizo ya utekelezaji, je, Serikali itakuwa tayari kutoa vitambulisho hivyo kwa Mikoa ya mipakani kama vile Kigoma, Kagera na Rukwa?*(Makofi)*

Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuzielekeza Taasisi zake utaratibu mzuri kama vile Jeshi la Polisi, Uhamiaji ili wafanye kazi zao vizuri zaidi badala ya kuwahangaisha wananchi maana si kweli kwamba wananchi wanasaini kwamba sisi tunatoka Burundi na sisi tunawajua hawatoki Burundi? Ahsante Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokiri katika majibu yangu ya msingi kwamba iko kero kubwa sana wahamiaji haramu katika Mikoa ya mpakani hasa Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Kagera na kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli tukianzisha utaratibu wa vitambulisho itaturahishia kumjua kwa urahisi zaidi nani Mtanzania nani si Mtanzania.

Suala la vitambulisho litafafanuliwa na Waziri wakati wa hotuba yake ya Bajeti lakini kwa kifupi tu nataka kusema kwamba Serikali inalifanyia kazi na kwamba nia yetu ni kweli kwamba tukianza kuitoa tuanze na Mikoa ya mipakani. Sasa hivi katika maandalizi hayo tumeweka madaftari ya kuorodhesha wageni katika Mikoa hiyo ili baadaye iturahisishie kujua nani mgeni nani si mgeni na zoezi hili linaendelea vizuri kwa mfano katika Mkoa wa Kigoma mpaka sasa wageni ambao sio Watanzania ambao wamekwishaorodheshwa huko Vijijini wanaozagaa Vijijini ni 37,870 na zoezi hili la kuwaorodhesha wageni linaendelea na litatusaidia sana wakati wa kugawa vitambulisho hapo vitakapokuwa tayari.

Kuhusu kuelekeza wataalam wa Idara za Uhamiaji na Polisi wafanye kazi kwa uadilifu badala ya kuwahangaisha wananchi kusema hivyo ndivyo inavyotakiwa wafanye na kwa sehemu kubwa taarifa tuliyonayo hii kazi wanaifanya vizuri walio wengi. Sasa wale wachache ambao wanafanya kazi hiyo bila uadilifu, wanaofanya kazi hiyo kwa kukomoa wananchi, tunaomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa sehemu inayohusika kwa kweli tuleteeni taarifa ili tushirikiane kuwadhibiti hawa wachache ambao wanafanya kazi bila uadilifu. Lakini kwa kiwango kikubwa wanajitahidi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote yamejibiwa sasa tunaendelea na tangazo la kikao cha Kamati ni Kamati moja tu ambayo imepanga kufanya kikao leo nayo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. John Malecela, ameomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Ulinzi na Usalama wahudhurie katika Ukumbi Na. 227 kuanzia saa 5.00 asubuhi hii.

Taaarifa inayofuata ni kwamba Makatibu Mezani wameshapokea maombi na wanaorodhesha maombi ya kuchangia Wizara ya Kilimo na Chakula, bado wanaorodhesha na itakwenda kuchapishwa lakini tunaanza na wale ambao hawajachangia katika hoja zilizotangulia.

Kwa hiyo, wafuatao wajiandae, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah na Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga. Hawa ni wachangiaji wanne wa kwanza wakati orodha inaendelea kutayarishwa.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge nina maelezo yafuatayo, katika kikao cha Ijumaa iliyopita kikao cha 13 cha Mkutano huu Bajeti, Mheshimiwa Abdillah Namkulala, aliomba kupata mwongozo wa Spika, akitaka kujua ni kwa nini kuna tofauti ya kutoa heshima kwa misiba inayotokea na akatoa mfano kwamba marehemu Dr. Omar Ali Juma aliyekuwa Makamu wa Rais alipofariki Kikao cha Bunge kiliahirishwa kama sehemu ya maombolezo ya kifo hicho.

Mheshimiwa Namkulala akasema lakini Mheshimiwa Yete Mwalyego, alipofariki juzi na kabla yake aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge wa Liwale Mheshimiwa Ngajulage alipofariki Bunge liliendelea na vikao vyake kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyekuwa kwenye Kiti cha Spika wakati huo alijibu kwamba jambo hilo halimo katika Kanuni kwa hiyo, akasema atalifikisha kwa Spika ili aweze kulitolea ufafanuzi.

Napenda basi kutumia nafasi hii kutoa ufafanuzi huo aliouahidi Mheshimiwa Naibu Spika. Ni kweli kwamba jambo hilo halimo katika Kanuni tulizonazo hivi sasa. Kwa kuwa haimo katika Kanuni uamuzi wa kuahirisha kikao chochote cha Bunge kisifanyike ni uamzi mzito ambao lazima ufanyike kwa misingi wa vigezo ambavyo vinaweza vikaelezeka vikaeleweka na vikakubaliwa.

Sasa kigezo pekee ambacho Spika, amekuwa akikitumia katika kufikia uamzi wa kuahirisha vikao vya Bunge ili kuomboleza msiba fulani ni pale ambapo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapotangaza kifo husika kuwa msiba wa Kitaifa na anaamuru bendera zote za Taifa katika nchi nzima zipepee nusu mlingoti kama sehemu ya maombolezo ya kifo hicho.

Sasa baada ya tangazo kama hilo kutolewe endapo kifo cha aina hiyo kinatokea wakati vikao vya Bunge vinaendelea ndipo Spika, anaahirisha kikao cha siku hiyo kama sehemu ya maombolezo ya Kitaifa ya msiba huo. Hivyo ndivyo ilivyofanyika alipofariki Marehemu Dr. Omar Ali Juma aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati ule na hivyo ndivyo vile vile ilivyofanyika wakati wa ajali mbaya ya treni iliyotokea karibu na hapa Dodoma ambayo kama tunavyokumbuka ilichukua roho za Watanzania zaidi ya 200 kwa pamoja. Kila moja ya matukio hayo mawili yalitangazwa na Mheshimiwa Rais kuwa ni msiba wa Kitaifa na aliamuru bendera zote zipepee nusu mlingoti. Wakati wa matukio yote mawili vikao vya Bunge vilikuwa vikiendelea hapa Dodoma. Kwa hiyo, Spika alichukua hatua ya kusitisha vikao husika kwa kutumia kigezo hicho cha msiba wa Kitaifa.

Kifo cha Mbunge yeyote hakijawahi kutangazwa na Rais kuwa ni msiba wa Kitaifa na hajawahi kuamuru bendera zote za Taifa zipepee nusu mlingoti ndiyo sababu vikao vya Bunge havikusitishwa katika matukio ya vifo ya Marehemu Ngajulage na Marehemu Mwalyego. Lakini pamoja na kutoahirisha kikao cha Bunge bado kama WaheshimiwaWabunge wanavyofahamu tunao utaratibu mzuri tu wa kuheshimu msiba wa Mbunge unapotokea wakati vikao vya Bunge vikiendelea.

Kwa hiyo, utaratibu ndiyo uliotumika hivi majuzi katika kushughulikia kifo cha Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego na ndiyo uliotumika kabla ya hapo katika kushughulikia kifo cha Marehemu Mheshimiwa Ngajulage. Naamini kuwa kigezo kilichotajwa cha msiba wa Kitaifa ambacho kimekuwa kikitumika katika kufanya uamuzi wa kuahirisha au kutokuahirisha vikao vya Bunge kinaeleweka na kinakubalika. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/2005
### Wizara ya Kilimo na Chakula

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi inayohusu Wizara ya Kilimo na Chakula na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja, kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuwakilisha Taifa letu katika Bunge la Kwanza la Afrika.

Wabunge hao ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini. Aidha, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Kwanza wa Bunge hilo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena na kwa kishindo kikubwa na wananchi wa Bariadi kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, kuwa Mbunge wao. Kuchaguliwa kwake ni ushahidi wa imani ambayo wananchi wa Bariadi wanayo kwa Chama cha Mapinduzi na kwake binafsi. Tunamkaribisha tena Bungeni na tunamwahidi ushirikiano katika juhudi zake za kuharakisha maendeleo ya jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mbunge kwa mara ya pili. Tunamkaribisha Bungeni na tunampa pole kwa kuumia katika ajali ya barabarani na tunamwombea arejee katika afya nzuri mapema. Nampa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa matatizo aliyoyapata. Vile vile nampa pole Mheshimiwa Estherina Kilasi, kwa ajali aliyoipata.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kupokea na kuchambua kwa makini taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo na Chakula ya mwaka wa 2003/2004 na Makadirio ya Matumizi ya mwaka 2004/2005 katika kikao kilichofanyika Dar es Salaam, tarehe 26 Mei, 2004.

Kamati ilitoa maelekezo ya maeneo yanayopaswa kuzingatiwa ili Taifa liondokane na tatizo la uhaba wa chakula na kuiwezesha sekta ya kilimo kutoa mchango mkubwa zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuondoa umaskini. Napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na ushirikiano wao. Maelekezo waliyotoa yamezingatiwa katika Makisio ya Matumizi ya fedha ya mwaka wa 2004/2005 ambayo nayawasilisha leo mbele ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Kamati ya Kilimo na Ardhi ilitembelea vituo vya utafiti wa mazao vilivyopo Kibaha, Mlingano, Tanga, Selian, Arusha, Lyamungo, Kilimanjaro, mashamba ya kahawa na maua yaliyopo Arusha na Kilimanjaro na mashamba ya mkonge yaliyopo Tanga na Morogoro. Katika ziara hizo, Kamati ilipata fursa ya kukutana na watendaji na wakulima na kutoa maoni na maelekezo ya kuboresha uzalishaji. Utaratibu wa Kamati kutembelea maeneo na vituo vya huduma za uzalishaji umeonyesha mafanikio katika kuiwezesha Kamati kuyaelewa vizuri matatizo yanayoikabili sekta ya kilimo na katika kuwatia moyo wadau wake. Katika mwaka wa 2004/2005, Kamati itaendelea kutembelea vituo vya kilimo na wakulima katika maeneo mengine ya nchi ambayo haijapata nafasi ya kuyatembelea.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Katibu Mkuu, Bwana Wilfred Ngirwa,

Wakuu wa Idara, Taasisi na asasi zilizoko chini ya Wizara, watumishi wote na wadau wa sekta ya kilimo kwa ushirikiano na ushauri wao katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2004. Watendaji hawa wameshiriki kikamilifu katika kutekeleza Mpango wa Kilimo wa mwaka wa 2003/2004 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka wa 2000. Aidha, wamechangia katika kuandaa taarifa mbalimbali ikiwemo Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka wa 2003/2004 na Makisio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa 2004/2005, ninayoiwasilisha mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 21 Juni, 2004 ambayo ilitoa taarifa juu ya hatua zilizochukuliwa na Serikali katika mwaka wa 2003/2004 kukuza kilimo na kukabiliana na tatizo la njaa lililozipata baadhi ya sehemu za nchi yetu. Aidha, alifafanua hatua ambazo Serikali inakusudia kuchukua kuongeza kasi ya ukuaji wa kilimo kwa lengo la kulihakikishia Taifa upatikanaji wa chakula, kuondoa umaskini na kuongeza mchango wa kilimo katika uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha alichukua hatua madhubuti za kuondoa vikwazo vinavyokwamisha kukua na uwekezaji katika sekta kubwa ya kilimo. Katika hotuba yake ya Bajeti ameondoa karibu kodi zote zinazowezekana kuondolewa kwenye sekta ya kilimo na ameweka vivutio vya kuwezesha wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika kilimo, ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kudhamini mikopo itakayotolewa kwa wakulima wadogo na wauzaji wa mazao nje ya nchi. Kama kuna kodi nyingine zilizosalia, ameahidi kuzishughulikia iwapo zitawasilishwa kwake. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa hatua zilizochukuliwa katika Bajeti ya mwaka huu na nina hakika matokeo yake yataonekana katika miaka michache ijayo.

Hotuba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ilichambua hali ya kilimo chetu, mchango wa kilimo katika uchumi wa nchi na athari zilizotokea kwenye uchumi katika mwaka uliopita kutokana na ukame uliosababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo. Waziri aliorodhesha hatua ambazo zikichukuliwa, kasi ya ukuaji wa uchumi wetu, uhakika wa upatikanaji wa chakula utaimarika na umaskini kupungua. Hotuba za Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji zimepitia karibu maeneo yote yanayohusiana na kilimo na kutoa maelekezo ya Serikali juu ya hatua za kuchukuliwa ili kuongeza mchango wa kilimo katika maisha na uchumi wa Taifa letu. Nawashukuru Mawaziri hao kwa kunipunguzia kazi na naomba hotuba zao zisomwe kama sehemu ya Makisio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa 2004/2005.

Karibu Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba zilizotangulia waligusia sekta ya kilimo. Michango yao ilichambua kwa undani matatizo yanayokifanya kilimo kidumae, dosari wanazoziona katika uendeshaji na usimamizi wa kilimo na walitoa ushauri juu ya hatua wanazoamini kwamba zikichukuliwa kilimo chetu kitakuwa bora zaidi. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliotoa maoni yao juu ya kilimo na nawahakikishia kwamba Serikali imewasikia na hatua zinazostahili zitachukuliwa kulingana na uwezo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zitakazochukuliwa tayari zimefafanuliwa na Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na nitatoa ufafanuzi zaidi katika Makisio ya Matumizi ninayowasilisha mbele ya Bunge hili Tukufu. Tunahitaji kuongeza sana uwekezaji katika kilimo lakini kiwango kitakachowekezwa kitategemea uwezo wa Serikali na vipaumbele vilivyopo.

Aidha, kukua kwa kilimo kutategemea michango ya wakulima, sekta binafsi, wadau wengine na Serikali ambayo itaendelea kujenga mazingira yatakayowezesha kuongezeka kwa uwekezaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alichaguliwa na wakuu wa nchi za *SADC* kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 25 Agosti, 2003. Katika hotuba yake ya kupokea wadhifa huo, Rais aliahidi kuyapa kipaumbele masuala ya amani, usalama, uhakika wa upatikanaji wa chakula na UKIMWI katika eneo la *SADC.* Kufuatia azma hiyo, Rais aliitisha Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi za *SADC* uliofanyika Dar es Salaam tarehe 15 Mei, 2004 kujadili hali ya kilimo na upatikanaji wa chakula katika nchi za *SADC* na kukubaliana juu ya hatua za kuchukuliwa kuongeza kasi ya kukua kwa kilimo na kuondokana na hali ya kutokea kwa upungufu wa chakula mara kwa mara katika eneo hili. Mkutano huo ulikuwa na mafanikio makubwa sana na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na kwa juhudi zake za kuongoza mapambano dhidi ya njaa na umaskini.

Tarehe 12 Machi, 2004, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa, alizindua Mpango wa Kuendeleza Uchumi wa Nchi za *SADC (Regional Indicative Strategic Development Plan - RISDP)* mjini Arusha. Katika hotuba yake ya kuzindua mpango huo, Rais alisisitiza umuhimu wa nchi wanachama wa *SADC* kutekeleza Azimio la Wakuu wa Nchi za Afrika *(Afirican Union).* Kuhusu Kilimo na Uhakika wa Upatikanaji wa Chakula walilolitoa katika mkutano wao uliofanyika Maputo, Msumbiji Julai, 2003. Azimio hilo linazitaka nchi za Afrika kuongeza kiasi cha Bajeti za nchi zao kinachotengwa kwa ajili ya kilimo hadi kufikia kiwango kisichopungua asilimia 10 ya Bajeti hizo katika kipindi cha miaka mitano tangu tarehe ya azimio hilo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2003/2004, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa alikuwa Mwenyekiti Mwenza wa Tume ya Utandawazi. Tume hiyo ilikamilisha kazi zake na kutoa taarifa nzuri sana inayoonyesha athari za utandawazi, hususan kwa nchi maskini kama yetu na njia ya kukabiliana nazo. Mapema mwaka huu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Mtanzania mwingine, Profesa Anna Tibaijuka, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa *(HABITAT),* waliteuliwa na Waziri Mkuu wa Uingereza kujiunga na Kamisheni ya Afrika kupendekeza ni nini kifanyike kulikwamua Bara la Afrika kutoka kwenye matatizo yanayodumaza maendeleo yake na kulifanya maskini. Rais ameweka bendera ya Tanzania juu ya Mlima Kilimanjaro na tunampongeza na kumshukuru kwa kuliletea Taifa letu sifa miongoni mwa mataifa ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba katika mwaka wa 2003/2004 nchi yetu ilikabiliana na upungufu wa chakula uliosababishwa na upungufu wa mvua katika baadhi ya maeneo ya nchi. Tarehe 31 Machi, 2003, Mheshimiwa Rais, katika hotuba yake kwa Taifa chini ya utaratibu aliojiwekea wa kufafanua masuala mbalimbali kwa umma kila mwisho wa mwezi, aliwatahadharisha wananchi juu ya kuwapo kwa uwezekano wa kutokea kwa upungufu mkubwa wa chakula nchini na akaelekeza hatua za kuchukuliwa na wakulima, Serikali na asasi zinazohusika.

Mheshimiwa Rais aliendelea kufuatilia hali ya chakula nchini na katika hotuba yake ya mwaka mpya kwa Taifa aliyoitoa tarehe 31 Desemba, 2004 alifafanua hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na upungufu wa chakula na alihimiza wananchi kutumia chakula kwa uangalifu, kulima mazao yanayostahimili hali za hewa katika maeneo yao na kila kaya kujiwekea akiba ya chakula. Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake na kwa maelekezo yake juu ya hatua za kuchukuliwa ili kulihakikishia Taifa uhakika wa upatikanaji wa chakula. Maagizo yake yamezingatiwa katika makisio ya matumizi ya mwaka wa 2004/2005 na yataendelea kuzingatiwa katika makisio ya miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, sherehe za Nane Nane mwaka 2003 zilifanyika Kitaifa kwa mara ya kwanza kwenye Viwanja vya Nane Nane vilivyoko Uyole, Mbeya ambako Rais Mstaafu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, alikuwa mgeni rasmi na sherehe hizo zilifanyika pia katika viwanja vya Taifa vya Nane Nane vilivyoko Morogoro ambako Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye, alikuwa mgeni rasmi.

Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, alisisitiza umuhimu wa kuwa na mipango madhubuti ya kilimo, aliwaasa wananchi kuchukua tahadhari za kupambana na hali ya ukame kama wanavyoshauriwa na viongozi na wataalam. Aidha, aliwataka wataalam na viongozi wa Serikali wasimamie utekelezaji wa maagizo hayo kwa uwezo wao wote ili Taifa liondokane na janga la njaa.

Namshukuru sana Rais Mstaafu Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, kwa kukubali kushiriki katika siku hiyo muhimu kwa wakulima. Maadhimisho ya Nane Nane ya Mbeya yalifanikiwa sana kutokana na juhudi kubwa zilizofanywa na Wakuu wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Wizara, Mashirika na wafanyabiashara binafsi walioshiriki katika maonyesho na mahudhurio makubwa sana ya wananchi. Nawashukuru sana viongozi na wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, hususan wananchi wa Mkoa wa Mbeya, kwa maandalizi mazuri, kujitokeza kwa wingi na kwa kufanikisha siku hiyo. Aidha, sherehe za Nane Nane zifanyika katika Viwanja vya Themi vilivyoko Arusha, Kaitaba, Bukoba na kwenye viwanja vingine vya Mikoa na Wilaya. Nawapongeza wote walioshiriki katika kuandaa sherehe hizo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Oktoba, 2003 Taifa liliadhimisha Siku ya Chakula Duniani katika Kijiji cha Maguu kilichoko kwenye Wilaya ya Mbinga, Mkoani Ruvuma. Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein alikuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo. Katika hotuba yake kwenye maadhimisho hayo, alizungumzia tatizo

la upungufu wa chakula na kuwataka wananchi waongeze juhudi za uzalishaji wa mazao ya chakula, kuhifadhi chakula na kutumia chakula walichokuwa nacho kwa uangalifu. Namshukuru sana Makamu wa Rais kwa kushiriki kwenye maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani na kwa maelekezo hayo muhimu ambayo tunaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, kilimo kimekuwa kikikua kwa wastani wa asilimia 3.7 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji wa watu cha asilimia 2.9 kwa mwaka. Tatizo kubwa la kilimo chetu ni kwamba kimeendelea kutegemea mvua ambazo hazitabiriki.

Kuanzia mwaka wa 1999 kilimo kimeanza kuonyesha dalili nzuri za kuongeza kasi ya kukua ambapo katika mwaka huo, kilimo kilikua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.9 katika mwaka wa 1998. Mwaka wa 2000 kilimo kilikua kwa asilimia 3.4, mwaka wa 2001 asilimia 5.5, asilimia 5.0 mwaka wa 2002 na asilimia 4.0 mwaka wa 2003. Ili kilimo kiweze kutoa mchango wa kuridhisha katika ukuaji wa uchumi, usalama wa chakula na kuondoa umaskini kinapaswa kukua kwa kiwango kisichopungua asilimia 10 hadi 11 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho kitaweza kufikiwa iwapo kilimo kitapatiwa mahitaji yake ya pembejeo, zana za kilimo, utaalam na masoko ya uhakika. Viwango vya sasa vya ukuaji wa sekta ya kilimo bado ni vya chini sana. Kushuka na kupanda kwa ukuaji wa kilimo kunatokana na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kunakosababishwa na ukame na mabadiliko ya bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003, sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 5.0 ya mwaka wa 2002. Sekta ndogo ya mazao ilikua kwa asilimia 3.6 tu ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka uliotangulia. Kushuka huku kwa ukuaji wa sekta ya kilimo, hususan sekta ndogo ya mazao, kulitokana na ukame uliotokea katika baadhi ya maeneo ya nchi ambao ulisababisha kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Kama itakavyofafanuliwa kwa kina zaidi baadaye, uzalishaji wa mazao ya chakula ulishuka kwa asilimia 10. Wakati uzalishaji wa mazao ya biashara, hususan korosho ulishuka kwa asilimia 15.78, pamba asilimia 26.92, kahawa asilimia 28.49 na pareto asilimia 33.33.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 kilimo kinatarajiwa kukua kwa zaidi ya asilimia tano. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha kwamba viwango tunavyofikia vya ukuaji wa sekta ya kilimo vinaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Lengo hilo litafikiwa iwapo tutaongeza uwekezaji katika kuendeleza raslimali za uzalishaji, usindikaji, miundombinu, upatikanaji wa masoko na kuimarisha usimamizi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Taifa lilikumbwa na upungufu wa chakula uliokisiwa kuwa asilimia 10 ya mahitaji ya chakula kwa mwaka. Mahitaji ya chakula kwa mwaka wa 2003/2004 yalikisiwa kuwa tani milioni 8.37, wakati uzalishaji katika msimu wa 2002/2003 ulikuwa tani milioni 7.55, hivyo kuwepo kwa upungufu wa tani 800,000 za chakula. Mwanzo wa msimu wa 2003/2004, Serikali ilikuwa na akiba ya tani 50,661 katika Hifadhi ya Chakula ya Taifa, wananchi walikisiwa kuwa na akiba ya

tani 300,000 na wafanyabiashara walikuwa na tani 100,000 na hivyo kufanya kuwepo kwa akiba ya chakula iliyokadiriwa kuwa tani 450,700 na kufanya pengo lililokuwepo kupungua kutoka tani 800,000 hadi tani 350,000.

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai, 2003 Serikali, kwa kushirikiana na wadau katika masuala ya usalama wa chakula, ilifanya tathmini ya kina ya hali ya chakula na kubaini kuwepo kwa wananchi karibu milioni mbili katika mikoa 16 ambao walikuwa na upungufu wa chakula na wangehitaji tani 77,490 za chakula kati ya miezi ya Oktoba, 2003 na Machi, 2004 kama mvua za vuli zingenyesha kwa kiwango cha kuridhisha. Kama mvua za vuli zisingenyesha kwa viwango vya kuridhisha, Taifa lingehitaji tani 149,295 za chakula kwa ajili ya kulisha familia ambazo zingekuwa na upungufu wa chakula kati ya Oktoba, 2003 na Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya Bajeti ya mwaka wa 2004/2005, upungufu wa chakula ulitokea katika maeneo mengi ya nchi katika msimu wa 2003/2004. Ili kukabiliana na upungufu uliojitokeza Serikali ilinunua tani 23,925 kutoka kwenye maeneo yenye ziada ya chakula kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa kwa shilingi 2,871,000,000/=.

Aidha, Serikali ilinunua tani 10,000 za mahindi kutoka Kenya kwa shilingi 2,099,556,432/=. Mahindi hayo yalisafirishwa hadi Musoma na Shinyanga kwa shilingi 1,264,576,000/=. Namshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alifanya mpango wa kupatikana kwa mahindi hayo alipotembelea Jamhuri ya Kenya mwezi wa Desemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, hatika mwezi wa Machi, 2004 Serikali ilinunua tani 22,000 za mahindi kwa *tender* kwa shilingi 6,568,165,862/=. Serikali iligharamia usafirishaji wa mahindi hayo kutoka bandarini hadi kwenye maghala ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa yaliyoko Kipawa kwa shilingi 114,161,400/=. Aidha, Serikali iligharamia uhamishaji wa tani 7,902 za mahindi kutoka Sumbawanga kwenda Shinyanga na Tabora kwa shilingi 225,360,000/=, tani 4,972 kutoka Songea kwenda Dodoma kwa shilingi milioni 200/=, tani 9,064 kutoka Makambako kwenda Kipawa kwa shilingi 233,831,724/=, tani 2,006 kutoka Kipawa kwenda Dodoma kwa shilingi 120,465,753/= na tani 4,500 kutoka Kipawa kwenda Arusha kwa shilingi 317,197,630/=.

Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali ilitumia jumla ya shilingi 15,614,314,801/= kununua chakula kutoka ndani na nje ya nchi na kusafirisha chakula kutoka kwenye vituo vya ununuzi kwenda kwenye vituo vya usambazaji ambavyo ni Kipawa, Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Tabora na Shinyanga.

Pamoja na jitihada hizo za Serikali, katika mwezi wa Agosti, 2003, Serikali iliziomba nchi na mashirika wahisani msaada wa tani 45,000 za chakula. Baadhi ya wahisani waliitikia wito huo na kutoa msaada wa chakula au fedha kupitia kwenye Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(World Food Programme -WFP).* Tani 29,068 za mahindi zilipatikana. Nchi zilizotoa msaada wa chakula ni Sweden *(US $ 1,500,000),*

Uingereza *(US $ 2,200,000),* Marekani (tani 15,000 za mahindi), Jamhuri ya Ireland *(US $ 65,000)* na Japan *(US $ 300,000)*.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya mchango huo, Serikali ya Japan, kupitia kwenye mpango wa *Kennedy Round I (KRI),* ilitoa tani 17,000 za mchele na tani 3,000 za ngano. Hadi tarehe 30 Mei 2004, jumla ya tani 42,694 za mahindi, tani 135,597 za mchele na tani 429,309 za ngano zilikuwa zimeingizwa nchini na wafanyabiashara. Aidha, Serikali ya India ilitoa tani 5,000 za mchele na tani 5,000 za ngano ambazo ziliwasili nchini mwezi wa Mei, 2004 na kuhifadhiwa kwenye maghala ya Hifadhi ya Chakula ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali kukabiliana na upungufu wa chakula zilijumuisha kutoa tani 30,224 za mahindi kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa na kuziuza kwa bei nafuu ya shilingi 50/= kwa kilo kwa wananchi waliokabiliwa na upungufu na ambao hawakuwa na uwezo wa kununua mahindi kwa bei ya soko. Aidha, Hifadhi ya Chakula ya Taifa iliuza jumla ya tani 28,612 za mahindi kwa taasisi na wafanyabiashara kwa bei ya shilingi 150 kwa kilo ili kupunguza makali ya bei za mazao ya chakula iliyokuwa ikipanda.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 27 Juni, 2004, jumla ya tani 40,287.165 za chakula zilikuwa zimehifadhiwa kwenye vituo vya Hifadhi ya Chakula ya Taifa vilivyopo Kipawa, Arusha, Dodoma, Shinyanga, Makambako, Songea, Sumbawanga na Musoma Aidha, wafanyabiashara walikuwa na jumla ya tani 116,767 na wananchi kwenye maeneo mengi ya nchi walikuwa wameanza kuvuna mazao ya chakula.

Akiba ya chakula katika vituo vya Hifadhi ya Chakula ya Taifa *(SGR)* hadi tarehe 27 Juni, 2004 ilikuwa kama ifuatavyo:-

| **Kituo** | **Akiba (Tani)** |
|---|---|
| DSM/Kipawa | 24,925.906* |
| Arusha | 3,650.500 |
| Dodoma | 590.016 |
| Shinyanga | 8,177.425 |
| Makambako | 1,123.919 |
| Songea | 1,043.036 |
| Sumbawanga | 179.701 |
| Musoma | 596.662 |
| Jumla | 40,287.165 |

Mheshimiwa Spika, alama * inajumuisha tani 14,925.906 za mahindi, tani 5,000 za mchele na tani 5,000 za ngano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Watendaji wa Serikali, Wananchi na Wahisani walioshiriki katika kuhakikisha kufanikiwa kwa zoezi la kukabiliana na upungufu wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2003/2004 inaonyesha kuwa uzalishaji utafikia tani milioni 9.0, zikiwemo tani milioni 4.93 za mazao ya nafaka na tani milioni 4.07 za mazao yasiyo ya nafaka.

Tathmini hiyo imeonyesha kuwa Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Mtwara, Lindi, Kigoma, Kagera, Tabora, Singida, Dodoma, Mwanza, Tanga, Morogoro na Mara itajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada. Hali hiyo inatokana na maeneo hayo kupata mvua za kutosha na matumizi mazuri ya mbolea, hususan katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ambayo ilinufaika na utaratibu wa Serikali wa kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea. Makisio ya mahitaji ya chakula katika mwaka wa 2004/2005 ni tani milioni 8.61. Kwa hiyo, Taifa litajitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ndogo ya tani milioni 0.39.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2003/2004 baadhi ya maeneo nchini hayakupata mvua za kutosha na yanatarajiwa kuwa na upungufu wa chakula. Maeneo hayo yako katika Mikoa ya Arusha, Wilaya za Arumeru na Karatu, Manyara, Wilaya za Simanjiro na Hanang, Kilimanjaro, Wilaya za Same na Mwanga, Shinyanga, Wilaya za Shinyanga Vijijini, Shinyanga Mjini, Kishapu, Maswa na Meatu, Pwani, Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Kisarawe na Mtwara, Wilaya ya Masasi. Maeneo mengine yako katika Mikoa ya Mwanza, wilaya za Magu na Kwimba, Mara, Wilaya ya Bunda, Singida, Wilaya za Manyoni na Singida Vijijini; Tabora, Wilaya za Igunga na Nzega, Dodoma, Wilaya ya Dodoma vijijini na Tanga Wilaya za Korogwe, Pangani, Muheza, Lushoto na Tanga.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa chakula unaotegemewa kuwepo katika baadhi ya maeneo nchini, Serikali itaendelea kuwahimiza wananchi kuhifadhi chakula cha kutosha kwa kila kaya hadi watakapokuwa na hakika ya mavuno ya msimu unaofuata. Katika maeneo yenye ziada ya chakula, wakulima wanahimizwa kuuza ziada baada ya kuhakikisha wameweka akiba ya kutosha mwaka mzima.

Aidha, wafanyabiashara wanahimizwa kununua chakula katika maeneo yenye ziada na kukiuza katika maeneo yenye upungufu. Hifadhi ya Chakula ya Taifa itaanza msimu ikiwa na tani 40,287 za chakula zilizohifadhiwa katika vituo karibu na maeneo yenye upungufu wa chakula. Aidha, Hifadhi ya Chakula ya Taifa inatarajia kununua kati ya tani 75,000 na 100,000 za mahindi na mtama kutoka kwenye maeneo yenye ziada ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* ya mwezi wa Aprili, 2004 kuhusu matarajio ya chakula katika mwaka wa 2004/2005, inaonyesha kwamba ingawa nchi za Zambia na Msumbiji zilipata mvua nzuri katika kipindi cha Februari na Machi, 2004, mafuriko yaliyozikumba baadhi ya sehemu za nchi hizo yaliharibu mazao mashambani na kuathiri upatikanaji wa chakula katika nchi hizo.

Aidha, nchi ya Kenya itakuwa na upungufu wa chakula kwa watu karibu milioni moja, wakati nchi ya Uganda itakuwa na hali ya wastani. Nchi za Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Burundi zitaendelea kuwa na upungufu wa chakula kutokana na migogoro ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 uzalishaji wa zao la tumbaku umeongezeka kutoka tani 32,693.62 zilizozalishwa mwaka wa 2002/2003 hadi tani 46,725 mwaka wa 2003/2004, sawa na ongezeko la asilimia 43, ukilinganishwa na uzalishaji wa mwaka wa 2002/2003. Ongezeko hilo limetokana na utumiaji wa aina mpya za mbegu bora za tumbaku ya mvuke na mbolea aina ya *NPK 10:18:24.* Mbolea na mbegu hizo ni bora zaidi kuliko zilizokuwa zinatumika awali.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa chai umeongezeka kutoka tani 28,028 mwaka wa 2002/2003 hadi tani 30,700 mwaka wa 2003/2004, sawa na ongezeko la asilimia 9.53. Ongezeko hilo linatokana na ufumbuzi uliopatikana kwa migogoro iliyokuwa ikivikabili viwanda vya Bukoba, Dabaga na Lupembe. Mipango ya kumpata mbia atakayeshirikiana na *Kibena Tea Company* kuendesha kiwanda cha Dabaga inakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa vyama vya wakulima wadogo wa chai kumechangia katika kuongeza uzalishaji wa chai. Kwa mfano, wakulima wadogo wa chai waliongeza uzalishaji wa majani mabichi kutoka tani 22,750 za mwaka wa 2002/2003 hadi tani 25,300 mwaka wa 2003/2004. Ongezeko hilo limetokana na upanuzi wa maeneo yanayolimwa chai ambapo jumla ya miche milioni 15.5 ya chai ilipandwa katika mwaka wa 2003/2004. Mwaka wa 2002/2003 wakulima walipanda miche milioni 4 ya chai.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa sukari, kufuatia ukarabati na upanuzi wa viwanda vya sukari na mashamba ya miwa uliofanyika baada ya zoezi la ubinafsishaji kukamilika, uzalishaji wa sukari umeongezeka kutoka tani 190,120 mwaka wa 2002/2003 hadi tani 228,000 mwaka wa 2003/2004. Aidha, wakulima wadogo wa miwa *(Cane outgrowers)* waliongezeka kutoka wakulima 5,800 mwaka wa 2002/2003 hadi kufikia wakulima 8,000 mwaka wa 2003/2004 na hivyo kuchangia katika kuwaongezea mapato wakulima katika maeneo yanayozunguka viwanda vya sukari.

Sukari iliyouzwa nje iliongezeka kutoka tani 10,200 mwaka 2002/2003 hadi tani 22,750 mwaka wa 2003/2004. Ongezeko lilitokana na hatua ya Tanzania kujiunga katika mpango wa *EU* unaoruhusu nchi maskini kuuza bidhaa zao bila ushuru katika soko la Ulaya *(Everything But Arms - EBA).* Kutokana na mauzo hayo Taifa liliweza kupata fedha za kigeni zaidi ya shilingi bilioni 16 katika msimu 2003/2004, ikilinganishwa na shilingi bilioni 12 zilizopatikana mwaka wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya korosho, kahawa na pamba ulishuka kutokana na hali ya ukame ulioyakabili maeneo mengi yanayolima mazao hayo. Kwa mfano, uzalishaji wa zao la korosho ulishuka kwa asilimia 15.78 kutoka tani 90,000 msimu wa 2002/2003 hadi tani 80,000 msimu wa 2003/2004. Aidha, uzalishaji wa kahawa ulishuka kwa asilimia 28 kutoka tani 52,439 hadi tani 37,500 na uzalishaji wa pamba ulishuka kwa asilimia 27 kutoka tani 188,690 hadi tani 137,899. Uzalishaji wa

pareto ulishuka kwa asilimia 33 kutoka tani 3000 hadi tani 2000 kutokana na tatizo la kutokuwa na soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kahawa na pamba katika msimu wa 2003/2004, mapato ya fedha za kigeni yaliyotokana na mauzo ya mazao hayo yaliongezeka. Mwaka wa 2003/2004 mapato yaliyotokana na mauzo ya kahawa yalikuwa dola za kimarekani milioni 50, ikilinganishwa na dola milioni 35.14 katika mwaka wa 2002/2003, sawa na ongezeko la asilimia 42.

Aidha, mapato yaliyotokana na mauzo ya pamba yalikuwa dola milioni 46.6, mwaka wa 2003/2004, ikilinganishwa na dola milioni 28.14 katika mwaka wa 2002/2003, sawa na ongezeko la asilimia 66. Ongezeko hilo la mapato linatokana na kuongezeka kwa ubora wa mazao hayo na bei katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zao la mkonge umeongezeka kutoka tani 23,641 zilizozalishwa mwaka wa 2002/2003 hadi tani 23,858 za mwaka wa 2003/2004. Ushirikishwaji wa wakulima wadogo katika kilimo cha mkonge, hususan katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Viktoria umesaidia kuongeza eneo linalopandwa mkonge kutoka hekta 1,562 mwaka wa 1998 hadi hekta 3,373 mwaka wa 2003. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya miliki za baadhi ya mashamba ya mkonge yanayobinafsishwa ili yaweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika uzalishaji wa zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji wa mazao makuu ya biashara hadi mwezi Machi, 2004 ni kama ifuatavyo kwa uzalishaji kwa Tani:-

| **ZAO** | **2001/2002** | **2002/2003** | **2003/2004** | **Asilimia ya ongezeko** |
|---|---|---|---|---|
| Tumbaku | 31,700 | 32,693.62 | 46,725 | 42.91* |
| Sukari | 164,000 | 190,120 | 228,000 | 19.92 |
| Chai | 24,732 | 28,028 | 30,700 | 9.53 |
| Mkonge | 23,540 | 23,641 | 23,858 | 0.92 |
| Korosho | 67,369 | 90,000 | 80,000 | -15.78 |
| Pamba | 149,091 | 188,690 | 137,899 | -26.92 |
| Pareto | 3,500 | 3,000 | 2,000 | -33.33 |
| Kahawa | 36,175 | 52,439 | 37,500 | -28.49 |

Mheshimiwa Spika, mazao ya mboga, matunda na viungo ni miongoni mwa mazao ambayo yana bei nzuri na soko lenye uhakika ndani na nje ya nchi. Uzalishaji wa mazao hayo unatoa fursa ya kuwaongezea wakulima uwezo wa kupambana na hali ya umaskini. Uzalishaji wa matunda unakadiriwa kufikia tani 823,000 katika mwaka wa 2003/2004, ambalo ni ongezeko la asilimia 33, ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 551,410 katika mwaka wa 2002/2003. Uzalishaji wa mboga unakadiriwa kulifikia tani 603,000 katika mwaka wa 2003/2004, ambalo ni ongezeko la asilimia 10, ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 542,700 katika mwaka wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, wastani wa tani 3,930 za maua na mboga zilizalishwa na kuuzwa nchi za nje kutoka msimu wa 2000/2001 hadi 2003/2004. Sehemu kubwa ya uzalishaji wa maua na mboga inayouzwa nje ya nchi inatoka katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mauzo ya mboga na maua mwaka wa 2002/2003 inaonyesha kwamba mauzo yaliongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 11.0 hadi kufikia dola milioni 25.7 katika mwaka wa 2003/2004 sawa na ongezeko la asilimia 133.64 Mapato yaliyotokana na mauzo ya mazao hayo kwa mwaka wa 2002/2003 yalikaribiana na mapato yaliyotokana na mauzo yote ya zao la chai kwa mwaka huo. Wakulima wa maua na mboga watapewa vivutio vya kuwawezesha kuzalisha kwa wingi na kwa ufanisi zaidi ili waweze kusafirisha mazao yao kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima 350 na wataalam 40 kutoka mikoa ya Iringa, Morogoro, Tanga, Pwani na Dar es Salaam yaliwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao mapya husan Paprika, vanilla na migomba bora.

Aidha, Wizara ilizalisha miche 35,000 ya mazao ya migomba, miembe, michungwa na minazi katika vituo vya kuzalisha vipando vilivyopo katika mikoa ya Tanga na Pwani na kuisambaza kwa wakulima katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 Wizara ya Kilimo na Chakula ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 54.15. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 22.63 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 31.52 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 6.44 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 25.08 zilikuwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iliomba na kupewa fedha kutoka kwenye Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan na kupata shilingi bilioni 0.94 zilizotumiwa kwa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji maji mashambani shilingi bilioni 0.795 na kukarabati vyuo vya mafunzo ya kilimo shilingi bilioni 0.145.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 21 Juni, 2004, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 22.63, sawa na asilimia 100 ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, shilingi bilioni 21.90 sawa na asilimia 96.77 ya fedha zilizoidhinishwa, zilikuwa zimetumika.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 21 Juni, 2004, shilingi bilioni 6.44 fedha za ndani zikiwa ni sawa na fedha zilizoidhinishwa zilikuwa zimetolewa. Hadi tarehe 21 Juni, 2004, miradi ilikuwa imetumia shilingi bilioni 18.0 ya fedha za nje. Matumizi hayo ni sawa na asilimia 71.6 ya fedha za nje zilizotengwa. Asilimia ndogo ya matumizi ya fedha

za nje inasababishwa na muda mrefu unaotumika kuagiza vifaa na magari na utaratibu mrefu uliopo wa kuwapata makandarasi kwa njia za zabuni.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2003/2004 ulikuwa mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme - ASDP).* Programu hii inatekelezwa katika ngazi ya Wilaya chini ya Mipango ya Wilaya ya Maendeleo ya Kilimo *(District Agricultural Development Plans - DADPs)* ikiwa ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini.

Jumla ya shilingi bilioni nne zilitengwa katika Bajeti ya mwaka wa 2003/2004 na kupelekwa kwenye wilaya 90 kwa ajili ya kutekeleza mipango hiyo. Fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miradi 67 ya umwagiliaji maji mashambani, ukarabati na uchimbaji wa malambo 35, ukarabati wa majosho 196, ujenzi wa sehemu za kupukuchulia na kusafishia kahawa *(central pulparies)* 34 na uimarishaji wa Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* 126. Umewekwa utaratibu ambao kwao Mikoa na Halmashauri za Miji na Wilaya zinatekeleza na kutoa taarifa za utekelezaji kwa Wizara za kisekta ambazo zinaratibu na kutoa maelekezo na ushauri wa kitaalam.

Mheshimiwa Spika, ipo miradi sita ambayo inatekelezwa katika Wilaya, lakini chini ya usimamizi wa Wizara za kisekta. Miradi hiyo ni Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory Agricultural Development Project - PADEP),* Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(Participatory Irrigation Development Programme - PIDP),* Mradi wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani Katika Mabonde ya Mito Pangani na Rufiji *(River Basin Management and Smallholder Irrigation Improvement Project- RBMSIIP),* Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Programme Support - ASPS),* Programu Maalum ya Usalama wa Chakula *(Speicial Programme for Food Security - SPFS)* na Mradi wa Huduma za Ugani *(National Agricultural Extension Project NAEP-II).* Maelezo kuhusu miradi hiyo yametolewa katika sehemu zinazohusika katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendelea kuwapatia wakulima teknolojia bora za uzalishaji ili kuwawezesha kuongeza uzalishaji na tija. Katika mwaka wa 2003/2004, mkazo uliwekwa katika matumizi ya mbinu shirikishi jamii ili kuibua matatizo na kuainisha mikakati ya kuongeza tija na uzalishaji. Jumla ya shilingi milioni 167 zilitolewa na kutumika kuanzisha mashamba darasa 267 katika wilaya 41 ambazo ni Iringa, Arumeru, Mbulu, Babati, Kibaha, Bagamoyo, Temeke, Dodoma, Njombe, Bukoba, Ngara, Kasulu, Hai, Kilwa, Musoma, Serengeti, Bunda, Rungwe, Mbeya, Ulanga, Singida, Mtwara, Ukerewe, Sengerema, Magu, Mpanda, Songea, Mbinga, Shinyanga, Kahama, Igunga, Urambo, Korogwe, Lushoto, Sumbawanga, Morogoro, Kongwa, Tabora, Mpwapwa, Arusha Mjini na Muheza. Wataalam 121, pamoja na wakuu wa Wilaya 24 kutoka wilaya za mikoa ya Mara, Kigoma, Tabora, Morogoro, Pwani na Dodoma walifanya ziara za mafunzo ya wiki moja moja mkoani Singida kujifunza mbinu shirikishi jamii.

Aidha, vipindi 52 vya mafunzo ya kilimo bora cha mazao na matokeo ya utafiti wa kilimo na ufugaji bora viliandaliwa na kutangazwa na Redio Tanzania. Wizara pia iliandaa mada tatu za video kuhusu kilimo cha Paprika na Vanila.

Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitumia shilingi milioni 830 kununua na kusambaza gari moja moja katika Wilaya 52 kwa ajili ya kuwawezesha wataalam wa ugani kuwafikia wakulima kwa urahisi zaidi. Magari hayo yalipelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya za Ngorongoro, Monduli, Babati, Simanjiro, Mbulu, Bagamoyo, Kisarawe, Kinondoni, Temeke, Dodoma Vijijini, Mpwapwa, Kilolo, Ludewa, Makete, Biharamulo, Bukoba, Ngara, Kasulu, Kibondo, Moshi Vijijini, Rombo, Mwanga, Tarime, Musoma Vijijini, Serengeti, Kilwa, Liwale, Chunya, Rungwe, Ileje, Mvomero, Kilombero, Ilemela, Misungwi, Namtumbo, Magu, Tandahimba, Newala, Sumbawanga, Mpanda, Manyoni, Iramba, Kishapu, Meatu, Maswa, Nzega, Urambo, Uyui, Lushoto, Kilindi, Korogwe na Mbinga.

Katika mwaka wa 2003/2004, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory Agricultural Development and Empowerment Project - PADEP)* ulianza kutekelezwa katika Wilaya za Morogoro Vijijini, Hai, Singida Vijijini, Iringa Vijijini, Hanang, Masasi, Nachingwea na Arumeru. Kazi zilizofanyika katika Wilaya hizo ni pamoja na kuandaa mipango ya kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Halmashauri, kusimamia shughuli za maendeleo ya kilimo, kuandaa miongozo na kutoa mafunzo ya matumizi ya mbinu shirikishi jamii. Aidha, mradi umeandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mradi kitaifa na mfumo wa usimamizi wa fedha kutumia kompyuta *(Computerized Financial Management System).* Hadi Mei 2004, Mradi ulikuwa umetumia jumla ya shilingi bilioni 2.10 kwa kazi hizo.

Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ilitoa kipaumbele katika ukarabati wa *scheme* na mabwawa yaliyojengwa zamani na kuharibika kwa uchakavu au kuharibiwa na mvua za *El-Nino,* kuendeleza ukanda wa kijani kuzunguka Ziwa Victoria, uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga mabwawa kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha umwagiliaji maji na matumizi ya nyumbani na ya mifugo.

Katika kipindi cha mwaka wa 2001 hadi 2004 jumla ya miradi 63 yenye jumla ya hekta 35,586 iliendelezwa, Hekta 4,806 ziliendelezwa katika mwaka wa 2001/2002 na hekta 11,242 katika mwaka wa 2002/2003. Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ilipanga kupanua eneo linalolimwa kwa kumwagiliwa maji kwa jumla ya hekta 29,397. Hadi mwezi wa Juni, 2004, hekta 23,970, sawa na asilimia 81.5 ya lengo, zilikuwa zimeendelezwa. Kutokana na uendelezaji huo, eneo linalolimwa kwa kumwagiliwa maji limeongezeka kutoka hekta 157,000 mwaka wa 1999/2000 kufikia hekta 227,486 mwaka wa 2003/2004, ongezeko la hekta 70,486 sawa na asilimia 44.89.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na *JICA,* ilianza maandalizi ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani. Mpango huo umeweka lengo la kuendeleza jumla ya hekta 30,000 kila mwaka. Ili lengo hilo liweze kufikiwa, Taifa linapaswa kuwekeza sio chini ya shilingi bilioni 30 kwa mwaka. Kiwango hicho cha uwekezaji kikiwezekana,

ifikapo mwaka wa 2017 jumla ya hekta 405,400 zitakuwa zikimwagiliwa maji, eneo ambalo litaliwezesha Taifa kujitosheleza kwa mpunga. Viwango vya uwekezaji kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji maji mashambani bado ni vidogo. Kiasi cha fedha kilichowekezwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji maji mashambani kati ya mwaka wa 2001/2002 hadi 2004/2005.

| Mwaka | Kiasi Kilichotolewa | Asilia ya Lengo (Lengo ni Sh.bilioni 30) |
|---|---|---|
| 2001/2002 | 4,436,120,000.00 | 14.79 |
| 2002/2003 | 6,435,529,813.00 | 21.45 |
| 2003/2004 | 9,012,670,550.00 | 30.04 |
| 2004/2005 | 6,003,300,000.00 | 20.01 |
| Wastani | 6,471,905,090.75 | 20.01 |

Awamu ya kwanza ya maandalizi ya Mpango ilikamilika mwaka wa 2002/2003 na ilibaini kuwepo kwa jumla ya hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Kati ya hizo, hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kuendelezwa, hekta milioni 4.8 zina uwezekano wa wastani wa kuendelezwa na hekta milioni 22.3 zina uwezekano mdogo wa kuendelezwa.

Awamu ya pili ya mpango huo ilianza kuandaliwa mwaka wa 2002/2003 na imekamilika mwaka wa 2003/2004. Mpango huo umeainisha skimu 10 kati ya skimu zilizopo nchini na kubaini gharama za ujenzi, uendeshaji na matengenezo kwa lengo la kuzifanya skimu za mfano zinazoweza kuigwa na skimu za aina hiyo nchini katika kupanga, kusanifu, kuendesha na kukarabati *scheme* za umwagiliaji maji mashambani zitakazotekelezwa katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya. Skimu zilizohusika ni Kinyope, Lindi Vijijini yenye ukubwa wa hekta 480, Magoma, Korogwe hekta 350, Pawaga, Iringa Vijijini hekta 2000, Musa Mwinjanga, Hai hekta 676, Mgongola, Morogoro Vijijini hekta 620, *Lower Moshi,* Moshi Vijijini hekta 2,300, Kisese, Kondoa hekta 120, Pamila, Kigoma Vijijini hekta 40, Nkenge, Bukoba hekta 500 na Luchili, Sengerema hekta 40.

Katika mwaka wa 2003/2004, ilikusudiwa kukarabati skimu 29, hadi tarehe 27 Juni 2004, skimu 26 zilikuwa zimekarabatiwa kwa gharama ya shilingi bilioni sita. Utekelezaji huo ni sawa na asilimia 89 ya lengo. Skimu tatu za Liyuni, Namtumbo (hekta 400), Nkonkwa, Kigoma vijijini (hekta 440) na Msambara, Kasulu (hekta 600), zenye jumla ya hekta 1,440 bado zipo katika hatua ya upimaji na usanifu. Katika mwaka wa 2003/2004, ilikusudiwa kukarabati na kujenga mabwawa mapya 11. Kati ya hayo mabwawa sita yalijengwa na kukamilika, sawa na asilimia 55 ya lengo.

Aidha, upimaji na usanifu wa mabwawa manne ya Tyeme-Masagi (hekta 200), Kironda-Datali, Iramba (hekta100), Mkomazi, Korogwe (hekta 200) na Mesaga, Serengeti (hekta 170) umekamilika na ujenzi wake unatarajiwa kufanywa mwaka wa 2004/2005.

Katika mwaka wa 2003/2004, mifereji na vigawa maji katika skimu 10 za zamani zenye jumla ya hekta 248 zinazomwagiliwa maji kwa kutumia pampu zilikarabatiwa. Kazi iliyobaki ni ufungaji wa pampu zinazotumia nishati ya upepo, mionzi ya jua na mafuta ya dizeli unaogharimiwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* na wakulima wenyewe.

Skimu hizo ni Bwanza (hekta 20) na Tamau (hekta 20) Bunda, Kahangara (hekta 20) na Ilungu (hekta 20) Magu, Luchili (hekta 48) Sengerema, Mkoma (hekta 20) Tarime, Nyabangu (hekta 20), Chanyauru (hekta 20) Musoma Vijijini na Nakatunguru (hekta 20) Ukerewe na Nyatwali (hekta 20) Bunda.

Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, vikundi 73 vya wakulima vimeundwa katika vijiji vya Nyakaboja, Magu (18), Mwamanyiri, Magu (17), Nyangwi, Nyamagana (23) na Nyaholongo, Misungwi (15). Vikundi hivi vya wakulima vimeanzisha mashamba madogo yenye jumla ya hekta 150 ambayo yameanza kumwagiliwa maji yanayotoka katika visima vifupi na Ziwa Victoria.

Katika mwaka 2003/2004, skimu sita za umwagiliaji maji mashambani, zenye jumla ya hekta 1,850 zilikarabatiwa kwa kutumia shilingi milioni 795.0 kutoka kwenye Mfuko wa Pamoja wa Msaada wa Chakula wa Tanzania na Japan. Skimu hizo ni Ghona, Moshi Vijijini (hekta 450, Yavayava, Mkuranga (hekta 100), Kirya, Mwanga (hekta 350), Segeni, Rufiji (hekta 100), Kitivo, Lushoto (hekta 450) na Mloa - Malizanga, Iringa Vijijini (hekta 400).

Katika mwaka 2003/2004, mradi huu ulikamilisha ujenzi wa skimu tatu zenye jumla ya hekta 1,060, Skimu hizo ni Kivulini, Mwanga, (hekta 410), Longoi, Hai (hekta 300) na Mapogoro, Iringa Vijijini, (hekta 350) kwa gharama ya shilingi bilioni 1.44. Aidha, wakulima 85 kutoka katika skimu hizo walipewa mafunzo ya uendeshaji wa skimu na matumizi bora ya maji. Kutokana na ujenzi huo, uzalishaji wa mazao katika skimu hizo umeongezeka kutoka wastani wa tani mbili kwa hekta hadi tani tano kwa hekta kwa zao la mpunga na kutoka tani moja na nusu kwa hekta hadi tani tatu kwa hekta kwa zao la mahindi. Utekelezaji wa skimu hizo tatu unakamilisha jumla ya skimu 15 zenye eneo la hekta 5,059 zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa chini ya mradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji mashambani *(Participatory Irrigation Development Programme -PIDP),* katika mwaka wa 2003/2004, skimu 21 zenye jumla ya hekta 4,669 katika Wilaya za Babati, Dodoma Vijijini, Manyoni, Nzega, Shinyanga na Kwimba zilijengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 4.1. Utekelezaji huu unatimiza lengo lililowekwa na programu. Aidha, malambo mawili ya Skimu za Mangisa (hekta 180) na Dongobesh (hekta 200) Mbulu, yalijengwa. Pamoja na utekelezaji huo, visima vifupi 33 vilichimbwa na kuwekewa pampu za miguu kwa ajili ya umwagiliaji wa bustani na vitalu vya mbegu ya mpunga. Visima hivi vilichimbwa katika Wilaya za Babati (6), Dodoma Vijijini (9), Nzega (5), Igunga (2), Manyoni (1), Misungwi (3) Kwimba (3) na Shinyanga Vijijini (4).

Kuhusu Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Programme Support - ASPS),* katika mwaka 2003/2004, programu hiyo inayotekelezwa katika Mikoa ya Iringa na Mbeya na kugharamiwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Denmark, imekamilisha upimaji, usanifu, na maandalizi ya mikataba ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji maji mashambani kwa kutumia shilingi milioni 60. Ukarabati wa skimu za Nyanzwa (hekta 760) na Irindi (hekta 610), Kilolo umeanza mwezi wa Juni 2004, na ukarabati wa skimu za Utengule Usongwe (hekta 600), Mbeya Vijijini na Naming'ongo (hekta 1000), Mbozi unatarajiwa kuanza mwezi wa Julai, 2004 baada ya kukamilisha taratibu za mikataba ya ujenzi. Ukarabati wa skimu zote nne unatarajia kugharimu shilingi bilioni 2.07.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa sehemu kubwa unategemea matumizi endelevu ya ardhi yetu. Hivi sasa nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la mmomonyoko wa udongo kutokana na matumizi mabaya ya ardhi. Udongo mwingi wenye rutuba unachukuliwa na maji ya mvua wakati wa mvua na upepo wakati wa kiangazi. Hali hii inaweza kudhibitiwa kwa kutumia teknolojia rahisi, kwa mfano kuzingatia kilimo cha matuta na kutengeneza makingamaji katika sehemu zenye miinuko. Ili kueneza matumizi ya teknolojia rahisi za kukabiliana na mmomonyoko wa udongo, katika katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ilitoa mafunzo ya hifadhi ya udongo kwa wakulima wakufunzi 450 na maafisa ugani 87. Baada ya kuhitimu, wakulima wakufunzi wamewafundisha wakulima wengine 1,600.

Mafunzo hayo yalijumuisha kupima na kuchimba matuta na makinga maji, kuanzisha mashamba ya mafunzo kwa wakulima, vitalu vya miche ya miti, kupanda miti kwa ajili ya kuendeleza kilimo mseto na kutengeneza matuta kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua mashambani.

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo yalifanyika katika mashamba ya wakulima katika wilaya za Dodoma Vijijini, Mpwapwa, Kasulu, Kigoma, Kilosa, Morogoro Vijijini, Singida, Shinyanga Vijijini, Geita, Muheza, Korogwe, Lushoto, Rombo, Hai, Monduli, Iringa Vijijini, Magu na Tarime. Maeneo hayo yalilengwa kwa kuwa yanakabiliwa na tatizo kubwa la mmomonyoko wa udongo. Jumla ya shilingi milioni 192.21 zilitumika kugharamia kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula iliendelea kufanya utafiti ili kutoa teknolojia mbalimbali zitakazowawezesha wakulima kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji. Utafiti huo ulilenga: kutathmini matatizo ya wakulima kwa kutumia mbinu shirikishi jamii, kutoa teknolojia kwa lengo la kumuongezea mkulima mavuno, tija na faida kuzalisha na kukuza mbegu bora za mazao mbalimbali, kuimarisha uwezo wa watafiti kutumia mbinu shirikishi katika kutathmini matatizo ya wakulima na kutoa ushauri kwa wakulima kuhusu jinsi ya kutumia teknolojia mbalimbali za kilimo na mifugo.

Katika mwaka wa 2003/2004, utafiti wa mazao ya kilimo uliendelea kutekelezwa katika kanda zote 7 zenye jumla ya vituo 18 vilivyoko chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Jumla ya shilingi bilioni 1.45 zilitumika kugharamia shughuli za utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 vituo vya utafiti vilikamilisha utafiti na kutoa aina mpya saba ya mbegu za mazao ya chakula. Kituo cha Ilonga, Morogoro kilitoa aina mpya ya kunde iitwayo Vuli-2 na mbegu ya mbaazi iitwayo Tumia. Vituo vya Kibaha na Naliendele vilitoa aina mpya za muhogo zinazoitwa Kibaha, Mumba na Naliendele, kituo cha Uyole kilitoa aina mbili za mbegu mpya ya mbegu za maharage zinazoitwa Uyole 03 na Urafiki.

Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za utafiti wa mazao kwa kukarabati na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani na nyumba za watafiti, kununua magari, vifaa na madawa ya maabara, na kompyuta. Ili kutekeleza kazi hizo Wizara ilitumia jumla ya shilingi bilioni 2.3

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija katika uzalishaji wakulima wanapaswa kuongeza viwango vya matumizi ya pembejeo muhimu katika kilimo, hususan mbolea na madawa ya kudhibiti visumbufu. Sababu moja kubwa ya tija ndogo ya mazao yetu mengi ya chakula na biashara inatokana na matumizi madogo sana ya mbolea. Wakulima nchini hutumia wastani wa kilo 7 za mbolea kwa hekta moja ikilinganishwa na matumizi ya kilo 16 nchini Ethiopia, Malawi 16, Afrika Kusini 51, India 103, China 279, Vietnam 365 na Uholanzi 578. Nchi nyingi zinazotumia mbolea chini ya kilo 103 kwa hekta huwa na tija ndogo, uzalishaji mdogo na huwa zinakabiliwa na upungufu wa chakula wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ili kuwasaidia wakulima kupata pembejeo kwa wingi na kwa wakati, katika mwaka wa 2003/2004 Wizara ya Kilimo na Chakula iliendelea kuratibu upatikanaji, usambazaji na matumizi ya pembejeo nchini. Katika mwaka huo, makadirio ya mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 185,500. Hadi tarehe 31 Mei, 2004, jumla ya tani 125,653 za aina mbalimbali za mbolea, sawa na asilimia 68 ya mahitaji zilikuwa zimesambazwa kwa wakulima. Katika msimu wa 2003/2004, ulikuwepo upungufu wa jumla ya tani 59,847 za mbolea. Upungufu huo ulitokana na baadhi ya makampuni kutoagiza mbolea kwa wingi kama ilivyokuwa imetarajiwa kutokana na kupanda kwa bei ya mbolea katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka wa 2003/2004 Serikali, kwa mara ya kwanza katika miaka zaidi ya 12, ilirejesha utaratibu wa kutoa ruzuku kwa mbolea kwa ajili ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa kutenga shilingi bilioni mbili kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwenda kwenye mikoa hiyo. Lengo la uamuzi huo lilikuwa ni kudhibiti bei za mbolea katika mikoa hiyo ili zisizidi shilingi 14,000 kwa mfuko wa kilo hamsini katika vituo vikuu vya kupokelea mbolea vilivyoko Iringa na Makambako katika mkoa wa Iringa, Mbeya, Songea na Sumbawanga.

Kamati za Taifa, Mikoa na Wilaya ziliundwa kusimamia usambazaji wa mbolea hiyo. Utaratibu huo ungeiwezesha mikoa kuzalisha chakula kwa wingi na kuwa na ziada ambayo ingetumiwa kulisha maeneo ambayo yangekabiliwa na upungufu wa chakula. Kamati za Mikoa zilipewa majukumu ya kuhakiki na kuratibu mbolea iliyopo, kusimamia utekelezaji wa mikataba na kutoa taarifa. Kamati za Wilaya zilikuwa na majukumu ya

kuteua wasambazaji wa mbolea, kuratibu bei ya kuuzia mbolea katika ngazi ya kijiji, usambazaji na uuzaji wa mbolea katika maeneo yao na kutoa taarifa za utekelezaji kwa kamati za Mikoa na Taifa. Wajumbe wa Kamati za wilaya walikuwa: Mkuu wa Wilaya (Mwenyekiti), Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya/Mji, Afisa Kilimo wa Wilaya (Katibu), Afisa Biashara wa Wilaya na Waheshimiwa Wabunge katika Wilaya.

Hadi mwezi Mei, 2003, jumla ya tani 38,935 za aina mbalimbali za mbolea zilikuwa zimepelekwa kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya, tani 14,016, Iringa, tani 14,955, Ruvuma, tani 8,771 na Rukwa, tani 1,193. Kati ya mbolea hiyo, tani 33,492 ziliuzwa chini ya utaratibu wa fidia: Iringa ziliuzwa tani 11,707, Ruvuma tani 7,932, Mbeya tani 12,850 na Rukwa tani 1,003. Kiasi hicho cha mbolea kilichouzwa ni asilimia 63.2 ya makisio ya mahitaji ya mbolea katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kwa mwaka. Jumla ya shilingi bilioni 1.27 zimetumika kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea. Kutokana na kudhibitiwa kwa bei za mbolea, wakulima waliongeza matumizi ya mbolea na kusababisha kuwepo kwa upungufu wa mbolea nchini kwa sababu kuongezeka kwa matumizi hakukuambatana na uingizaji wa mbolea kutoka nje. Hii ilitokana na uamuzi kufanyika katikati ya mwaka jambo ambalo halikuwezesha wafanyabiashara kuagiza mbolea kuuwahi msimu. Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika msimu wa 2003/2004, utaratibu huu utapanuliwa katika mpango wa 2004/2005.

Mahitaji ya viuatilifu katika msimu wa 2003/2004 yalikuwa tani 21,000 za madawa ya unga na lita milioni 4.6 kwa madawa ya maji. Kati ya hizo, tani 6,000 sawa na asilimia 28 za mahitaji ya madawa ya unga na lita milioni 2.1 sawa na asilimia 45 za mahitaji ya madawa aina ya maji, zilipatikana na kusambazwa kwa wakulima. Upatikanaji wa viuatilifu ulikuwa chini ya malengo kwa sababu wafanyabishara walihofu athari za ukame kuathiri soko la madawa kwa baadhi ya maeneo yanayozalisha mazao yanayotumia madawa kwa wingi, hususan mazao ya nafaka, pamba, korosho na kahawa. Jumla ya shilingi 3,592,500 zilitumiwa kugharamia uratibu wa upatikanaji, usambazaji na kufundisha wakulima na wasambazaji wa madawa ya kilimo matumizi bora na salama ya madawa ya hayo.

Mheshimiwa Spika, mbegu bora ni muhimu sana katika uzalishaji. Matumizi ya mbegu bora na mbinu sahihi za kilimo yanaweza kuongeza uzalishaji wa mazao kwa kiasi kikubwa sana. Kwa mfano, mbegu bora za mpunga zinaweza kuzalisha mara tano zaidi ikilinganishwa na mbegu za kawaida. Ili kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima, Wizara iliendelea kuratibu upatikanaji wa mbegu bora, kusimamia ubora wa mbegu hizo na kuzalisha mbegu za msingi katika mashamba ya mbegu yanayosimamiwa na Wizara. Katika mwaka wa 2003/2004 jumla ya hekta 898.8, sawa na asilimia 90 ya lengo (hekta 1,000) zililimwa na kupandwa mazao ya mbegu za nafaka, mikunde na mbegu za mafuta katika mashamba ya Serikali ya Arusha (hekta 380.2), Dabaga (hekta 136.4), Mwele (hekta 100), Kilangali (hekta 80) na Msimba (hekta 202.2). Kutokana na hekta hizo jumla ya tani 1,300 za mbegu zinatarajiwa kuvunwa. Jumla ya shilingi 623,050,000 zilitengwa kwa uzalishaji wa mbegu ambapo jumla ya shilingi 419,810,000 zilitumika. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi katika mashamba ya mbegu na ya wakulima wadogo wa mbegu vijijini wanazolisha mbegu za ubora wa kuazimiwa. Jumla ya sampuli

1,439 za mbegu zilichukuliwa kwa ajili ya kukaguliwa katika maabara za Wizara zilizopo Morogoro, Njombe na Tengeru, Arusha.

Mheshimiwa Spika, ili kuwawezesha wananchi walioathirika zaidi na ukame katika mwaka wa 2003/2004, Serikali iliomba msaada wa mbegu kwa ajili ya kuzigawia kaya 302,026 katika maeneo yaliyokuwa yamekabiliwa na upungufu wa chakula. Baadhi ya wahisani waliitikia wito huo na kutoa jumla ya dola za Kimarekani 1,494,000 zilizotosha kununua na kusambaza tani 915.8 za mbegu kupitia Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO).* Aina mbalimbali za mbegu zikiwemo za mahindi, mpunga, mtama, maharage na kunde zilinunuliwa. Wahisani waliotoa fedha za kununulia mbegu ni *FAO,* dola za kimarekani 400,000, Jamhuri ya Ireland, dola 220,000, Norway, Dola 282,000, Sweden dola 400,000 na Canada, dola 192,000.

Napenda kuzishukuru nchi zote na mashirika wahisani yaliyotoa msaada wa fedha zilizotumika kununulia mbegu za wakulima katika msimu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya maandalizi ya kuanzisha Wakala wa Serikali wa Mbegu utakaosimamia uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora nchini. Maandalizi hayo yamefikia hatua za mwisho na kibali cha kutangaza nafasi ya Mtendaji Mkuu kimetolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, jumla ya matrekta makubwa 246, matrekta madogo ya mkono 121, majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 44,811 na majembe ya mkono 2,705,580, yaliingizwa nchini. Aidha, Chama cha Wadau wa Pamba *(Tanzania Cotton Association)* kimeagiza matrekta 100 yatakayomilikiwa na viwanda vya kuchambua pamba ili kutoa huduma ya ukodishaji matrekta kwa bei nafuu kwa wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitumia shilingi milioni 326.65 kukarabati na kuvipatia zana za mafunzo vituo 25 vya wanyamakazi. Kati ya hivyo, vituo 18 vipo chini ya Halmashauri za Wilaya na saba vipo chini ya vyuo vya kilimo. Vituo hivyo vipo katika Mikoa ya Mwanza (3), Shinyanga (1), Tabora (2), Mtwara (1), Singida (3), Mbeya (2), Mara (1), Iringa (3), Ruvuma (1) na Tanga (1) na kituo kimoja kimoja katika Vyuo vya Uyole, Ukiriguru, Mlingano, Mtwara, Igurusi, Ilonga na *KATC.* Aidha, vituo vya Rujewa, Mbarali, Kate (Nkasi), Nyololo (Mufindi), Mayale (Njombe), Malya (Kwimba), Ibologero (Igunga), na Ilongero (Singida) vimeanzisha mashamba ya mfano kwa ajili ya kuwafundisha wakulima matumizi ya wanyamakazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa uliendelea kukusanya madeni yenye thamani ya shilingi 5.8 yanayotokana na mikopo iliyotolewa katika kipindi cha mwaka wa 1995/1996 hadi 1998/1999. Hadi tarehe 31 Mei, 2004 jumla ya shilingi bilioni 3.1 zilikuwa zimerejeshwa. Juhudi za kufuatilia madeni yaliyobaki zinaendelea, ikiwa ni pamoja na kuuza dhamana za wadaiwa ili kurejesha mikopo. Jumla ya dhamana za wadaiwa 57 zimeuzwa na zimewezesha kurejeshwa kwa shilingi milioni 343.3.

Mheshimiwa Spika, kuanzia msimu wa 2002/2003 hadi msimu wa 2003/2004, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo uliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 5.4 ambazo zilipelekwa benki za Ushirika za Kagera, Kilimanjaro, Exim na Benki ya Wananchi ya Mufindi na Shirikisho la Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa *(SCCULT).* Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2004, jumla ya shilingi bilioni 4.97 zilikuwa zimekopeshwa na shilingi bilioni 1.76 zilikuwa zimerejeshwa. Mgawanyo wa mikopo hiyo ni kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na. 4. Aidha, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo ya moja kwa moja yenye thamani ya shillingi milioni 452.2 kwa ajili ya kukarabati matrekta mabovu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, jumla ya waombaji 340 walipitishwa na Bodi ya Mfuko wa Pembejeo kupewa mikopo ya kukarabati matrekta. Waombaji 103 tayari wamepata mikopo yao kama ifuatavyo: Mwanza saba, Morogoro 29, Dar es Salaam mmoja, Shinyanga watano, Iringa tisa, Mbeya 11, Pwani watatu, Kilimanjaro watano, Manyara wawili, Arusha 27, Mara mmoja, na Dodoma watatu. Waombaji 237 wako katika hatua mbali mbali za kukamilisha taratibu za kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, aidha, waombaji 69 wamepitishwa na Bodi kwa ajili ya kununua matrekta mapya ambapo sita tayari wamepata mikopo hiyo (mmoja mmoja kutoka mikoa yaKilimanjaro, Ruvuma, Arusha, Dodoma na Iringa wawili). Aidha, makampuni mawili yamepatiwa mikopo ya kununua jumla ya matrekta tisa kwa ajili ya kuanzisha vituo vya kukodisha matrekta.

Katika mwaka wa 2004/2005 na miaka inayofuata Mfuko utakopesha kupitia benki za wananchi, vyama vya kuweka na kukopa, vyama vya ushirika na vyama vya wakulima hivyo kuondokana na tatizo la ukosefu wa mali za kuweka rehani.

Mheshimiwa Spika, hali ya Mfuko Kifedha kwenye mabenki yanayotoa mikopo ya Mfuko wa Pembejeo Kuanzia Msimu wa 2002/2003 hadi tarehe 31 mwezi wa Mei, 2004 kama ifuatavyo:-

| **BENKI** | **KIASI WALICHOPEWA** | **MIKOPO ILIYOTOLEWA** | **KIASI KILICHO-REJESHWA** |
|---|---|---|---|
| *EXIM Bank* | 2,800,000,000 | 2,718,344000 | 1,342,902,485 |
| *Kagera Coop Bank* | 278,450,000 | 278,450,000 | 3,035,477 |
| *Kilimanjaro Coop Bank* | 200,000,000 | 103,000,000 | 107,676,230 |
| *Mufindi Community Bank* | 700,000,000 | 553,000,000 | 160,849,000 |
| *SCCULT (1992) LTD* | 1,326,000,000 | 1,326,000,000 | 145,688,738 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla | 5,404,450,000 | 4,972,794,000 | 1,760,151,930 |

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitoa mafunzo kwa wataalam na wakulima ili kuwawezesha kuendesha kilimo cha kibiashara. Mafunzo kwa vitendo yalitolewa katika mashamba ya vyuo ambavyo vililima jumla ya hekta 372.8. Aidha, mitaala ya mafunzo kwa wataalam wa kilimo iliboreshwa kwa kujumuisha stadi za kilimo cha kibiashara, hifadhi ya mazingira, mazao ya biashara na udhibiti wa virusi na ugonjwa wa UKIMWI. Uboreshaji wa mitaala hiyo uligharimu shilingi milioni 14.7

Wizara ilitoa udhamini kwa wanafunzi katika vyuo vya kilimo ambapo wanafunzi 150 walipewa udhamini katika vyuo vya Mlingano, Tanga (20), Ukiriguru, Mwanza (25), Uyole, Mbeya (40), Ilonga, Kilosa (25), Tumbi, Tabora (20) na Igurusi, Mbeya (20). Aidha, Serikali iliendelea kudhamini mafunzo ya wanafunzi 100 waliopo mwaka wa pili katika vyuo hivyo. Gharama za udhamini kwa wanafunzi zilifikia shilingi milioni 95.5.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 Wizara ilitoa mafunzo ya matumizi na matengenezo ya matrekta madogo ya mkono kwa maafisa zana 42 kutoka mikoa ya Mara (4), Tabora (4), Singida (5), Dodoma (2), Morogoro (8), Kilimanjaro (3), Arusha (2), Kigoma (6), Mbeya (2) na Rukwa (6). Lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha kutoa huduma za mafunzo na matengenezo ya matrekta madogo kwa wakulima katika maeneo yao. Aidha, maafisa ugani 360 kutoka mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mtwara, Singida, Mbeya, Mara, Iringa, Ruvuma na Tanga walipatiwa mafunzo juu ya matumizi bora ya zana zinazokokotwa na wanyamakazi.

Katika mwaka wa 2003/2004 mashine ndogo 84 za kubangua korosho zilinunuliwa na kutumika katika kutoa mafunzo kwa maafisa zana 30 kutoka Halmashauri za Wilaya za mikoa ya Ruvuma (9), Pwani (6), Tanga (9) na Mtwara (6). Baada ya mafunzo maafisa hao walipewa mashine hizo ili wazitumie kutoa mafunzo kwa wakulima katika maeneo yao. Shilingi milioni 16 zilitumika kugharamia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya iliendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa ugani na kuwapatia vitendea kazi ili kuwawezesha kuwahudumia wakulima kwa urahisi. Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ilitumia jumla ya shilingi milioni 18 kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya mbinu shirikishi jamii na shamba darasa kwa wataalam wawezeshaji 22 kutoka wilaya za Serengeti, Bunda, Babati, Mbinga, Ngara, Magu, Musoma, Muheza, Arumeru na Mbeya kwa lengo la kueneza mbinu hizo katika wilaya ili wawe wakufunzi katika wilaya zilizokuwa hazikupata fursa ya mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mbinu shirikishi jamii katika shughuli za utafiti, Wizara ilitoa mafunzo kwa watafiti 36 kutoka kanda saba za Utafiti ili kuwawezesha kuchambua matatizo ya wakulima kwa kutumia mbinu hiyo. Aidha, Wizara ilikamilisha uandaaji wa vitabu vya kufundishia kozi ya dhana ya Mifumo ya Kilimo *(Farming Systems Approaches - Training Manuals: Volumes 1 and 2)* na kuvisambaza kwa watafiti na wadau wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2003/2004 mafunzo ya teknolojia za hifadhi ya mazao ya nafaka na mikunde yalitolewa kwa wataalam wawezeshaji 104 wa Halmashauri za Wilaya za Babati, Mbulu, Hanang, Kiteto, Simanjiro, Arusha, Monduli, Karatu, Ngorongoro, Singida Mjini, Singida vijijini, Iramba, Manyoni, Kondoa, Dodoma vijijini, Dodoma mjini, Mpwapwa na Kongwa. Aidha, Mafunzo ya teknolojia za usindikaji wa mazao ya muhogo na viazi vitamu yalitolewa kwa wataalam wawezeshaji 114 wa Halmashauri za wilaya za Lindi vijijini, Kilwa, Nachingwea, Mtwara vijijini, Masasi, Tandahimba, Tunduru, Mbinga, Namtumbo, Songea vijijini, Songea mjini, Sikonge, Urambo, Uyui, Bariadi, Kahama, Bukombe, Sengerema, Geita, Ukerewe, Musoma, Bunda na Serengeti . Jumla ya shilingi milioni 160 zilitumika kugharamia mafunzo hayo.

Wizara ilitoa mafunzo ya udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao ghalani kwa wataalam kutoka Halmashauri za Wilaya za mikoa ya Singida, Arusha na Manyara. Aidha, viongozi na wataalam wa Serikali za Mitaa kwa mikoa ya Tanga, Dodoma, Morogoro, Mbeya, Rukwa, Lindi na Mtwara walipatiwa mafunzo kama hayo ili waweze kusimamia utekelezaji na uenezaji wa mbinu hizo kwa ufanisi. Jumla ya washiriki 115 wakiwemo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walishiriki.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza taaluma ya pembejeo za kilimo mwaka wa 2003/2004 mawakala wa pembejeo 210 kutoka mikoa 9 ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Iringa, Rukwa, Morogoro, Dodoma, Arusha na Kilimanjaro walipata mafunzo kuhusu wajibu wao kwa wakulima katika kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo kwa wakati na zenye ubora kwa mujibu wa kanuni na sheria.

Aidha, mafunzo kuhusu ukusanyaji na kuratibu takwimu sahihi za pembejeo za kilimo yalitolewa kwa wataalam 28 kutoka katika mikoa na wilaya za Nyanda za Juu Kusini. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa kuanzisha na kuendeleza mfumo endelevu wa upatikanaji wa takwimu. Jumla ya shilingi 15,195,500 zilitolewa na kutumika.

Katika mwaka wa 2003/2004, Wizara iliendelea kuimarisha taaluma za wataalam wa kilimo kwa kuwapatia nafasi za kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu nje ya nchi ili kuboresha utendaji wao wa kazi. Jumla ya watumishi 75 (wanawake 24 na wanaume 51) walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali za kilimo nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakulima 5,768 katika vyuo vinane vya kilimo, *Kilimanjaro Agricultural Training Institute (KATC)* Moshi, Uyole, Igurusi, Ilonga, Ukiriguru, Mlingano, Mtwara, Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu - Kilombero na Chuo cha Igabiro kinachomilikiwa na Kanisa la Kiluteri Dayosisi ya Kaskazini Magharibi. Aidha, mafunzo yalitolewa katika vyuo vya wakulima vya Mkindo wilayani Morogoro, Bihawana wilayani Dodoma Vijijini na Inyala wilayani Mbeya Vijijini. Mafunzo hayo yalihusu kilimo bora cha mpunga korosho, pamba, kahawa, chai, viazi vitamu, nyanya, usindikaji wa mazao, hifadhi ya mazingira, kuandaa mipango, kanuni za masoko, mbinu za uwekezaji, matumizi ya wanyama kazi, na mazao

yanayostahimili ukame. Chuo cha *KATC*-Moshi kinachofundisha stadi za uzalishaji wa mpunga kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kilifundisha jumla ya wakulima 2,373 ambapo serikali ilitumia jumla ya shilingi milioni 33.0 kugharamia mafunzo hayo.

Aidha, chuo kilitoa mafunzo kwa wanafunzi 274 kutoka Kenya, Malawi, Uganda na Zambia na Serikali za nchi zao zilitumia jumla ya shilingi milioni 76 kugharamia mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuboresha mazingira ya kuendeshea mafunzo ya wataalam na wakulima vyuoni, Wizara inaendelea na ukarabati wa mabweni saba, ofisi za wakufunzi tano, madarasa manane, nyumba za waalimu 16 maktaba tano na mabwalo ya chakula kwa wanafunzi manne katika vyuo vya kilimo nchini. Kazi hiyo ya ukarabati inaendelea na itagharimu shilingi milioni 332.6 itakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kuratibu hali ya upatikanaji wa chakula nchini inabidi iratibu ukusanyaji na tathmini ya takwimu na taarifa za upatikanaji wa mvua, maeneo yaliyolimwa, hali ya mazao mashambani, kiasi cha mavuno na akiba ya chakula kilichopo kwa wakulima, wafanyabiashara na taasisi zinazohifadhi na kusindika chakula. Kama sehemu ya kuimarisha uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu hayo, mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilitekeleza mambo yafuatayo: -

(i) Iliendelea kuboresha mfumo wa kukusanya takwimu na taarifa za hali ya mvua, mazao mashambani na hali ya chakula kutoka ngazi ya wilaya hadi Taifa;

(ii) Ilifanya tathmini tatu kati ya mwezi Julai 2003 na mwezi Mei 2004 ya maeneo na idadi watu walioathiriwa na hali ya ukame nchini; na

(iii) Ilinunua na kufunga vifaa vya kupimia upatikanaji wa mvua 100 katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza mtandao wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa za mvua. Jumla ya shilingi milioni 89.61 zilitumika kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuweka mfumo endelevu wa kuratibu maswala yote yanayohusu usalama wa chakula Wizara ya Kilimo na Chakula iliandaa Rasimu ya Sera ya Usalama wa Chakula na mwongozo wa kutekeleza Sera hiyo. Maandiko hayo yatatumika katika kurekebisha Sheria ya Usalama wa Chakula Na. 10 ya mwaka 1991. Jumla ya shilingi milioni 12.50 zilitumika.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa mwaka 2003/2004 Wizara ilitumia jumla ya shilingi milioni 41.4 kudhibiti viwavijeshi katika mikoa ya Mtwara, Dodoma, Morogoro na Pwani, Dar es Salaam, Arusha, Singida na Shinyanga ambapo jumla lita 16,000 za dawa zilitumika zilinyunyuzia hekta 15,800.

Kiasi cha shilingi milioni 98.4 kilitumika katika kudhibiti ndege aina ya kwelea kwelea msimu wa mwaka 2003/2004. Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani *(DLCO-EA)* ilidhibiti ndege aina

ya kwelea kwelea milioni 23 katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mara na Tabora kwa kutumia lita 1,250 za dawa ambapo ndege milioni 60.0 waliuawa na hivyo kuokoa kiasi cha tani 830 za nafaka. Aidha, shilingi milioni 475.1 zilitolewa kama mchango wa Taifa katika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani *(DLCO-EA)*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 jumla ya shilingi milioni 132.5 zilitumiwa na Wizara kudhibiti Nzige Wekundu. Wizara ikishirikiana na Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige Wekundu *(International Red Locust Control Organisation for Central and Southern Africa)* iliendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo yote ya mazalia ya asili yaliyoko katika mbuga za Wembere, Malagarasi, Iku/Katavi, Bahi na Nsimba ili kuhakiki wingi wa nzige.

Aidha, nzige walioonekana katika mbuga hizo walidhibitiwa kabla hawajaruka na hivyo kuokoa zaidi ya tani 680 za mazao. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 171.3 zilitolewa kama mchango kwa Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige Wekundu.

Katika mwaka wa 2003/2004 milipuko ya panya ilitokea katika wilaya za Mvomero na Morogoro Vijijini ambapo kilo 200 za sumu zilitumika katika kudhibiti milipuko hiyo. Wizara ilitumia jumla ya shilingi milioni 79.5 kugharamia kazi hiyo. Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula imeandaa kilo 4,000 za dawa ya panya ambazo zitasambzwa katika maeneo yanayoshambuliwa na panya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi uliofanyika mwaka wa 2003 ulibaini kuwepo kwa nzi wanaoshambulia zao la miembe wanaojulikana kwa jina la kitaalamu kama Bactrocera dorsalis katika ukanda wa Pwani. Nzi hao ni hatari sana na wakienea wataikosesha nchi yetu fursa ya kuuza maembe nchi za nje. Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula Duniani *(FAO)* na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Wadudu *(ICIPE),* Nairobi ilitoa mafunzo kwa wataalam watano watakaoongoza uchunguzi nchi nzima kubaini kasi ya ueneaji wa wadudu hao na kuwadhibiti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 Wizara ilitumia jumla ya shilingi milioni 69 kupambana na magonjwa ya batobato kali ya muhogo na mnyauko fusari wa kahawa katika Ukanda wa Ziwa Viktoria. Aidha, utafiti wa mbegu zenye stahimilivu ya magonjwa hayo uliendelea kufanyika, ikiwa ni pamoja na kuweka karantini kuzuia uenezaji wa mimea yenye magonjwa na kung'oa na kuchoma moto mibuni 3,632 iliyoathirika na mnyauko fuzari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 Wizara ilitumia kiasi cha shilingi milioni 214.7 kutekeleza kazi za udhibiti husishi wa mazao. Udhibiti husishi umeonyesha mafanikio makubwa katika udhibiti wa visumbufu vya mazao ya pamba katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kahawa na mboga katika mikoa ya Nyanda za Juu Kaskazini.

Zaidi ya wadudu 5,000 maadui wa utitiri wa muhogo walizalishwa na kusambazwa ili kudhibiti ugonjwa wa batobato ya muhogo katika Kanda za Ziwa na

Pwani. Aidha, jumla ya hekta 1,514 za muhogo ulioathirika na ugonjwa huo ziling'olewa na kupandwa vipando milioni 5.58 vya muhogo wenye ukinzani wa ugonjwa wa batobato kali ya muhogo katika Kanda ya Ziwa. Ili kudhibiti funza wa mabua, manyigu 3,000 walizalishwa na kusambazwa katika mikoa ya Tanga na Morogoro kati ya mwezi wa Oktoba na Desemba 2003.

Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilizalisha na kusambaza mbawakavu katika Ziwa Viktoria na katika mabwawa ambapo udhibiti wa gugumaji umefanikiwa kwa asilimia 95. Hata hivyo, udhibiti katika mito Kagera na Mara haujawa na mafanikio na hivyo mito hiyo imeendelea kuingiza gugumaji kwenye ziwa. Utafiti unafanywa na Wizara ya Kilimo na Chakula katika eneo la Kyaka, Kagera ili kubaini sababu zinazofanya wadudu wa mbawakavu kushindwa kuzaliana na kusababisha udhibiti wa gugumaji katika mito hiyo kuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa chakula kinachovunwa kinahifadhiwa katika hali ya usalama na kupunguza uwezekano wa kuharibika kunakotokana na mashambulizi ya wadudu, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara iliandaa, kuchapisha na kusambaza kwa wataalam wawezeshaji, wakulima jumla ya nakala 5,000 za mwongozo wa kudhibiti dumuzi na wadudu wengine waharibifu ghalani katika Halmashauri za Wilaya za mikoa ya Singida, Arusha, Manyara, Dodoma na Tabora. Aidha, nakala nyingine 6,500 zinachapishwa kwa ajili ya kusambazwa katika mikoa mingine nchini.

Wizara iliandaa, kuchapisha na kusambaza nakala 9,330 za vitabu vya teknolojia bora za hifadhi na usindikaji wa mazao ya nafaka, mikunde, mboga na matunda, mbegu za mafuta, mizizi na viungo kwa ajili ya wataalam wawezeshaji, wakulima na wadau wengine, hususan wasindikaji. Jumla ya shilingi milioni 8.3 zilitumika katika uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vitabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma iliendelea kubinafsisha mali za mashirika na mashamba yaliyo chini ya Wizara. Mashamba ya ngano ya West Kilimanjaro *(Kanamondo, Harlington, Matadi na Journeys end)* yalipimwa kwa lengo la kutenga maeneo yaliyojengwa makazi ya kudumu ya wananchi kabla ya kuyabinafsisha.

Aidha, mashamba mawili ya ngano ya *Gawal* na *Warret* yaliyoko Mkoani Manyara yatakabidhiwa kwa Wilaya ya Hanang ili wananchi wanaoishi jirani na mashamba hayo wamilikishwe. Karakana pamoja na mashamba ya Gidagamowd, Mulbadaw, Murjanda, Setchet na Basuto, yamekabidhiwa kwa Mfilisi *(LART - Loans and Advances Realisation Trust)* kwa ajili ya kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, mashamba ya mahindi ya Mbozi na Namtumbo yamekwisha tangazwa kwa ajili ya kuuzwa kwa wawekezaji. Aidha, *PSRC* wanakamilisha taratibu za kutangaza mashamba ya mpunga ya Mbarali na Kapunga ili yauzwe. Shamba la mpunga la Dakawa limekabidhiwa kwa Utawala wa Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kuuzwa kwa

wakulima wadogo wadogo. Shamba la Mpunga la Ruvu litauzwa kwa wakulima wadogo wadogo ambao wameanza uzalishaji katika shamba hilo.

Katika mwaka wa 2003/2004, mali zilizotangazwa na kupata wanunuzi ni zifuatazo:-

- Maghala 5 ya Shirika la Usagishaji la Taifa *(NMC),* vinu vya mpunga vya Isaka, Shinyanga na Mzizima; kiwanda cha chai cha Lupembe, shamba la chai la Mlangali na Shamba la mkonge la Muheza/Kitisa.

- Viwanda kumi na viwili vya korosho nchini vimetangazwa kwa ajili ya kuuzwa kwa wawekezaji. Aidha, *PSRC* ilitangaza uuzaji wa hisa za jineri ya Manawa ili kumpata mbia wa kuendesha jineri hiyo. Vyama vya Ushirika vya Kagera vimeonyesha nia ya kununua hisa asilimia 54.3 kati ya 64.3 zinazomilikiwa na Serikali kwenye Kampuni ya *TANICA.*

Ufuatiliaji wa maendeleo katika mashamba na viwanda vilivyobinafsishwa umebaini kwamba wawekezaji katika mashamba ya mkonge yaliyouzwa kwa Kampuni ya *Katani Limited,* Kiwanda na Shamba la Chai la Dabaga vilivyoko Iringa na mali za *NMC* zilizoko Mwanza, wameshindwa kutekeleza mikataba ya mauzo. Serikali inaendelea kujadiliana na wahusika ili kufikia muafaka wa jinsi ya kuendeleza mashamba na viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004 Wizara ilitumia jumla ya shilingi 19,878,250 kwa ajili ya kuandaa, kuhuisha na kufuatalia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamiwa na Wizara. Sheria za Bodi za Sukari, Tumbaku, Kahawa zilizopitishwa na Bunge mwaka wa 2001 zilianza kutekelezwa katika mwaka wa 2002/2003.

Aidha, Sheria ya Pamba Na. 2 ya mwaka wa 2001 itaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai mwaka wa 2004, baada ya matatizo ya deni la Bodi ya Pamba kupatiwa ufumbuzi na Serikali. Sheria ya Hakimiliki za Wazalishaji na Watafiti wa Mbegu Mpya *(Plant Breeders' Right Act No. 22 of 2002)* iliyopitishwa na Bunge mwezi Novemba 2002, ilianza kutekelezwa tarehe 1 Feburuari, 2004. Aidha, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ilirekebisha Kanuni za Sheria zinazosimamia mazao ya Korosho, Sukari, Tumbaku, Pamba na kuandaa Kanuni za sheria ya Hakimiliki ya wazalishaji wa mbegu mpya.

Mwaka wa 2003/2004 Bunge liliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea na Mazao wa mwaka 1952 *(The International Plant Protection Covention - IPPC)* na Mkataba wa Kimataifa wa Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula wa mwaka wa 2001 *(International Treaty on Plant Genetic Resource for Food and Agriculture).* Wizara ya Kilimo na Chakula ikishirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)* imeanza taratibu za awali za kuandaa sheria itakayosimamia uvunaji na usimamizi wa nasaba za mimea kwa ajili ya kilimo na chakula *(Plant Genetic Resource for Food and Agriculture (Exploitation and Control) Bill).*

Aidha, Wizara imeanzisha Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki za Aina Mpya za Mbegu na Mimea *(Plant Breeders Rights Office)* kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Hakimiliki ya Aina Mpya za Mbegu na Mimea *(Plant Breeders' Rights Act No. 22 of 2002).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Sheria mpya ya Mbegu *(Seed Act No.18 of 2003)* iliandaliwa na kupitishwa na Bunge hili. Sheria hiyo imeweka mfumo mzuri wa kuratibu uzalishaji, uingizaji, uuzaji na utumiaji wa mbegu za mazao ya kilimo hapa nchini. Aidha, muundo wa sheria hiyo unatekeleza makubaliano kati ya nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kuhusu utaratibu wa kuthibitisha na kusambaza mbegu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara iliendelea na zoezi la kupandisha vyeo na kurekebisha ajira za watumishi wake. Jumla ya watumishi 385 walipandishwa vyeo na mamlaka mbalimbali za ajira wakiwemo watumishi 99 wa ngazi ya KAMUS na watumishi 286 wa ngazi ya TUMEAJIRI.

Aidha, zoezi la kuwatambua watumishi ambao hawajafikia vyeo wanavyostahili lilifanyika. Kutokana na zoezi hilo, jumla ya watumishi 3,705 waliombewa kibali cha kupandishwa vyeo kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Wizara inaendelea kushirikiana na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ili kuhakikisha watumishi wote wanapandishwa vyeo kufikia ngazi wanazostahili.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na wadau wengine huadhimisha sikukuu za wakulima na wafugaji, Nane Nane na siku ya chakula duniani. Lengo la maadhimisho hayo ni kutoa fursa kwa wakulima, wafugaji na wataalam kijifunza mbinu bora za uzalishaji, usindikaji na kuwawezesha wakulima kujua wapi teknolojia hizo zinapatikana. Katika mwaka wa 2003/2004,Wizara ya Kilimo na Chakula ilitumia shilingi milioni 17 kuratibu sikukuu na Maonyesho ya Nane Nane iliyofanyika mkoani Mbeya na Siku ya Chakula Duniani iliyofanyika Kitaifa wilayani Mbinga mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ofisi za Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilifanya sensa ya kilimo na mifugo. Sensa hiyo imelenga kupata takwimu sahihi za kilimo na mifugo nchini zitakazosaidia katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP).* Uchambuzi wa kina wa takwimu zilizokusanywa unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Wizara ya Kilimo na Chakula wa mwaka wa 2004/2005 unalenga katika kuendeleza na kuimarisha juhudi za miaka iliyopita kwa kuhimiza uzalishaji wa kilimo utakaolifanya Taifa lijitosheleze kwa chakula na kuwa na hifadhi ya kutosha katika ngazi ya kaya na Taifa.

Aidha, Mpango huo unalenga kutekeleza mikakati itakayowezesha kuongeza eneo la uzalishaji, tija na ubora wa mazao ya biashara ili kukiwezesha kilimo kitoe mchango mkubwa katika uchumi wa nchi na katika kuondoa umaskini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwa na mifumo madhubuti ya upatikanaji wa pembejeo za kutosha na zana bora kwa wakati, kuongeza eneo linalomwagiliwa maji, kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno, kuimarisha usindikaji wa mazao na huduma za ugani, utafiti, mafunzo na kuweka na kutekeleza mifumo ya usimamizi.

Katika mwaka wa 2004/2005 hatua za kufanya sekta ya kilimo iwavutie wawekezaji wa ndani na wa nje, wadogo na wakubwa zilizotangazwa na Waziri wa Fedha katika hotuba yake ya Bajeti, zitatekelezwa. Hatua hizo zinaifanya sekta ya kilimo kuwa na vivutio vingi. Wadau wengi wa kilimo wameeleza kuridhishwa na vivutio hivyo. Wizara ya Kilimo na Chakula itashirikiana na Wizara ya Fedha kufafanua vivutio hivyo katika lugha rahisi katika kijitabu ili wakulima na wawekezaji katika sekta ya kilimo waweze kuvielewa vizuri na kuvitumia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Serikali itaendelea kutekeleza Mipango ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs),* ambayo ni sehemu ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Jumla ya shilingi bilioni 4 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango hiyo. Miradi yote inayotekelezwa katika Wilaya, ikiwa ni pamoja na ile inayopata misaada ya wahisani, itaingizwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya. Ili kutekeleza azima hiyo, Serikali imeagiza miradi yote inayoendelea na ile itakayoanzishwa siku zijazo iwe inazingatia mambo yafuatayo:-

(a) Kuwekeza katika miradi ya kilimo itakayoibuliwa na jamii au vikundi vya wakulima;

(b) Kujenga uwezo wa wakulima, vikundi vya wakulima na Wilaya kutekeleza miradi ya maendeleo ya kilimo, hususan katika kuibua, kuandaa na kutekeleza miradi.

(c) Kuhakikisha wakulima wanapata teknolojia bora za uzalishaji kwa mfano, mbegu bora, mbolea, zana za kilimo na udhibiti wa visumbufu vya mazao;

(d) Kuwapatia wakulima mikopo na mitaji kupitia kwenye vikundi vyao vya ushirika na vyama vya kuweka na kukopa; na

(e) Kuwasaidia wakulima kuzalisha kibiashara na kuwapatia masoko yenye uhakika kwa mazao yao.

Mheshimiwa Spika, wazo la zao moja la chakula na zao moja la biashara linafutwa kwa sababu uamuzi wa mazao yatakayopewa kipaumbele katika Wilaya unaachiwa Wilaya zenyewe. *(Makofi)*

Katika kuchagua mazao, Wilaya zinashauriwa kuzingatia ulazima wa kujihakikishia usalama wa chakula, azma ya kupambana na umaskini na mchango wa kilimo katika uchumi wa Taifa. Aidha, ni sharti Wilaya zichague mazao yanayostahimili

mazingira ya maeneo yao. Utafiti unaonyesha kwamba watu wanaoishi kwenye maeneo yenye mazao ya uhakika ya biashara wanakuwa na hali nzuri zaidi za uchumi kuliko wale wasiokuwa na mazao ya uhakika ya biashara. Wilaya zinashauriwa kuzingatia ukweli huu.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali kwa mara ya kwanza katika miaka zaidi ya kumi, ilitoa ruzuku iliyokusudiwa kudhibiti kupanda kwa bei za mbolea. Pamoja na mapungufu machache yaliyojitokeza, mpango huo ulikuwa na mafanikio makubwa, uliwezesha wananchi kutumia mbolea kwa wingi zaidi na hivyo kuongeza sana uzalishaji wa mazao. Tumejifunza mengi kutokana na utekelezaji wa mpango huo. Katika mwaka wa 2004/2005, mpango huo utaendelezwa na kupanuliwa.

Mheshimiwa Spika, wanzo ilikusudiwa kutekeleza mpango huo kwenye mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini na katika mikoa inayopata mvua za kuaminika na inayopakana na mikoa inayopata ukame mara kwa mara. Kutokana na Serikali kutenga fedha za kutosha, mpango huo sasa utatekelezwa katika nchi nzima.

Chini ya mpango huo, Serikali Kuu itadhibiti bei za mbolea hadi kwenye makao makuu ya mikoa na vituo vikuu vya kupokelea mbolea katika mikoa na Kamati za Mikoa na Wilaya zitaendelea kuanzia hapo. Hata hivyo, wilaya zenye matatizo maalum, kwa mfano zilizoko mbali sana na vituo vya kupokelea mbolea, zitapewa msaada maalum ili wakulima wasiadhibiwe kutokana namatatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ni upatikanaji wa mbolea kwa wingi na kwa wakati. Katika mwaka wa 2004/2005 inakisiwa kwamba Taifa linahitaji tani 385,000 za mbolea. Serikali itaendelea kuwahimiza wafanyabiashara binafsi kuingiza mbolea nchini kwa wingi. Kuingiza mbolea nchini hakuhitaji kibali na mbolea haitozwi kodi. Mbolea itakayoingizwa nchini na wafanyabiashara itasambazwa na itafaidika na ruzuku ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalipa suala la upatikanaji wa mbolea uzito wa juu kabisa. Mazungumzo na Benki ya *BADEA* yenye lengo la kupata mkopo wa kununulia mbolea na mahitaji mengine ya kilimo yanakaribia kukamilika. Mkopo huo utatuwezesha kuagiza mbolea na mahitaji mengine ya kilimo kutoka kwenye nchi za Kiarabu *(Middle East).*

Mheshimiwa Spika, juhudi za Serikali za kutoa ruzuku ili kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea zinalenga kumwezesha mkulima kuongeza matumizi ya mbolea ili azalishe mazao mengi zaidi. Kutokana na mpango huo, tunatarajia mavuno makubwa ya mahindi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na pia katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, ili kumwezesha mkulima kupata soko la uhakika na lenye bei nzuri, Hifadhi ya Chakula ya Taifa, kwa mara ya kwanza tangu ianzishwe, italenga kununua takriban tani 100,000 za mahindi na mtama katika mwaka huu na kadri

itakavyowezekana, ununuzi utafanywa kwenye vituo vya kuuzia mazao vya vijijini ili wakulima wafaidike na bei inayotolewa na *SGR* moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza, hifadhi ya Chakula ya Taifa itanununua mtama. Kiasi kitakachonunuliwa kitategemea upatikanaji wa mtama wenye ubora unaokubalika. Lengo ni kuongeza mtama katika mazao yanayohifadhiwa na Hifadhi ya Chakula ya Taifa, kutoa mtama kama chakula wakati wa dharura, kuwapatia wakulima soko la mtama ili kuwashawishi walime zao hilo kwa wingi kwa kutumia Hifadhi ya Chakula ya Taifa kama mahali pa kuhifadhi mbegu ya mtama ili ipatikane kwa urahisi itakapohitajika.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2003/2004, nilitoa taarifa kwamba Wizara ilikuwa ikitekeleza kwa majaribio mradi unaojulikana kama Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory Agricultural Development and Empowerment Project-PADEP).*

Katika mwaka wa 2004/2005, Mradi huo utatekelezwa kwa kasi na ukamilifu zaidi katika mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Kilimanjaro, Morogoro, Tabora, Tanga, Iringa (Wilaya ya Iringa vijijini), Mtwara (Wilaya ya Masasi), Lindi (Wilaya ya Nachingwea) na Wilaya mbili za Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mpango huu una vipengele vingi ambavyo vinajibu matatizo yanayokikabili kilimo na mkulima mdogo. Muhimu katika hivyo ni:-

(a) Maendeleo ya Kiuchumi ya Jamii katika Vijiji. Wakulima watapatiwa asilimia 50 ya fedha za ununuzi wa mbolea, mbegu bora, zana, maksai na vifaa vyake ili waendeleze mazao muhimu ya kiuchumi vijijini kwao. Aidha, wakulima watapewa ruzuku ya asilimia 80 katika ujenzi wa miundombinu ya uchumi kwa mfano, ujenzi wa mabwawa, mifereji, vizuizi vya umwagiliaji maji mashambani, miundombinu ya hifadhi ya ardhi na barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, wakulima watachangia asilimia 20 ya gharama kwa kufanya kazi kama kuchimba mifereji na makinga maji. Kuhusu usindikaji wa mazao (matunda na mbegu za mafuta), Mradi utachangia asilimia 80 ya gharama na walengwa watachangia asilimia 20. *(Makofi)*

(b) Uwekezaji kwa vikundi vya wakulima. Mafunzo ya teknolojia mpya yatatolewa kwa wakulima, husussan yanayohusu uzalishaji wa mazao kibiashara, ufugaji, hifadhi ya mazao na usindikaji. Aidha, watajengewa uwezo wa kupata taarifa za masoko na kuhifadhi mazao yao hadi bei katika soko zitakapokuwa nzuri.

Vyama vya Kuweka na Kukopa *(SACCOs)* vitasaidiwa mafunzo na fedha katika kujenga mtandao wa taasisi za kifedha vijijini na kuunganishwa na mabenki ili viweze kuwakopesha wakulima kupitia *SACCOs* hizo.

(c) Elimu ya biashara na uendeshaji.Wakulima watapatiwa mafunzo ya kitaalam na ya kibiashara katika uzalishaji wa mazao ya kilimo wanayoyazalisha.

(d) Usimamizi na uratibu. Halmashauri za Wilaya, hususan ngazi ya kata, zitaimarishwa ili ziweze kusimamia utoaji wa mahitaji ya wakulima na upokeaji wa teknolojia na raslimali za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha mipango ya kukopa kutoka kwenye Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* dola za kimarekani milioni 57.0 za kugharamia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo katika wilaya za mikoa ya Shinyanga, Kigoma, Mara, Mwanza na Kagera. Mradi huo utajulikana kama Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agricultural Sector Investment Project - DASIP).*

Mheshimiwa Spika, Mradi huu umebuniwa kufanana na Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(PADEP).* Mradi ulianza kuandaliwa mwezi wa Februari, 2004 na umekuwa ukiandaliwa kwa kasi kubwa *(fast track)* kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji utaanza katika nusu ya pili ya mwaka wa 2004 ili wakulima wafaidike na Mradi huo katika msimu wa kilimo wa 2004/2005. Naishukuru sana Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ushirikiano wao na kwa kukubali kutoa mkopo huo kwa utaratibu wa *fast track.* Serikali itaendelea kutafuta mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya kuendeleza kilimo.

Aidha, mpango huu utatekelezwa kwa kutumia mbinu shirikishi jamii kwa maana ya kwamba wananchi wenyewe ndio watakaoibua mambo wanayoyataka kutekeleza kwa kutumia fedha za mpango na mahitaji ya vikundi mbalimbali katika wilaya yataunganishwa kwanye Mpango wa Maendeleo ya Kilimo na kugharamiwa na Mradi. Namshukuru sana Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu, ambaye ndiye mwanzilishi wa Mradi huu.

Aidha, Serikali imekubaliana na baadhi ya wahisani kurekebisha miradi wanayoifadhili kwa kuzingatia utaratibu wa kuandaa mipango ya maendeleo ya kilimo katika wilaya na dhana zilizopo katika *PADEP* na *DASIP.* Kwa mfano, Shirika la Maendeleo la Denmark *(DANIDA)* litagharama mipango ya maendeleo ya kilimo katika wilaya za mikoa ya Iringa na Mbeya chini ya utaratibu wa *DADPS.* Shirika la Maendeleo la Finland *(FINIDA)* litagharamia miradi ya maendeleo ya kilimo ya wilaya katika mikoa ya Mtwara na Lindi kupitia Mradi wa Uwezeshaji Kiuchumi na Kijamii Wilayani *(District Economic and Social Empowerement Project - DESEP).* Kwa wakati uliopo, Serikali itaendelea kugharamia mipango ya maendeleo ya wilaya katika mikoa ambayo haina mipango maalum ya maendeleo ya kilimo hadi hapo juhudi za kupata mikopo au misaada zitakapofanikiwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuandaa na kutekeleza Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya unazitaka kila Halmashauri za Wilaya kupanga miradi kwa kuzingatia mahitaji na uwezo wa uzalishaji wa kilimo katika maeneo yao. Tatizo kubwa la uzalishaji ni usimamizi, ngazi ya wiliaya, tarafa, kata hadi vijijini. Tunapaswa kuimarisha usimamizi katika ngazi zote hususan katika kuhakisha wakulima wanayo

ardhi ya kutosha, wanazalisha mazao yanayokubalika na kwa viango vinavyokubalika. Ipo haja ya kutumia utaratibu wa mpango shirikishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na wahisani ambao wanatusaidia kuendeleza sekta ya kilimo kwa lengo la kuwashawishi warekebishe miundo ya miradi yao ili ifanane na *PADEP,* yaani izingatie mahitaji ya wakulima katika maeneo yao na kuweka utaratibu wa kuyatimiza.

Aidha, mipango yao iwe ni sehemu ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo katika Wilaya. Wahisani wote walishiriki katika maandalizi ya Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Strategy-ASDS)* na Mfumo na Mchakato wa Kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme -ASDP - Framework and Process)* kwa hiyo, hakutakuwepo sababu za kutokutekeleza miradi wanayohisani kwa utaratibu tuliokubaliana.

Mheshimiwa Spika, mkataba juu ya matumizi ya fedha za *STABEX* ulitiliwa saini kati ya Serikali na Jumuia ya Ulaya tarehe 10 Februari, 2003. Chini ya makubaliano hayo fedha za *STABEX* zilizokuwepo, *Euro 38.0* milioni, ziligawanywa kama ifuatavyo:-

(a) Utafiti wa kahawa na huduma za ugani kwa wakulima, *Euro* 9,000,000, Kazi za utafiti zitatekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa *(Tanzania Coffee Research Institute - TACRI),* Lyamungo na vituo vyake vilivyoko Ugano, Mbinga, Mbimba, Mbeya na Maruku, Kagera. Mradi unalenga kupunguza umaskini na kuongeza tija kwa kuwekeza kwenye utafiti na kuwawezesha wakulima kupata miche na utaalam wa kilimo cha kahawa.

(b) Barabara katika maeneo ya kahawa *Euro* 10,000,000, usimamizi wa utekelezaji wa matengenezo ya barabara na matumizi ya fedha utakuwa chini ya Wakala wa Barabara wa Taifa *(TANROADS). Tender* ya kubainisha barabara zitakazotengenezwa ilifunguliwa tarehe 13 Februari, 2004 na kampuni ijulikanayo kama *Roughton Internation Ltd. UK.* ilishinda. Kazi ya kubaini barabara zitakazojengwa inatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Juni au Julai, 2004 na ujenzi wa barabara unatarajiwa kuanza mwezi wa Septemba, 2004 na inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka mmoja.

(c) Mpango wa maendeleo ya kilimo *(ASDP), Euro* 18,000,000. Kipengele hiki kimegawanyika kwenye sehemu kuu nane.

(i) Mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya, *Euro* 6,308,693;

(ii) Uboreshaji wa kahawa, *Euro* 2,500,000 (Zitatumika katika ujenzi wa mitambo ya kumenya kahawa *(central pulparies)* ili kuinua ubora wa kahawa);

(iii) Utafiti wa chai na pamba, *Euro* 2,500,000;

(iv) Sensa ya kilimo, *Euro* 2,661,307;

(v) Kurekebisha mifumo ya bodi za mazao, *Euro* 450,000;

(vi) Ufafanuzi wa sheria ya vijiji *Euro* 400,000;

(vii) Tafiti za sera na udhibiti, *Euro* 800,000; na

(viii) Maandalizi ya *ASDP*, *Euro* 3,380,000.

(d) Uratibu wa programu na uandaaji wa mipango, *Euro* 3,380,000.

(e) Uratibu, ufuatiliaji na tathmini, *Euro* 1,440,413.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kuratibu na kusimamia uendelezaji wa mazao makuu ya biashara hususan chai, kahawa, pareto, pamba, tumbaku, korosho, miwa na mkonge ili kuongeza tija na uzalishaji.

Aidha, Wizara itahakikisha mazao hayo yanakuwa na ubora wa hali ya juu utakaoyawezesha kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi. Wakulima wataelimishwa umuhimu wa kutunza ubora wa mazao mashambani na kuyapanga katika madaraja wakati wa kuyauza. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za ukaguzi wa mazao na kuhakikisha mazao hayo yanauzwa kwa vipimo na katika vituo vilivyoidhinishwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mazao yetu ya kilimo hukosa soko la uhakika kwa sababu mazao hayo huuzwa kabla hayajasindikwa, ili kuyaongezea ubora na thamani. Mwaka wa 2004/2005, Wizara itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na *UNIDO* kuendelea kujenga uwezo wa vikundi vya wananchi kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao ya kilimo kabla ya kuyauza, hususan mazao ya chakula.

Aidha, Serikali inakamilisha mpango wa kutoa vivutio kwa wawekezaji katika viwanda vya kati na vikubwa katika usindikaji wa mazao ya kilimo. Wizara kwa kupitia Bodi za Mazao itaendelea kusimamia uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kusindika mazao makuu ya biashara. Matarajio ya uzalishaji na usindikaji wa mazao makuu ya biashara katika msimu wa 2004/2005 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa chai unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 30,700 zilizozalishwa mwaka wa 2003/2004 hadi tani 33,146 katika msimu wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hilo litatokana na ukarabati uliofanyika kwenye viwanda vya chai, soko la uhakika la majani mabichi ya chai, hususan kutoka kwa wakulima wadogo, uboreshaji wa utafiti wa zao la chai na usambazaji wa miche bora kwa wakulima unaotekelezwa na *TRIT* kwa kutumia fedha za *STABEX.*

Mheshimiwa Spika, ili kuinua kilimo cha chai kupitia wakulima wadogo, Wizara itaendelea kuimarisha vikundi na vyama vya wakulima wadogo wa chai katika maeneo ya Rungwe, Lupembe, Mufindi, Dabaga, Usambara, Kagera na Tarime ili viweze kusajiliwa kama *SACCOs* na kuwawezesha wakulima kupata mikopo ya kununulia pembejeo za kilimo cha chai.

Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha Chama Kilele cha Wakulima Wadogo wa Chai *(Tanzania Smallholder Tea Growers Association - TSTGA)* ili kiweze kusaidia vyama vya wakulima wadogo wa zao hilo katika kuandaa na kutekeleza miradi ya kupanua maeneo yanayolima zao la chai, kupata miche bora na mikopo ya pembejeo. Wizara itaendelea kuhimiza kuanzishwa kwa kilimo cha chai katika maeneo mapya kama vile Dabaga, Tarime, Kigoma, Mbinga na Ludewa. Jitihada za kuhamasisha wawekezaji ili wajenge viwanda vya kusindika chai, hususan katika maeneo mapya ya chai nazo zitaendelea.

Mheshimiwa Spika, zao la kahawa linatarajiwa kuongezeka kutoka tani 37,500 zilizozalishwa katika msimu wa 2003/2004 hadi tani 45,800 katika msimu 2004/2005 sawa na ongezeko la asilimia 18. Ongezeko hilo litatokana na tabia ya zao la kahawa kuzaa kwa wingi msimu mmoja na kupunguza uzalishaji katika msimu unaofuata. Msimu wa 2004/2005 utaangukia wakati kahawa inazaa kwa wingi.

Aidha, wakulima watahimizwa kuongeza maeneo ya kilimo cha kahawa na tija kutokana na Serikali kuweka utaratibu wa kuwaruhusu wakulima wanaozalisha kahawa zenye ubora wa hali ya juu kuuza kahawa zao moja kwa moja. Utaratibu huo utawezesha upatikanaji wa bei nzuri kwa kahawa hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ubora wa kahawa Serikali kwa kushirikiana na Jumuia ya Nchi za Ulaya inaandaa mpango maalum wa kuinua ubora wa kahawa, hususan kwa kujenga viwanda vya kupukuchukua kahawa *(pulperies)* na matumizi ya teknolojia zinazohakikisha kahawa inayozalishwa na wakulima inakuwa ya ubora wa hali ya juu. Mpango huo utagharimu jumla ya shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2004/2005, uzalishaji wa sukari unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 228,000 zilizozalishwa mwaka wa 2003/2004 hadi tani 280,300, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Ongezeko hilo litatokana na kuongezeka kwa ufanisi wa uzalishaji katika viwanda baada ya kufanyiwa ukarabati, ufufuaji wa mashamba ya miwa na kuongezeka kwa wakulima wadogo wa miwa kutoka wakulima 8,000 mwaka wa 2003/2004 hadi wakulima 10,000 mwaka wa 2004/2005. Wakulima wadogo wa miwa wa Kilombero na Mtibwa wanategemewa kuzalisha tani 637, ambapo wakulima wadogo wa Kilombero watazalisha tani 402 na wakulima wadogo wa Mtibwa tani 235.

Aidha, katika mwaka wa 2004/2005, Kampuni ya Sukari ya Kilombero itaanza kuzalisha sukari nyeupe kwa ajili ya matumizi ya viwandani. Inategemewa kuwa katika mwaka 2004/2005 takriban tani 30,000 zitazalishwa. Kiwanda cha Sukari cha Kagera

kitaanza kuzalisha sukari ya kawaida kuanzia mwezi wa Julai 2004 na kinategemewa kuzalisha tani 25,000 katika mwaka wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwahamasisha wawekezaji waanzishe mashamba ya miwa na viwanda vya sukari katika maeneo ambayo utafiti umeonyesha kuwa yanafaa kwa kilimo hicho, hususan katika mabonde ya Mto Kilombero, Mto Mara na eneo la Mahurunga katika mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali nzuri ya hewa inayotarajiwa, uzalishaji wa zao la korosho unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 95,000 msimu wa 2003/2004 hadi tani 100,000 katika msimu wa 2004/2005 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 5. Wizara itaendelea kuwahimiza wawekezaji kupanua ubanguaji wa korosho hapa nchini kwa kutumia teknolojia rahisi zitakazotoa ajira kwa wananchi wengi, hususan wanawake. Aidha, Serikali itakamilisha ubinafsishaji wa viwanda vya korosho na kuweka vivutio vya kuhamasisha usindikaji na uuzaji wa korosho iliyobanguliwa.

Kuhusu uzalishaji wa zao la tumbaku unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 46,725 zilizozalishwa katika msimu wa 2003/2004 hadi tani 51,000 msimu wa2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia tisa. Ongezeko hilo litatokana na kuendelea kuongezeka kwa bei ya mkulima hadi kufikia wastani wa shilingi 830 kwa kilo kutoka shilingi 763 kwa kilo mwaka wa 2003/2004, kupanuliwa kwa maeneo yanayozalisha tumbaku nchini, kuimarishwa kwa upatikanaji wa pembejeo muhimu kutokana na makampuni ya ununuzi wa tumbaku kuendelea kutoa huduma hizo kwa ufanisi zaidi na matumizi ya mbegu zenye tija kubwa zilizoanza kutumika katika msimu wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa zao la pamba katika msimu wa 2004/2005 unatarajiwa kufikia tani 250,000, sawa na ongezeko la asilimia 80 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 137,899 msimu wa 2003/2004. Uzalishaji unatarajiwa kuongezeka kutokana na ongezeko la ufanisi wa uzalishaji baada ya kuanza kutekelezwa kwa mpango wa kitaifa wa pembejeo za pamba unaowaongezea wakulima uwezo wa kununua pembejeo kwa kutumia utaratibu wa vocha; kuanzishwa kwa kilimo cha pamba katika maeneo mapya, hususan katika wilaya za Kasulu, Kibondo, Ngara, Uyui, Urambo, Iramba, Manyoni na Singida, wakulima kuendelea kuhamasika kutokana na bei nzuri ya pamba ya shilingi 280 kwa kilo waliyolipwa katika msimu wa 2003/2004 ikilinganishwa na shilingi 180 kwa kilo mwaka wa 2002/2003. Aidha, ongezeko hilo litatokana na matumizi ya aina bora zaidi ya mbegu ya pamba aina ya *UK. 91* na aina ya *ALAI* 90 zilizopandwa katika msimu wa 2003/2004.

Katika msimu wa 2004/2005, Wizara itaendelea kuhakiki ubora wa pamba inayozalishwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha inafikia viwango vya kimataifa kwa:-

- Kuanzisha na kuendesha mashindano ya kilimo cha zao la pamba kiwilaya, kimkoa na kikanda;

- Kuanzisha kilimo cha mkataba ambapo jumla ya hekta milioni 2 zitalimwa kwa mikataba kati ya makampuni na wakulima.

- Kuanzisha mfumo mpya wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba kwa kutumia wakulima wa mkataba kwa lengo la kusambaza aina mpya za mbegu za *UK 91* kwa Kanda ya Magharibi na *ALAI 90* kwa Kanda ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2004/2005 uzalishaji wa pareto unategemewa kuwa tani 1,000, ambao ni sawa na tani 1,000 chini ya uzalishaji wa mwaka wa 2003/2004. Kushuka kwa uzalishaji wa pareto kumesababishwa na bei ya pareto katika soko la dunia kuendelea kuwa chini, hali iliyosababisha takriban tani 2,300 za pareto kubaki mikononi mwa wakulima.

Aidha, mwekezaji wa kiwanda cha pareto kilichopo Iringa amekosa uwezo wa kununua pareto baada ya kushindwa kupata soko na kufanya wakulima kukata tamaa ya kuzalisha pareto na kuanza kupanda mazao mbadala. Ili kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imeidhamini kampuni ya *Tanzania Pyrethrum Processing and Marketing Company Limited* ili ipate mkopo wa benki wa shilingi bilioni 1.48 wa kununulia pareto iliyopo mikononi mwa wakulima.

Aidha, katika msimu wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko itaendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa matatizo ya soko na uziduzi wa pareto. Wizara itahimiza kilimo cha pareto katika maeneo mapya yanayoweza kustawisha zao hilo, hususan katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha na itahakikisha kwamba wakulima wanapata miche bora ya pareto inayozalishwa kwa njia ya vikonyo yenye sumu nyingi zaidi na tija kubwa ya wastani wa kilo 800-1000 kwa hekta.

Uzalishaji wa zao la mkonge unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 23,859 msimu 2003/2004 hadi tani 25,000 katika msimu wa 2004/2005, sawa na ongezeko la asilimia 4.5. Ongezeko hilo litatokana na kuanzishwa kwa utaratibu wa kutumia wakulima wadogo wa mkonge katika mikoa ya Kanda ya Ziwa Viktoria, upanuzi wa mashamba makubwa ya mkonge na bei nzuri ya katani katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudi za kuongeza ufanisi wa matumizi ya bidhaa za mkonge. Ujenzi wa kiwanda cha majaribio cha karatasi kwa kutumia mkonge ambao umeanza unatarajiwa kukamilika mwaka wa 2005/2006. Aidha, kiwanda cha majaribio ya kutoa nishati kwa gesi kwa kutumia taka za mkonge, kimeanza kujengwa. Utafiti wa pombe, citric acid na bidhaa nyingine zitokanazo na zao la mkonge utaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itakarabati na kujenga upya miundombinu mbalimbali katika bustani za Serikali za Mpiji mkoani Pwani na Bugaga mkoani Kigoma. Aidha, Wizara itatoa mafunzo maalum ya mbinu bora za umwagiliaji maji mashambani kwa wataalam na wakulima ili wazalishe miche mingi yenye ubora unaotakiwa. Aidha, mashamba ya mfano 50 ya mazao ya maembe, vanilla, paprika na migomba yataanzishwa

katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Arusha, Dodoma na Tanga. Wakulima watawezeshwa kutembelea mashamba ya mfano ili kujifunza uzalishaji wa mazao mapya. Nakala 2,000 za vitabu vya mwongozo wa uzalishaji wa mazao hayo vitachapishwa na kusambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kufanya utafiti ili kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia bora za kilimo kwa wakulima. Juhudi za kuzalisha kwa wingi mbegu za mazao zitaendelea pamoja na uchunguzi wa mbegu mpya zitakazoweza kumpatia mkulima mavuno mengi na kuongeza tija katika mazingira ya uzalishaji.

Wizara ya Kilimo na Chakula, kupitia vituo vya utafiti, inatarajia kutoa mbegu mpya tatu za mazao ya nafaka (mahindi na ngano), mbili za mazao ya jamii ya mikunde (maharage na mbaazi), tatu za mafuta (karanga na ufuta) na mbili za mazao ya jamii ya mizizi. Mbegu hizo zitakuwa na sifa za mavuno mengi, kustahimili magonjwa na kuvumilia hali ya ukame.

Aidha, ili kupunguza tatizo la upatikanaji wa mbegu, vitalu vya kuzalisha miche na mbegu vitaanzishwa katika vituo vya utafiti na kwenye baadhi ya vijiji. Miche itakayozalishwa itagawanywa katika mashamba ya wakulima kwa ajili ya uchunguzi zaidi. Miche na mbegu zenye sifa zinazokubalika zitasambazwa kwa wakulima na mashamba ya maonyesho vijijini ili zizalishwe zaidi.

Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kukusanya na kutathmini nasaba za mazao ya mbaazi, dengu, njegere, *safflower, macadamia, vanilla,* matunda, mboga na viungo ili kuongeza wigo wa mazao ya biashara kwa mkulima. Kazi hii itafanyika kwenye vituo vya Katrin, Maruku, Uyole, Tengeru na Ukiriguru. Aidha, mbegu mama za mazao ya jamii ya nafaka, mikunde na mafuta zitaendelea kuzalishwa. Vituo vya utafiti vitaendeleza tafiti zake katika vituo mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Vituo vya Tengeru, Kibaha, Uyole na Hombolo vitaendelea kueneza teknolojia ya kuandaa na kutumia mazao ya jamii ya mizizi kwa mfano muhogo na viazi ili kuyaongezea thamani na matumizi;

- Vituo vya Tumbi, Selian, Uyole na Ukiriguru vitaendelea kufanya utafiti wa miti inayoweza kutumiwa katika kilimo mseto ili kukabiliana na kuzidi kupungua kwa rutuba ya udongo na kuongezeka kwa mmomonyoko wa udongo katika maeneo mengi nchini;

- Vituo vya Katrin na Dakawa vitazalisha mbegu mama za mpunga aina ya *TXD 85, TXD 88* na *TXD 306 ( SARO5);*

- Vituo vya Maruku na Tengeru vitaendelea kuzalisha na kusambaza miche bora ya migomba kwa wakulima. Pamoja na kazi hizo vituo vitandelea kuwaelimisha wakulima mbinu bora za kilimo cha migomba; na

- Vituo vya Ukiriguru na Ilonga vitaendelea kuzalisha mbegu mama za pamba aina ya *UK 91* na *ALAI 90.*

Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kuziendesha maabara za tissue culture zilizopo Mikocheni, Tengeru, Uyole na Ukiriguru ili zianze kutoa miche bora na mingi ya migomba, pareto, muhogo na mananasi. Utumiaji wa teknolojia hii utachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa mbegu bora za mazao mbalimbali. Aidha, Wizara itaendelea na tafiti zifuatazo:-

- Kutafiti, matumizi ya wanyamakazi na zana mbalimbali za kilimo katika kutayarisha mashamba, kupanda, kupalilia na kubeba mizigo. Utafiti huo utafanyika Uyole na Ukiriguru na utashirikisha wakulima katika mashamba yao.

- Kutafiti mbinu mbali mbali za uvunaji maji ya mvua *(rain water harvesting)* ili kuyatumia katika uzalishaji wa mazao na matumizi ya nyumbani. Kazi hii itafanyika kwenye vituo vya Ukiriguru na Uyole kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

- Kufanya tafiti za sayansi jamii na uchumi kwenye kanda ili kuboresha ufanisi katika kutoa ushauri sahihi wa matumizi ya teknolojia katika mazingira ya wakulima;

- Kuandaa na kuendesha mafunzo kwa watafiti 80 kuhusu mbinu shirikishi za utafiti unaolenga mahitaji halisi ya wakulima; na

- Chini ya mradi wa *PADEP,* kukarabati maabara za udongo katika vituo vya utafiti vya Mlingano, Uyole, Selian na Ukiriguru na kutoa mafunzo kwa wataalam ili ziweze kutoa huduma ya upimaji wa udongo kwa mashamba ya wakulima na kutoa ushauri kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na kununua dawa na vifaa vitakavyotumiwa na maabara za udongo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kuimarisha vyuo vya Wakulima vya Bihawana, Dodoma, Mkindo, Morogoro na Inyala na Ichenga, Mbeya ili viweze kufundisha wakulima kilimo cha kibiashara. Wakulima 720 watapata mafunzo katika vyuo hivyo. Wakulima hao wataweza kuwafundisha wakulima wenzao baada ya kupatiwa mafunzo hayo. Vyuo hivyo pia vitajihusisha katika uzalishaji wa mazao na ufugaji wa wanyama ili hapo baadaye viweze kujitegemea.

- Kuimarisha Kitengo cha Elimu kwa Wakulima (Ukulima wa Kisasa) makao makuu Dar es Salaam na kwenye kanda ili kiweze kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kutangaza vipindi vya kilimo redioni. Vituo vya redio za kanda vitatumika ili kufikisha haraka mafunzo hayo kwa wakulima;

(b) Kutengeneza mikanda ya video kwa ajili ya mafunzo ya kilimo katika vyuo vya mafunzo vya wakulima. Aidha, mikanda hiyo itatumiwa na wataalam wilayani kwa ajili ya kueneza teknolojia za kilimo kwa wakulima.

(c) Kuchapisha na kusambaza kwa wakulima majarida mbali mbali ya kilimo kama vijitabu vya kilimo bora, gazeti la Ukulima wa Kisasa, vipeperushi na mabango. Aidha, mashine za uchapishaji pamoja na studio za redio na video vitaimarishwa.

(d) Kutangaza kazi za Wizara ya Kilimo na Chakula ili kuelimisha umma kuhusu shughuli na mafanikio ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya husika, itaendelea kutekelezwa katika wilaya za Hai, Morogoro vijijini, Singida vijijini, Iringa vijijini, Masasi, Nachingwea, Hanang na Arumeru. Aidha, mradi utaanza kutekelezwa katika wilaya nyingine 18. Kazi zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo: -

- Kuzindua mradi katika Wilaya 18 zitakazoanza kutekeleza mradi katika mwaka wa 2004/2005 ikiwa ni pamoja na kuunda timu za uwezeshaji za wilaya na kata ili kujenga uwezo wa kuandaa miradi, kufuatilia utekelezaji, udhibiti na uwajibikaji katika matumizi ya fedha;

- Kuendesha mafunzo ya mbinu shirikishi kwa timu za wawezeshaji za Taifa, wilaya na kata ili kujenga uwezo wa kushirikisha jamii katika kupanga mipango ya kuendeleza Kilimo na Ufugaji;

- Kuwezesha jamii katika vijiji 160 vya wilaya zitakazotekeleza mradi katika mikoa ya Manyara, Singida, Tanga, Kilimanjaro, Tabora, Arusha, Iringa, Lindi, Mtwara na Morogoro, kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo ya kilimo kwa kutumia teknolojia sahihi na endelevu. Miradi midogo isiyopungua 600 inatarajiwa kuandaliwa na kutelezwa na jamii katika vijiji hivyo;

- Kuwezesha wilaya 18 zilizochaguliwa kutekeleza mradi katika mwaka wa 2004/2005 kuandaa na kutekeleza programu za kuimarisha uwezo wa kiutendaji katika kusimamia shughuli za maendeleo ya kilimo; na

- Kuwezesha uboreshaji wa sera za kitaifa, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zikiwemo ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: -

- Kuandaa mtaala na kutekeleza mafunzo ya muda mrefu ya Kilimo cha biashara kwa vijana 50;

- Kufundisha wakulima 160 kanuni za kilimo bora cha kibiashara;

- Kuandaa mtaala wa kufundisha elimu ya kuhimiza vita dhidi ya baa la UKIMWI katika sekta ya kilimo. Elimu itatolewa kwa walengwa mbalimbali watakaohudhuria mafunzo katika vyuo vya Kilimo;

- Kuandika vijitabu vya rejea kwa matumizi ya wakulima watakaohudhuria mafunzo ya Kilimo cha biashara vyuoni;

- Kudhamini mafunzo ya muda mrefu kwa wataalamu 250 wenye astashahada kwenda kiwango cha stashahada na astashahada kwa vijana 150 waliomaliza kidato cha sita wanaotarajiwa kujiunga na fani ya Kilimo;

- Kudhamini mafunzo ya shahada ya uzamili na falsafa kwa wakufunzi wanne (4) na mafunzo ya rejea kwa wakufunzi 15 wa vyuo vya Kilimo;

- Kukarabati vyuo vinane (majengo, mifumo ya maji na mifumo ya umeme) na kuvipatia vifaa vya mafunzo kwa vitendo;

- Kuimarisha vitengo vya kuendesha mafunzo ya matumizi ya wanyamakazi katika kilimo;

- Kutoa mafunzo kwa wakulima, vijana na wataalamu kuhusu Kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga katika Chuo cha Wakulima Kilimanjaro *(KATC).*

Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula imelenga kuongeza eneo la uzalishaji kwa kutumia kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kwa jumla ya hekta 27,124. Ongezeko hilo litafanya jumla ya eneo la kilimo cha umwagiliaji maji mashambani nchini kufikia hekta 254,610 kutoka hekta 227,486 za mwaka wa 2003/2004. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaendelea na ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji maji mashambani, ujenzi wa mabwawa na uvunaji wa maji ya mvua. Wizara itaendelea kuhimiza na kusimamia uanzishaji wa mashamba ya mfano katika maeneo yanayozunguka Ziwa Viktoria kwa lengo la kutengeneza ukanda wa kijani wa mazao ya kilimo kuzunguka Ziwa hilo.

Aidha, ili kuongeza ufanisi katika uchimbaji wa mabwawa madogo na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, Wizara itavifanyia ukarabati vifaa vinavyotumika katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani vinavyomilikiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendelea kusimamia skimu zote za umwagiliaji maji mashambani ili kuhakikisha kwamba malengo ya tija na uzalishaji yaliyowekwa katika skimu hizo yanafikiwa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya matumizi bora ya

maji, uendeshaji na usimamizi wa skimu za umwagiliaji maji mashambani kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula itakamilisha awamu ya tatu ya Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani kwa kuthibitisha takwimu na kufanya usanifu wa miradi 10 ya umwagiliaji maji mashambani. Kazi hiyo itaainisha aina za skimu za Umwagiliaji Maji Mashambani zinazoweza kuanzishwa hapa nchini. Lengo ni kupata gharama za ujenzi na mifumo ya uendeshaji na usimamizi ambayo itatumika kama mwongozo katika uandaaji na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji maji mashambani, ambayo itaandaliwa na kutekelezwa chini ya Mipango ya Wilaya ya Kuendeleza Kilimo *(DADPs)*.

Aidha, chini ya Mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani, Wizara itakamilisha mfumo wa utunzaji na utoaji wa takwimu za umwagiliaji maji mashambani zitakazotumiwa na wawekezaji katika kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Skimu 21 za umwagiliaji maji mashambani zilizoainishwa chini ya Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani zitakarabatiwa. Aidha, ujenzi wa skimu za Nyanzwa, Kilolo (hekta 760), Irindi, Kilolo (hekta 610), Utengule Usongwe, Mbeya vijijini (hekta 600) na Naming'ongo, Mbozi (hekta 1,000) ambazo zinaendelezwa na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASPS)* zitakamilishwa.

Skimu tisa zenye jumla ya hekta 2,544 zitaendelezwa chini ya Mfuko wa Pamoja wa Tanzania na Japan wa Msaada wa Chakula *(Food Aid Counterpart Fund)*. Skimu hizo ni Kikafu Chini, Hai (hekta 641), Mvumi, Kilosa (hekta 293), Mlali, Morogoro Vijijini (hekta 80), Chechami Nkonga, Iringa Vijijini (hekta 50), Shamwengo, Mbeya Vijijini (hekta 230), Mlenge, Iringa Vijijini (hekta 500), Malolo, Nzega (hekta 200), Mkula, Kilombero (hekta 250), Ruaha Mbuyuni, Kilolo (hekta 300).

Skimu 15 za mashamba ya mfano za umwagiliaji maji mashambani zitaendelezwa katika Ukanda wa Kijani unaozunguka Ziwa Viktoria (hekta 600). Katika skimu hizo, Wizara itaonyesha matumizi ya teknolojia zinazofaa kwa kuvuta maji kutoka katika Ziwa Viktoria kwa kutumia nishati inayotokana na upepo, mafuta ya dizeli na mionzi ya jua. Aidha, visima vifupi na pampu za miguu vitatumika katika maeneo ambayo yako mbali ya mwambao wa ziwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Serikali itajenga mabwawa 12 ambayo ni mabwawa ya Mwele, Muheza, Kakola, Igunga (hekta 100), Ikowa, Dodoma Vijijini (hekta 150), Maneke, Musoma (hekta 200), Nkiniziwa, Nzega (hekta 200), Usoke, Urambo (hekta 50) na Ruvu *NAFCO,* Kibaha (hekta 100) yatakarabatiwa. Mabwawa ya Mkomazi, Korogwe (hekta 200), Tieme - Masagi, (hekta 200) Nyaisozi, Karagwe (hekta 500) Kiserian, Monduli (hekta 30) na Kironda - Datali, Iramba (100).

Kuhusu Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(Participatory Irrigation Development Programme - PIDP),* katika mwaka wa 2004/2005, Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani itaendelea

na ujenzi wa majaruba ya mpunga na miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika skimu 15 zenye ukubwa wa hekta 3,100. Skimu hizo ziko katika wilaya za Misungwi (3), Maswa (3), Mpwapwa (2), Igunga (2), Mbulu (2) na Iramba (3).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itaendelea kutekeleza miradi iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa 2003/2004 na kuanza kutekeleza miradi mipya iliyopendekezwa chini ya Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya katika mwaka wa 2004/2005. Mipango hiyo imeainisha miradi ya umwagiliaji maji mashambani yenye eneo la hekta 12,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Wizara itaendelea kuweka msukumo mkubwa katika kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo ili kukabiliana na madhara yanayotokana na mmomonyoko wa udongo. Aidha, Wizara itaendelea kupima mashamba kwa lengo la kuboresha mipango ya matumizi ya ardhi na umilikishwaji wa mashamba hayo kwa wakulima. Kazi zitakazo zitatekelezwa: -

- Kuwafikishia wakulima teknolojia za kilimo cha matuta na makingamaji, kilimo mseto na uvunaji wa maji ya mvua mashambani na kuhimiza matumizi yake katika wilaya 36 za mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Mwanza, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Iringa na Ruvuma;

- Kupima mashamba kwenye miradi mitatu ya umwagiliaji maji mashambani ya Lumuma, Kilosa, Kikafu chini, Hai na Ruvu, Bagamoyo na kuweka mipaka ya kila shamba ili kuwawezesha wakulima kumilikishwa mashamba hayo;

- Kuhifadhi ardhi ya kilimo kwenye maeneo yanayozunguka skimu za umwagiliaji maji mashambani ili kudhibiti uharibifu wa miundombinu katika skimu za Lumuma, Kilosa na Kikafu chini, Hai; na

- Kuandaa miongozo ya matumizi endelevu ya ardhi na kuhimiza matumizi miongozo hiyo ili kuongeza uwajibikaji wa wananchi katika kuzingatia matumizi endelevu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mbolea katika msimu wa 2004/2005 yanakadiriwa kuwa tani 385,000, madawa ya kilimo ya unga yatakuwa tani 21,000 na madawa ya maji lita milioni 4.0. Ili kuhakikisha pembejeo hizo zinapatikana kwa wingi na kwa wakati. Aidha, Serikali itaendelea kuwawezesha wananchi kuongeza matumizi ya mbolea kwa kupanua utaratibu wa kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea nchini kote.

Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula itaweka mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za pembejeo kwa kutoa mafunzo kwa wataalam 120 wa kilimo wanaoshughulikia pembejeo katika wilaya zote hapa nchini. Mfumo huo utaiwezesha Wizara kuwa na takwimu sahihi za mahitaji na matumizi ya pembejeo za kilimo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbegu unategemewa kuwa jumla ya tani 13,300 ambao utatokana na uzalishaji katika makampuni binafsi nchini (tani 3,600), wakulima wadogo (tani 800), uagizaji kutoka nje (tani 7,600) na uzalishaji katika mashamba ya Serikali (tani 1,300). Ili kufikia lengo hilo, kazi zifuatazo zitafanyika: -

- Kulima hekta 1,000 ili kuzalisha tani 1,500 za mbegu za msingi na zilizothibitishwa kwa mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta katika mashamba ya Dabaga, Msimba, Mwele na Kilangali.

- Kufanya tathmini ili kuweka miundo mbinu ya umwagiliaji maji katika mashamba mawili ya mbegu ya Dabaga na Msimba, ili kuongeza uzalishaji wa mbegu wakati wa kiangazi.

- Kuwezesha Wakala wa Ukaguzi na Udhibiti wa Mbegu *(TOSCA)* kudhibiti ubora wa mbegu nchini, kwa kukagua mashamba ya mbegu na kuchukua sampuli za mbegu kwa ajili ya kupima ubora wa mbegu katika maabara. Aidha, wataalam wa kilimo 50 watapewa mafunzo kuhusu ukaguzi wa mbegu katika wilaya 50 zilizo chini ya Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(PADEP).*

- Ili kuongeza matumizi ya mbegu bora katika ngazi za vijiji, mpango wa kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(quality declared seed)* kwa kutumia wakulima wadogo chini ya Mradi wa Kusaidia Sekta ya Kilimo *(ASPS)* utaendelezwa katika mikoa ya Dodoma, Iringa, Morogoro, Lindi na Mtwara. Aidha, Serikali itatoa mafunzo ya uzalishaji mbegu vijijini kwa kuwafundisha wakulima wadogo katika mikoa ya Pwani, Kigoma, Kagera na Rukwa mbinu za kuzalisha mbegu zenye ubora wa kuazimiwa.

- Kukamilisha uundwaji wa Wakala wa Mbegu, kuimarisha shughuli zake na kuupatia mali ambazo zilikuwa za *TANSEED* katika matawi ya Morogoro na Njombe yakiwemo maghala ya kuhifadhia mbegu na nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wakulima kupitia Mfuko wa Pembejeo ili kuwawezesha kukarabati matrekta mabovu na kununua mapya. Jumla ya matrekta 200 yatakarabatiwa na matrekta mapya 20 yatanunuliwa chini ya mpango huu. Halmashauri za Wilaya kwa kutumia wataalam wake zitafanya tathmini ya awali ya matrekta na kutoa mapendekezo ya wakulima wanaokidhi masharti ya mkopo kabla maombi hayo hayajawasilishwa kwenye Mfuko wa Pembejeo. Aidha, vituo viwili vya kukodisha matrekta vitakavyoendeshwa na sekta binafsi vitaanzishwa katika wilaya zitakazokidhi masharti ili vitoe huduma kwa wakulima.

Wizara itaendelea kutoa mafunzo kuhusu matumizi na matengenezo ya matrekta madogo ya mkono na mashine ndogo za kubangua korosho. Mafundi sanifu 55 wa Halmashauri za Wilaya katika mikoa ya Shinyanga (3), Kagera (8), Lindi (4), Ruvuma (6), Tanga (8), Mtwara (6), Pwani (4), Arusha (4), Manyara (4) na Mbeya (8) watapata mafunzo hayo na watawezeshwa ili watoe mafunzo hayo kwa wakulima katika vijiji husika.

Wizara itaendelea kuweka mkazo katika matumizi ya wanyamakazi kwenye mikoa yenye matumizi makubwa ya wanyamakazi na mifugo mingi kama Mwanza, Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Dodoma, Morogoro, Arusha, Mbeya, Rukwa, Iringa na Manyara. Vituo 20 vya wanyamakazi katika mikoa hiyo vitakarabatiwa na kupatiwa zana ili viweze kutoa mafunzo na kufanya maonyesho kwa wakulima juu ya matumizi bora ya teknolojia ya matumizi ya wanyamakazi katika kilimo. Aidha, kila kituo kitaanzisha shamba la mfano la hekta mbili kwa ajili ya kutoa mafunzo na maonyesho kwa vitendo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya matumizi ya zana bora zinazokokotwa na wanyamakazi yatatolewa kwa maafisa ugani 400 na vikundi vya wakulima 100. Vikundi hivyo vya wakulima vitawezeshwa kwa kupatiwa zana ili vitoe mafunzo kwa wakulima wenzao vijijini kwa kushirikiana na maafisa ugani, hivyo kuwezesha wakulima wengi zaidi kupata mafunzo katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Mfuko wa Pembejeo utaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya uagizaji na usambazaji wa pembejeo na zana za kilimo kwa kupitia mabenki na taasisi nyingine za fedha. Aidha, Mfuko utatoa mikopo kwa ajili ya kununulia matrekta mapya pamoja na kukarabati ya zamani. Mikopo itatolewa kwa masharti ya ukopeshaji ya benki na wakopaji watapaswa kurejesha mikopo kwa kufuata utaratibu uliokubaliwa kati yao na benki.

Mheshimiwa Spika, ili kufikisha huduma za Mfuko wa Pembejeo kwa Wakulima na Wafugaji Mfuko utaendelea kutoa huduma za mikopo Mikoani kwa kupitia taasisi zifuatazo:-

- Benki ya Exim katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Mtwara, Lindi, Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Morogoro, Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora na Kigoma.

- Benki ya Ushirika Kilimanjaro katika Mkoa wa Kilimanjaro.

- Benki ya Wananchi ya Mufindi katika Mikoa ya Iringa, Rukwa na Mbeya.

- Benki ya Wananchi ya Mbinga katika Mkoa wa Ruvuma.

- Benki ya Ushirika ya Wakulima Kagera katika Mkoa wa Kagera.

- Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *Tanzania (1992) Ltd, (SCCULT (1992) LTD)- SACCOS/SACCAS* zitakazohudumia wanachama wake nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Pembejeo itaendelea na ukusanyaji wa madeni ya miaka ya nyuma ikiwa ni pamoja na uuzaji wa dhamana za wadaiwa baada

ya kupata hukumu za kesi za madai zilizopo mahakamani. Hadi sasa jumla ya kesi 64 za wadaiwa bado zinaendelea kusikilizwa kwenye mahakama.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula itaweka mkazo katika masuala yafuatayo: -

(i) Kuendelea kuhamasisha wakulima wa mikoa ya Kigoma, Singida, Mtwara, Morogoro, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, na mikoa ya Kanda ya Ziwa kutumia mbinu ya Udhibiti Husishi wa visumbufu vya mimea kama njia pekee endelevu, salama na yenye gharama nafuu katika kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao;

(ii) Kuendelea kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Taasisi mbali mbali ikiwa ni pamoja na mashirika ya kimataifa yanayodhibiti milipuko ya nzige na kwelea kwelea ya *DLCO-EA* na *IRLCO-CSA* katika kukagua maeneo ya mazalio ya visumbufu hao na kuwadhibiti mapema ili kuokoa mazao ya wakulima;

(iii) Kuimarisha huduma za utabiri wa milipuko hususan milipuko ya viwavijeshi na panya;

(iv) Kuendeleza shughuli za kuchunguza na kudhibiti gugumaji;

(v) Kuwafundisha wakulima mbinu endelevu za kukabiliana na visumbufu hususan teknolojia za udhibiti husishi *(IPM);* na

(vi) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea ya mwaka 1997 *(Plant Protection Act of 1997).* Mkazo utawekwa katika kuboresha huduma ya karantini ya mimea na ukaguzi wa madawa ya kilimo yanayoingizwa au kutolewa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Hifadhi ya Chakula ya Taifa itanunua jumla ya tani 100,000 za mahindi na mtama yenye ubora unaokubalika. Chakula hicho kitahifadhiwa katika kanda saba za Hifadhi ya Chakula ya Taifa ili kiweze kusambazwa na kuuzwa kwenye maeneo yatakayokuwa na upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula ina Jukumu la kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula wakati wote. Katika mwaka wa 2004/2005 Wizara itaendelea kutekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuandaa maandiko ya kitaalamu kwa ajili ya kurekebisha sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka 1991;

(b) Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu na taarifa za hali ya Chakula nchini;

(c) Kukusanya taarifa za mvua na mazao na kufanya tathmini ya kaya zitakazoathirika na upungufu wa chakula;

(d) Kuendesha kampeni ya kuhifadhi chakula cha kutosha katika ngazi ya kaya;

(e) Kutoa mafunzo ya teknolojia za hifadhi ya mazao ya nafaka na mikunde katika mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Rukwa, Ruvuma, na Mbeya;

(f) Kutoa mafunzo ya usindikaji, matumizi na hifadhi ya mazao ya mizizi, mboga na matunda katika mikoa ya Kigoma, Ruvuma, Morogoro, Tanga, Iringa, Dodoma na Pwani; na

(g) Kutoa mafunzo kwa wataalamu wawezeshaji juu ya uboreshaji na matumizi ya vyakula bora kwa watu waishio na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na *PSRC* itaendelea kuyabinafsisha mashamba ya mahindi ya Mbozi na Namtumbo, Viwanda 12 vya korosho, Kiwanda cha Kahawa cha Kagera *(TANICA)* na Jineri ya Manawa.

Kuhusu ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba ya mashamba na mashirika yaliyobinafsishwa ili kuweza kubaini mafanikio na matatizo ya utekelezaji utaendelea. Wawekezaji watakaobainika kushindwa kutekeleza mikataba ya mauzo watachukuliwa hatua za kisheria zinazostahili, ikiwa ni pamoja na kusitishwa mikataba yao na hatimaye kubinafsisha upya mashamba na mashirika yatakayohusika.

Aidha, kwa kushirikiana na uongozi wa mikoa, Wizara itaendelea kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kushirikiana na wawekezaji katika maeneo yao ili kujenga na kuimarisha mahusiano mema kati ya wawekezaji na wananchi wanaoishi jirani na maeneo yaliyobinafsishwa. Mikakati ya kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha sekta binafsi kuwekeza katika kilimo cha kibiashara itaendelea kuwekwa ikiwa ni pamoja na kuwapatia vivutio mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara itaendelea kuweka utaratibu mzuri wa kuratibu usambazaji na matumizi ya mbolea kwa kuwasilisha Bungeni Mswada wa Sheria mpya ya Mbolea *(Fertilizer Bill),* sheria hiyo, pamoja na mengine, itafuta Sheria ya Mbolea na Vyakula vya Mifugo *(Fertilizer and Animal Feed Stuffs Ordinance No. 19 of 1962).* Aidha, Wizara inatarajia kuwasilisha Bungeni Mswada wa Sheria ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(Irrigation Bill)* ili kuweka utaratibu unaofaa wa kusimamia na kuratibu kilimo cha umwagiliaji maji mashambani na kuhakikisha kuwa ardhi inayotumika kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani inatumiwa kwa ufanisi mkubwa.

Katika mwaka wa 2004/2005 Wizara imepanga kuwasilisha Miswaada ya kurekebisha Sheria za Kudhibiti Visumbufu vya Mimea *(Plant Protection Act No. 13 of 1997), Tropical Pesticides Research Institutions (TPRI), Act No 18 of 1979* na Sheria ya Usalama wa Chakula *(Food Security Act, No.10 of 1991).*

Aidha, Wizara itaendelea na uandaaji na usimamizi wa utekelezaji wa Kanuni mbalimbali za Sheria za mazao. Wizara itaendelea kushirikiana na Benki ya Dunia kukamilisha uchunguzi wa marekebisho ya majukumu, kazi na miundo ya Bodi za Mazao ili sheria zinazosimamia mazao na taasisi hizo ziweze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara ya kilimo na Chakula itaendelea kukamilisha zoezi la kuwapandisha vyeo watumishi wa wizara na kuingiza kumbukumbu sahihi za watumishi katika mfumo wa kompyuta. Wizara itaandaa na kutoa mafunzo mbalimbali juu ya mabadiliko yanayoendelea katika utumishi wa umma na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa mafunzo ya watumishi ili kuwawezesha watumishi kuwa na ujuzi wa kazi wanazozifanya. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kwa watumishi ya namna ya kujikinga na maambukizo ya UKIMWI na pia masuala ya jinsia katika maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa wabunge kwa michango yao waliyoitoa wakati wakichangia hotuba zilizotangulia, yenye lengo la kuboresha hali ya kilimo chetu na kukifanya cha kisasa, chenye tija na kinachokidhi malengo ya Taifa. Jukumu la kusimamia kilimo ni la viongozi wote kuanzia kijiji hadi Taifa. Tunachopaswa kufanya ni kutambua vikwazo vinavyofanya kilimo kisikue kwa kasi tunayotaka na kubuni mikakati ya kuviondoa ndani ya uwezo wa nchi uliopo. Katika hotuba yake ya mwisho wa mwezi Mei, 2004, Mheshimiwa Rais alitukumbusha kwamba rasilimali tulizonazo ni chache na zisizotosha kugharamia mambo yote ambayo tungependa kufanya. Alitukumbusha kwamba kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Spika, tupunguze muda tunaokaa maofisini na twende vijijini kuwasaidia wananchi kuandaa mipango yao ya kilimo na kuweka utaratibu wa kuitekeleza na kuisimamia. Tukitumia vizuri rasilimali tulizotengewa mwaka huu, tutapiga hatua katika kilimo hata kama hatua hiyo haitakuwa kubwa kama ambavyo tungetaka.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mbunge wa Namtumbo, Katibu Mkuu Bwana Wilfred Ngirwa, Wakuu wa Idara, Taasisi na asasi zilizoko chini ya Wizara, watumishi wote na wadau wa sekta ya kilimo kwa ushirikiano na ushauri wao katika mwaka wa fedha unaoishia June, 2004. Watendaji hawa wameshiriki kikamilifu katika kutekeleza mipango ya kilimo ya mwaka 2003/2004 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000. Aidha, wamechangia katika kuaandaa taarifa mbalimbali ikiwemo taarifa ya utekelezaji ya mwaka 2003/2004 na makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2004/2005, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yanaendelea kuisaidia Wizara ya Kilimo na Chakula katika juhudi za kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo. Nchi hizo ni Dernmark, China, Canada, Finland, India, Ireland, Israel, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Misri,

Ubeligiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Sweden na *European Union. (Makofi)*

Napenda pia kuyashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kama ifuatavyo, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *BADEA, UNDP, FAO, JICA, DFID, EU, UNICEF, WFP, IFAD, CIMMTY, ICRISAT, ASARECA, USAID, GTZ, IITA* na *Sasakawa Global 2000.* Bado tunahitaji misaada na ushirikiano wao ili kuendeleza kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wakulima wa Tanzania kwa kazi kubwa sana wanayoifanya katika kuendeleza kilimo na kutoa mchango mkubwa sana katika upatikanaji wa chakula, malighafi za viwandani, fedha za kigeni na kuinua Pato la Taifa.

Aidha napenda kutoa shukrani za pekee kwa mchango mkubwa unaotolewa na wanawake na wazee waishio vijijini katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na shughuli nyingine za uzalishaji katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, natoa shukrani za pekee wako Mheshimiwa Spika, kwa kuendesha Bunge hili kwa umakini mkubwa sana na kwa MpigaChapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 64,074,053,600 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2004/2005. Kati ya hizo, shilingi 34,976,612,100 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 29,097,441,500 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, shilingi 6,436,433,200 ambayo ni sawa na asilimia 22.12 ni fedha za ndani na shilingi 22,661,008,300 ambayo ni sawa na asilimia 77.88 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Chakula, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, naomba kutoa maelekezo yafuatayo:-

Kwa mujibu wa Kanuni ya 81 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka 2003/2004 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2004/2005. Awali ya yote, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii ambao ni Mheshimiwa

Eliachim Simpasa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Anatory Choya, Mheshimiwa Charles Kagonji , Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Salama Khamis Islam, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Gwassa Sebabili , Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na Mheshimiwa Paulo Makolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo kadhaa, yote yakiwa na lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii muhimu kwa maisha ya Watanzania. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Wizara imeyafanyia kazi maeneo hayo.

Pamoja na utekelezaji huo Kamati yangu iliona kuna umuhimu wa baadhi ya maeneo kuendelea kufanyiwa kazi na tumetoa ushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilijulishwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa fedha uliopita. Baadhi ya mafanikio hayo ni haya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kutekelezwa kwa utafiti wa kilimo katika kanda saba za utafiti zilizo chini ya Wizara hii.

(ii) Kuendesha mafunzo kwa watafiti 36 kutoka kanda hizo kuhusu uchambuzi wa matatizo ya wakulima na namna ya kuyatatua kwa kutumia mbinu shirikishi.

(iii) Vituo vya utafiti kuendelea kuzalisha kwa wingi mbegu mama ambazo zinatumiwa na mashamba ya mbegu kuzalisha mbegu za msingi.

(iv) Kukamilisha kwa ramani za mifumo ya kilimo.

(v) Kuwapatia wakulima mafunzo kutoka katika Vyuo vya Kilimo nchini.

(vi) Kupambana na milipuko ya visumbufu mbalimbali vya mimea na mazao kama vile kweleakwelea, nzige, viwavijeshi na panya.

(vii) Kuendeleza kazi za udhibiti wa magugumaji kwa kusambaza mbawakavu katika Ziwa Victoria na katika mabwawa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara pia ilikumbana na matatizo kadhaa katika utekelezaji wa malengo yake. Kamati yangu ilielezwa kuwa mojawapo ya matatizo hayo ni:-

(i) Ukame uliojitokeza katika maeneo mengi nchini na hivyo kuathiri ufanisi wa uzalishaji wa mazao mashambani na katika vituo vya majaribio.

(ii) Upungufu wa fedha zilizokuwa zinatolewa kwa kila robo mwaka nao umekuwa ni tatizo kwani umesababisha baadhi ya kazi kuchelewa kutekelezwa kulingana na ratiba.

(iii) Ubovu wa miundombinu hususan barabara za vijijini ambao umeathiri usambazaji wa pembejeo na upatikanaji wa masoko ya mazao.

(iv) Ukosefu wa wawekezaji wakubwa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata maelezo ya kina juu ya malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2004/2005 pamoja na kazi zilizopangwa kufanyika. Kamati inaipongeza Wizara kwa mipango yake inayolenga kuboresha kilimo nchini kama ilivyofafanuliwa kwenye taarifa ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia kuongeza tija katika kilimo ni lazima jitihada zilengwe kwa wakulima wadogo wadogo, kwani mafanikio yatakayoyapatikana yatasaidia kuondoa matatizo ya njaa kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa.

Hata hivyo, Kamati inaamini hapa nchini bado wakulima wadogo wadogo hawajajengewa mazingira ya kuboresha kilimo chao. Bado wanatumia jembe la mkono, bado hawapati kwa uhakika pembejeo, zana za kisasa za kilimo wala huduma za ugani. Kamati inashauri Wizara iongeze jitihada katika kuboresha huduma kwa wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, asilimia 50 ya Pato la Taifa inatokana na kilimo. Aidha, asilimia 70 ya fedha za kigeni zinatokana na kilimo na karibu asilimia 70 ya ajira nchini inatokana na kilimo hicho hicho ambacho pia kinategemewa na zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wote wa vijijini. Hata hivyo, inaonekana mkazo bado haujawekwa katika bajeti kulingana na umuhimu wa mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Taifa. Kamati inashauri msisitizo uwekwe katika kilimo kwani ndiyo msingi wa kuweza kuleta mabadiliko hapa nchini. Tunashauri kilimo kitengewe shilingi bilioni moja kutokana na makusanyo ya kila mwezi ya *TRA* ili kipate kuendelezwa kama Serikali inavyotoa kwa Wizara ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 70 ya wakulima wanatumia jembe la mkono, asilimia 20 wanatumia wanyamakazi na ni asilimia 10 tu ndio wanaotumia matrekta. Aidha, asilimia 70 ya wakulima ni wanawake na wazee na kufanya asilimia inayobaki tu kuwa ndiyo vijana. Hii inaonyesha wazi kuwa ni vijana wachache sana ndiyo wanaojihusisha na kilimo. Sababu zaweza kuwa nyingi lakini cha msingi yawezekana vijana hawajihusishi na kilimo kutokana na uduni wa teknolojia ambao unasababisha mtu kutumia nguvu nyingi na muda mrefu zaidi ya faida inayopatikana.

Kamati yangu inashauri kuwa Serikali ihakikishe kunakuwepo na mipango thabiti ya kuendeleza kilimo kitaalam kulingana na mabadiliko yanayotokea duniani hasa ya sayansi na teknolojia na kuwezesha uwezo wa kushindana katika soko la dunia ili pamoja na faida nyingine vijana wavutike kujihusisha na kilimo badala ya kukaa tu siku nzima bila shughuli yoyote ya kuwaongezea kipato. Ushauri huu utafanikiwa sana iwapo Serikali itajenga miundombinu ya kilimo itakayowavutia wazee wastaafu na vijana waliohitimu masomo ya Vyuo Vikuu pamoja na wale vijana waliojiajiri mijini na vijijini. Kamati pia inaamini utekelezaji wa ushauri huu utapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la ajira na njaa.

Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha kilimo cha kisasa, Kamati inashauri kuwe na mikakati maalum ya kuhakikisha upatikanaji wa matrekta kwa Mikoa yote nchini. Utaratibu uliotumika Mkoani Ruvuma usambazwe nchi nzima. Kamati iliarifiwa kuwa katika kuendeleza matumizi ya zana bora, Dayosisi ya Songea ilipatiwa mkopo wa kununua matrekta matano na zana zake kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kukodisha matrekta kwa wakulima Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mikoa ya Kusini hawaridhiki na kitendo cha Serikali kuzuia kilimo cha pamba katika Mikoa hiyo. Kumekuwepo na madai kuwa kilimo hicho kimepigwa marufuku kutokana na kuwepo kwa mdudu anayeweza kuleta madhara. Hata hivyo hakuna uhakika kama utafiti kuhusu suala hili umefanyika. *(Makofi)*

Kamati yangu inashauri kilimo cha pamba kiruhusiwe katika Mikoa ya kusini. Serikali itafute utaratibu wa kuhakikisha wananchi hao wanapatiwa nyenzo na utaalamu wa kuendesha kilimo hicho. Aidha, Wizara iwasiliane na nchi wanachama wa *SADC* kama vile Msumbiji na Malawi ambao wanalima pamba kwa mafanikio makubwa ili kuelewa wao wanatumia mbinu gani kukabiliana na mdudu huyo. Wakati mawasiliano haya yanaendelea, wananchi wa Mikoa ya Kusini waruhusiwe kuendelea na kilimo cha pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo bado kilimo cha umwagiliaji hakijapewa mkazo unaostahili hasa ikizingatiwa kuwa umwagiliaji unaolengwa na Wizara ni ule wa vipindi vya mvua za vuli au masika wakati ambapo maji yanakuwepo kwa wingi na mtu hahitaji kumwagilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati haielewi ni kwa vipi nchi kama Tanzania yenye utajiri wa vyanzo vya maji inashindwa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji na matokeo yake kila mara majanga ya njaa hayaishi na Serikali inatumia fedha nyingi kwenda kununua chakula katika nchi ambazo katika hali ya kawaida tunao uwezo wa kuzilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo Kamati inashauri umwagiliaji utiliwe mkazo hasa katika mabonde yaliyotengwa kama vile Bonde la Mto Pangani, Rufiji, Ruaha, Lukuledi, Ruvu, Kagera, Wami, Malagarasi, Kilombero na kadhalika. Pia kwa kujenga mabwawa na kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kuhusu kutokuwepo kwa viwanda vya usindikaji hali inayosababisha upotevu mkubwa wa mazao kwa kuharibika. Ni ukweli kuwa Serikali imejitoa katika biashara, lakini hata hivyo Kamati inaamini kuwa si busara wala haki wakulima wakaachwa bila kusaidiwa na nguvu zao zipotee bure kwa kigezo tu kuwa biashara sasa ni huria

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali itafute mkakati maalum wa kuwasaidia wakulima hawa ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu muhimu na kupitia upya sera zake ili kuvutia wawekezaji wa kweli hasa kutoka katika nchi zenye uzoefu katika sekta hii kama vile China ili waje waingie katika maeneo ambayo hayana wawekezaji lakini yana wingi wa mazao. Hii itasaidia kuboresha hali za watu na kuongeza pato la Taifa. Kwa upande mwingine Kamati inashauri wasindikaji wakubwa wanaokuja nchini wasihodhi soko hilo na kuwaumiza wale wadogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imearifiwa kwamba Serikali imepanga kuzipatia Wilaya zetu shilingi bilioni nne ili zitumike kwa ajili ya kuendeleza kilimo. Ili Waheshimiwa Wabunge waweze kushiriki katika kufanikisha utekelezaji wa mipango iliyolengwa pamoja na ufuatiliaji, Kamati inashauri ufafanuzi utolewe juu ya namna fedha hizo zilivyopangwa kutumika katika kila Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya chakula, wakati Serikali inaagiza chakula kutoka nje ya nchi hapa nchini wakulima katika baadhi ya Mikoa kama vile Rukwa bado walikuwa na akiba ya chakula majumbani kwao. Kamati imeelezwa kwamba mojawapo ya sababu iliyosababisha chakula kiagizwe kutoka nje ni gharama kubwa ya kutoa chakula kutoka katika Mkoa mmoja hadi mwingine hapa nchini ukilinganisha na kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kusingekuwa na haja ya kuagiza chakula kutoka nje ya nchi kama Wizara ingekuwa makini katika kutafuta takwimu sahihi za mahitaji ya chakula kwa nchi nzima. Iwapo hali ya msimu inaonyesha kutakuwa na upungufu wa chakula, basi wakati wa mavuno chakula kinunuliwe kwa wingi kutoka kwa wakulima hapa hapa nchini na kuhifadhiwa. *(Makofi)*

Aidha, inapobidi chakula cha ziada kununuliwa, Serikali ihakikishe wakulima wenye akiba ya chakula hapa nchini wanapata nafasi ya kukiuza kwanza kabla ya kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa Serikali ianzishe Benki ya kuhudumia wavuvi, wakulima na wafugaji. Benki hii ni njia mojawapo ambayo ingesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha shughuli za makundi haya kuwa za kisasa zaidi na kuongeza kipato. Kamati inashauri uzoefu uliopatikana katika Mfuko wa Pembejeo utumike katika kuanzisha na kufanikisha Benki ya wakulima, wavuvi na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba mazao mengi ya biashara yana Bodi ambazo pamoja na mambo mengine zinasaidia katika mipango ya kilimo husika, kwa

mfano masoko na kadhalika. Hata hivyo mazao ya nafaka ambayo ndiyo yanayolimwa kwa wingi nchini bado hayajaundiwa bodi. Kamati inaamini kuwa kuwepo kwa bodi za mazao ni muhimu sana katika kuongeza ubora wa mazao husika. Hii imeonekana kwa mazao mbalimbali yenye bodi kama vile tumbaku, pareto, pamba na sukari. Hivyo tunashauri sasa mkazo uwekwe katika kuanzisha bodi kwa mazao ya nafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua wazo la Serikali la kuanzisha wakala wa mbegu. Hata hivyo tunashauri wakala huyo afanye kazi chini ya maelekezo na usimamizi wa Wizara kwa manufaa ya wakulima nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utafiti Kamati inashauri jitihada zifanyike katika kukarabati vituo vyenye hali mbaya kama kile cha Mlingano, pamoja na kuvipatia vifaa muhimu vya kufanyia kazi. Aidha, utafiti unaofanyika na matokeo yake viwafikie wakulima.

Mheshimiwa Spika, katika ziara mbalimbali za Kamati tumeshuhudia jitihada zinazofanywa na wakulima wadogo wadogo kwa mazao ya chakula na biashara kama vile miwa, chai, mkonge, matunda na kadhalika. Hata hivyo jitihada hizi zinakwamishwa na miundombinu hafifu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo na mafanikio ya kuridhisha katika sekta ya elimu kupitia mpango wa MMEM na MMES, Kamati inashauri Wizara ya Kilimo na Chakula ibuni Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Kilimo (MTAMAKI). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imearifiwa kwamba mashirika ya wahisani yanayotoa misaada kwa Wizara ya Kilimo na Chakula yamepangwa katika kanda. Kamati inapongeza mpango huo. Aidha, tunashauri mashirika hayo yawajibike chini ya Wizara. Kanda hizo ziwe na Bodi chini ya Wakuu wa Mikoa kama ilivyo kwa *TANROADS.*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumshukuru sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Charles Keenja, Naibu Waziri, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa kwenye Kamati. Tunawapongeza kwa jinsi walivyoweza kufafanua hoja mbalimbali zilizotolewa na Wajumbe wa Kamati yangu. Aidha, nawapongeza wataalam wote wa Wizara kwa jinsi walivyoshiriki katika kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa napenda kuishukuru Ofisi yako ikiongozwa na Katibu wa Bunge Ndugu Kipenka Msemembo Mussa na wasaidizi wake hasa Makatibu wa Kamati hii, Bi. Nenelwa Mwihambi na Ndugu Abdallah Hancha, kwa kuihudumia vyema Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu iliombwa iidhinishe shilingi 64,074,053,600/= ambapo shilingi 34,976,612,100/= ni za Matumizi ya Kawaida na shilingi 29,097,441,500/= kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(b)(c), Toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitoe pole kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua umuhimu wa Wizara hii ya Kilimo na Chakula kwa sababu ndio msimamizi Mkuu wa Sekta ya Kilimo ambayo kwa miaka yote imekuwa kinara katika uchangiaji wa Pato la Taifa. Wakulima wadogo wadogo ndio ngao ya Taifa. Kwa kipindi cha miaka takriban 10 na mpaka leo mchango wa Kilimo ni zaidi ya asilimia 48 kwa majumuisho yote ya Pato la Taifa *(G.D.P).* Zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wamejiajiri kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, Mpango na Dira ya Taifa ya 2025 kuondoa umaskini inaweza kufanikiwa tu, kama Serikali itarekebisha sera zake za matumizi ya kiutawala na kuingiza kwenye sekta hii yenye asilimia kubwa ya Wachangiaji wa Uchumi. Kwani sekta hii ndipo kwenye uwanja wa vita kati ya umaskini na utajiri na tutashinda tu kama uwajibikaji na sera zenye mwelekeo wa kumjali mkulima zitakapotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, hii inatokana na sababu nyingi, mojawapo ni pale wakulima wanapojitahidi kuzalisha lakini wakakosa soko la uhakika la mazao yao na sio hilo tu bali hupata hasara kubwa kwenye kuvuna *(Post harvest loss)* pia kwenye uhifadhi wa mazao yao, kitu kinachosababisha kukosa bei nzuri kwenye soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali yafuatayo:-

(a) Kuhusu *Strategic Grain Reserve* kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya *SGR* ili waweze kununua chakula cha kutosha kwa kipindi kisichopungua miezi sita:

(b) Kutunga sheria itakayohakikisha kuwa *SGR* inatunza chakula kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje na kuuza kwa bei isiyo na riba. Mfano, kama mavuno ya mwaka unaofuata yanaonyesha yatakuwa mazuri, basi nafaka zilizohifadhiwa *SGR* ziuzwe ndani au nje ya nchi kufuatana na soko.

(c) Kwa chakula kitakachouzwa ndani ya nchi toka *SGR* kiuzwe kwa bei ya kununulia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upotevu wa mazao baada ya uvunaji, kwa kuwa inafahamika kuwa zaidi ya 40% ya mavuno hupotea mashambani wakati wa kuvuna na kuhifadhi, ambavyo hutokana na utaalam duni wa wakulima, Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

(a) Katika kila Kijiji itolewe semina kila msimu wa kuvuna unapokaribia juu ya namna bora ya kuvuna na kutunza nafaka ili zisiharibiwe na wadudu au uharibifu wa aina nyingine yoyote.

(b) Utaalam unaoweza kutumika katika mazingira husika ya mazao husika.

(c) Maafisa ugani, kuhakikisha na kuwafundisha wanakaya namna ya kutunza vizuri akiba ya chakula.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kuhakikisha, inawapa ruzuku wakulima ili waweze kupata motisha ya kuzalisha zaidi, hii itaongeza tija na kuwafanya vijana wapende shughuli za kilimo. Tumepokea kutoka *World Bank* na *IMF* ushauri kwamba kama nchi inataka kuwa na *sustainable development,* basi nchi hizo lazima ziondoe ruzuku kwa mazao ya kilimo. Wazo hili ni baya kama Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini ruzuku iondolewe kwa wakulima wa dunia ya tatu tu mbona Amerika na *Eupean Union* pamoja na Japan ambao ni marafiki zetu wanaendelea kutoa ruzuku zaidi ya asilimia 50 kwa wakulima wao?

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa inayowafanya watoe ruzuku kwa wakulima wao ni kama ifuatavyo:-

(a) Gharama za uzalishaji kwa wakulima wao zinapungua na hivyo bei ya mazao yao kwenye soko inakuwa *Competitive.*

(b) Hivyo wanaweza kupanua soko la bidhaa zao kwenda kwenye nchi ambazo uzalishaji wa mazao hauna ruzuku! Kwa hiyo, wanaifanya kwenye nchi maskini ambazo hazitoi ruzuku. Usishangae ukienda *Shoprite* utakutana na nyanya ya *New Zealand, South Africa,* Australia na kadhalika inauzwa kwa bei ndogo kuliko inayotoka Dabaga.

Namnukuu Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, alisema kuwa: "Mwenye *Shoprite* anaona ni afadhali kununua bidhaa kutoka nje kuliko hapa nchini kwa sababu vya nje vinauzwa kwa bei ndogo kuliko vya ndani."

Haya hata Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala anayajua kama alivyosema katika moja ya hotuba zake kwenye kikao cha *NEPAD* na hapa nanukuu: "...*Because of these subsidies, (Shoprite a supermarket in Tanzania), will find it easier to import something than buy it locally. This is because Tanzanian farmers find it very difficult to compete with western farmers because their production costs are much lower."* Mwisho wa kunukuu.

Kama hili tunalifahamu na kwamba *first world* ndiyo wanaolisimamia, kwanini dunia ya tatu kwa kupitia *Regional Organization* kama *NEPAD, SADC ECOWAS, COMESA* na kadhalika tusiwe na sauti moja kukataa wazo hili la kutotoa ruzuku kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo mmoja kati ya Makamishna wa *United Nations* alisema: *"...However, others, including Dr. K.Y. Amoaka, the Head of the UN's Economic Commission for Africa, believes there is a need for a more collective voice and through regional organizations such as the New Partnership of African Development (NEPAD), change can be brought about. It comes to our capacity to negotiate International agreements. African countries have not been able to negotiate, but if we pool together and do our homework, this can change, "he said during a visit to Tanzania."* Mwisho wa kunukuu. Hapa tunao viongozi wa Afrika wakikaa pamoja na kutoa sauti moja kuhusu ruzuku Mataifa makubwa yatasikia. Wazo hili halijakubalika kwa viongozi wengi na wengi wamekata tamaa kama Profesa Pius Mbawala, alivyodhihirisha hapa.

Lakini Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala anaamini hivi na hapa nanukuu: *"It is not so easy faced with the economic powers of the US and European Union, he says that developing Nations like Tanzania are in a difficult position to call for change in agricultural policy and when they do, are told not to interfere."* Hii ni kauli ya kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, ruzuku iliyotolewa kwa mbolea kwa Mikoa ya Kusini, haitaisaidia wakulima wote wa nchi hii. Kwamba ruzuku ni kwa zao moja tu la chakula (mahindi).

Kambi ya Upinzani inashauri ruzuku kama hiyo itolewe kwa wakulima nchi nzima na kwa mazao yote. Dodoma, Babati, Kiteto, Kilimanjaro na kadhalika wanalima sana mahindi na maharage kwanini wasipate ruzuku? Pamba inalimwa na watu zaidi ya milioni tano hapa nchini kwanini nao wasipate ruzuku? Kahawa huko Moshi, Kagera, Mara, Mbinga na kadhalika kwanini wasipewe nao ruzuku. Kwani hawa hulima mazao yanayoliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali isaidie uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo katika maeneo husika ili kuongeza bei ya mazao ya wakulima *(added value)* na pia kutoa ajira kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali isaidie kuanzisha na kuimarisha masoko ya ndani ya nchi, ndani ya Kanda za kiushirikiano na kiuchumi kama *PTA, COMESA, SADC* na nchi nyingine katika Afrika. Ndiyo maana tunasema kuwa, it is illogical kujitoa kwenye *COMESA* kwani pia tunapata hasara kubwa kibiashara. Kambi ya Upinzani inashauri turudi kwenye *COMESA*.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais akiongea na viongozi wakuu wa nchi za *SADC* alitoa ushauri mzuri kuwa katika bajeti za kila nchi asilimia kumi ya bajeti

itengwe kwa kilimo. Je, hapa Tanzania Wizara ya Kilimo na chakula imetekeleza kwa kiasi gani agizo hilo? Kama Wizara ya Fedha haikutekeleza ushauri huo ni kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali halisi ya kilimo nchini na ukuaji wake imebaki ya kusuasua tu kwa kipindi kirefu, ukuaji wake toka mwaka 1993 mpaka 2003 umekuwa kwa wastani wa chini ya asilimia nne kwa mwaka. Kama tutazingatia ushauri na kuwekeza zaidi kwenye kilimo kwa maana ya kuongeza miundombinu ya kilimo, kutoa mafunzo na ushauri kwa wakulima kutoa motisha kwa wataalam wa kilimo, kuimarisha masoko ya mazao ya kilimo na pembejeo. Kwa njia hii ya ruzuku, uzalishaji wa mazao utapanda na hivyo sekta ya kilimo itakuwa na maana halisi katika Dira ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kama ambavyo tumeshuhudia bajeti zilizopita, bajeti hii vile vile imejaa maneno mengi matamu, yenye malengo mengi yasiyotekelezeka kama inavyokuwa miaka ya nyuma. Mathalani, mwaka wa fedha 2003/2004, kwa mbwembwe zote Waziri wa Fedha alitangaza kutenga fedha kwa ajili ya mpango wa zao la Biashara na Chakula kwa kila Wilaya. Tujiulize ni Wilaya ngapi zimepata fedha hizo? Mbona Waziri haongelei tena mafanikio ya mpango huo wa mwaka jana kabla ya kuendelea na huu anaouzungumzia? Tupate maelezo ya mafanikio.

Mheshimiwa Spika, mpango wa pembejeo (mbolea) ulioahidiwa kwa Mikoa ya Nyanda za juu Kusini matokeo yake yalikuwaje? Tunahitaji maelezo. Mbona Serikali inapata kigugumizi kwa ahadi zilizopita na inakuwa nyepesi kutoa maneno matamu mapya?

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji Benki ya Wakulima na Mikopo yenye unafuu wa riba kwa wafanyabiashara wadogo ni dhana ya kufikirika tu, Idealism kwani kutekelezeka hakuonyeshi njia.

Mheshimiwa Spika, mipango yetu katika kilimo bado haiko sawa na nchi yetu itaendelea kupata tatizo la njaa mwaka hadi mwaka. Hata hizo pesa kidogo zilizotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo maadam hakuonekani mkakati madhubuti wa usimamizi, impact yake kwa mkulima wa kawaida haitaonekana na sana sana zitaishia kwenye urasimu.

Mheshimiwa Spika, mkakati wetu wa kilimo bado haujajikita kwenye mahitaji au matakwa halisi ya wakulima wetu wa hali ya chini, ambao ni wengi. Pia tunataka kujua kuhusu wizi wa fedha zaidi ya milioni 80 zilizoibiwa Makao Makuu ya Wizara hii. Hatujapata taarifa yake imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, tunashauri kwamba Serikali ianze kuweka mfumo shirikishi ambapo wakulima kwa kila ngazi na kwa kila mazingira yao husika wasaidiane na wataalam kuainisha mahitaji yao halisi yanayozingatia fursa waliyonayo na vizingiti vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia lengo la kisekta kukua kwa hii sekta ya kilimo na kupunguza kama si kuondokana na umaskini uliokithiri, yafuatayo ni muhimu kuangaliwa na kufanyiwa kazi:-

(a) Kilimo cha Umwagiliaji maji; na

(b) Kuwe na Wizara pekee ya Umwagiliaji *(Irrigation Ministry),* nilisisitiza kwa kurudia mara mbili. Badala ya kila mwaka Waziri kulijulisha Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali itatilia mkazo kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, tulitegemea angalau kwa mwaka huu wa Bajeti ya Serikali itaje ongezeko la kasma ya *Sub-vote 2002,* inayohusu umwagiliaji na *(technical service)* iongezeke badala yake imepungua kwa kulinganisha na kasma iliyotolewa katika Bajeti ya 2004/2005. Kwa mfano, maeneo ya *River Basin Management Smallholder* imetengewa shilingi 250,000,000/= mwaka huu ukilinganisha na shilingi 300,000,000/= mwaka 2003/2004.

*Participatory Irrigation Development Programme* Bajeti ya 2003/2004, ilitengewa jumla shilingi 4,632,704,550/= wakati katika Bajeti ya sasa 2004/2005, imetengewa jumla ya shilingi 3,803,300,000/=. Kuna tofauti ya shilingi 829,404,550/= ambazo zimepunguzwa katika Bajeti ya mwaka huu. Hayo yote yamo kwenye Makadirio ya fedha za Serikali, mipango ya maendeleo. Kwa uangalizi wa haraka, bajeti hiyo inaonyesha namna gani Serikali haijalielewa somo la Kilimo cha Umwagiliaji ambapo ingeweza kuinua uzalishaji wa mazao ya kilimo na hivyo kupunguza ufukara na dhiki vilivyokithiri miongoni mwa jamii kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa kwa nchi kama yetu yenye utajiri wa mito mikubwa isiyokauka kwa kipindi chote cha mwaka, wananchi wake kufikia hatua ya kula mizizi pori na wengine kufariki. Kwa hili tunashindwa kuelewa kabisa uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi wake, aibu kubwa ni kupima maendeleo na mafanikio kwa kuangalia wakazi wa Mijini tu hasa Dar es Salaam, Arusha na Mwanza. Tupime maendeleo kwa kuangalia maisha halisi ya wakazi wa Vijijini na huko ndiko Watanzania halisi waliko tujenge miundombinu Vijijini na kugawa mashamba yote yanayofaa kwa kilimo kwa wenye uwezo.

Mheshimiwa Spika, kwa mlinganisho wa Kasma ya *Research Development* kwa Bajeti ya 2003/2004 na 2004/2005 ni kuwa Bajeti hii kuna upungufu wa shilingi 1,732,518,631/=. Hii inatupa wasiwasi mkubwa kuwa hata misaada toka kwa nchi wahisani inashindwa kufanya kazi iliyokusudiwa kutokana na kupewa taarifa za mipango ambazo hazikufanyiwa utafiti, kama vile aina ya udongo, kitu ambacho ni muhimu iwe kwa kilimo cha umwagiliaji, aina ya mazao na uwezo wa mashine zitakazotumika katika eneo husika. Mfano, ni ule mradi wa Bonde la Ifakara kati ya Tanzania na Korea *(KOTACO),* Mradi haukufanyiwa utafiti kwa ujumla na matokeo yake umekufa. Nadhani Waziri anaweza kulielezea vizuri Bunge lako tukufu ni kwanini mradi haukufikisha malengo kama ilivyotarajiwa wakati unaanzishwa pamoja na *Lower Moshi Irrigation Scheme,* bado pia haujafikia malengo yake. Tunataka maelezo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo linaonekana ni tabia ya kutoheshimu na kuthamini ushauri wa kitaalum *(Professional Abuse)* na hii sio tu kwenye Sekta ya Kilimo ila ni katika Sekta nyingi nadhani Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga katika mchango wake aligusia hilo. Wataalam walio kwenye *Extension Offices* hawashirikishwi vizuri kwenye *demonstration field* ya *reseach* hii ni makosa na ikitokea dosari wanakuwa hawaelewi! Jambo ambalo ni hatari.

Mheshimiwa Spika, tuangalie mbegu bora ili bidhaa zetu ziwe bora! Mfano, Zabibu za Misri ni tofauti na Zabibu za Dodoma au pamba ya Misri ni tofauti na ya Shinyanga. Yao ni nzuri zaidi, *why?*

Kutokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, inaonyesha kuwa mashamba ya mbegu ya Dabaga, Msimba, Mude na Arusha yamepata hasara ya shilingi 17,433,777/= inayotokana na uendeshaji katika mashamba hayo. Kambi ya Upinzani haioni mikakati yoyote ambayo inafanywa na Wizara pamoja na Serikali ili mashamba hayo yaondokane na kutengeneza hasara ya kila mwaka, kitu kinachosababisha upungufu mkubwa wa mbegu bora kwa wakulima, ukizingatia kuwa mbegu zinazouzwa na Makampuni ya Kigeni ni Ghali ukilinganisha na zile ambazo zilikuwa zinazalishwa na kuuzwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, utendaji mzuri kwenye mashamba haya ya mbegu ni muhimu sana. Hivyo katika kasma ya Wizara ya Matumizi ya Maendeleo, mashamba haya yafikiriwe! Ufuatiliaji wa karibu ni muhimu kwani watendaji wake hujisahau na kuona kama mashamba na miradi na ni mali yao binafsi. *Report* anazoletewa Waziri huwa ni tofauti na hali halisi ilivyo. Mkakati mzuri wa kuyafanya yafanye faida badala ya hasara ni muhimu sana. Serikali ichunguze hili.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhakiki uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kwenye miradi iliyo chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula, juu ya uendeshaji na uwajibikaji kwa fedha za wafadhili, ilionekana kuwa miradi inaendeshwa kwa kasi ndogo kwani kati ya *USD* 12,680,130 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo ni kiasi cha *USD* 5,897,922 zilizokuwa zimetumika ambazo ni sawa na 47% ya Bajeti nzima. Mradi huu wa *Smallholder Irrigation Improvement Project.* Ulishindwa kutekelezeka kama ilivyotarajiwa kwa muda uliopangiwa, kwani fedha za kumalizia zilikosekana. Sasa hapo unakuta *contradiction* mara fedha zinabaki mara fedha za kumalizia zinakuwa hazipo. Kwa hiyo, kunakuwa na urasimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Sekta hii ya Kilimo katika maendeleo ya nchi yetu, ukiangalia takwimu za Wafadhili, Wizara ya Kilimo inaongoza kwa kuwa na miradi mingi ya wafadhili, lakini cha kushangaza na pia kuwakatisha tamaa ni kwamba udhibiti na upangaji wa Miradi mingi haifanyiwi *feasibility study* ya kutosha ila watu wanaandika kuwashawishi tu wafadhili ili walete misaada. Matokeo yake ni Miradi kushindwa kukamilika na kutowanufaisha walengwa na Taifa kwa ujumla.

Mwishowe hata Wahisani watachoka kwani ni kama wanamwaga maji kwenye gunia na kuvuja tu, maana kuna wachache wanatumia mwanya huo wa kufilisi Miradi. Kama taarifa ya *Auditor General* inavyojieleza.

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha kusikitisha sana kuona mpaka sasa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo una wadeni sugu kiasi cha Sh. 4,432,232,000/=. Na hawa sio kama taarifa zao hazipo na sio wakulima walalahoi ni watu wenye uwezo lakini wanaachwa tu, tunataka taarifa zao. Sasa hatuoni kama Serikali iko makini kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inamshauri Waziri, kuwa atengeneze sheria ya kulazimisha benki ya wakulima kuajiri *Extension Officers"* wa kilimo ili waweze kuwaelekeza na kufuatilia vizuri mikopo ya wakulima na kilimo bora. Tunaamini kabisa sheria hii ikitungwa na kufanya kazi haraka, mfuko huu utajiendesha na faida yake itaonekana kwa mkulima wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, nilijifunza mengi nilipokwenda Misri. Katika Safari ya Misri tumejifunza mengi yanayohusiana na Kilimo, pia tumejifunza kuhusu namna bora ya matumizi ya maji kwani pamoja na Misri kuwa jangwa lakini kwa kutumia maji kidogo waliyonayo wameweza kulima hadi kuuza mazao mbalimbali yakiwemo na matunda nchi za nje ikiwa ni pamoja na Uingereza. Sisi hapa Tanzania tuna mito mingi lakini tunashindwa utaalam wa kuyachota hayo maji na kuyaweka ardhini kwa nia ya uzalishaji na kukuza uchumi. Jambo lingine ni kwamba Misri wanafundisha Watanzania zaidi ya 280 kuhusu mambo ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kumhoji Waziri wa Kilimo wa Misri ambaye pia ni Naibu Waziri Mkuu kuhusu kuanzisha Chuo kama hicho kilichopo huko Misri cha Umwagiliaji hapa Tanzania, jambo ambalo alikubaliana nami kwamba Misri wako tayari kufanya *demonstration* ya vyuo vya aina hiyo hapa kwetu Tanzania, sisi tunampongeza kwa kukubali ili hiyo elimu iwe karibu na wananchi hivyo naamini tutafaidika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Misri wanafaulisha Chuo Kikuu wanafunzi 700,000 *Graduates* kila mwaka wakati sisi tunafaulisha 700,000 Shule ya Msingi na 3,000 Chuo Kikuu. Jambo kubwa hapa ni kwamba tuko nyuma sana hivyo tuongeze bidii na kuhakikisha kuwa tunaowafaulisha wametumika ipasavyo kama vile kuwakopesha ardhi ya kulima na kumwagilia na kuwalipa mishahara kama wanavyofanya huko Misri. Misri wanasema hivi: "Hakuna Nile hakuna Misri. Hakuna Nile hakuna Maendeleo." Hivyo sisi tuige hiyo! Hakuna umwagiliaji mashamba hakuna maendeleo wala hakuna Tanzania. Tunaomba Serikali iachane na mawazo ya zamani juu ya kilimo, ijenge mikakati mipya na sera mpya za kilimo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu hoja niliyowahi kuitoa hapa Bungeni juu ya madawa ya Kahawa aina ya *Pyrinex* yaliyoharibu Kahawa na wakulima kupata hasara kubwa, jambo ambalo Serikali ilithibitisha kuwa madawa hayo yalikuwa kweli hayafai na kuyapiga marufuku. Wakulima wa Kahawa wanataka fidia kwa hilo. Tunaomba majibu yake hapa. Pia

tupate maelezo ya kina ni kwa nini mafungu mengine ya fedha za kilimo zinawekwa Ofisi ya Waziri Mkuu badala ya kuachwa moja kwa moja kwenye Wizara hii ya Kilimo? Pia tunataka maelezo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba hii muhimu ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijasema chochote nipende kutoa utangulizi wa kutoa salamu za rambirambi kwa mwenzetu aliyetangulia mbele za haki, mwenzetu aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini marehemu Yete Mwalyego. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, la pili, nipende kutoa salaam kwa wananchi wa Jimbo la Baridia kwa kutuletea Mbunge mpya kupitia Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Danhi Makanga. Mimi namhakikishia Mheshimiwa Danhi Makanga pamoja na wananchi wa Bariadi kwamba wamechagua chaguo sahihi hivyo wategemee kuwa na maendeleo zaidi katika Jimbo la Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula nimeisoma vizuri na kwa kweli nimemsikiliza wakati akiisoma hotuba yake, lakini mimi nilikuwa napenda kujielekeza katika pande tatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kilimo kama kilimo ni ajira kwa wananchi wote na sisi wote hapa ni wakulima ambao tunategemea kilimo cha wakulima hao wadogo wadogo. Misimu hii miwili 2003/2004 na msimu huu wa sasa imeelekea kuwa ni misimu ambayo haikuwa na mvua za kuridhisha. Lakini nisiwe mnyimifu wa fadhila nipende kuishukuru Serikali kwa juhudi ambayo ilifanya kuwapatia chakula wananchi wa Mikoa mbalimbali wakiwemo na wananchi wa Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile hali ya mwaka huu siyo mzuri. Katika Wilaya yangu ya Nzega nina Tarafa nne. Katika Tarafa hizo nne, mbili zimeweza kuvuna vizuri lakini Tarafa mbili hazikuweza kuvuna vizuri hivyo kutakuwa na upungufu wa chakula na kwa kawaida yetu sisi Kanda ya Ziwa huwa hatuna kawaida ya kuomba chakula lakini katika hili napenda kutuma maombi ya kuomba chakula kwa Mikoa hiyo ya Kanda ya Ziwa siyo Nzega tu lakini ni pamoja na Mkoa wa Shinyanga, Wilaya za Kishapu na Kanda yote ambayo inazunguka Ziwa Victoria kwa kweli hazikupata mvua vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii kama alivyokuwa amezungumza mwanzoni Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba Serikali imedhamiria kutoa ruzuku kwenye mbolea. Napenda kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa sababu kama hatutatumia mbolea kama tutalima tu bila kutumia mbolea na mbegu bora kwa kweli kilimo tukubali

tukatae tutakuwa tunajidanganya kwa sababu ardhi imeishachoka tunahitaji kutumia mbolea.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo mengi ya kujifunza juu ya suala hili la mbolea. Suala la mbolea linaonekana kama ni mtego wa mtaji wa baadhi ya wafanyabiashara wachache kujinufaisha kwa gharama ya wakulima wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nakupongeza kwa kuanzisha Kitengo cha Utafiti hapa kwenye Bunge lako na juzi tu nilikuwa naangalia kwenye Internet nikaulizia bei ya mbolea kule Dubai, bei wanayonunua Dubai wananunua kwa shilingi 8, 000 kwa mfuko wa kilo 50. Sasa ukiweka gharama ya usafirishaji na bandari na hivi weka shilingi 2,000 jumla yake inakuwa ni shilingi 10,000/=. Ajabu inayokuja inatokea namna gani kutoka pale Bandarini kwenda kwa wakulima wenyewe bei inapanda mara mbili wakati kodi imefutwa kwenye mbolea. Hamuoni huu ni ujanja wa wafanyabiashara kumnyonya mkulima! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yetu bei ya mbolea inafika mpaka shilingi 25,000 kwa mfuko mmoja. Lakini huyu mfanyabiashara kanunua mfuko kwa shilingi 10,000 gharama yake yote ukiweka ya usafirishaji kwenye treni ungeweka hata shilingi 2,000 zingine labda ingekuwa angalau 12,000 au shilingi 13,000 ambapo kama mkulima angekuwa ananunua kwa bei ya namna hiyo wakulima wengi wangeweza kununua na wakulima wengi wangeweza kutumia mbolea katika mashamba yao, kuliko sasa hivi mkulima inabidi auze magunia mawili ya mahindi au matatu ili kuweza kununua mfuko mmoja wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, jambo hili kwa kweli kama hatukuliangalia pamoja na sera nzuri ya Serikali ya kujiondoa katika kusimamia masoko mbalimbali na kufanya biashara huria, lakini katika hili naomba Serikali ilisimamie ili iweze kupanga hata bei ya mbolea kwa sababu inamuumiza mkulima. Mimi naamini hii faida inayokwenda kwa wafanyabiashara pengine inawanufaisha wao zaidi kwa sababu wafanyabiashara hao wakubwa wa mbolea wala siyo Watanzania wanafanya mambo mengine ambayo hayana manufaa kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi kuhusu hili kwa kweli nilikuwa napenda kabisa Serikali ijiingize kwa hali na mali kuhakikisha bei ya mbolea inashuka na mbolea inaweza kununuliwa kwa sababu kama wakulima wanaweza kuinunua kwa bei rahisi itasaidia hata kufanya mazao yawe mengi, itasaidia hata wakulima wengi waweze kutumia mbolea na hili kama Serikali haijakubali kwa kweli sisi kama Wabunge tunatoa kilio cha wananchi wetu ambao wametuchagua kwamba pamoja na kuondoa kodi basi ihakikishe hata zile gharama za usafirishaji ziweze kuingiliwa na Serikali ili bei iweze kuwa nzuri ambayo itawafanya wakulima wanunue mbolea kwa wingi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nilikuwa nataka nizungumzie katika hilo kwa sababu kama utalima kwa kutumia mbolea lakini bado hujatumia mbegu bora

matokeo yake mazao ni hafifu. Kwa hiyo katika hili juzi nilitoa wazo la kumwomba Mheshimiwa Waziri aweze kulielezea Bunge kama ni kweli Serikali imeondoa kodi kwenye mbegu na tunapozungumza mbegu ni zile mbegu ambazo zinastahimili na zimefanyiwa utafiti na wataalamu wa kilimo. Mbegu za mahindi, mbegu za mtama na mbegu za mihogo. Mbegu za Mahindi kama *Cagri* zina bei kubwa sana kwa mfuko mmoja wa kilo mbili unauzwa shilingi 3,000/= ekari moja inabidi utumie kilo 10, sasa ukifanya hesabu tatu mara kumi mkulima hawezi ndiyo maana wakulima wengi wanatumia zile mbegu za zamani ambazo haziendani na hali halisi ya hali ya hewa. Sasa Serikali katika hili kwa kuweka mbolea lazima ihakikishie imeweka na ruzuku kwa ajili ya mbegu ziweze kuwa na bei ya chini ili ziweze kununuliwa na wakulima wengi waweze kutumia mbegu ambazo zinafanyiwa utafiti.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili la mbegu vilevile mimi nilikuwa naomba Serikali iweze kuwa makini vilevile katika Kanda za Kulima. Sasa hivi unatoka Dar es Salaam mpaka Mwanza watu wote wanalima mahindi, lakini katika maeneo yote si kwamba yanastawi mahindi, kuna maeneo kama Dodoma ukilima mahindi unajua haupati, hapa nashangaa watani wangu Wagogo nao wanalima mahindi wakati wanajua watakosa tu. Labda ndiyo maana ombaomba wako wengi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani pamoja na tamko nzuri la Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alipoingia kwenye Wizara hii baada ya kuondoka kwenye Tume ya Halmashauri ya Jiji, alisema kabisa hakuna njaa katika nchi hii, lakini bado hakuchukua hatua muhimu sana ya kuhakikisha kwamba katika maeneo mengine ambapo hapastahili kulimwa mazao mengine yasilimwe. Maeneo ambayo yanayostahili kulimwa mtama yalimwe mtama ambao umefanyiwa utafiti, maeneo yanayostahili kulimwa mihogo yalimwe mihogo ambayo imefanyiwa utafiti na mahindi yalimwe kwenye sehemu zilizofanyiwa utafiti ili mazao yaweze kupatikana bila matatizo na ndipo tutaondokana na balaa hili la njaa.

Mheshimiwa Spika, njaa kwa kweli katika dunia hii ya utandawazi itatuuza tena kwa bei rahisi sana, tutauzwa hivi hivi kwa sababu ya njaa. Angalia Urusi, Urusi imesambaratika kwa sababu ya njaa na sisi kama hatukuangalia kila mwaka tunalia njaa, kila mwaka tunalia njaa tutauzwa kijumla jumla wala hakuna mtu atakayetutetea kwa sababu tumejitakia wenyewe kwa sababu tunatumia nguvu zaidi kuliko kutumia mbolea pamoja na mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo mimi bahati mbaya pale kwenye *gate* wamenikataza, ningekuja kuwaonyesha jembe la mkono, wamenikataza nisiingie na jembe hilo lakini ninamwomba Mheshimiwa Waziri akalione mwenyewe hilo jembe la mkono, kwa sababu ndilo linalosababisha tuchelewe na ingewezekana ningemwonyesha jembe lile lile waliyokuwa wanatumia babu zetu ndiyo hilo hilo linalotumika leo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza kwamba mwaka jana Serikali ilitoa matrekta 170 kwa nchi nzima.

Sasa unapozungumza matrekta 170 unazungumzia trekta moja kila Wilaya na nchi yetu ina vijiji karibu zaidi ya 12,000. Tungekubaliana kama tungelizungumzia

matrekta 20,000 au matrekta 30,000. Pamoja na kwamba wananchi wetu wengi wanatumia jembe la mkono sasa lazima tuweke mikakati ya kuondokana na jembe la mkono tuanze kuweka matrekta, lakini katika maeneo ya wafugaji tuhakikishe tunapeleka majembe yanayokokotwa na wanyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda wangu unaenda haraka sana sijui kwa sababu gani. Lakini lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni kuhusu hizi fedha za *PADEP.* Katika wa ukurasa 23 Mheshimiwa Waziri amesema naipongeza Serikali kwa kuongeza Wilaya zingine ambayo hazikuwepo mwaka jana, mwaka jana ametumia karibu bilioni 2.1 katika kufanikisha malengo hayo. Lakini wazo langu hapa nilikuwa nadhani kwamba bora hizo fedha ziende moja kwa moja kuimarisha uwezo wa wakulima. Hapa nimeona kuna maandalizi na kuna mipango lakini mimi ningesema bora ziende moja kwa moja kuimarisha mpango wa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nataka kuzungumzia juu ya suala la umwagiliaji. Umwagiliaji ndiyo nyenzo ambayo itatukomboa mimi naishukuru na kuipongeza Serikali kwa hatua ambayo imefikia hasa katika kuhimiza matumizi ya maji ya Ziwa Victoria. Wananchi wa Kanda ya Ziwa kwa kweli wamefurahi na kupokea kwa hamu sana. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji wahakikishe mabonde yote ambayo yanatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kuliko ilivyo sasa hivi katika Kanda ya Ziwa wameweka ekari 200 tu na hata pale Nzega wameweka ekari 200 tu bado hazitoshi bila kilimo cha umwagiliaji bado tutakuwa tunalia njaa kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa nataka kusema ni mikopo hii ya wakulima hasa juu ya *EXIM* Benki. Lengo letu lilikuwa ni kutoa mikopo mbalimbali kwa wakulima wa kawaida, lakini Serikali inasema kwamba imejiondoa kwenye biashara nakubali, lakini imejiingiza kwenye biashara na inaji-*contradict* yenyewe, angalia mikopo ambayo inakwenda kwenye *EXIM* benki. Kwanza hailipwi na waliokopa siyo wakulima, wamekopa wafanyabiashara wakubwa. Mimi nadhani kama tungewakopesha wakulima wetu ni waamini wangeweza kulipa na kwa nini wamewapa *EXIM* benki sielewi. Tulipitisha sheria hapa hapa *Procuremt Act* ambayo inataka kila mtu aingize kwenye *tender.*

Mimi siamini kama *tender* ilipita ya *EXIM* benki. Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake ahakikishie anatueleza kama *EXIM* Benki ilipitishwa kweli kwenye *tender.* Ukiangalia hata riba ni kubwa mno, wanatozwa wakulima wetu asilimia 18 wakati ukikopa kwenye benki zingine unalipa asilimia 5 au 6 kwa kutumia *dollar* za Kimarekani. Ukikopa kwa shilingi ya Tanzania hapo unaweza ku- *negotiate* na unaweza kulipa kwa riba ya asilimia 10. Sasa iweje wakulima wadogo wadogo ambao hawana uwezo, hawana masoko, mvua zenyewe zinawapiga chenga, hawana uhakika wa kupata mtaji, hawana uhakika wa kupata raslimali wanafanyiwa riba ya asilimia 18. Hiyo kwa kweli namwomba Mheshimiwa Waziri ageuze *EXIM* Benki hatuitaki na haifai kama *NMB* wanaweza kwa nini msiwape *NMB.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningefurahi sana benki ambayo ina mtandao mkubwa kuliko hii benki, kwanza hii benki iko Mjini Mjini tu kule kwetu hakuna ambapo ndiyo kwenye wakulima. Dar es Salaam utawapata wapi wakulima wakati kuna wafanyabiashara na wanaangalia rangi. Nina ushahidi kuna Waheshimiwa Wabunge wenzangu humu humu waliomba mkopo weusi kama mimi akapewa mweupe ambaye walikuwa wanatoka katika Mkoa mmoja hii ni dhambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele imegongwa na nimezungumza kwa haraka sana naomba tu niishie hapo. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wa Wilaya ya Mbeya Vijijini kwa kifo cha mwenzetu Yete Sintemule Mwalyego, aliyefariki hivi majuzi, Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata ajali Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, pamoja na Estherina Kilasi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi alioupata na kurudi Bungeni kwa tiketi ya CCM. Nina hakika tutashirikiana ili kuleta maendeleo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo tumekuwa tukilizungumza kila mwaka, tunasema kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hii na takwimu zilizotolewa zinajieleza wazi asilimia 50 ya pato la Taifa linatokana na kilimo na asilimia 70 ya fedha za kigeni zinatokana na kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kiasi gani Serikali ya Tanzania inawekeza katika kilimo kinacholeta asilimia 70 ya fedha za kigeni na asilimia 50 ya pato la Taifa kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Nadhani bado tuna muda mrefu kuweza kukibadilisha kilimo ili kiweze kuleta mafanikio mazuri yanayotarajiwa na wananchi katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika msimu uliopita tumeshuhudia njaa ambayo imetuletea matatizo makubwa tukalazimika hata kupitisha fedha za ziada ili kuweza kuinusuru nchi hii isiathirike zaidi na njaa. Tunaishukuru Serikali imefanya kazi nzuri ya kupeleka chakula kwa wananchi. Lakini hebu tufikirie kwamba hizi fedha zilizotumiwa kwa ziada katika nchi hii kwa ajili ya kunusuru Taifa hili katika njaa zingetumika katika kuendeleza umwagiliaji maji katika Mikoa mbalimbali na mito tuliyokuwa nayo tungekuwa wapi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, mimi nina uhakika kabisa tungefanya maajabu makubwa sana. Mimi nadhani bado hatujatilia maanani suala hili ili kuweza kujinasua na matatizo ya njaa katika nchi hii. Umwagiliaji maji mashamba ni kitu cha msingi sana. Mito tunayo lakini Wizara inayaangalia maji yote hayo yanakwenda katika bahari na wala hayatumiki kwa kilimo tunasema hewala tunasubiri kitu gani?

Maji ya Maziwa yetu, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa ma Ziwa Victoria, yote yapo pale yatatembea maji yale mpaka yakafike katika bahari ya *Mediterranean* na Bahari ya Atlantiki kule na Bahari ya Hindi hakuna popote ambapo tunayatumia maji haya kuweza kubadilisha kilimo na bado tunapiga kelele njaa.

Mheshimiwa Spika, Mito yetu yote inaelekea baharini na katika maziwa hatuitumii yaani kuyachukua maji tu kutoka kwenye mto ili kuweza kuyafikisha yamwagilie mashamba hatuwezi bado tuna *Program* na *scheme* ndogo ndogo ambazo wala haziwezi zikaleta mafanikio makubwa. Nadhani sasa Serikali ifike mahali ambapo itaamua kutumia *scheme* kubwa za Mito tuliyonayo ili kumwagilia mabonde mazuri ya mito tunayokuwa nayo katika nchi hii na tutapata chakula cha kutosha na wala hatutazungumzia tena njaa. Lakini kama tutaendelea hivi hivi tutaendelea kulalamika kuhusu njaa mwaka nenda rudi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mbolea mwenzangu aliyetangulia amelizungumzia vizuri, lakini na mimi nilizungumzie. Suala la mbolea na ruzuku ilitolewa tunaishukuru Serikali lakini niseme kwa Mkoa wa Rukwa na Mikoa mingine kama Mbeya na Ruvuma ile mbolea ya ruzuku ilichelewa kufika na wananchi waliendelea kununua mbolea kwa bei ya juu mpaka ilipofika kwenye mwezi wa Novemba na Desemba, ambapo msimu wa kilimo unakuwa umeishafikia mahali ambapo mbolea ile haikuweza kupatikana kwa bei ya chini.

Tunaomba katika Bajeti hii Wizara ihakikishe kwamba zipo fedha za kutosha na mbolea inapelekwa katika Mikoa ile ya Nyanda za Juu Kusini, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa. Mbolea ipatikane mapema ili tuweze kuwahi msimu unaokuja ili tuweze kulima mazao ya mahindi na tutazalisha kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, lakini suala hili la mbolea inaonekana ni biashara ambayo wafanyabiashara wa kati ndiyo wanaofaidika. Pili, mkopo wa mbolea kuja kupata katika *EXIM* benki nchi nzima tukusanyike wote twende katika *EXIM* Benki Dar es Salaam kwenda kufanya biashara hiyo. Kilimanjaro wanayo benki yao ambayo tayari wameishapeleka kule wananchi wanaweza kukopa pale.

Sasa nchi nzima kwenda kukusanyika kufanya biashara katika benki moja wakati tuna benki yenye mtandao. Wizara ya Kilimo na Chakula itafute jinsi ya kuishauri *NMB* na kuishawishi ili iweze kuchukua kazi hii lakini suala la kung'ang'ania *EXIM* Benki kwa sababu ndiyo waliokubali tunaacha mtandao wa Benki ambao upo tayari kwa kweli hatutendi haki kwa Watanzania wengine.

Wewe fikiria mfanyabiashara au mkulima atoke Rukwa Sumbawanga kilomita 1,500 akafanye mpango wa kupata mkopo kutoka *EXIM* Benki akae wiki tatu, mwezi mzima, miezi mitatu, anafanya kitu gani unategemea kweli mbolea atakwenda kuiuza kwa bei nzuri. Mimi nafikiri hatuko makini kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mikopo. Wananchi vijijini wanalalamika sana wanaona Serikali imewatupa. Wafanyakazi Serikalini wanapata mikopo, wafanyabiashara wanapata mikopo, mkulima huyu maskini ana mipango gani. Tunaishukuru Serikali imezungumza vizuri kuhusu suala la kuwapatia mikopo na kupelekewa benki za wakulima karibu nao.

Lakini utekelezaji utakuwa namna gani ndiyo ule ule wa kupeleka *EXIM* benki. Utakuwa ni mpango wa kupeleka *EXIM* Benki ili wananchi wafuate hizo fedha mbali hatutakuwa tumewasaidia. Mimi nimetembea katika tarafa ya Mwimbi, nimetembea katika Tarafa ya Matai, vijiji vya Mwanzye, Matai, Ulumi na sehemu nyingine wanalalamika sana wanasema Serikali imetuondolea kodi lakini imetuacha solemba haitusaidii katika kutupatia mikopo midogo midogo ili tuweze kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa suala hili ambalo linakuja la mikopo tunaomba litengenezewe mpango mzuri ili wananchi waweze kufikiwa na hii mikopo na siyo kuipeleka mahali ambapo haiwezi ikafikia wananchi kwani malalamiko yataendelea kuwa pale pale.

Tutakuwa hatujawasaidia wananchi lazima tuweze kuwafikishia wananchi, kama MMEM imeweza kufika kwa wananchi na wakaweza kushiriki vizuri kwa nini Wizara ya Kilimo na Chakula na yenyewe isitafute mpango kama uliopendekezwa na Kamati iliyochambua makadirio ya Wizara hii. Uwepo Mpango utakaowafikia wananchi mpaka vijijini ili waweze kupata hii mikopo ili waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la zana kwa kweli tunapozungumzia suala la matrekta sijui 100 au 200 katika nchi ya Tanzania ni kichekesho tu. Hatuwezi tukaondokana na umaskini kama tutaendelea kuzungumzia zana mbovu tunazokuwa nazo.

Ni lazima tubadilike kabisa Wizara ya Kilimo na Chakula hapa ndiyo mahali ambapo wanapaswa sasa kufanya kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba tunatoa ruzuku ya mbolea, tunahimiza kilimo bora kifanyike, tunahimiza *scheme* za umwagiliaji maji lakini matrekta ndiyo yanaletwa mawili au matatu ambayo hayatoshi kwa nchi nzima. Nadhani hatupangi vizuri kuhusu suala la kilimo.

Tunatakiwa tunapozungumza juu ya kumwendeleza mkulima wa Tanzania basi tufanye kazi pia ya kuhakikisha kwamba na matrekta yanapatikana ya kutosha kuweza kusambazwa katika nchi nzima, ikiwezekana kama hatuwezi kuyasambaza kwa njia ambayo inajulikana ya kuwakopesha wananchi, basi tuanzishe *centres* angalau kila Kata au kila Tarafa kuwepo na *centres* sehemu ambazo wananchi watakwenda kukodisha hivi vifaa ili waweze kulima na kuweza kujipatia chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kupambana na wadudu waharibifu katika mashamba yetu. Wananchi wanalima mazao, lakini mazao mengi yanapotea kwa sababu ya utunzaji mbaya au mazao mengine yanaliwa na wadudu kiasi ambacho kinapunguza pato hili la mazao tunayolima hasa mazao ya nafaka. Madawa yanayotumika inaonekana wala hayafai. Inaonekana kuwa watu wanafanya biashara ya madawa ya mazao wanaleta dawa mbovu makusudi ili yasiweze kutusaidia kuua wale wadudu. Kila siku watu wanatumia dawa hizi lakini haileti manufaa yoyote. Je, Serikali haioni kwamba wananchi wanaendelea kupata usumbufu.

Kwa nini Serikali haikai kafanya utafiti hapa hapa nchini Tanzania kwa kutumia wataalamu wetu ikatafutwa dawa ambayo itakuwa accepted, itakuwa na matokeo mazuri na iwe na bei nafuu iweze kusambazwa nchini tuweze kutumia ile. Kwa sababu madawa haya tunayopata kutoka nje inaonekana kuna mchezo unaochezwa hapa watu wanatuletea madawa ya ajabu ambayo hayawezi kuua wadudu au yanaua kidogo na vitu vingine vinabaki. Najua kuna wataalamu wanasema inategemea na *stage* ya wale wadudu wanavyozaliana. Ukiwaua katika hatua fulani wakati mwingine wadudu wale wanakuwepo tu hawafi. Tutafute dawa sisi wenyewe ambayo tunaweza kuifanyia utafiti katika vituo vyetu vya kilimo tuweze kuona ni jinsi gani ya kuondokana na tatizo hili. Watu wanafanya biashara tu na tunaendelea kuteketea na madawa mengine inawezekana ni sumu kwa ajili ya afya zetu wenyewe.

Kuhusu suala la hivi vituo vya kilimo vitusaidie wakulima huko vijijini wapate mbegu zilizo bora. Tafiti hizo zisiishie tu katika maeneo fulani fulani mbegu hizo ziende zikawasaidie wakulima kule ambako wanahitaji hizi mbegu. Kwa sababu gharama ya mbegu hizi ikiwa kubwa ndiyo wananchi wanaendelea kutumia mbegu za asili na wanatumia mbegu ambazo wanavuna kutoka mashambani ambazo hazileti mafanikio mazuri. Sasa hivi tafiti tunazozifanya za mbegu bora haziwafikii wakulima hatuwezi kutegemea kupata mafanikio makubwa inabidi tutafute jinsi ya kuweza kuwapatia mbegu bora lakini kwa bei nafuu. Kama ikiwezekana ziwe subsidized Serikali itoe ruzuku hata kwa mbegu ili tuweze kuzalisha mazao yatakayotusaidia kwa ndani. Kuhusu ukosefu wa Maafisakilimo katika vijiji. Nilipotembelea katika jimbo langu vijiji vingi sana nimekuwa nikilalamikiwa kuhusu Maafisakilimo. Inaonyesha wananchi wana nia sana ya kupata ushauri wa wataalamu, lakini wataalamu wanapatikana wapi? Unakuta katika Kata moja labda yuko Afisa kilimo mmoja huyo hawezi kutembea vijiji vinane, tisa au kumi ambavyo viko ili kuweze kutoa ushauri. Sasa wananchi wanapiga kelele, Wizara ina mpango gani wa kuwafundisha hawa watu waweze kuja kutusaidia wananchi. Wizara iwe na mpango madhubuti wa kufundisha watu hawa watakaokwenda kule. Hili suala la kuwa na vyuo na kupeleka wakulima tutawapeleka wakulima wachache tu. Ni lazima tutafute wataalamu waliofundishwa waende kuwasaidia wananchi kwenye kilimo. Wawasaidie kule kule waliko. Lakini tukitegemea kuwapeleka kwenye vyuo hivyo kama taarifa alivyosema Mheshimiwa Waziri hapa tutakuwa tunapeleka wakulima wachache sana ambao hawataleta mabadiliko makubwa katika jamii hii. Lakini tukiwapeleka wataalamu kule Maafisa Ugani watatusaidia sana kuweza kuwaelewesha wananchi ili waweze kufanya kazi nzuri na kuweza kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu suala la ushauri wa kuunda Bodi ya Mazao ya Nafaka. Inaonekana tunashindwa kupata maendeleo mazuri ya kilimo cha mazao ya nafaka kwa sababu sisi hatuna bodi yoyote inayoshughulikia jambo hili tunakwenda kiholelaholela. Kahawa ina Bodi, tumbaku ina Bodi na mazao mengine yote yana Bodi lakini Wizara haijawahi kuzungumzia hata siku moja ni jinsi gani ya kuweza kuweka Bodi inayoshughulikia mazao ya mahindi na mazao mengine haya ya nafaka. Kwa njia hii na sisi tutakuwa na mahali ambapo tutazungumzia tupeleke matatizo ya wakulima ili chombo hiki kiweze kuona ni jinsi gani kitakavyoweza *co-ordinate* na kuweza kuona jinsi gani tutakavyoeneza kilimo cha nafaka. Njaa ilivyotokea nafaka kutoka katika mikoa hii minne niliyoitaja imeonekana ni muhimu sana na mmeishughulikia sana kuweza kupata mahindi kupeleka kule kulikokuwa na upungufu. Lakini tungekuwa na chombo kama hiki Bodi ya Mazao ya Nafaka nadhani tungepata manufaa mazuri zaidi ili tuweze kupata maelekezo mazuri na jinsi gani ya kuweza kupata manufaa mazuri ya kilimo cha mahindi.

Ningeomba Wizara tujifunze kutoka nchi nyingine ambazo zipo katika jangwa na zimefanya kazi nzuri sana ya kutumia maji kama Misri. Wako wengi wametaja kuhusu suala hili na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo alikwenda kutembelea kule, mambo waliyoyaona ni ya kufurahisha sana. Mimi nadhani Wizara ya Kilimo tutafute jinsi ya kuweza kupata hata kama ni fedha za mkopo ulio nafuu upatikane ili tuweze kuanzisha *scheme* kubwa za kilimo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja hii ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kilimo kinaambatana na mfuatano ambao unakwenda kwa wakati mmoja. Mfuatano huo unahusu upatikanaji wa mbegu bora, maji, pembejeo, miundombinu, soko, mtaji, zana za kilimo na uadilifu. Kupatikana kwa mfuatano huo ndiko kunakokamilisha kilimo. Kukosekana kwa mambo hayo ndiko kunakodhoofisha kilimo. Kwa hiyo, mimi naishauri Wizara iangalie mambo hayo kwa sababu ndiyo process ya kuendeleza kilimo chetu. Kama mambo hayo yatagongana kilimo chetu hakiwezi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ni kitu muhimu sana katika kuwawezesha wakulima wadogo wadogo, wakulima wakubwa na wakulima wa kati. Lakini ili kujenga miundombinu hii inahitajika lazima Serikali iweke dhamira ya kutaka kujenga miundombinu hiyo. Kwa hali ilivyo sasa kwa miaka mingi Wizara ya Kilimo imekuwa inategemea sana fedha kutoka kwa nchi au Mashirika wahisani katika miradi yake ya maendeleo. Wakati tunapata fedha hizo mipango yetu inaendelea lakini utafika wakati watasitisha kutupatia misaada na wakisita kufanya hivyo tutapata pengo kubwa sana la kuleta maendeleo ya kilimo chetu. Kwa ajili hii mimi naungana na maelezo ya Kamati yetu kwamba ipo haja kubwa sasa kwa Serikali kuweka dhamira ya kutenga kila mwezi shilingi bilioni moja kwa ajili ya sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia na kimsingi mimi nakubali kabisa kwamba tunahitaji wawekezaji kutoka nje katika kilimo chetu. Lakini Serikali lazima itambue kwamba nchi hii ina vijana waliokuwa vyuo vikuu, sekondari, na shule za msingi hawa ajira yao kubwa kwa vyotevyote vile itakuwa ni kilimo. Kwa hiyo kama tusipojenga miundombinu mizuri ya kuwavutia hawa vijana wetu kujiunga na kilimo tutapata matatizo makubwa sana ya ajira siku za usoni. Kwa ajili hii namshauri Mheshimiwa Waziri afikirie kwa makini sana namna nzuri ya kuweza kujenga miundombinu na kuhusisha vijana hawa katika uendelezaji wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wamezungumzia kilimo cha umwagiliaji na mimi nisingependa kukaa bila na mimi kuchangia kilimo cha umwagiliaji. Lakini mimi nina mtazamo tofauti. Kwanza naipongeza Serikali, Wizara ya Kilimo kwa jitihada zake za kujaribu kupanua miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwa nchi nzima. Lakini jambo ambalo ninalotaka kumshauri Mheshimiwa Waziri ujengaji wa miundombinu ya umwagiliaji zaidi sana huwa inahitaji elimu ya uhandisi. Mara chache sana unapata wachumi wa kilimo cha umwagiliaji kushiriki katika mambo hayo. Kwa hiyo, nilikuwa namshauri awe na kitengo cha umwagiliaji katika Wizara ya Kilimo. Najua kwa sasa kipo, lakini kwa uzoefu mdogo niliokuwanao nilichokiona kitengo hiki kinahusika zaidi na ujengaji wa mifereji na baada ya hapo hatuna kitu cha kuweza kusimamia menejimenti ya matumizi ya maji katika mifereji hiyo. Kwa sababu hatuna kitu kinachosimamia menejimenti ya maji katika mifereji hiyo gharama hii tunayoitumia katika ujengaji wa mifereji siku moja itakuwa kazi bure. Naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri katika jambo hili afikirie sana kuweka kitengo cha menejimenti ya maji ya kilimo. Ni vizuri zaidi kwa sababu amesambaza ujengaji wa miundombinu mifereji karibuni nchi nzima afikirie sasa kuwa na Bodi ya Menejimenti ya Matumizi ya Maji ya Kilimo ambayo Mwenyekiti wake awe Mkuu wa Mkoa ili kusudi kujua namna gani maji yanaweza kutumika kwa faida ya kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya sasa Wizara ya Kilimo mimi naona pia nimshauri Mheshimiwa Waziri afikirie kurudisha kile kitengo cha *Marketing Development Bureau.* Najua kitengo hiki au kazi hii ya *marketing* inafanywa na Wizara ya Ushirika na Masoko. Lakini lazima afahamu katika *biological process* kwenye *agriculture marketing* ina *aspect* kubwa sana katika *process* hiyo. Kwa hiyo, kama utakuwa huna kitengo hicho utakuwa huwezi kutoa utabiri kwa wakulima wako mazao gani yalimwe kwa kipindi gani, kwa msimu gani.

Katika hotuba yako ulivyosema uchumi wa kilimo, sifa moja ya uchumi wa kilimo ni kujua nilime nini nikauze wapi. Kule ninakokwendauza nakwenda uza kwa nani. Maana leo ukilima mahindi upeleke Rukwa utakuwa ule uchumi wa kilimo hunao. Kwa sababu kule kilimo chao ni mahindi. Sasa unachotakiwa kujua kule Rukwa wana ukosefu gani basi ndiyo unahimiza mikoa mingine walime kile kitu ambacho kule hakipo kipelekwe katika misimu tofauti. Kazi hii ingefanywa vizuri sana na kitengo chako cha *Marketing Development Bureau.* Zamani nakumbuka kitengo hiki ndicho kilichokuwa kinasaidia kutoa taarifa hata ya hali ya njaa, kutoa taarifa chakula kiasi gani kinunuliwe ili kusudi kihifadhiwe katika ghala la Taifa. Kwa hiyo, kila wakati Wizara ya Kilimo ilikuwa *up to date* na mambo haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kumalizia kwa kusema kwamba katika suala zima la ujengaji wa miundombinu naomba sana kumshauri Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kutambua vijiji vyetu vingapi Tanzania na vijiji hivyo tulivyokuwa navyo vina barabara ngapi za vijijini. Ukishatambua barabara za vijijini na kujaribu kuziboresha barabara za vijijini utakuwa umetatua tatizo kubwa sana la mkulima mdogo mdogo vijijini. Aidha, washirikiane kupeleka wakulima Chuo Kikuu cha Sokoine wakati *Under-Graduates* wanapokuwa likizoni ili kuwewezesha kupata mafunzo ya *Farm Management*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu na mimi vile vile naomba niungane na wenzangu kutoa rambirambi kwa aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mungu aiweke mahali pema roho yake. *(Amin)*

Vile vile nampongeza ndugu yangu Danhi Makanga kwa kuja Bungeni kwa kupitia Chama cha Mapinduzi, karibu sana. Taarifa binafsi ya Mheshimiwa Ngawaiya ya Ijumaa inaonyesha naye karibu atakuwa *out.* Kwa hiyo, naye karibu sana Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nianzie kuzungumzia suala la upungufu wa chakula hasa katika Wilaya ya Mpwapwa. Mwaka 2003 Wilaya ilikuwa na upungufu wa tani 35,300. Nashukuru Serikali na taasisi nyingine zilitoa msaada wa chakula tani 1,453 tu. Kwa hiyo kwa mwaka 2003 tayari bado kuna upungufu ule ambao haujakamilika. Msaada huu ulielekezwa kwa wale ambao wangeweza kulipia chakula hicho. Nataka niiarifu Wizara kwamba mwaka huu Wilaya bado inakabiliwa sana na upungufu wa chakula hasa Kata ya Kibakwe vijiji vya Lukole, Kingiti, Ijenge na Kibakwe yenyewe. Hali ni mbaya vile vile katika Kata ya Mima, Berege na Godegode. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake hapa Waziri anaonyesha kwamba Dodoma itajitosheleza kwa chakula. Siyo kweli. Naomba nirudie takwimu za Waziri zinaonyesha kwamba Dodoma itajitosheleza kwa chakula sio kweli. Nataka nitoe maelezo. Kilichofanyika katika kumbukumbu zile ni kuangalia mavuno dhidi ya mahitaji na kuona kama kuna upungufu au hakuna. Sasa utaratibu huu hauwezi kukupa nafasi ya kujua Wilaya kwa Wilaya, Kata kwa Kata, Kijiji kwa Kijiji kuna upungufu kiasi gani. Kumbukumbu hizi zitakupa takwimu ya jumla ya mkoa ambayo ni hatari sana. Kwa sababu ukishapata kumbukumbu ya jumla ya mkoa kuna mambo mawili yanatokea hapo. La kwanza unategemea kule kulikozalishwa mazao yatakwenda kule ambako hakuna mazao ambayo si kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano unaweza ukawa umezalisha mazao ya kutosha Kondoa lakini ukawa na upungufu Mpwapwa huwezi ukategemea mazao yatatoka Kondoa yatakwenda Mpwapwa. Kwa sababu gani, kwa sababu mfanyabiashara wa Kondoa yeye ataangalia soko. Kwa hiyo hatapeleka mazao Mpwapwa. Lakini

mwananchi wa Mpwapwa atajuaje kwamba Kondoa ndiko kwenye mahindi. Je, anao uwezo wa kufuata mahindi Kondoa. Katika kumbukumbu za jumla zinaonyesha kwamba Dodoma ina mavuno ya kutosha. Sasa mimi nasema dhana hii ni potofu na mtazamo huu hautaisaidia Wizara kujua hali ya upungufu wa chakula nchini. Lazima iende chini ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upungufu wa mwaka 2003 na 2004 sasa ina maana kwamba wananchi wengi hawana chakula katika Kata hizo nilizozisema. Waathirika zaidi ni wazee vikongwe, wajane na vilema ambao katika chakula cha msaada cha mwaka 2003 hawakupata. Kwa sababu kilichokwenda kule ni cha kununua. Kwa hiyo, hali zao sasa hivi zimekuwa mbaya kama nilivyosema katika Kata ya Kibakwe, Mima, Berege na Godegode. Hali ni mbaya. Chakula kinahitajiwa sasa. Nitazungumza baadaye kwa nini kuna tatizo la ku-*manage* majanga kama ya njaa. Nchi yetu bado ina tatizo kubwa sana, haijajiwekea uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa hivi katika Kata hizo nilizosema watu hawajiwezi kabisa. Wengine hawatoki nje. Ukiongea nao lazima upeleke sikio karibu sana ili uweze kuwasikia. Watoto sasa wameanza kushindwa kwenda shule. Kwa hiyo, hatua za haraka zinatakiwa kuchukuliwa na Serikali kunusuru maisha ya wananchi wa Kata hizi za Kibakwe, Mima, Berege na Godegode. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile kwa sababu hakukuwa na mvua za kutosha mwaka 2003/2004 sio tu wale ambao hawakuwa na uwezo hawakupata chakula cha msaada lakini sasa hivi kinatakiwa chakula cha kununua kwa bei nafuu ili wananchi waweze kununua chakula hiki kule kule vijijini. Nataka niikumbushe Wizara mavuno yajayo ni Juni 2005 na hii kama mvua itanyesha. Lakini wananchi wataweza kulima katika msimu huu iwapo watapata chakula cha kuwawezesha kuhimili kipindi cha kilimo. Kwa sababu kunapokuwa na upungufu wa chakula wananchi wanashindwa kulima kwa hiyo kunakuwa na mzunguko wa upungufu wa chakula siku zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu bado inahitaji kujiwekea uwezo wa kutosha na mipango kamambe ya kukabiliana na majanga kama ya njaa kwa ufanisi mkubwa kuliko ilivyo sasa. Utaratibu wa kufanya tathmini ya hali ya chakula unahitaji kuboreshwa kuliko ilivyo sasa. Hapa anakuja mwezi Machi kufanya tathmini lakini hiyo haitoshi, harudi tena.

Lakini la pili, kati ya taarifa ya upungufu kutolewa na siku ya kuletwa chakula chenyewe nako kunachukua muda mrefu. Kipindi hiki kinatakiwa kitazamwe upya. Tathmini ya mwaka 2003 ndiyo iliyoleta chakula mwaka 2004.

Kwa hiyo ukifanya tathmini mwezi Machi maana yake chakula hakiji mpaka mwaka kesho na muda huu ni mrefu na watu huumia. Kwa hiyo kuna haja ya kufanya menejimenti nzuri zaidi baina ya kupata taarifa ya upungufu wa chakula na siku ya kupeleka chakula cha msaada katika maeneo yaliyoathirika.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi ni kwa Serikali yenyewe kuwa na uwezo wa kutosha wa kukabiliana na njaa, Serikali haina. Kwanza utabiri wa upungufu haufanywi vizuri unaangalia kwa ujumla tu. Lakini la pili chakula cha akiba hakiwekwi cha kutosha kwa sababu Serikali haitengi fedha za kutosha. Lakini kilicho zaidi ya hapo ni kwamba chakula cha akiba kinanunuliwa wakati chakula chenyewe kimekwisha malizika kuuzwa sokoni.

Hapa Mheshimiwa Waziri anaomba pesa akanunue chakula cha akiba, chakula cha akiba kimekwishauzwa hakipo. Watu wamekwishauza siku nyingi na kama Waziri anategemea akishatoka hapa kwenye Bajeti akipata fedha za kununulia chakula maana yake mwezi Agosti chakula kitakuwa hakipo tena. Wafanyabiashara watakuwa wameshanunua. Kwa hiyo maana yake hataweza kufikia lengo la kununua tani 100,000 kama alivyoomba hapa.

Kwa hiyo, nataka niseme chakula cha akiba hakinunuliwi kwa wakati muafaka na matokeo yake chakula kingi kinatoka nje na kufanya akiba kukosekana ndani ya nchi. Hii ndiyo hoja yangu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho menejimenti ya maafa kama ya njaa ni sayansi. Watu watasomea. Haiji kwa uzoefu tu. Haiji kwa kusema wewe kaa hapa usaidie, hapana ni sayansi. Inahitaji wataalamu, inahitaji nyenzo na uwezo wa kufanya mambo kwa wakati, kwa sababu unashughulika na maisha ya binadamu. Ingekuwa ni suala la ku-*manage* mifereji na barabara kitu kingine hapa una-*manage* maisha ya binadamu.

Kuna haja ya Waziri hapa kurekebisha yale niliyosema. Kufanya menejimenti ya maafa kama njaa, kutafanyika kwa uzuri zaidi na ufanisi zaidi kuliko inavyofanyika sasa hivi. Sisi Wabunge tukisema kwamba maeneo yetu yana njaa wanasema ngoja tukafanye utafiti, tukapate kumbukumbu. Kumbukumbu si hizi tunakuambia. Sasa ukienda kule ukirudi mwaka umekwisha na watu wamekwishaathirika zaidi. Kwa hiyo, lazima katika ile menejimenti lazima kuwe na sehemu ya wawakilishi wananchi kutoa taarifa za muhimu zinazoweza kushughulikiwa na Serikali mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa kweli hayo ndiyo waliyonituma wananchi wa Kibakwe kuja kuomba chakula cha njaa. Tuna upungufu wa chakula na tunakiomba kiende mara moja. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Awali ya yote naomba niungane na wenzangu kwa kweli kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mbunge mwenzetu, Marehemu Yete Mwalyego. Marehemu Mwalyego kwa kweli kututoka kwake kumetupa pengo kubwa sio sisi tu, lakini pia wananchi wa Mbeya Vijijini. Tuliokuwa tukikaa naye karibu tunamfahamu katika Kamati yetu alikuwa ni mtu anayependa kutumikia watu. Kwa kweli kazi ya Mungu

haina makosa kwa hivyo tunamwombea Mwenyezi Mungu roho yake aiweke mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia, napenda kutoa pole kwa ndugu zetu ambao waliopata matatizo ambao ni Mama Anne Kilango Malecela , Mheshimiwa Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Kilasi. Wote hawa tuna hakika kwamba Mwenyezi Mungu atakuwa amewatuliza kwa sasa na wale ambao wana majeraha basi yataendelea kupona na tutaendelea kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee nazitoa kwa Mheshimiwa Makanga na Wananchi wa Bariadi Mashariki kwa kuchaguliwa kwake kwa mara ya pili kurudi Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze pia Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya kwa niaba ya Watanzania katika Sekta hii muhimu ya Kilimo. Pia, ninapongeza hotuba yake ambayo ina mwelekeo mzuri wa kutupa matumaini na mwelekeo wa kitu gani ambacho tunakusudia kukifanya katika nchi yetu kwa kipindi kijacho katika Sekta hii muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado ninaamini kabisa kwamba kilimo siyo tu kwamba ni Sekta Kiongozi au ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, lakini nafikiri kwamba bado Taifa letu linategemea kwa kiwango kikubwa zaidi kujinasua na matatizo tuliyonayo kwa kutumia kilimo na kwa hivyo bado tunawajibika kwa pamoja na hasa Serikali yetu kuona kwamba inatoa kipaumbele cha kwanza kabisa katika kilimo kwa kuzingatia kupanga ni kuchagua na mimi bado naamini kama wenzangu walivyosema kwamba inawezekana hatujawa makini sana katika suala zima la kukipa uzito kilimo chetu hapa nchini. Tunaweza kuwa tumepanga na tumeanza na mambo mengine kama ya elimu ambayo ni jambo la msingi kwa kweli, lakini ni vizuri zaidi pia tukazamia katika kilimo hasa katika maeneo mbalimbali ambayo yanaweza yakatufanya tukafanikisha kilimo chetu na tukajinasua katika hali ngumu ya uchumi tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo ninataka nichangie ni suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Kama ambavyo Waziri ametaja pia katika hotuba yake kwamba ziko hatua madhubuti zinazochukuliwa katika suala hili, lakini nafikiri utumiaji wa mito na maziwa yaliyoko katika nchi yetu haujafanyika katika kiwango ambacho tunaweza tukaimarisha kilimo chetu na tukaondokana na malalamiko haya ambayo yanasemwa mara kwa mara ya kuomba njaa. Sikusudii kulalamika kama ndugu yangu, mtani wangu Mgogo hapa ambaye ametoka sasa hivi kuomba, maana wao wameshaamua kuanzisha Umatonya, wao kila wakati wanaomba. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini tunafikia hapo kwa sababu pengine ni kwa sababu ya hali halisi kwamba kama tungeweze tukajitahidi kuweka mipango madhubuti ya kutumia maji yetu tuliyonayo katika nchi yetu ambao ni utajiri mkubwa, tungeweza kufanikisha kuondokana na aibu ya njaa na kwa kuwa sisi kule Usukumani siyo sera yetu hii ya kuombaomba, basi nafikiri hili linaeleweka katika Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nichangie pia sehemu nyingine katika utekelezaji wa miradi. Bahati nzuri katika Jimbo langu kuna miradi ya umwagiliaji katika sehemu inayoitwa Nduguti na Nyida. Kwa bahati nzuri skimu hii ambayo iko chini ya *PIDP* ilikuwa inaendelea katika kiwango cha kurekebisha mifereji tu. Naibu Waziri alipotutembelea kupitia kwake, kwa niaba ya Serikali na baada ya kushauriana naye tuliona kwamba kwa kweli kilimo hicho cha umwagiliaji hakiwezi kufana kama hakuna mabwawa na kwa hivyo mto huo ungezibwa likatengenezwa bwawa zuri ambalo linaweza likafanya sasa kilimo kikawa endelevu. Lakini kumwagilia kwa kutumia mvua ambayo unaitegemea kwa miezi kadhaa na wakati mwingine haitokei, matokeo yake sasa ndiyo inakuwa tu kama mtu unatengeneza mfereji wa kupitisha maji yapite kwenye mashamba halafu baadaye yaishie kwenye mto.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukubaliana kuwa kutatengenezwa bwawa pale, nasikitika mpaka leo bwawa hilo halijaanza kutengenezwa. Kwa hiyo, mipango yenyewe inasuasua. Tunataka kutumia nafasi hii kumuomba Waziri aone umuhimu kwamba kama tunasisitiza suala la utekelezaji wa miradi na hasa katika suala la umwagiliaji, basi mipango hii ya kuanzisha mabwawa na hasa katika eneo letu hili ambalo nimelitaja ni vizuri bwawa hilo likakamilishwa ili kilimo kile kiwe cha kisasa zaidi kuliko mpango uliokuwepo wa kutegesha maji yapite kwenye mfereji halafu baadaye yaishie mtoni. Kwa hiyo, hautaweza kulima hata mara mbili kwa mwaka mmoja. Nadhani Mheshimiwa Waziri atalichukulia uzito suala hili.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwa kweli sijui inakuwaje, maana kiongozi wa nchi anaposema kwa nafasi yake, kwa niaba ya Serikali, sijui uhusiano huu wa watumishi chini ya Wizara wanafanyaje. Nilitegemea kwamba agizo hilo likishatolewa basi lifanyiwe kazi na hasa kama fedha zenyewe zipo. Siamini kwamba watendaji hawa labda walipuuza kauli hiyo, maana kupuuza kauli ya Waziri ambaye amechaguliwa na Wananchi maana na yeye ni Mbunge, ni sawa na kupuuza kauli ya Mbunge, Mbunge ambaye anawakilisha Wananchi. Kwa mfano, mimi hapa ninawakilisha takriban watu laki tatu, msukumo wangu ni mkubwa zaidi katika hoja ya Wananchi ninayoieleza kuliko mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, sikusudii kuchongea watendaji wale, lakini mwalimu wangu mmoja alinifundisha akasema kwamba: “Serikali hutembea katika karatasi.” Pengine watu wanaweza wakapuuza wakasema: “Aah, sasa maneno haya si maneno tu ya kisiasa alisema tu kuwafurahisha pale.” Kwa hiyo, nataka kushauri kwamba labda kama maneno yale yaliishia kwenye mdomo, basi yawekwe rasmi kwa sababu Serikali inatembea kwa *circular.* Maandishi hayo yafanyike ili tupate hilo bwawa ambalo tuna hakika litafanya kilimo katika eneo hilo kiwe kizuri zaidi na mafanikio yake yawe makubwa sana ya kilimo cha mpunga.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la ufufuaji wa matrekta. Ulikuwepo mpango mzuri ulioelezwa na Wizara hapa kwamba watu waandikishe matrekta ambayo ni mabovu yatatolewa fedha. Nasikitika kwamba mpango huu sidhani kama umefanikiwa vizuri sana katika maeneo mengi katika Wilaya

mbalimbali. Kwangu mimi kuna watu ambao wameomba, lakini bahati mbaya fedha hizo hawakupata na kwa hiyo zoezi hili halikufikia ufanisi kama ambavyo Wizara ilikuwa imekusudia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni lile la mikopo kutoka Benki ya *EXIM.* Kama ambavyo wenzangu wamesema, masharti pengine ni magumu mno. Kama sisi kweli tuna nia, Serikali ina nia ya kusaidia Wananchi katika Sekta hii ya Kilimo ambayo kila mtu anajua umuhimu wake, nafikiri ni vizuri zaidi tuangalie masharti hayo na kama ambavyo imependekezwa, basi kama benki hii labda imeachiwa ifanye masharti yake yenyewe, tuone masharti hayo kweli yatatufikisha katika suala zima la kufanikisha hilo lengo tunalolikusudia au la. Kama kuna upungufu, basi upungufu huo tuuondoshe ili azma ya kuwawezesha wakulima iweze kufikiwa na kwamba wakulima wenyewe nao waweze kujinasua na hali ngumu waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni suala la hoja ya watumishi walioko katika Wizara ya Kilimo. Utaona kwamba katika ngazi ya Wilaya na nadhani katika ngazi pia ya Tarafa kuna Maafisa Kilimo na Mifugo. Binafsi naona utata huu wa watumishi hawa pamoja na kwamba ni Serikali moja kuwajibika katika Wizara mbili, kwenye Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, lakini hapo hapo kwenye Wizara ya Kilimo na Chakula. Sasa, sijui ninyi mnaliratibu vipi hili, lakini nafikiri kwamba labda hili nalo lina utata wake katika namna ya uendeshaji. *(Makofi)*

Aidha, ni vizuri watumishi hao wa kilimo kwa kweli wakaenea mpaka kwenye ngazi ya Kijiji, kuishia tu kwenye Tarafa sidhani kama inasaidia sana maana wakulima walio wengi wanaopaswa wapewe Elimu ya Kilimo wako Vijijini. Utashangaa kwamba katika karne hii ya 21 ya Sayansi na Teknolojia bado wako wakulima ambao hawajaelewa kilimo cha kisasa hata lile suala la upandaji tu. Watu bado wanachota mbegu wanaweka kwenye chombo halafu wanazisia, wanamwaga, wanaziambia tu: "Tangulieni tutakutana wakati wa palizi." Kilimo cha namna hiyo huwezi ukategemea kwamba mtu huyu atavuna mazao ambayo yatakuwa ya kutosheleza. Kwa hiyo, bado hoja ya watumishi wa kilimo kusambazwa katika maeneo ya Vijiji ni jambo la msingi sana ili kuwasaidia wakulima wetu waweze kulima kilimo cha kisasa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kama ambavyo wenzangu wamesema, kama tunafanya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ya Sekta mbalimbali kwenye nchi yetu, basi ni muhimu pia tukaweka uwekezaji hata kwenye kilimo.

Kama wako watu wenye uwezo mzuri ambao wanaweza kutusaidia wakawa wana mitaji mizuri, wana nyenzo nzuri na wanaweza wakasababisha ajira fulani, basi itatusaidia pia katika nchi yetu tukipata wawekezaji ambao wanaweza wakashiriki katika suala hili la kilimo ili kuondokana na tatizo la njaa na uchumi kwa ujumla kwa sababu ni eneo moja muhimu ambalo tunategemea sana katika ufanisi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Mimi mwenyewe ni Mwenyekiti wa Kamati ambayo imetoa mapendekezo ambayo naamini kwamba wenzangu wataendelea kuyasoma na baadaye kuboresha.

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza nataka nitoe rambirambi kabisa kwa ndugu yangu, kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kupoteza Mbunge wao, Marehemu Yete Sintemule Mwalyego.

Mheshimiwa Spika, pia, nakushukuru sana pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu wa Bunge na Wabunge wote kwa ujumla kwa moyo ambao sisi Wabunge wa Mbeya mmetufariji sana kwa jinsi mlivyoshughulikia msiba ule ulipotupata sisi wote. Kwa niaba ya wengine wote tunasema ahsante. Kwa hiyo, binafsi nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la kwanza, wamezungumza wenzangu habari ya mikopo kutoka kwenye benki hiyo ya *EXIM.* Mara nyingi sana watu wamekuwa wakiuliza hii Benki ni ya nani, lakini hakuna mtu ambaye amekwishapata jibu. Tunataka benki zote ziendelee. Mimi sijakopa kule, lakini waliokopa kule wanasema wanapata tabu sana, wanasema kuna ubaguzi na ina mambo mengi na urasimu mwingi. Kwa hiyo, nadhani sasa tungeweza kufikiria kuipa benki yetu ya *NMB* nafasi ya kuimarisha na kufanya shughuli hiyo kama uwezo upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua *NMB* ina mtandao mpaka vijijini. Hii *EXIM bank* inaonekana iko mijini zaidi kuliko hiyo *NMB.* Kwa hiyo, tungepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwamba hebu tuanze na kuangalia kutumia kile tulichonacho sisi, kwa nini *EXIM* inaanza kupewa sana nafasi kubwa kuliko hata *NMB?* Kwa hiyo, nawaunga wenzangu mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la mbolea ambalo tunalizungumza. Binafsi sielewi, lakini kwa jinsi inavyozidi kuendelea nimepata habari. Sisi tuko kwenye Kamati hii na bahati nzuri sana wewe mwenyewe ulinituma nilikuwa Uingereza. Kule tulipata nafasi tukatembelea mashamba fulani, sasa watu wa kule hawatii mbolea ya chumvi chumvi kwenye mashamba yao. Karibu robo tatu ya ulimwengu hawataki kula vyakula vilivyozalishwa na mbolea ya chumvi chumvi. Kama niko *wrong* nitaomba nisahihishwe baadaye. Lakini nadhani ndiyo mwelekeo wa dunia watu kutopenda mbolea ya chumvi chumvi kwa sababu wanasema ina athari kubwa katika miili ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, nadhani kungekuwa na mkakati tuanze sasa kutumia mbolea inayokubalika ya samadi au mboji, ndiyo move yetu kubwa ielekee huko. Kama tukiendelea kung'ang'ana na mbolea ya chumvi chumvi hatutauza mazao, wakishajua kwamba mlivuna mazao lakini mlitumia mbolea ya chumvi chumvi, basi inawezekana hata mazao yetu yatakosa soko. Sasa kama hilo lipo, basi Wizara inayohusika ni vema kabisa ianze kufanya taratibu tuweze kutumia mbolea inayokubalika, mbolea za asili

ambazo zipo sasa na zinakuwa zina bei ya chini kwa sababu zinapatikana kwani ng'ombe wapo, kuku wapo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo nilitaka niliseme maana naona tumekazania mbolea ya chumvi chumvi na mahali pengi sana imeharibu ardhi na imekuwa ni biashara ambayo ni ngumu sana kwetu. Nafikiri tuelekee kwenye samadi, kwenye mboji na mambo mengine na kwa hiyo itatusaidia. Suala la tatu ni hiki kilimo cha umwagiliaji. Tumeongea sana kwenye Kamati na bahati nzuri tulikuwa na Waziri. Kwanza mimi nataka niseme kwamba, ni kweli Wizara hii ni ngumu. Siku moja nilikuwa namtania Mheshimiwa Keenja kwa sababu tunataniana. Siku moja nikamwambia: "Itabidi ukazane sana katika Wizara hii, kwa sababu wanaopita kwenye Wizara hii wakitoka pale wanakwenda Wizara ya Kazi, wakitoka Wizara ya Kazi wanakosa Uwaziri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tumhurumie kwa sababu kwa kweli Wizara yenyewe ni kubwa na nchi yenyewe ni kubwa na tangu tumetoka huko hatujawa na mkakati wowote wa kilimo cha kisasa, tumekuwa na kilimo cha kubabaishababaisha tu. Sasa tunataka kubadilika tuingie katika mfumo wa kilimo kizuri kama wanavyopendekeza Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa ni lazima tuondokane na kilimo cha jembe la mkono tuingie kwenye jembe la kukokota la ng'ombe au matrekta kwa sehemu zingine. Kwa hiyo, Wizara ni ngumu na umaskini tulionao, kubadilisha Wananchi itakuwa ni kazi. Kwa hiyo, nafikiri sisi tujitahidi kuwaunga mkono hao wenzetu na Serikali yetu ili tufike kwa pamoja, lakini nao wakituongoza kwa sababu hii Wizara wamepewa wao, sasa wao watuonyeshe tuwasaidie nini. Sisi kwetu wanasema: "Ukibeba mtu mgongoni inatakiwa anayebebwa naye awe anasogelea juu, asiwe anaporomoka chini." Akiporomoka unamrudisha, anaporomoka unampandisha juu, basi mwisho unachoka unamweka chini.

**MBUNGE FULANI:** Unamwachia.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Kwa hiyo, sisi hatutaki kuachia, tunataka tusaidiane na wenzetu. Wizara hii ni ngumu, tunaona waliopita pale mambo waliyoyapata hata kama walikuwa ni Mawaziri *very strong.* Kwa hiyo, tusione kama ni jambo dogo, anaweza akaenda mtu yeyote pale akaona ni mzigo mzito. Sisi tunachotaka ni kwamba wao watuonyeshe njia wanataka tufanye nini katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, mmoja wetu ameongea hapa amesema tumeua na nguvu kazi. Ndiyo tumeua, maana wakulima ni vijana wetu, lakini asilimia kubwa sana ya vijana wako mijini na hawafanyi kazi yoyote ni kukimbiza soda, maji, *biscuit* na hii *institution* ni kubwa. Mimi naogopa, sijui macho yangu ndiyo yanayoona peke yangu, ukifika pale Chalinze vijana watavamia gari, ukienda Morogoro vijana wanavamia gari, *everywhere* vijana ni wengi. Tunafanya nini ili hawa vijana tuwape elimu, tuwazoeze wajue kwamba hiyo biashara wanayofanya haiwakomboi, ila labda waende hata kwenye mabonde ya Mto Rufiji, mabonde ya huko Malagalasi, yako mabonde mengi wakalime. Kama wangepata *guidance and counselling* nzuri wale vijana wangeweza kufika mahali wakasema: "Lakini kweli hii biashara tunayoifanya ni ya sifuri." Lakini ndiyo hivyo vijana tumewaacha, sijui watakimbia namna ile na zile bidhaa milele na milele na hatujui

kama watajikomboa. Kwa hiyo, tunataka mabonde haya yaweze kufanya kazi ya kumwagilia na katika kumwagilia kule tutapata chakula kingi sana, lakini kama tutategemea wazee tu waliobaki vijijini ndiyo waendelee kufanya kazi ya kilimo na vijana hawajifunzi kilimo kwa kweli tunafanya kazi ya sifuri. Itafika mahali fulani watu wote wako Mjini, basi hakuna kitu kinachofanyika. Hilo nilitaka nilizungumze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la nne ni suala la chakula. Wale ambao wanasoma *Qoran* na wanasoma Biblia vizuri wanakumbuka kwamba Farao alipolala na aliota ndoto akakuta ng'ombe wametokeza wanene na wakondefu, halafu wale waliokonda wakawa wanawameza wale wanene. Alipoamka akafadhaika sana, maana zamani ndoto zilikuwa na maana, siyo ndoto za leo hizi tumejaa dhambi ndiyo maana hazileti hata maana, zile ndoto zilikuwa za kitakatifu kabisa. Alipolala tena akakuta masuke, kama masuke haya ya mtama yako saba. lakini membamba na manene, yale membamba yakameza yale manene na akataka tafsiri ya ndoto hii. Alipoipata kutoka kwa mtu anaitwa Yusuf, alikuwa mfungwa akaambiwa: "Wewe hii ni dalili ya kuonyesha kwamba ndani ya miaka saba kutakuwa na neema kubwa sana katika nchi yako na ndani ya miaka saba inayofuata kutakuwa na njaa kubwa sana katika nchi yako. Kwa hiyo, sasa tafuta mtu atakayesimamia ukusanyaji wa chakula katika miaka saba ya neema ili saba itakayokuja yenye njaa muwe mnakula tu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, tafuteni watu wenye hekima na busara, wakae kila Mkoa wakihisi kwamba hapa kwenye Mkoa wetu kutakuwa na njaa, basi kila Mkoa uwe na eneo lake la kuhifadhi chakula, wawe wenyewe kwenye Mkoa, acha hii ya Taifa. Iwe ni kwenye Mkoa tu mfano Mbeya, Iringa, Arusha na kadhalika. Kuwe na hiyo mnasema *SGR* ipo kule. Tafuteni watu maana kunapokuwa na njaa mtaona kwamba kutakuwa na njaa, sasa hivi Mheshimiwa Mwaga amesema kuna njaa na rafiki yangu amesema kuna njaa. Hilo ni moja tunajua; je, tumejiandaa vipi katika kukusanya chakula kama hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, sisi katika Mkoa wetu wa Mbeya hatuelewi! Kulikuwa na kilimo cha pamba ambacho kimelimwa Mbeya Vijijini, Mbarali yote, sehemu ya Mbozi na sehemu nyingine mbalimbali hata kule Lindi na Mtwara, sehemu yote ya Kusini kule. Kilimo hiki kilianzishwa na Bryson akiwa Waziri wa Kilimo na Magani alikuwa Bwana shamba wa Mkoa wakati huo. Sasa ikatokea tangazo kwamba, mdudu ameonekana pale ambaye ni hatari anaweza kuruka kwenda Mikoa ya Shinyanga huko. Lakini Wananchi mdudu yule hawajamwona, wala shamba la huyo mdudu halipo, sasa Serikali imepiga marufuku na kwa hiyo Mkoa umeathirika kimapato ukilinganisha Chunya hawana kitu chochote ni jangwa tu kule. Pia, Mbeya Vijijini na sehemu nyingine, tunajumlisha pamoja na Kusini kwingine kule Lindi na Mtwara, hatuoni!

Mheshimiwa Spika, baadaye wananchi wametufuata sisi Wabunge wa Mbeya wamesema: "Kama hamwezi kuleta pamba hiyo ikalimwa maana sisi mdudu huyo hatujamwona, ninyi hamchaguliwi tena." Tumekaa kama Wabunge, lakini Wabunge wamenituma nipeleke kwenye Kamati ya Kilimo na Ardhi. Bahati mbaya kule mimi ni Katibu na huku ni Mwenyekiti. Sasa tumemwandikia Waziri barua, Kamati yangu ya

Kilimo na Ardhi imeamua kwamba Waziri wa Kilimo ajibu barua hiyo kwamba ni nani alitoa hiyo *order, GN* namba ngapi, mdudu alipatikana wapi, *research* gani iliyofanywa na mipango gani inafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo barua sijajibiwa kama Mwenyekiti wa Kamati. Humu hakuna kinachosemwa tena, kinachoelezwa kwenye pamba ukurasa ule unaeleza mambo mengine ya sehemu zingine. Sasa mimi nasema, mimi kama Mwenyekiti nimetumwa na Wajumbe na Kamati imeamua kwamba kile kilimo kilimwe. Malawi wanalima na wana-*control* yule mdudu na Malawi na Mbeya ni pua na mdomo, kama anaweza kutoka Mbeya basi hata kutoka Malawi anaweza kwenda tu kule kwa sababu ni pua na mdomo. Zambia wanalima ni pua na mdomo na Mkoa wa Mbeya na Msumbiji wanalima, lakini kama wale wana-*control* sisi tunashindwaje ku-*control?* Sasa Wananchi wa Mbeya wanaona ni hujuma kabisa kama wanavyosema wao. Ndiyo nia ya Serikali, lakini Wananchi wa kawaida hawawezi kuelewa kwa sababu mdudu hawakumwona na wala *research* sasa hivi haijafanywa na miaka yote hii hakuna kusema tumefanya *research* mdudu yupo au hayupo na tulime lini. Tunaomba Bunge hili litusaidie sasa. Mimi Mwenyekiti nimeandika, lakini hakuna barua iliyojibu na humu humu nasoma hamna kitu, kwenye hotuba hakuna kitu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kuogopa kabisa kama hatuwezi kujibiwa *yes or no,* naanza kuogopa. Sasa nasikia na tumbaku inaanza kuwa shida kule Chunya. Kwa hiyo, watakuwa wanakaa tu hakuna kitu chochote na Mwalyego Marehemu huyu juzi nilimpa karatasi kwamba: “Bwana karatasi hii tumeishamuandikia yule Waziri ameisoma.” Akasema: “Ngoja na mimi nitachangia.” Mungu amrehemu huko aliko na amepata shida sana Mwalyego ndiyo maana mimi nilipokuta amefariki pale, nilipata *shock* na kwa kweli nilishindwa hata kushiriki. Jamani, tuwe tunajibizana basi hata kama haiwezekani, lakini mdudu yuko wapi? Kwa nini Malawi wanalima? Kwa nini wana-*control?* Kwa nini Zambia wana-*control?* Kwa nini Msumbiji wana-*control?* Si tunapakana pale, sisi tunashindwa jamani ndugu zangu! Msitukamate ubaya, Mkoa utashindwa kuwaeleweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo alikuwa msemaji wa mwisho kwa asubuhi hii. Msemaji wa kwanza kipindi cha mchana atakuwa Mheshimiwa Kilontsi Mprogomyi, ajiandae na kwa kipindi cha wiki hii, vipindi vyote vya mchana mpaka Ijumaa vitakuwa vinaongozwa na Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Anne Makinda na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ili na wao wapate uzoefu.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa pole kwa msiba wa ndugu yetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyetutoka hivi karibuni, ninatoa pole kwa familia yake na kwa wapiga kura wa Mbeya Vijijini. Lakini pia ninatoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, ambao wamefiwa na mzee wao. Mungu azilaze roho zote hizo mbili mahali pema peponi. *Amen.*

Lakini pia ninatoa pole kwa wale ndugu zetu waliopata ajali, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, pamoja na Mbunge wa Mbalali, Mheshimiwa Estherina Kilasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na mimi nichangie hoja hii iliyopo mbele yetu kwani ni hoja muhimu sana. Mimi kwa kweli sijachangia hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula toka mwaka 2001. Leo ni mara yangu ya kwanza kuchangia hoja hii. Lakini ninachangia kwa sababu *I am overly disappointed* na hotuba iliyotolewa na Waziri wa Kilimo. Kwa hiyo, kwanza, mimi nina ugomvi na Hotuba ya Waziri wa Kilimo. Hotuba hii ina mapungufu mengi na sisi ni Wabunge, tunaowakilisha watu maskini kutoka vijijini na hayo mapungufu ni lazima tuyashughulikie. Kusema kweli mimi ninasema hivyo si kwamba hoja ya Wizara ya Kilimo na Chakula siikubali, ninaiukubali na ninaiunga mkono kabisa, lakini mipango iliyomo katika hotuba hii haiko sawa. *(Makofi)*

Mtoa hoja anazungumza kama naye ni mchangiaji. Ukiisoma naye anazungumza analalamika kama mmoja wa Wabunge ambao hawako *responsible for the implementation* ya programu hizi za Wizara ya Kilimo na Chakula. Nitatoa mifano, kwa mfano ibara ya pili, mipango ya kukua kwa kilimo hasa ile iliyoorodheshwa katika ibara hii nani afanye na nani atekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi nani awekeze katika kilimo? Wakulima wetu wameshafanya yale yote yanayopaswa kufanywa, wanachohitaji ni mazingira mazuri yanayowekwa na Serikali ili kuweza kufanya kazi nzuri katika kilimo, wapewe pembejeo na mambo mengine yafuate pamoja na mafunzo na vitu vingine anavyozungumzia Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Kwa hiyo, mimi ninasema Serikali lazima iwapatie wakulima pembejeo kwa wakati na kwa kutumia *institutions* zinazoweza kutoa pembejeo hizo kwa wakati unaofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 19 anazungumzia juu ya viwango kwamba, kiwango hicho kitaweza kufikiwa iwapo kilimo kitapatiwa mahitaji yake, nani awapatie mahitaji ya pembejeo, zana za kilimo na masoko ya uhakika? Viwanda vya sasa vya ukuaji wa sekta ya kilimo bado ni vya chini sana. Tunaomba Waziri huyu atupe matumaini maana na yeye kwa maneno yake haya anatukatisha tamaa.

Pia ibara ya 21, lengo la ukuaji wa sekta ya kilimo litafikiwa iwapo tutaongeza uwekezaji katika kuendeleza raslimali za uzalishaji, usindikaji, miundombinu, upatikanaji

wa masoko na kuimarisha usimamizi. Sentesi hiyo inarudiwa tena katika ibara moja baada ya hiyo anairudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anazungumzia habari ya Mikoa inayoweza kujitosheleza kwa chakula na ambayo haikupata ruzuku ya mbolea. Sasa ninachoomba hapa mikoa hiyo ipewe ruzuku hiyo ili izalishe zaidi na nchi ipate amani, nyumba za wananchi wetu zipate amani, maana nyumba yenye njaa haikosi kasoro na haikosi kelele. Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anasema tumhurumie huyu Waziri na tumuunge mkono, tunamuunga mkono, lakini tumhurumie kwa yepi? Kilimo hakitakuwa na manufaa maana yake ni kwamba, tukifanya hivyo kilimo hakitakuwa na manufaa kwa Watanzania wote. Umaskini utaendelea kuongezeka maana ni kilimo tu ndicho kinachoweza kuikwamua nchi hii na lindi kubwa la umaskini. Matamshi ya rafiki yangu, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, yanaonyesha kukata tamaa na mwisho wake Watanzania tutakufa maana hatima yake ni njaa kali itakayoleta vifo kwa Watanzania walio wengi.

Tukitaka kujikwamua na matatizo makubwa yanayokikabili kilimo kwanza, Wizara yenyewe, Mikoa, watalaam wawekwe katika *farm levels* . Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, alitembelea Mkoa wa Kigoma na anaujua sana Mkoa huu maana alikaa kwa miaka minane. Matatizo ya Mkoa ule anayajua, ameeleza mapungufu, anayajua mapungufu ya watalaam wa kilimo. Huyo anayeitwa mshauri wa kilimo katika Mkoa wa Kigoma sina uhakika kama huo uwezo unaomfanya kuwa mtaalam anao kweli, hana na pengine nchi nzima wataalam ni kama huyo. Sasa hicho kilimo kweli kitaendelea kwa maana ya utalaam huo unaozungumzwa ambao mimi ninautolea mfano kwa Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 68 inazungumzia habari ya matumizi ya mbolea, madawa na mbegu bora, yote haya ni *function* ya Serikali, ukiwapa utaratibu mzuri na kugawa mbolea kwa wakati unaofaa. Kwa mfano, vyombo vya Serikali kama vile *Tanzania Fertilizers Company (TFC)* na vyombo vya wananchi kama vile *TFA,* vina uzoefu mkubwa wa ku-*handle* usambazaji wa pembejeo. Waliopewa kusambaza mbolea katika nchi hii ni watu ambao huo uwezo hawana. Uwezo walionao huko Mikoani ni kidogo sana, lakini wamepewa *TFC* na *TFA,* walipouliza kwamba sasa tufanye nini wakaambiwa nendeni mkapige magoti kwa wale waliopewa, waombe huko na wanunue huko. Maana yake ni kwamba, hawa watu watakaponunua mbolea huko watainunua kwa bei ya juu na watakapoipeleka kuiuza kwenye maduka yao, hii mbolea pia itakuwa ya bei ya juu. Kwa hiyo, gharama za uzalishaji katika kilimo zinaendelea kupanda kwa utaratibu usiofaa, ambao unamkatisha tamaa mkulima. *(Makofi)*

Mimi ningefikiri kwamba, uwakala huu yangekuwa yamepewa haya mashirika. Ni vyombo ambavyo tungevi-*transform* na vingeweza kufanya kazi inayotakiwa. Kwa sababu hiyo, mimi ninasema tunahitaji maelezo fulani fulani yatolewe hapa ndani. Maana mengi tunayoyaona kama haya yanatia mashaka mengi. Sisi Wabunge mnapotuletea maamuzi ambayo ni *half cooked* mnatukwaza. Kwa nini Serikali haipendi kutumia *establishment* zilizopo zenye *capacity* nzuri na ambazo zilihitaji msaada mdogo kama zile za *TFA* na *TFC* kisha Serikali ikasimamia ipasavyo? Waheshimiwa Wabunge, labda

niseme kuwa, maneno ambayo yameandikwa katika hotuba hii ni *a tail of farm fallacies that will continue to hurt the poor in Tanzania.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia habari ya mipango ambayo kwa kweli hairidhishi ninaomba niwaambie kwamba, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa hivi karibuni alikuwa akifungua Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Biashara na Maendeleo kule Sao Paulo Brazil na ninaomba ni-*quote* baadhi ya maneno aliyotumia. Maana kama ni mategemeo ya kutegemea misaada na vitu vingine, basi tumekuwa tunategemea haya yatatokea. *"The world has had years of experience that have tought us what works and what doesn't. We have new technologies that protect the environment and spread a wealth of information, we have unprecedented political consensus around the millenium development goals. What we lack all two often is coherence. He stressed that policies ought not to give with one hand and take with the other. Rules designed to liberate or not to create new barriers, countries which press countries to liberalize trade should be willing to do the same themselves if they don't, we politely call it lack of coherence and we could just as accurately call it discrimination. (Makofi)*

Kwa hiyo, tunapoitegemea misaada wakati wote tunakaa tunategemea misaada ndiyo tuna-*implement* tunafikiri itatusaidia, *tell me,* huyu naye anayekwambia msaada huu kwa mkulima wake atafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayoyasema haya yana maana sana kwa kilimo chetu, mipango hakuna, *inputs* hakuna na watu karibu asilimia 90, ukizidisha asilimia 90 mara ile 35 milioni ya Watanzania unakuta Watanzania milioni 32 wanaishi vijijini na wanategemea kilimo. *Most of them are small farmers and northern agricultural policies are destroying the markets on which they depend.* Nchi tajiri zinatumia karibu dola bilioni 300 ambayo ni mara sita ya misaada wanayoitoa kwa nchi maskini. Sasa ukiangalia kama ningekuwa na muda nikaeleza yale yanayotendeka huko ni mazito sana, misaada yao ku-*subsidize* kilimo, ku-*support* kilimo ni mikubwa, sisi mpaka tuombe ruhusa kwa nani? Mipango yako unataka mpaka ipate *approval* kutoka nje, *why can't we do it ourselves? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kuomba Wizara ya Kilimo mwaka ujao watuletee hotuba ambayo inatosheleza, yenye maneno machache na inayozungumzia mipango ya kilimo ili tubaki na matumaini ya kukua kwa kilimo na kuondokana na umaskini na jinsi tutakavyofika huko kama tutakuwa *in control of the policy space,* maana kinachotupa tatizo hapa ni *policy space. Are we in control of our development dimension, our development policies et cetera? This is a very important aspect of the development of Tanzania. (Makofi)*

Sasa ukurasa wa 83 anazungumzia juu ya ubinafsishaji. Kwanza, katika haya yote *challenge* ya kwanza ni *Tanzania Food Security.* Lakini tumejifunza nini kutokana na misaada, *economic reform with liberation?* Ni vyema tuka-*mainstream trade with poverty reduction with coherent policies* ya sera zetu, zikiwa na uwiano tutafanya mengi mazuri kwa Tanzania. Kilimo ndiyo msingi wa kufanya yote tunayotaka kuyafanya katika nchi hii, hakuna njia nyingine ni kilimo tu.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka kutoa mfano wa nchi kama Cambodia. Miaka kumi iliyopita Cambodia wali-*liberalize* na wali-*reform economy* yao. Lakini walisema nini? Waliamua ni kweli tuna-*encourage investment* lakini *investment that belong to Cambodian Nationals,* mtu mwingine akija lazima aingie *joint venture* na watu wetu. Lakini mambo ya kusema unawapa *wholesale,* miaka ijayo hadithi itakuwa tofauti, humu ndani tutakuwa tunazungumza hadithi tofauti. Ukiwa na *private sector, run after it* usii-*guide private sector,* iache ifuatilie wanafanya nini kisha ui- *integrate provisional strategies* zako ziwe *linked* na *National Strategy then you have a program* ya *development* ya sekta muhimu unazozihitaji kisha hizo zote ziwe *linked* pamoja Kitaifa. Haya ndiyo mambo muhimu kama unataka ku-*gain from the liberation strategy and so is the globalization strategy* ambayo tunaizungumzia na tunai-*embrace*. *We in Tanzania, should understand that it is only true that international finance institutions do provide only a tool, gains from international trade can not be delivered by comparative advantage but by competitiveness.* Sasa hili siyo tena swali la *comparative advantage* ni *competitive advantage. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja na niwapongeze kwa hayo waliyofanya lakini mwaka kesho wafanye vizuri zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kama ilivyoandikwa katika hiki kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni machache. Kwanza, ninataka nichukue nafasi ya kutoa salamu za rambirambi kwa wafiwa wa marehemu rafiki yangu, Mheshimiwa Yete Mwalyego.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ninataka niuelekeze kwa wakulima wadogo wadogo. Asilimia 80 ya Watanzania, wanaoishi vijijini ni wakulima na wakulima hawa wanaishi katika hali mbaya sana. Tukichukua idadi ya Watanzania wanaoishi Mijini na Vijijini wengi wao wanawategemea wakulima wanaoishi vijijini, kwa sababu wakulima ndiyo wanaoishi vijijini na ndiyo wanaolima kwa kuwategemea watu wa mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka mchango wangu niuelekeze kama ifuatavyo: Serikali ingekuwa na lengo la kuwa mkulima alime sehemu ndogo, avune mazao mengi, huo ndiyo ungekuwa msimamo mzuri wa Serikali. Sasa katika ukurasa wa 66 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaelekea kuwa hakuna malengo yaliyopangwa kwa mkulima alime sehemu ndogo, avune mazao mengi. Sasa nafikiri Serikali ingekuwa na mpango huo kwamba wakulima wengi sasa hivi wanaolima wanajilimia tu, mtu analima hekta kumi au hekta moja, lakini mazao anayovuna hayatoshi. Sasa nafikiri Serikali ingekuwa na mpango wa kuhakikisha mkulima huyo huyo analima sehemu kidogo, anavuna mazao mengi, hapo tungeondoa umaskini na wakulima wetu wangefaidika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mbolea. Serikali tunaishukuru kwa kupunguza bei ya mbolea, lakini upunguzaji wenyewe mpaka sasa hivi ninafikiri mbolea si chini ya shilingi elfu 20,000/= kwa mfuko mmoja. Jambo la kujiuliza ni kwamba, je, wananchi wanaweza wakaununua huo mfuko? Jibu ni kwamba, hawawezi. Sasa kama hawawezi Serikali itabidi ifanye kazi ya kupunguza bei ya mbolea angalau iwe shilingi 5,000/=, au shilingi 7,000/=. Sasa kama hailipi basi tutafute njia za kufidia ili wakulima walio wengi waweze kununua hii mbolea. Lakini hiyo mbolea, kuna mbolea zina chumvi nyingi hazihitaji kununua kwa mfano mbolea ya mboji, mbolea ya samadi, ni kazi tu ya Wizara ya Kilimo kupeleka watalaam wake huko vijijini wawafundishe wananchi wetu kutumia hizi mbolea. Nafikiri wakifundishwa kutumia mbolea ya samadi na kutumia mbolea ya mboji wala watu hawatakuwa na haja ya kununua hii mbolea ya Serikali. Hilo moja. *(Makofi)*

Lakini lingine juu ya mbolea hiyo hiyo ya samadi, kazi ya mbolea ya samadi na mbolea ya mboji ni kuilinda ardhi isiharibike. Kuna mwenzangu Mheshimiwa Mbunge mmoja, alikuwa akizungumzia juu ya mbolea ya chumvi chumvi. Kuna ushahidi ulio hai kuwa mbolea ya chumvi chumvi baadhi ya maeneo inaharibu ardhi. Sasa ni vyema Serikali ingefanya utafiti, je, katika ardhi fulani tutumie mbolea gani? *(Makofi)*

Kwa mfano tuchukue mfano wa madaktari tu hospitalini hawababahatishi hata kidogo, huwezi kutibu mgonjwa wakati huna uhakika na ugonjwa alionao. Sasa ni vyema tungehakikisha hii mbolea tunayoipeleka huko vijijini inakidhi mahitaji ya ardhi? Kwa maana hiyo, nataka niseme kwamba, Watalaam wa kilimo ni lazima wafanye utafiti wa udongo, wahakikishe kuwa mbolea inayotumika pale, ni mbolea inayokidhi haja ya ardhi ile inayotumika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka nizungumzie suala la kitaalam kidogo, mtanisamehe kwa sababu na mimi ninatokea huko huko, kuna *erosions* za aina tatu, kuna *shit erosion, wind erosion* na *soil erosion.* Sasa wenzetu wa Wizara ya Kilimo sidhani kama waliwafundisha wakulima wetu hizi *erosions* katika vijiji. Endapo hawakufundishwa unaweza pengine ukapeleka mbolea kwenye *wind erosion* halafu ikaondoka au kwenye *soil erosion* ukapeleka mbolea yako ikaondoka. Je, Wizara imefanya utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba, ukulima huu na matumizi haya ya mbolea yanatumika kama inavyotakiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninataka nizungumzie matrekta. Wakulima wengi sasa hivi wanatumia majembe madogo madogo ya mkono, halafu mara nyingine tunasema kuwa wataondokana na umaskini, sidhani kama wataondokana na umaskini wakati pengine mtu analima mita minne, mita sita, kwa siku, halafu umaskini utaondoka lini? Mimi ninafikiri kwa sehemu zile ambazo yanafika matrekta, Serikali ingeweka lengo la kuhakikisha kuwa kilimo cha matrekta kinapewa kipaumbele. Matrekta hayo hayo lazima tutofautishe, kuna wengine wana uwezo, lakini kuna wengine hawana uwezo. Sasa Serikali ingepanga mipango maalum ya wale wavuja jasho au wanyonge wasaidiwe kilimo cha matrekta ili na wao waneemeke katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni kwamba, wakishavuna wananchi, maana umeshafanya kazi zote za kusaidia mbolea, kilimo kiko tayari, mavuno tayari, sasa suala la kujiuliza ukishavuna mazao yako unakwenda nayo wapi? Kuna wakulima wengi tu hapa wanaweza wakalima lakini wakishalima hawajui wakauzie wapi mazao yao. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya Kilimo na Chakula, pamoja na Wizara ya Ushirika na Masoko, ziwe na uhakika wa mazao ya wakulima yatauzwa wapi. Kwa mfano, pale Mbeya kuna watu chungu nzima wana vyakula, wana mchele, wana ndizi, lakini hawajui wakauzie wapi sasa. Lakini kama kungekuwa kuna mpango maalum wa kuwatafutia masoko basi mtu angelima kwa nguvu zote na bidii zote akimaliza kuvuna anatafuta mahali anauza. Kwa hiyo, suala la soko lingesaidia zaidi katika kuhakikisha wakulima wetu wakilima wapi watapata soko la kuuzia bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumzia ni kwamba, sisi tuna wataalam wa kilimo katika vijiji. Lakini suala la kujiuliza hivi hawa watalaam wako vijijini au wako maofisini? Nasema hilo kwa sababu ili mtaalam aelimishe kilimo cha kisasa au kilimo bora lazima na yeye aonyeshe shamba lake. Lazima aonyeshe shamba langu mimi hili hapa. Sasa hii itaisadia kama mnakwenda kwenye bonde kuna mtaalam na yeye atafute shamba lake, atofautishe faida ya kulima kwa utaalam na hasara ya kulima bila kutumia utalaam. Nafikiri tukifanya hivyo, watu wengi wataweza kuelewa utaalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wananchi wengi ukizungumza utalaam wala hawakuelewi kabisa, hawaelewi kabisa kuwa utalaam ni kitu gani. Sasa mimi ninasema Maafisa wa Kilimo waende huko vijijini watafute mashamba kwenye mashamba ya wanyonge walime kitaalam ili wakulima waone mfano. Wakulima wakishaona mfano, ukimwambia mtu alime kitalaam atakuelewa. Lakini wewe unakwenda kule unamwambia lima kitaalam, wewe mwenyewe hulimi, sasa utalaam huo ataupata wapi? Kwa hiyo, mimi naomba watalaam wa kilimo waende vijijini wakalime mashamba kwa kitalaam ili na wakulima na wao watofautishe kulima kwa utalaam na kutolima kwa kitalaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi sasa hivi wanapata matatizo ya mavuno kutokana na kutokuwa na uhakika wa mapato. Mtu anaweza akalima, kwa mfano, kule kwetu tunatumia eka, unaweza ukalima eka moja ya mpunga ukavuna gunia moja, kumbe kisheria eka moja unatakiwa uvune magunia 14 au zaidi mpaka magunia 25. Wako wakulima wadogo wadogo wanaovuna hivyo? Sasa hiyo ni kazi ya Wizara ya Kilimo na Chakula kuhakikisha kuwa, mkulima analima anavuna magunia zaidi ya 12, 14 au badala ya mkulima kuvuna ile mbegu aliyopanda tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niishie hapo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe maoni yangu katika hoja hii ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

Kwanza kabisa, ningependa niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha ghafla cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye Mwenyezi Mungu, amemchukua. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Kalenga, ninaomba nitoe pole zangu kwa familia ya marehemu, pamoja na wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Namwomba Mwenyezi Mungu, ampe raha ya Milele Mbinguni. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaunga mkono hoja hii. Lakini nina ushauri ambao ningependa kuutoa kutokana na matatizo mbalimbali ambayo tunayapata katika kilimo. La kwanza ni juu ya mbolea, hasa hii mbolea ambayo tuliinunua na kuweka ruzuku ili tuweze kuipeleka kwenye mikoa minne ambayo ingeweza ikawa kama *security* ya kupata chakula cha kutosha kwa Taifa zima. Sasa mimi nisingependa nizungumzie yaliyotokea, lakini hilo la msingi ni kwamba, inatupasa yaani hasa Serikali kuhakikisha kwamba, baada ya kufanya maamuzi hayo ya kuweka ruzuku kweli wakulima wapate mbolea kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Pili, mbolea hii iagizwe kutoka huko nje inakonunuliwa mapema na iwafikie wakulima mapema. Sasa kama ule mfano uliotolewa na Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega kwamba, amepata kwenye mtandao kwamba huko Dubai mfuko mmoja wa mbolea wa kilo 50 ni shilingi 8,000/=, kama haya maneno ni ya kweli, basi hakuna sababu zozote za kiuchumi au sijui za utalaam wa aina gani ambazo unaweza uka-*justify* bei ya kufikia shilingi 20,000/=, shilingi 25,000/= au shilingi 30,000/=. Unafikiaje hapo kama bei ni shilingi 8,000/=? Sasa hayo yanayoongezeka huwezi kufika huko, haiwezekani. Kwa hiyo, kuna tatizo hapa la msingi. *(Makofi)*

Sasa katika mambo ambayo ni ya muhimu kama kilimo ni muhimu sana kwamba hatuachii nguvu za soko ndiyo zituamulie mambo yote, kwa sababu hawa wafanyabiashara wakubwa huwa wana-*gang up,* wanaunda *cartels* na kupandisha bei za pembejeo. Kwa hiyo, mkulima anakuwa amebaki peke yake, anabaki mkiwa, hakuna mtu wa kumsaidia na sisi tunasema hivi ni lazima tuheshimu nguvu za soko kama vile imekuwa ni ibada. Katika masuala kama haya, lazima Serikali iingilie kati ifanye *intervention (Makofi)*

La kwanza, ninapendekeza kwamba, tuiimarishe *Tanzania Fertilizer Company (TFC),* kama chombo cha Serikali, kipewe nguvu na kiagize mbolea. Hii mbolea tunayotegemea ya wakulima wadogo hii iagizwe na *TFC* ya kutosha kutoka huko nje pamoja na Minjingu. Halafu *TFC* isitosheke na kufikisha mbolea kwenye vituo vya mikoa kwa mfano, Mkoa wa Iringa kufikisha Mjini Iringa na Makambako halafu wanaona kazi yao wamemaliza, haiwezekani! Kwa sababu ikifika hapo kwanza unaruhusu wale wafanyabiashara wakubwa walioshindwa kule Dar es Salaam watakuja kuichukua kule na kuuza sasa kwa bei wapendazo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, *TFC* iwe na wajibu wa kufikisha mbolea vijijini, iwe na mawakala vijijini, kwa mfano, kama Vyama vya Ushirika na wakulima wengine ambao wanaweza wakafanya biashara hiyo wakawauzia wananchi wengine kama mawakala wa *TFC* na

*TFC,* ihakikishe kwamba mbolea kweli imefika vijijini, isitosheke na utaratibu maana tumeweka utaratibu, lazima wahakiki.

Sasa wafanyabiashara wakubwa waruhusiwe na wao kununua mbolea kama kawaida, halafu washindane bei na bei hii ya *TFC* ambayo lazima itakuwa ni nafuu. Kwa hiyo, ni wazi bei zitashuka chini. Mimi sio mchumi lakini nafikiri *it makes sense.*

Jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni mikopo kwa wakulima. Kwanza, ninatoa shukurani kwa Serikali kwamba katika Jimbo langu la Kalenga, Vyama vya Ushirika vimepata mikopo kutoka Mfuko wa Pembejeo wa Taifa kupitia *SCCULT* na safari hii naona mipango ipo kama ya mwaka 2003 kwa mkondo huo wa *SCCULT*. Ni wazi wakulima wetu hawataweza kutoka katika limbo bila kuwawezesha kupata mitaji. Azimio la Arusha linasema ili tuendelee tunahitaji vitu vinne. Sasa hivi tumeongeza kwamba, kunahitajika kitu cha tano nacho ni mitaji na hakuna mbadala wa mitaji. Kwa hiyo, lazima wapate mikopo kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo limenishangaza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ambalo limeachwa ni juu ya mipango ya mikopo kwa wakulima, ni hili lifuatalo: Mwanzoni mwa mwaka huu tumepitisha Sheria ya Ardhi kurekebisha Sheria ya Ardhi ili kila mwanakijiji mwenye shamba aweze kupata hatimiliki kupitia Serikali zao za Vijiji ili hati hizi zitumike kama dhamana kwenye mabenki *(collateral),* waweze kukopa. Walengwa katika marekebisho haya ni wakulima, yaani hawa wakulima wadogo ambao Wizara hii ndiyo inawashughulikia. Sasa zana imetolewa hii hapa, lakini katika mipango ya Wizara sikuona *any operational plan* itakayowaongoza wakulima ili waweze kupata mikopo kupitia hatimiliki za Vijiji. Ukiacha kupima ardhi yenyewe ambayo ni suala la wataalam wa Wizara ya Ardhi, lakini vile vile kuandaa mabenki yetu. Mabenki yameandaliwa yapokee hizi hati? Maana wanaweza wakakataa ukakuta pengine ni *Exim Bank* peke yake ndiyo inayokubali kupokea hati hizo na Benki yenyewe ni ndogo namna hiyo. Kwa hiyo, ninashauri kwamba, wataalam wa Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ardhi na Wizara ya Fedha, wangekaa pamoja wakaandaa *an operational plan* inayoweza ikatekelezwa. Pengine wanaweza wakaoanisha na huu Mradi mpya, Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji *(Participatory Agricultural Development and Empowerment Project),* ambao ni mpango mzuri.

Suala la tatu ambalo ningependa nilizungumzie ni juu ya kilimo cha umwagiliaji. Nasisitiza maoni ambayo niliyatoa wakati wa hoja ya Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango kuwa, kwa vile nchi yetu ina uwezo mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji kwamba unaweza ukamwagilia zaidi ya hekta milioni 29, lakini sasa hivi tunaweza tu kumwagilia zaidi ya hekta laki mbili. Kwa hiyo, ili tuweze kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa nguvu sana, lazima tufanye mabadiliko ya sera kwamba, *source* kuu ya upatikanaji wa umeme huko miaka ijayo iwe ni makaa ya mawe na *gas*. Hiyo ndio iwe *source* kuu. Mwenyezi Mungu, ametupa makaa ya mawe ya kutosha kule Mchuchuma, *gas* ya Songosongo, *Mnazibay* na nyingine, pengine tutagundua huko baadaye. Kwa hiyo, maji yawe ni *source* ya ziada na sio *source* kuu. Kwa hiyo, ukiacha matumizi ya maji majumbani na mifugo, nguvu kubwa ielekezwe katika kilimo cha umwagiliaji na tusiwe tunagombania maji kama sasa ambavyo maji ni *source* kuu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Iringa yote ikiwa ni pamoja na Jimbo zima la Kalenga, kilimo cha umwagiliaji kinawezekana sana. Zaidi ya miradi michache iliyopo na inayokamilishwa, tunaweza tukawa na kilimo cha umwagiliaji, kwa mfano, Magubike tunaweza kuwa na mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji. Tarafa nzima ya Kiponzero, halafu mabonde ya Vijiji kwa mfano Vijiji vya Isakalilo, Tosamaganga, Kalenga mpaka Mkoga, bonde hilo lote linaweza likamwagiliwa. Unaweza vile vile ukaunganisha na Kijiji cha Mangalali pamoja na mabonde kama Weru, Kibebe, Ibangamoyo na Kalenga inaunganika. Halafu kuna mabonde ya Vijiji vya Tanangozi, Wenda unaunganisha na Tosamaganga na *system* ya Kalenga. Kuna mabonde ya Kaning'ombe, Sadani, unaunganisha na Tosamaganga. Kuna mabonde ya Ibumila, Mgama, Lyamgungwe na Kikombwe, eneo hilo lote linaweza kuwa ni eneo kubwa la kilimo cha umwagiliaji. Halafu bonde la Lwiga kwa ajili ya Vijiji vya Ikuvilo, Nyabula na Tagamenda. Halafu Bonde la Maguliwa na kadhalika. Hiyo ni mifano tu. Hili ni Jimbo tu la Kalenga, hujaenda Jimbo la Isimani, hujaenda Kilolo wala sehemu nyingine. *(Makofi)*

Jambo la nne ambalo ningependa kulizungumzia ni kilimo cha tumbaku ambapo kwa Wilaya ya Iringa tumbaku hulimwa katika Jimbo langu. Huko nyuma kilimo hiki kilikuwa na matatizo makubwa sana. Bei zilikuwa ni za chini sana na mikopo iliyokuwa inatolewa ilikuwa ni ya masharti magumu kwamba, mkulima akikopa, akilipa ule mkopo, basi anaishiwa kabisa. Kwa hiyo, kilimo cha tumbaku kilikuwa *not sustainable.* Kwa hiyo, wakulima wakubwa kutokana na matatizo hayo *production* ilishuka sana na kwa wakulima wadogo kilimo kilikuwa karibu kimekufa.

Ningependa nimshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Charles Keenja kwamba, mwaka 2003 nilimwomba niwalete wakulima wakubwa kutoka Chama cha *Southern Highlands Tobacco Growers Association* na niliwaleta tukaonana hapa Dodoma na baadaye akaungana vile vile na Mheshimiwa *Sir* George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko. Baada ya mazungumzo yetu kuna mambo mengi sana yamefanywa. Kwanza, hawa wakulima wakubwa na wadogo walikubaliana na ushauri wangu kwamba, washirikiane wawe na umoja. Wote ni wakulima wa tumbaku, kwa hiyo, wasiwe wanakwenda *in different ways*, wale wanunuzi wanaweza wakawahujumu, wawe kitu kimoja.

Halafu vile vile tukapata mnunuzi mwingine wa tumbaku ambaye ni wa kampuni inayoitwa *Dimon,* ambayo ilikubali kununua kwa bei nzuri na vile vile kutoa mikopo kwa masharti yaliyo nafuu. Kwa mfano, anatoa mbolea kwenye vikundi lakini kila mmoja anachukua kutokana na kilimo chake kwamba eka moja anatoa mifuko minne ya *NPK,* halafu anatoa mfuko mmoja wa *CAN* kwa ajili ya kilimo cha mahindi. Yaani lima ekari moja ya tumbaku, lima ekari moja ya mahindi usije ukasahau chakula. Halafu vile vile huyu mnunuzi ameleta mpango mkubwa wa upandaji miti ukiwa *funded* na *Dimon.* Kwa hiyo, miti hii inapandwa inakuwa mali ya wakulima halafu ndiyo itatumika kukaushia tumbaku. Tulifanya uhamasishaji mkubwa wa kilimo hiki kwa msimu uliopita tukiwa tumeandamana, yaani mimi kama Mbunge wao, hawa *Southern Highlands Tobacco Growers Association,* wakulima wadogo, *Dimon* na Maafisa Kilimo, tulipita kwenye

Vijiji mbalimbali katika Kata ya Kiwere, Mangalali, Nzihi, Magubike na kadhalika na wengi wameweza kuitikia wito wetu. Matokeo yamekuwa mazuri sana. Uzalishaji wa tumbaku kwa wakulima wakubwa na wadogo umekuwa mkubwa sana *(Bumper Crop)*. Ni mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii mchana huu nichangie katika hoja hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda nitoe pole na rambirambi kwa familia ya Marehemu Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyefariki ghafla hapa Dodoma wiki iliyopita na nimwombe Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi, *amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niwapongeze wenzetu wa Wizara ya Kilimo kwa bajeti yao waliyotusomea leo asubuhi. Ukiisikiliza bajeti hii na kama hujasikiliza bajeti nyingine huko nyuma, utaona kwamba, matatizo yote ya wakulima yamemalizika. Lakini mwaka wa 2001 Wizara hii tuliwapa shilingi bilioni 24 na mwaka uliofuata tukatoa shilingi bilioni 34, mwaka 2003 shilingi bilioni 54 na mwaka huu wa 2004 tutawapa shilingi bilioni 60. Lakini kama ukiangalia kazi ya mwaka 2003 na mwaka 2002, hazina tofauti na mwaka 2001. Sababu yake hasa ni nini? Sababu yake hatuna Mpango wa Maendeleo wa kilimo wa nchi yetu. Hatuna! Tunataka kuendeleza kilimo kwa kutoa fedha nyingi tu, lakini fedha hizi hazisemi kwamba tutafanya nini wakati tukishazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kabisa kwamba hapa ndio tungeanzia halafu tukishakuwa na mpango tuseme gharama ya mpango ni shilingi ngapi halafu sasa ndio tuchukue bajeti tuweke huko kwenye mpango, tutekeleze kitu tunachokihitaji. Lakini hapa tunaletewa pesa tu, hakuna mahali patakapowekwa, panawekwa huku, panawekwa huku mwaka unakwisha huoni kitu. Kwa hiyo, tuanzie hapa, tuwashauri wenzetu watutengenezee mpango wa kuendeleza na kuboresha kilimo hapa nchini. Tutengeneze *National Agricultural Modernization Program,* ambayo ita-*modernize agriculture* na tuwe tunajua tunataka ku-*modernize* mpaka wapi, sio tunatoa fedha tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu lazima uanzie kwenye Wilaya, kila Wilaya iwe na *District Agricultural Modernization Program* yake na Wilaya katika Mkoa ziunganishe ziwe na *Sub-Program* ya Mkoa ya kuendeleza kilimo. Halafu ndio tuwe na mpango wa nchi nzima utakaoratibu mipango hii ya Wilaya moja moja. *(Makofi)*

Sasa tunayo mipango rejareja imetajwa reja reja. Mpango wa *PADEP* mwaka 2003 tuliongea hapa tukakubaliana kwamba, mpango huu una fedha nyingi, uanzishwe nchi nzima na Mheshimiwa Waziri alikubali. Leo tunaambiwa imeongezwa iko Mikoa

sita. Nikaenda nikasoma Jedwali Na.7 nikakuta mpango huu wala haufiki Wilaya 30 zile tulizoambiwa mwaka 2003. Tunataka kutumia Shilingi bilioni 76 kwa ajili ya mpango huo. Sasa mwaka huu tumeletewa jipya hapa, mpango mwingine unaoitwa *DASIP* nao unakopa Shilingi bilioni 57. Jumla ya pesa hizi zote ni Shilingi bilioni 143. Sasa fedha zote hizi kwa nini tusiwe na mpango wa nchi nzima? Ukifanya hesabu juu ya bahasha, maana hotuba tumeisikia hapa leo, utakuta kila Wilaya kati ya Wilaya 117, hata Dar es Salaam muwape pesa hizo, kila moja itapata Shilingi bilioni 1.22. Fedha hizi ukizichukua kwa mpango wa miaka mitano, kila Wilaya itapata Shilingi milioni 245 kama unapeleka kwenye Mikoa yote na Wilaya zote. Sasa kitu gani hiki mnatuletea vitu vya rejareja hapa? *I am very serious about this!* Lazima mwende mkapange upya, msiwe na mipango ambayo tunakuja Ofisini kwenu tunawaomba bwana utaleta lini kwenye Wilaya yangu? Tunakopa fedha hizi na tutalipa wote. Lazima fedha hizi zitumike vizuri, zisitumike kununulia magari ya kifahari kwa wataalam, zisitumike kununua *computers* mpya, nyingine zinaangalia chini na nyingine zinaangalia juu, zisitumike kwa shughuli za kiofisi. Katika Bajeti hii mnaomba tuwape Shilingi bilioni 64. Fedha hizi zinatosha kufanya mambo hayo. Hizi za mikopo tupeleke kwenye Mikoa zisaidie katika kuendeleza kilimo cha nchi hii. Hatuwezi kuendeleza kilimo kwa kufanya vitu vya reja reja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili ninashauri kwa nguvu kabisa kwamba, mpango wa fedha hizi hizi utengenezwe, hakuna haja ya kuleta nyingine. Fedha ziko hapa za kupeleka teknolojia, pembejeo, mbegu bora, madawa, matrekta na vipuri kwa wakulima. Ni vyema Waziri akituahidi hapa afanye kama anavyotuahidi. Ametuahidi *PADEP* itakwenda nchi nzima, leo haikwenda. Tunataka maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa kusema, hili ninapenda kuipongeza sana Wizara ya Kilimo kwa hatua ambazo zimechukuliwa na mahali walipofika katika kutekeleza azma ya kusambaza kilimo cha umwagiliaji hapa nchini. Ninadhani hili wamefanya vizuri. Kitu ambacho kinatukwamisha ni *speed* tunayokwenda na kiasi cha fedha ambazo tunaweka kwenye mpango huu. Mwaka huu tumetoka kwenye njaa. Sasa watu wenye njaa nadhani wangekuwa wanaona njaa kama changamoto ya kufanya mipango, tusirudi tena njaa itokee. Tusiende tena kwa Mheshimiwa William Lukuvi, kila siku kuomba chakula, ni aibu kubwa. Tunahitaji ili tufikie mahali tunaweza kujilisha. Kwa kubadilisha *speed* ya *investment* tunayofanya sasa. Kwa *speed* ya uwekezaji wa sasa tunahitaji miaka 15 ndio tuweze kujitosheleza kwa chakula kwa fedha ambazo zimewekwa kwenye Bajeti hii. Kama tunakwenda kwa *speed* hiyo na ili tufikie kiwango cha kumwagilia hekta laki tano tunahitaji miaka 15. Sasa kwa nini tufanye hivyo? Tuongeze *speed* ya uwekezaji. Mimi ninashauri kwamba, tu-*invest* kabisa maana tunahitaji kuwekeza kama Shilingi bilioni 40 ili tuweze kujilisha kwa umwagiliaji. Hata tungefuta hii *PADEP* tukaweka pesa huko tungeweza kufika huko. Lakini hakuna haja ya kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji tuweke Shilingi bilioni tisa mpaka kumi kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano katika umwagiliaji ili tufike mahali tusimwombe mtu chakula na tusilale na njaa. Tunahitaji tu-*invest at that level,* tuwekeze kwa Shilingi

bilioni nane mpaka kumi kwa kipindi cha miaka mitano ili tuweze kufikia kiwango cha hekta laki tano chini ya umwagiliaji. Tukifika hapa hatuwezi tena kwenda kumwomba mtu chakula. Uwezo wa kuwekeza shilingi bilioni kumi tunao. Nitoe mfano mmoja tu, hata kama unatoka nje ya Bajeti hii. Wakati *Geita Gold Mine* na *Kahama Mining Corporation* walipoanza kuchimba na kutoa dhahabu, bei ya *ounce* moja ya dhahabu ilikuwa chini ya Dola 300. Leo *ounce* moja ya dhahabu inazidi Dola 400. Sasa *windfall* hii wanachukua wenyewe? Lazima tugawane na kama tukigawana *windfall* hii, tunaweza kuwekeza kwenye eneo hili bila matatizo yoyote. Lakini hata nje ya hapo, katika Bajeti tunaweza kuwekeza na tukaweza kutekeleza azma hii kama kuna mpango, lakini kama tunafanya hivi hivi tu hakuna mpango, hatuwezi kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninataka niliseme kidogo ni kuhusu chakula cha njaa na mbolea. Tumeelezwa katika Bajeti hii kwamba, kodi nyingi za kilimo zitaondolewa na tumeelezwa kwenye Bajeti ya Waziri wa Fedha kwamba, kodi nyingi zitaondolewa. Lakini *experience* yetu ni nini? Chakula cha njaa kilicholetwa hapa nchini kiliondolewa kodi zote. Lakini chakula hicho kimepanda bei, kimezidi chakula kile ambacho hakikuondolewa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mbolea katika Soko la Dunia, kule Dubai alikosema Mheshimiwa Lucas Selelii leo asubuhi, kabla ya kupanda bei ya mafuta ilikuwa ni Dola tano mpaka sita kwa gunia la kilo 50. Lakini mbolea hapa nchini ni Sh.25,000/= inakuwaje? Sasa tunaambiwa kwamba, watu waliopewa tenda ya kununua chakula walichaguliwa. Tenda ya chakula cha njaa haikutangazwa wazi. Sasa tungependa tuelezwe ni kwa nini na tusiambiwe njaa ilikuwa nyingi tukafanya haraka, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mbolea kama alivyosema Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ilipewa watu ambao hawana uzoefu na kilimo cha nchi hii. Kwa nini? Tunataka tuelezwe na hatutaki tuelezwe kwamba ni kwa sababu ilikuwa inatakiwa haraka, maana haikuja haraka. Sasa ni namna gani kodi hizi ambazo zimeondolewa zitamletea ahueni mkulima kama chakula cha njaa kilichoondolewa kodi kimekuwa ghali zaidi ya chakula ambacho hakikuondolewa kodi? Mkulima atapataje ahueni? Kwa hiyo, lazima Wizara ituambie kwamba itachukua hatua gani za kuhakikisha kweli mbolea ambayo imeondolewa kodi ikienda kule Mwanga itakuwa mbolea rahisi? Lazima tuambiwe! Haiwezekani tukae tu tunasema tumeondoa kodi ya pembejeo, tumeondoa kodi ya mbolea halafu mbolea ikija ni Sh.30,000/= badala ya kuwa Sh.10,000/=. Lazima tuelezwe hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nimalizie kidogo, labda unipe na dakika mbili maana wamenitibua hawa. Lakini tungependa kabisa na hili nasema wazi kabisa kwamba, zabuni hizi za pembejeo, mbolea, vipuri na mambo mengine lazima viwe wazi. Haiwezekani tualikane marafiki tulete tenda kwa ajili ya kuwahudumia wananchi, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni pesa hizi za barabara za kahawa za *STABEX.* Hizi zimeandikwa hapa, mimi sikubali kwamba kuna Mwingereza anatoka

huko London anajua barabara za Mwanga za Kahawa kuzidi Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga. Mimi sijui hiyo na hili sikubali kabisa. Huyo Mzungu sijui anaitwa Stentom mfukuzeni kabisa! Haiwezekani pesa ambazo tunaambiwa tutapewa mwaka 2003, mwaka mzima umekwisha, mwaka huu unakwisha hakuna pesa, wakulima wanataka pesa zao za barabara hapa hakuna. Tunaambiwa hapa hadithi tu, kuna Mzungu ametoka London amekuja. Hatuwezi kukubali mambo haya! Mwambieni yule Mzungu arudi kwao, tunataka fedha hizi zipelekwe kwenye Halmashauri zetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, jioni hii ili nichangie katika hoja ya Waziri wa Kilimo na chakula. Lakini kabla ya kuanza mchango wangu, nitoe salamu za rambirambi kwa msiba wa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, alikuwa jirani yetu hapa, amefariki ghafla. Nitoe salamu hizi kwa mkewe, pamoja na Wananchi wa Jimbo lake la Mbeya Vijijini. Tunawapa pole sana, tunawaomba wavute subira, hii ni mipango ya Mwenyezi Mungu, hatuwezi kuizuia.

Baada ya kutoa pole hizo, sasa nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, ambaye Wizara yake iko katika Kamati yangu ya Kilimo na Ardhi. Ni kweli tulikuwa tukifanya naye kazi katika Wizara hiyo katika mazingira magumu kwetu na kwake. Lakini katika Bunge hili ningependa kuchangia yale ambayo yanawahusu wananchi wetu ambao wanatusikiliza katika Bajeti hii ya kilimo. Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, leo wanasikiliza wataletewa nini kutoka kwa Wizara ya Kilimo na Chakula na hasa kwa sababu ni miezi michache tu wamenusurika na baa la njaa wakati Wizara ya Kilimo na Chakula ipo na wao wanakufa na njaa. Nchi hii ina mito mingi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, tuna maziwa mengi, tuna milima mingi ya kuvuna maji ya mvua lakini wananchi wanakufa na njaa. Leo wanasikiliza tunaongea nini hapa.

Lakini pamoja na hayo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea Bajeti yake hii ambayo ina mambo mengi mazuri humu ndani, hayana mpangilio, hayana mpango wowote kwetu. Vile vile nimpongeze kwa sababu katika kipindi kifupi ameweza kukarabati Vyuo vingi vya Utafiti, vimekarabatiwa kweli kweli, ukipita utaona vinapendeza. Lakini kule tulikokwenda kufanya ziara, tulikwenda Sokoine, Arusha, *TPRI,* tulikuta wataalam wanasema tuko hapa tu kama maboya, pesa za *research* ni kama hakuna. Kwa hiyo, tumekarabati Vyuo ili vitusaidie kufanya utafiti, lakini utafiti haufanyiki. Tumeingiza pesa nyingi kweli, lakini ninakupongeza kwamba, vile Vyuo vinafaa kumwonesha mdeni kwamba tulikuwa na Vyuo vimekufa sasa vimepona.

Lakini kwa jinsi michango yetu tunayotoa hapa ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nitoe mfano mmoja wa kukusaidia vita mbele ya safari. Mfugaji mmoja wa mbuzi alifuga mbuzi wake, asubuhi akakuta mbuzi wameng’atwa katika mkia na chui. Akasema mwenyewe huyu chui mjinga sana huyu, angekuwa na akili angemshika kwenye shingo angeweza kumla mbuzi wangu lakini basi kamkwaruza tu kwenye mkia.

Usiku uliofuata chui akaja, kumbe alikuwa kwenye kichaka anasikia maneno ya mwanadamu kwamba alimshika kubaya. Safari hii aliporudi sasa akawashika kwenye shingo na sio mbuzi mmoja, ni wanne, watano. Sasa ndugu yangu mpaka tukimaliza michango yetu nadhani utajua pa kushika ni wapi. *(Kicheko/Makofi)*

Mchango wangu uko katika maeneo matatu. La kwanza, ni miundombinu ya kilimo, pili, utafiti na tatu, mkakati wa kupambana na umaskini kwa kutumia kilimo. Miundombinu ya kilimo ni muhimu sana. Sisi tumeanza kubeza kilimo chetu na raslimali tulizonazo katika nchi yetu kwa kuanza kusoma ile mistari mizuri kwenye Biblia na Korani. Tunasema mahali fulani panafaa na mahali fulani pengine hapafai. Si kweli. Watu wamekwenda Misri ni jangwa, wame-*reclaim land* kwenye jangwa wanalima, wanavuna, wanauza nchi za nje na lile ni jangwa, sisi Tanzania tuko katika jangwa?

Zimbabwe hawategemei kilimo cha mvua. Wana milima mikubwa kama ya kule kwetu Same. Wanavuna maji ya mvua, mwaka hadi mwaka na wanavuna chakula na hata wakati fulani walituuzia chakula. Kwa hiyo, kama tunataka tuondokane na baa hili la umaskini wa kilimo lazima tuboreshe miundombinu yetu kwa kutumia maziwa yetu, mito yetu, tuna Mto Pangani, Mto Rufiji, Mto Malagarasi na Mto Wami, yote hiyo itumike. Tuna maziwa, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, yatumike katika kilimo na mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani Mheshimiwa Waziri aliniambia bwana kule kwako Same kuna ukame tu kule. Nikamshangaa kwamba haelewi Same pako vipi. Same tuna mito mitano ya kudumu ya maji ambayo haikauki hata mara moja. Kumbe amesoma mstari mmoja tu wa Biblia ambao unampendezesha, pale anapopita pale kwenye *high way.* Kule milimani kuna mito ambayo ningependa kuitaja. Kuna Hingilili, Yongoma, Saseni, Nakombo na huo wa Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na huko wananchi wanamwagilia kwa kilimo cha umwagiliaji wa asili *(traditional irrigation).* Walikuja Wadachi wakatusaidia kidogo mwaka 1974, baada ya hapo Serikali ikatuacha wenyewe. Mheshimiwa Waziri alishangaa wakati wa kiangazi akakuta watu wa Kata moja ya Makanya manavuna mahindi kwa wingi *(Bumper Harvest)*, mengi tu kwa kuvuna maji ya mvua kutoka milimani na alikwenda pale akayaona. Nikamwambia sisi tunachohitaji ni kuwezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wakiwezeshwa wanaweza, hawana tatizo. Kwa hiyo, ningekuomba Mheshimiwa Waziri, haya mambo uliyotuwekea hapa, yasije yakawa Hekaya za Abunuwasi. Yaende yakatekelezwe. Najua Abunuwasi alisema shika nyumba yako juu nachukua ya kwangu chini. Sasa sijui sisi tutakapochukua nyumba yetu ya chini ya kwako itakuwaje. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti, kule *TPRI* kuna Kituo kikubwa kilikuwa cha Afrika Mashiriki wakati ule, ilipovunjika kikakabidhiwa kwa Serikali yetu. Kile Chuo kina-*work under capacity,* kiko *under utilized,* hakitumiki sawasawa, lakini

Serikali inapeleka ruzuku pale. Sasa wakati umefika Chuo kile kitumike. Kinaitwa *Tropical Pesticide Research Institute. Tropical* maana yake kingeweza kusaidia nchi zote za Afrika Mashariki na *SADC* katika utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafanya kilimo bila utafiti na kilimo bila utafiti hakitatufikisha mahali popote pale. Wenzetu Ulaya wanataka kununua mazao yetu ambayo yana *quality* na ambayo yana thamani. *Quality and high value crops* ndiyo wanayotaka kununua kutoka kwetu, hawataki kununua mazao ambayo labda yangewekewa mbolea ya chumvi chumvi au yamepuliziwa madawa. Wanataka chakula ambacho ni cha asili na nafikiri hii inatoa nafasi nzuri kwa ndugu zangu Wasukuma na Wanyamwezi kwamba, wangeweza kuuza mbolea yao ya mifugo wakafunga katika mifuko kama wanavyofunga hiyo mbolea ya chumvi chumvi wakajipatia fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ile mbolea ya asili inatoa mazao ya asili, sisi tunabeza mbolea ya asili. Kwa nini tuibeze sehemu ambayo inaweza kutumika iendelee kutumika kwa sababu katika utandawazi hatutauza mazao ambayo yamepuliziwa madawa ama yakatumika madawa katika kulisha mmea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningekuomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kukarabati vile Vyuo vya Utafiti, vipewe fedha za utafiti, bajeti tunayowapa ni ndogo sana ya ndani. Bajeti kubwa ni ya nje na hata ukiangalia Bajeti yako mwenyewe pesa nyingi ni za kutoka nje. Lakini wakati fulani Mheshimiwa Waziri Mkuu, akiongea hapa alisema jamani haya matatizo siyo ya Waziri wa Kilimo na Chakula, ni mvua. Lakini mimi nasema tena ni pamoja na ukosefu wa fedha. Serikali yetu inatenga fedha kidogo sana kwa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika kitabu hiki cha Benki Kuu, wanasema kwamba, Sekta ya Kilimo imechangia Pato la Taifa kwa asilimia 47.5. Madini yamechangia asilimia 2.7 tu na ukiangalia hapa kilimo ndicho kinaongoza. Unakuja kwenye utalii asilimia 16.6 na unakija kwenye biashara asilimia 10. Sasa kwa nini kilimo kisiwezeshwe kama ndicho kinachoipatia Taifa letu pato kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla, mwaka ujao wa fedha, tunategemea kilimo kitapewa fedha nyingi na kitawekewa mpango mkubwa ambao utaweza kuinasua hii nchi yetu na matatizo ya kiuchumi. Sasa niongelee suala la mwisho kuhusu umaskini. Kilimo kitaondosha umaskini wa chakula, umaskini wa kipato na umaskini wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niitahadharishe Serikali yetu kuwa watu wetu sasa wanauza hata miwani, chokoleti, karanga, kwa sababu hakuna miundombinu ya kilimo. Watu wetu ni maskini wa chakula, wewe kama ni Mbunge ama ni Waziri, ama Katibu Mkuu, ndani ya nyumba yako unakula, jirani aliyekupigia kura hali, atakukata na panga, amani itakosekana. Kwa hiyo, tuliangalie hili tatizo la umaskini katika kilimo kwamba ni sehemu ya kuwapatia watu wetu ajira na uwezo wa kuishi. Tuwajengee miundombinu ya kilimo wananchi wetu kule wanalima kwa njia zao wenyewe, wanatengeneza mifereji yao wenyewe isiyo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilimwuliza Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, kuhusu mifereji yangu ya kule Ruvu akaniahidi kwamba, itaangaliwa katika Bajeti. Ninategemea kwamba, bajeti ya leo itatoa fedha kwa mifereji yangu kule Ruvu na kama haimo basi kuna mahali ambapo tutaelewana tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya maendeleo katika kilimo *in fact* eneo lolote ni kufanya kazi sana. Watu wetu wamelegea sana, hawafanyi kazi. Twende tukawahimize wafanye kazi. Kule vijijini wanaofanya kazi sana ni wanawake. Miaka karibu 40 iliyopita, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliliona hili na alilisema. Alisema vijijini wanawake ndiyo wanaofanya kazi siku zote Jumamosi na Jumapili, hawana hata sikukuu ya kupumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunataka kuendeleza kilimo kule akina mama wawezeshwe kwa mitaji ya kuwawezesha kukiendesha kilimo kwa kutumia utaalam wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni pesa ya *STABEX*. Kwa nini hii pesa inakuwa ni kitendawili. Sisi Watanzania tunahitaji mtaalam wa kutoka Ulaya kutuambia barabara zetu za kahawa, kama Mbunge aliyeko hapa hajui barabara zake za kahawa hastahili kuwa Mbunge. Wadau wa kwanza ambao wangemfahamisha Mheshimiwa Waziri barabara za kahawa ni sisi tulioko hapa. Sasa tunashangaa anachukuliwa mtu kutoka Ulaya anakuja hapa tunaambiwa amepita majimboni kwetu anapitia kwa nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani wakati nchi yetu ikijitawala tulikuwa na kile chombo cha usalama tunapima mpaka kiatu cha mtu. Sasa siku hizi watu wanaingia katika nchi yetu wanavyopenda tu. Tunaambiwa wamezunguka huko hivi walipitia wapi kwa *DC? DC* hajui, Mkurugenzi hajui, Mbunge hajui! Sasa kama hii barabara inatengezwa na pesa ya *STABEX,* kwa ajili ya watu waliompigia kura Mbunge, kwa nini Mbunge asishirikishwe? *DC* hajui, Mkurugenzi hajui, huyo mzungu alipitia wapi? Tunapenda tupate majibu. Tufahamishwe kwamba hii fedha miaka mitatu inaendelea kukaa benki, imezalisha riba kiasi gani ama ilikaa benki bure tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niunge mkono kwa shingo upande nikiwa na imani kwamba, Mheshimiwa Waziri ataangalia kule kwangu, atakumbuka kumshika shingo badala ya mkia. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula. Kabla sijafanya hivyo, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia, kwa niaba ya Wananchi wangu wa Arumeru Mashariki, nitoe salamu zangu za rambi rambi kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kufiwa na ndugu yetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyefariki hapa Bungeni. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi, *amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu zangu za rambi rambi naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Watendaji wake, kwa kutekeleza vizuri bajeti ya mwaka 2003, yaani mwaka huu tunaoumaliza sasa na kuandaa bajeti hii ambayo wameleta mbele yetu. *(Makofi)*

Aidha, nataka nichukue nafasi hii, niipongeze Serikali kwa kufuta kodi zote katika Sekta ya Kilimo. Natumaini hii itakuwa ni hatua nzuri ya kutuhamasisha wananchi na wawekezaji kutoka nje kuwekeza katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kukiri kwamba, sote hapa tumekuwa tunaeleza umuhimu wa Sekta ya Kilimo kwamba inachangia kuajiri asilimia 80 ya Watanzania kuchangia kwenye Pato la Taifa, kwa asilimia 50 na fedha za kigeni kwa asilimia 50. Yote hayo tumekiri na kwa umuhimu huu naomba basi kusema kwamba, sekta hii ni vema tukawa na mipango na usimamizi madhubuti wa kusimamia uzalishaji, usindikaji wa mazao ya kilimo, utafiti wa mbegu bora, matumizi ya kilimo bora na hatimaye uuzaji wa mazao yetu nchi za nje kwa kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme baada ya kukiri umuhimu wa sekta hii ya kilimo ni vizuri basi tukaiambia Serikali yetu ijitahidi kwa umuhimu huu kuwekeza kwenye sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaelekeze ama niseme jambo moja kuhusu kipaumbele ambacho kinatakiwa kupewa Sekta hii ya kilimo. Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya leo ukurasa wa 8 na 9 ambao wenzangu wameshau-*quote paragraph* ile ya mwisho anasema: "Ili kilimo kiweze kutoa mchango wa kuridhisha katika ukuaji wa uchumi, usalama wa chakula na kuondoa umaskini, inapaswa kukua kwa kiwango kisichopungua asilimia 10 hadi 11 kwa mwaka. Kiwango hicho kitaweza kufikiwa iwapo kilimo kitapatiwa mahitaji yake ya pembejeo, zana za kilimo, utaalam na masoko ya uhakika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, *statement* hii inaonyesha kwamba, hata Waziri mwenyewe hajaridhika na fedha alizopewa na Serikali kwa sekta hii ya Kilimo. Sote tunajua kwamba, Serikali yetu uwezo wake ni kiasi gani, lakini tunataka kuiambia Serikali pamoja na uwezo wake mdogo, wakati umefika sasa itoe kipaumbele kwa Sekta hii ya Kilimo kwa kuitengea fedha zinazotosha kuendeleza kilimo katika nchi yetu ili tuondokane na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, mapungufu mengine yaliyoko kwenye Sekta ya Kilimo ni pamoja na hali ya mvua isiyotabirika. Ukichanganya tatizo la kutokuwa na fedha za kutosha katika sekta hii ya kilimo, ukaweka na hili la mvua kutotabirika katika sekta hii ya kilimo, basi matatizo haya yanakuwa makubwa na ndiyo tunaona wote tunalalamika kuhusu ukuaji wa sekta hii ama *performance* ya sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati tukilizungumzia suala zima la sekta hii ya kilimo tujue kwamba, kwa sasa hivi asilimia kubwa ya kilimo chetu inategemea mvua. Kwa hiyo, kuna hilo ambalo hatutaweza kulisahihisha bila kuweka mkazo katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya hali ya chakula nchini. Kumekuwepo na hali mbaya ya chakula kwa miaka kadhaa, hili linatokea mara kwa mara na katika msimu uliopita wa 2003/2004, tumekuwa na uhaba wa mvua katika nchi yetu. Tunashukuru, tunaipongeza Serikali yetu kwamba, pamoja na uhaba huo wa chakula, hakuna maafa makubwa yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu haya yanatokea kila baada ya miaka kadhaa, tumejifunza nini kama Watanzaia? Kwa hakika tumejifunza kwamba, hatuwezi kutegemea mvua tu ambazo hazitabiriki katika kilimo chetu. Kwa hiyo, ni sharti tujielekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji ili ki-*complement* kilimo hiki ambacho kinategemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili naomba niseme kwamba, nasisitiza maelezo na maelekezo ya Kamati ya Kilimo na Ardhi katika ule ukurasa wa 6 uliosema, Kamati inashauri umwagiliaji utiliwe mkazo hasa katika mabonde yaliyotengwa kama Bonde la Mto Pangani, Rufiji, Ruada, Lukuledi, Ruvuma, Kagera, Wami, Malagarasi, Kilombero na kadhalika. Pia kujenga mabwawa na kuvuna maji ya mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifuata ushauri huu wa Kamati hii ya Kilimo na Ardhi, ninafikiri tutafika mahali. Mimi nisingejali sana fedha hizi zinazotumika katika programu mbalimbali za kuendeleza kilimo. Ninachojali mimi ni matokeo yake. Kwa hiyo, katika hili na katika fedha hizi zote ambazo watapewa Wizara ya Kilimo na Chakula, baadaye tukubaliane katika hoja hii tunamwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake watupe baadaye, yaani baada ya Bajeti ya 2004/2005, watupe matokeo ya fedha hizi kwamba watakuwa wametumia kwa njia gani na kwa matokeo yepi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tunajifunza kutokana na hili ni kuweka hifadhi ya chakula katika ngazi zote na katika hili ngazi ya Taifa, Kitengo chetu cha *SGR* kiwe kinaweka chakula cha akiba na kitumike kwa dharura peke yake na chakula hicho kisiuzwe mpaka kuwepo na uhakika wa chakula msimu ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwa kifupi tu utabiri wa hali ya hewa. Ni lazima tutilie mkazo utabiri wa hali ya hewa katika nchi yetu ili tuweze kuwa na mbegu ambazo zinaendana na kiasi cha mvua ambacho kinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie juu ya mikopo ya wakulima. Dhana ya mikopo ya wakulima imechukuliwa ama inachukuliwa kwa nyakati mbalimbali kwamba wakulima wanataka mikopo ya bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawataki mikopo ya bure. Wanataka mikopo kwa maana ya mikopo. Kitu kinachoombwa hapa na wakulima ni kwamba,

*interest rates* ziwe ambazo tunaweza kuzimudu. Lakini siyo kwamba wakulima wanataka mikopo ya bure na katika hatua hii basi naipongeza Serikali yetu kwa kuthubutu kuanzisha benki ya kilimo katika nchi yetu na tunaomba hiyo benki ianze katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie juu ya matumizi bora ya ardhi. Tuna ardhi kubwa sana ambayo haitumiki hapa nchini. Lakini nisengataka hasa kuendelea kusemea ardhi ambayo haijatumika kabisa. Ningependa kuzungumzia mashamba yale ambayo yalikuwa ya *NAFCO,* ambayo kwa miaka karibu 10 sasa tangu tuanze zoezi la ubinafsishaji hayatumiki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninependa kuishauri Serikali itazame kwa undani haya mashamba ya *NAFCO* ili kama Waziri alivyosema yagawiwe na kabla hayajagawiwa kama kugawa itachukua muda mrefu wananchi wapewe kuyatumia. Nasema hivyo nikiwa na shamba ambalo ni zuri kwa kilimo la *Themi Holding Ground,* ambalo liko katika Wilaya ya Arumeru, ambayo sasa hivi wananchi wanalivamia kutoka sehemu mbalimbali nje ya Arumeru na ndani ya Arumeru kwa sababu limekaa muda mrefu bila kufanyiwa chochote na Serikali haiendeshi shamba hili ipasavyo. Tunaomba wananchi wa Arumeru wapewe shamba hili ili waweze kuendeleza kilimo na kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda umeisha. Naomba kwa hayo machache, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwanza, kutoa rambi rambi kwa familia ya aliyekuwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Yete Mwalyego, naomba kutoa pole sana kwa familia hiyo na naomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, *amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2001, Waziri wa Kilimo na Chakula alikuja hapa Bungeni tukamwidhinishia shilingi bilioni 24. Mwaka 2002 akarudi tena hapa Bungeni na hadithi, tukamwidhinishia shilingi bilioni 34. Mwaka 2003 akaja na mkakati mwingine tukamwidhinishia shilingi bilioni 54. Kwa hiyo, jumla alizokula mpaka sasa hivi katika Wizara yake ni shilingi bilioni 112.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri niseme tu kwamba, Bajeti hii imeandaliwa katika mazingira ambayo si ya kumnufaisha sana mkulima kwa sababu ina mambo mengi mazuri sana lakini hakuna kitu ambacho mkulima atanufaika nacho moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri amekuja akiomba shilingi bilioni 64 na katika fedha hizi shilingi bilioni 34.9 ni kwa matumizi ya kawaida. Lakini shilingi bilioni 29 ndiyo shughuli inayotegemewa kwa ajili ya kuendesha miradi na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ukiiangalia inalenga zaidi utendaji kazi na siyo kumsaidia mkulima. Mimi ningeshauri sana kwamba, Bajeti hii kwa kweli sasa iwe na mtazamo tofauti. Bahati nzuri Waziri wa Kilimo na Chakula, ana uzoefu wa kuchapa kazi sana. Nadhani alipopewa Wizara hii mara ya kwanza Watanzania wengi walitegemea kwamba atafanya miujiza. Lakini bahati mbaya sana matazamio mengi ya Watanzania bado hayajakamilika. Wizara hii ina miamba wawili, kuna mtani wangu Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala kule akisimama pale utamwona jinsi alivyo, kuna Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Sasa wote ukiwaona ni miamba kweli kweli, lakini Wizara haiendi. Sasa hii jamani namna gani kuna tatizo gani au tuweke mama pale asaidie labda kusiukuma Wizara hii. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa sababu akina mama wanafanya kazi sana sana. Sasa sielewi miamba miwili imekaa pale lakini kazi inakuwa kidogo inatia wasiwasi. Nimeona nianze na hiyo kwa sababu Wizara hii kwa kweli imekuwa ikilaumiwa mwaka hadi mwaka. Matumaini ya Watanzania si suala la kusikia hadithi ni kuona kwamba nchi hii inajitosheleza kwa kilimo, inakuwa na mazao ya kutosha, hakuna suala la njaa. Hivi leo Tanzania unaambiwa kuna njaa kila mwaka kuna njaa, Mheshimiwa William Lukuvi aende kutafuta pesa za njaa. Anatuletea *mini-budget* hapa Bungeni. Hii tutaishi mpaka lini? *(Makofi)*

Kwa nini Wizara ya Kilimo na Chakula sasa msiachane na mikakati, tunataka kuona vitu *on the ground.* Hebu anzisheni miradi ya umwagiliaji tuone kwamba mwaka huu tunafanya hiki na tuone *solidarity* ya haya mambo ya hadithi hadithi mara fedha sijui kwa ajili ya nini. Tunatenga fedha kwa ajili ya mafunzo, kwa ajili ya wataalam wa ugani, mara fedha kwa ajili ya kununua magari na kadhalika. Hii tuachane nayo. Mimi nadhani Mtanzania wa leo hii anategemea kwamba, Serikali hii sasa suala la njaa liwe ni hadithi. Unaposema kwamba tunategemea mvua, nchi hii ni aibu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije hapa kwenye suala la kuwekeza katika miundombinu ya kilimo. Tuna mabonde mengi sana, kila siku Waheshimiwa Wabunge hapa wanakuja na maelezo mazuri sana na Serikali inatoa maelezo mengi sana. Lakini hatujaona mkakati wa kuona kwamba sasa mabonde haya yanatekelezwa. Kwa nini Mheshimiwa Waziri sasa usiseme kwamba pamoja na mikakati mizuri hii tuanze kuonyesha vitu moja kwa moja kama unaamua suala la kilimo cha umwagiliaji na ndiyo sehemu kubwa sana kuweza kuokoa tatizo kubwa.

Sasa hivi ukiangalia kwenye kitabu kiambatanisho cha saba, kuna mikoa ambayo ina matatizo ya njaa mwaka hadi mwaka. Lakini sijaona Shinyanga, sijaona Mwanza hapa, sijaona hata Dodoma hapa kwa Wagogo watani zangu hapa. Nimeona kuna Kilimanjaro, Arusha na Tanga. Sasa hii jamani mbona tumeelekea upande mmoja tu. Hivi njaa wanaosikia ni watu wa Kilimanjaro, Tanga, Arusha na kwingineko? Mimi nafikiri kuna haja ya suala hili kuliangalia kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mpango wa zao la biashara kwa kila Wilaya, mimi katika Wilaya yangu wala sijui ni zao gani la biashara wala ni zao gani la chakula. Mpaka sasa sijui. Lakini mwaka 2003, Mheshimiwa Waziri ulikuja kutuambia kwamba

kila Wilaya sasa itenge zao la biashara na zao la chakula. Bajeti imekwenda hivyo na unaomba shilingi bilioni 64 tukupe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba sana Mheshimiwa Waziri hili suala ajaribu kuliangalia. Tunaamini kwamba, haya mambo sasa tuachane na hadithi. Nadharia imeshapitwa na wakati, tufanye kazi. Mheshimiwa Charles Keenja una sifa nzuri sana ya kufanya kazi. Hata Msaidizi wako, Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, lakini sasa hebu fanyeni kazi tuone basi, acha porojo, acha manjonjo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la pamba. Hili lazima nilizungumzie kidogo. Katika zao la pamba sasa hivi mkulima anauza pamba shilingi 300 kwa kilo moja. Lakini mkulima huyo huyo amenunua mbolea, amenunua madawa, amenunua mbegu. Gharama ya kuzalisha sasa hivi kilo moja ya pamba ni kubwa sana. Mkulima huyo huyo wa zao la pamba unakuta anagubikwa na baadhi ya kodi zingine. Kwa mfano, kuna *cotton development fund* ambayo anakatwa shilingi 20 kwa kila kilo. Kuna *cess* anakatwa shilingi 15 kwa kila kilo.

Kuna mfuko wa elimu, anakatwa shilingi 5/= kwa kila kilo. Kuna hii Bodi ya Pamba wanamkata shilingi 5/= kwa kilo na kijiji kinamkata shilingi 10/= kwa kila kilo. Jumla shilingi 55/=. Hivi kwa nini huyu mkulima hizi pesa asingepewa iwe ni sehemu yake ya mapato anapouza pamba yake. Kwa sababu unakuta mkulima huyu ameingia gharama kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tulipokuwa watoto wadogo sisi baba zetu walikuwa wakilima pamba, wanaoa wanawake, wananunua baiskeli wanajenga nyumba. Lakini siku hizi imekuwa ni hadithi kusema nilime pamba ninunue ng'ombe, imekuwa ni hadithi kwa sababu unakuta gharama anazotumia mkulima kulima pamba hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kuangalia eneo hili hapa ili mkulima wa pamba aweze kupata nafuu. Pamba tunaiita ni dhahabu nyeupe. Wengi tumesoma kwa pamba, nchi inapata pato kutokana na pamba, sasa kwa nini tusimwangalie mkulima wa pamba? Naomba sana suala hili lijaribu kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijana mmoja alikuwa Mjumbe wa Bodi ya Chuo Kikuu, akaenda kuomba kwenye Bodi waongezewe muda kwa sababu ilikuwa ikifika saa nne wasichana wanazuiliwa kwenda kwenye mabweni ya wavulana.

Sasa alipokuwa kwenye kikao kile cha Bodi, Profesa mmoja akamwuliza unataka nini? Akasema nataka angalau wasichana wafike mpaka kwenye saa sita za usiku ili tuweze kupata muda mzuri wa kubadilishana mawazo. Yule Mwenyekiti wa Bodi ile akamwambia kama imefika saa nne hujaweza kufanya kitu chochote kile hata ukipewa saa sita utafanya nini?

Mheshimiwa Charles Keenja na wewe usisubiri mpaka saa sita, tunataka saa nne tuone matokeo mazuri. Wizara yako hii ni Wizara ambayo ni ngumu sana kwanza ni

dubwasha la Wizara, Wizara yako ni pana sana, haistahili jinsi unavyofanya kazi sasa hivi kwa sababu Wizara hii ina mambo mengi lakini pamoja na wingi wake huu basi u-*focus* mambo mbalimbali ambayo yanakulenga moja kwa moja. Miaka mitano utabaki unasema naandaa mikakati, mbinu, ushirikishi, miaka inakwenda na kilimo kinabaki pale pale. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, ujaribu kuliangalia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni suala la ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao. Wizara yako inaingiliana kwa karibu sana na Wizara ya Ushirika na Masoko, lakini leo hii mkulima anapolima mazao yake yakizidi au akivuna mavuno mengi sana soko linaanguka. Ninaamini mwaka huu wananchi wengi wamelima sana zao la pamba na dalili zinavyoonyesha pengine bei ya pamba itashuka lakini gharama za mzalishaji ziko pale pale. Ukienda Tanga wanalima sana matunda lakini hakuna viwanda, kwa nini tusiamue kwamba safari hii basi tuanzishe kiwanda ambacho kitasaidia ku-*process* matunda yanayozalishwa Tanga, Ukerewe, ili wakulima waweze kunufaika na kuboresha mazao yao? Naomba sana suala hili liangaliwe na wawekezaji wasaidiwe katika maeneo haya ya kilimo tusiangalie tu, wawekezaji wanaokuja kwa ajili ya sekta nyingine bali wanaokuja katika sekta za kilimo wapewe kila namna ya ushirikiano na wawezeshwe kuwekeza katika mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, kila mwezi tunatenga shilingi bilioni 1.8 kwa nini na Wizara ya Kilimo tusiwe na mfumo wa namna hiyo, tutenge mahususi kwa ajili ya kuendeleza kilimo? Kama ni kwa ajili ya umwagiliaji basi fedha hizo ziende moja kwa moja kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna takwimu ambazo zinatumika sio sahihi sana, hizi za uhaba wa chakula. Wewe unakuta takwimu zinafanywa miezi tisa iliyopita kwamba, hawa wameonyesha wana uwezo wa kuwa na chakula chao lakini inapokuja kwenye hali halisi, wananchi wale wale hawana chakula cha kutosha. Sasa ni vema takwimu hizi zifanyiwe kazi kwa muda muafaka sio kutumia takwimu ambazo zimekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uanzishaji wa Benki, bila kuanzisha Benki ya kumsaidia mkulima, hatujamsaidia. Sasa hivi tuna Benki hii inayoitwa *Exim,* ni wakulima wachache tu wanaoweza kupata huduma. Kwa nini tusitumie mtandao wa Benki ambayo mkulima akiwa kule Busega ataweza kui-*access,* Nzenga aweze kui-*access,* akiwa Sumve na sehemu nyingine hata akiwa Kongwa aweze kui-*access*? Unaposema *Exim Bank* imepewa *mandate,* hizi Benki ziko mjini, mkulima huyu hawezi kupata nafasi ya kupata huduma hii. Naomba sana Wizara yako iangalie suala la kudumisha *SACCOS* ili zipewe *mandate* ya kupeleka pembejeo na mikopo kwa wakulima kwa karibu zaidi, hii itarahisisha sana badala ya kutegemea tu suala la *Exim Bank.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tunahoji *Exim Bank* ilipataje tenda hiyo? *Exim Bank* ni ya nani? *Exim Bank* tunaweza kuiwajibisha namna gani? Asubuhi wenzangu walisema mnakwenda kuomba mkopo baadhi ya watu wanapewa na wengine

wananyimwa wakati wote wanatoka sehemu moja. Ni lazima tuangalie sana suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusu ruzuku. Ruzuku kwa wakulima ni muhimu sana. Mataifa ya nje yanasema tusitoe ruzuku lakini ng'ombe aliyeko Ulaya anapewa ruzuku zaidi ya dola mbili kwa siku wakati Mtanzania aliyeko Tanzania hana ruzuku kwenye kilimo. Kwa hiyo, ng'ombe aliyeko kule ni bora zaidi kuliko Mtanzania aliyeko hapa, ambaye ana-*struggle* kulima kwa kutumia jembe la mkono, ana-*struggle* kulima kwa kutumia mifugo yake ambayo haina hata afya nzuri. Kwa nini sasa Serikali isijielekeze katika suala hili, tufumbe macho ili mkulima aweze kupewa ruzuku na kuondokana na matatizo ya kilimo. Tusipofanya hivi itakuwa ni hadithi, hizi hadithi zimeshapitwa na wakati, wakati mwingine ni kuwa maskini jeuri, hebu tuthubutu kufanya badala ya kusubiri mpaka watu watuamlie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina sehemu nzuri sana, ina mabonde mazuri, ina mito mizuri lakini kusema kwamba tutegemee mvua ndio Wziri wa Kilimo na Chakula atambe hapa Bungeni, ninadhani sio sahihi. Mheshimiwa Waziri sasa usitegemee mvua, fanya mikakati kilimo kiendelee. Kwa mfano, mimi katika Jimbo la Busega kuna eneo kule Kalemela, ninashukuru sana Mheshimiwa Waziri tumeanzisha pale mradi wa umwagiliaji lakini eneo kubwa zaidi bado halijatekelezwa.

Hebu tujaribu kuangalia yale maeneo, naona Mheshimiwa Prof. Pius Mbawala, ananinyooshea kidole, safi, kazi nzuri, kwa hilo ninakusifu, lazima nikubali, hebu tujaribu kuangalia maeneo ya namna hiyo tujaribu kuyaendeleza. Ukanda wa Ziwa una mabonde mazuri, una sehemu nzuri ambazo kama zikiendelezwa kwa kilimo, zitasaidia sana kuondokana na njaa. Ni aibu kuona tunalia njaa wakati maji yako pale, maziwa yako tele pale, sasa Mtanzania ni lini ataachana na hadithi hizi?

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, abadilike na ninajua hatasubiri mpaka saa sita za usiku ndio aanze kubadilika, kuanzia saa nne hii afanye kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nataka kuungana na wenzangu, kutoa mkono wa rambirambi kwa marehemu, Mheshimiwa Yete Mwalyego. Ni mitihani wa Mwenyezi Mungu, hauepukiki kila binadamu utamkuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, nataka nimwunge mkono Mheshimiwa Waziri, kwa asilimia mia kwa mia, pamoja na Watendaji wake wote. Nataka niwe mkweli kutokana na uwazi alioutumia katika hotuba yake hii, ni kazi yetu sisi Viongozi na Watanzania wote kusimama kidete kupeleka mbele hili gurudumu kwa mafanikio makubwa sio kulaumiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa uwazi alioonyesha kwenye ukurasa wa nne. Amesema karibu Wabunge wote waliochangia

hotuba zilizotangulia, waligusia sekta ya kilimo. Wabunge wote waliotoa maoni yao juu ya kilimo nawahakikishia kwamba, Serikali imewasikia na hatua zinazostahiki zitachukuliwa. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana. Naomba kigezo hiki ukichukue hivyo maelezo ya Wabunge uyafanyie kazi juu ya mikopo, pembejeo, hofu ya hii Benki ambayo fedha hizi zimepelekwa na hata juu ya kumaliza tatizo la pesa za *STABEX,* hivi kwa nini Mheshimiwa Waziri hulimalizi, hebu Serikali imwondoe katika lawama Mheshimiwa Waziri. Ni imani yangu atalifanyia kazi kwa mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nataka niseme kwa uwazi kwamba, Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania. Nataka nirudie kusema kwamba, sisi viongozi wote hatuna budi kufanya kazi kwa ajili ya kuleta mabadiliko haya ambayo yanakusudiwa, tumsimlaumu Waziri wa Kilimo na Chakula, hili ni suala la Serikali na sisi sote tunahusika kwenye Serikali, ndio maana tunaipitisha Bajeti yake hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda katika ukurasa wa nane, tumeelezwa kuwa tatizo la kilimo chetu ni kwamba, kimeendelea kutegemea mvua ambazo hazitabiriki, afanye nini Mheshimiwa Waziri? Amejivua! Sasa ni kazi yetu Serikali impe fedha Waziri wa Kilimo na Chakula, tuyatumie mabonde yale kama maporomoko ya Rusumo, Mto Kagera, Ziwa Victoria ile ni Bahari lakini Mungu kaifanya kuwa na maji baridi na maeneo mengine ya Tanzania tuweze kufanya kazi kwa mafanikio makubwa sana. Kwa hiyo, hili nataka niseme kwa uwazi na kwa kweli, tusitupiane lawama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 22 amezungumzia juu ya huduma za ushauri wa kitaalam. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri na ukasema kwamba Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendelea kuwapatia wakulima teknolojia bora za uzalishaji ili kuwawezesha kuongeza uzalishaji na tija, hongera sana lakini sio teknolojia tu, tusimamie sasa uzalishaji. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, wewe na wataalam wako mtaingia vijijini kuwasimamia wakulima pamoja na Wizara hii husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Serikali imefuta kodi nyingi sana, kwa hiyo, Watendaji wa Halmashauri za Vijiji watasimamia kilimo. Naomba Serikali ijipange vizuri ili kuwapa majukumu mengine wale Watendaji wa Halmashauri za Vijiji kwa sababu Wizara yako inashirikiana na Wizara ya TAMISEMI na maeneo mengi Wizara ya TAMISEMI inayajua kwa hiyo mtafanya kazi ili kuondoa hofu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 24, Waziri amezungumzia juu ya Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani *(National Irrigation Master Plan).* Hakuna hofu kwa sababu ukishakuwa na mipango mizuri, haiwezekani usifanikiwe. Kwa hiyo, kama iko hii Mheshimiwa Waziri, tunaomba uifanyie kazi kwenye miezi hii ili bajeti inayokuja tusikutupie lawama.

Lakini vile vile umesema katika mwaka 2001/2002, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na *JICA,* ilianza maandalizi ya mpango kamambe wa kilimo cha

umwagiliaji maji mashambani. Sasa ni kuendeleza tu. Kama mwaka 2001/2002, uliufanyia kazi sawasawa malalamiko yasingekuwepo katika nchi hii, maji tunayo mengi sana. Kwa hiyo, zile kasoro ulizoziona na hili shirika linatokea Japan, wenzetu ni wataalam sana, tuombe watusaidie kujenga uchumi wa nchi yetu kwenye suala hili, tusioneane haya na kubwa Serikali itoe fedha kwa Wizara hii. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake, wakae waondoe kiu ya wananchi juu ya kushughulikia tatizo la kilimo katika nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni msingi muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu Tanzania. Nataka nithibitishe hili kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliyoiwasilisha hapa Bungeni wiki zilizopita na nataka ninukuu sehemu nne, zinatuthibitishia vipi kwamba kilimo ni msingi muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania. Tunaomba Watendaji wa Wizara ya Kilimo pamoja na sisi viongozi tulifanyie kazi kwa mafanikio makubwa. Tusilumbane tu bila kuwa na sababu za maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza inasema Pato la Taifa linategemea kilimo kwa asilimia 45. Namba mbili, kwa fedha za kigeni kilimo kinategemewa kwa asilimia 75. Tatu, Watanzania zaidi ya asilimia 80 wanategemea kilimo kwa maisha yao na nne, inasema kilimo ni sehemu moja muhimu katika ukuaji wa uchumi na maisha ya watu wetu. Haya ni maeneo muhimu sana. Kwa hiyo, tunao wajibu kama Taifa, mihimili mitatu ya nchi Bunge, Serikali na Mahakama, tuhakikishe inafanya kazi kulifanikisha hili kwamba Bunge lisimamie sheria za nchi na utaratibu wa kupitisha bajeti na Serikali itenge fedha kwa Wizara zake. Haya ni maeneo ya kuangalia na tutaondokana na lawama kwa faida ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda tena katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukurasa wa 65, amesema maendeleo mazuri ya uchumi wetu yanatokana na mazingira ya amani na utulivu yaliyopo nchini. Kwa hiyo, usalama wa jamii unahitajika, njaa ni hatari sana. Tunahitaji amani katika jamii. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tufanye kazi kwa faida ya Taifa hili, ondoka ofisini twende mashambani tukafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wetu wawe wakweli, mnaelewana huko isijekuwa kuna *sabotage* hapo ndani yake, hivi kusemwa ninyi hamuogopi, wala hamwoni vibaya? Rais ametangaza kwamba, hawa wa kwake ni Askari wa Miamvuli, wewe Watendaji wako wako vipi, tuna maji mengi sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao kilichopita tulifanya ziara Kagera. Mheshimiwa Waziri nilikuambia niliyasikitikia maji ya Mto Kagera yanayopotea, tuliyaona maporomoko ya maji pale kwenye Daraja la Rusumo, nimeliona Ziwa Victoria na wako wenzangu niliwaambia hii ni bahari, Mungu kapitisha rehema zake tu kui-*change* kuwa maji baridi na bahati nzuri Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, imetumia maji yale kuyapeleka Shinyanga, miaka yote tulikuwa wapi? Naomba sasa hivi twende sambamba na sera zako, lazima tuimarishe kilimo kwa nguvu zote, epukana na lawama, wapange vizuri watendaji wako au haya magari Ma-*VX* haya hawana, ingieni vijijini mkafanye

kazi, ndio! Isije kuwa magari ni yako wewe tu wape na wale magari wafanye kazi, tukasimamie wakulima kuwafikisha pale ambapo wamekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi kupambana na majanga haya ya njaa. Mimi sishangai hapa juzi juzi kuna watu walisema ooh hata India wanatupa msaada, hata Ethiopia, hapana ni Serikali zinatoa misaada sio kwamba, nchi yao hakuna maskini, Serikali inakuwa na *stock* yake ya Kiserikali, siamini kama chakula kile kimekusanywa kutoka kwa wakulima wa kawaida mitaani. Tukubali Serikali inaposema kwamba, nchi yetu maskini lakini wapo wengine maskini zaidi, India maskini, *population* yao ni kubwa, hivi karibuni walikuwa wanatoa matangazo kwamba, kwa siku moja India njia ya treni inasafirisha karibu watu milioni 12 hebu *imagine population* yao iko vipi. Lakini vile vile tulikuwa kwenye semina ile ya *population* pale tulionyeshwa hali ya umaskini huko Bangladesh, India na maeneo mengine, hata watu hawana nyumba za kukaa, jiko liko baharini kwenye mashua au anajisaidia baharini, ng'ombe wako kwenye mitaa wanaishi na binadamu. Kwa hiyo, Taifa linapozungumzia umaskini, tusifananishe utajiri wa Mataifa mengine, kuna Mataifa yako zaidi ya miaka 200 sisi tuko kwenye miaka 40 na yote ilikuwa migogoro, mitupu tumeingia kwenye vita katika Bara la Afrika, vita na Uganda, tumeanza mwaka 1984, miaka 20 tutafanya nini? Tuombe Watanzania watupe tena miaka 40 tuangalie hali ya nchi itakuwa vipi.

Mheshimiwa Waziri, nakuunga mkono kwa mafanikio makubwa sana lakini nakuomba sana haya yaliyozungumzwa tuyafanyie kazi sana na niiombe sana Serikali ikupe fedha. Umesikia kauli za Wabunge na ni za wananchi kwamba, wamechoka aibu, wamechoka balaa, njaa ni balaa moja kubwa sana. Nchi yetu haina vita, tujipange vizuri twende kwenye kilimo tuyatumie mabonde yetu tuliyonayo tuache maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, namtakia mafanikio Mheshimiwa Waziri na namwunga mkono asilimia mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nikupongeze wewe kwa kunipa fursa hii jioni ya leo ili nami niweze kuchangia katika hoja ya Waziri wa Kilimo na Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa heshima kubwa, nimetumwa na wakazi wote wa Wilaya ya Mbeya, nije nitoe shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa ikiongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, pamoja na Kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ofisi ya Spika, Wabunge wenzangu wa Bunge hili, wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, kwa msaada wenu mliotupatia katika kusindikiza mwili wa Marehemu Yete Mwalyego, ambaye alikuwa ni Mbunge mwenzangu, lakini sio Mbunge mwenzangu vile vile ni kaka yangu ananizidi mwaka mmoja. Kwa hiyo, tunawashukuru sana na walishangaa sana kwamba kumbe Serikali hii inajali watu wake, naomba mzipokee. Ingawa yupo kiongozi ambaye aliiwakilisha Serikali lakini haya ninayoyazungumza ni ya ndani kabisa kwamba, nifikishe shukrani hizi za dhati kutoka kwa Wananchi wa Wilaya ya Mbeya kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Charles Keenja, kwa yale yote aliyoweza kuyasimamia vizuri. Mimi sina ugomvi na Mheshimiwa Charles Keenja, kwa sababu nilimletea matatizo yangu ya Chuo cha Kilimo Uyole pamoja na Chuo cha Utafiti, yeye mwenyewe alifika, alitembelea na baadhi ya mambo ameyarekebisha na yamefanyika. Kwa hiyo, nampongeza sana, sina cha kuzungumza katika hilo kwa sababu yale niliyoyaleta kwa kiasi kikubwa yametekelezwa na naamini kabisa Mungu atamwongezea nguvu na ujasiri ili aweze kuyasukuma yaliyosalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naliomba sana Bunge lako Tukufu linionee huruma kwa sababu ya haya yaliyotukuta, ninakuja kwenu kujenga hoja sina sababu ya kulalamika lakini nataka tujenge hoja kama wananchi tunaotakiwa kuijenga nchi hii kwa pamoja. Hoja hii ninasimama kwa niaba ya wananchi milioni mbili na laki mbili wa Mkoa wa Mbeya na vile vile maamuzi ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi Mkoa na vile vile *RCC* nayo imetoa kauli kuhusu jambo ambalo nataka nilete hoja mbele ya Bunge hili ili muweze kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijabobea sana katika uchumi lakini nimesoma uchumi ule unaoniwezesha ni-*survive* mpaka leo. Katika Dira yetu ya 2025 ya Kuondoa Umaskini, tumeeleza wazi wazi na Tanzania sio nchi ya kwanza tunajaribu kurejea katika vitabu mbalimbali namna gani wenzetu wamejitahidi katika kurekebisha uchumi wao mpaka sasa tunaziona ni nchi zilizoendelea. Hakuna njia ya mkato lazima tufuate hatua kwa hatua, tusipofuata yale ambayo wenzetu wameyafuata basi itatuchukua muda sana kufanya mabadiliko katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wameanza kwanza kwa kuangalia ni sekta ipi katika nchi ambayo wanaona inawaajiri watu wengi zaidi ndio wameipa kipaumbele. Wameipa kipaumbele hata katika Pato la Taifa kwamba, tuipe msukumo hii, kama tutakipa msukumo kilimo kwa hapa Tanzania ina maana wengi walioajiriwa na kilimo hatutakuwa na matatizo hasa katika kuondoa umaskini. Hakuna nchi iliyowahi kupiga hatua ya mabadiliko katika uchumi wake kwa njia ya kuwagawia wananchi fedha au mikopo bali kwa kuimarisha shughuli zao wanazozifanya kitu ambacho na sisi tunatakiwa tukifanye. Wameelekeza wazi wazi kwamba kilimo lazima kiende sambamba na viwanda, tunaanzia pale ili kulinda fedha za kigeni lazima uwe na viwanda vyako ndani ambavyo vinaweza ku-*process* mazao. Hivi kweli tunahitaji ku-*import juice, biscuits*, tutakuwa tunapoteza fedha za kigeni bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Waziri wa Klimo na Chakula ni kamisaa wetu, tumpe ushauri na yeye achukue yale mawazo yetu yale yanayoweza kufanya kazi ili *think tank* yake iliyoko kule iweze kumsaidia na iweze kujenga nchi na kusaidia Tanzania kwa ujumla. Lakini yapo maamuzi mengine yanayofanyika yanaumiza wananchi zaidi kuliko kujenga. Mathalani upigaji marufuku ulimaji wa zao la pamba sehemu za kusini hususani Mbeya. Mimi nimesema leo nazungumza kwa masikitiko, sitasema sana lakini nataka hoja yangu ijibiwe kitaalam kwa haya nitakayoleta. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, ninakuomba sana unijibu kitaalam, ninahitaji

majibu ambayo nikirudi nyumbani niieleze Halmashauri Kuu ya CCM na *RCC* kwamba, uamuzi wa Serikali yake ni upi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwanza tunataka tujue *Government Notice* Namba ngapi iliyopiga marufuku kilimo cha pamba Mbeya na Kusini kwa ujumla? Hilo tunataka tulijue, si zipo naomba mrejee. Pili, hoja yetu sisi kama wana-Mbeya tunataka mtueleze ni vijiji vipi ambavyo huyo mdudu, funza mwekundu, alipatikana. Naomba nipewe *mapping* yake kwa sababu tunasema unapofanya *experiment* au *research* ya namna fulani lazima ufanye *mapping* ya namna fulani halafu ndio uandike *confirmatory test* kwamba, sasa haya ndio matokeo yake. Tatu, naomba Vijiji na Wenyeviti gani wa Vijiji walishirikishwa katika hali hii. Sio vijiji tu naomba majina ya wakulima mmoja baada ya mwingine ambapo mdudu huyu alipatikana kwao eeh kama tumeweza kutuma Tume ya Wataalam kwenda *South Africa,* nitaomba Wabunge wote wa Mbeya pamoja na Wizara yako na Wataalam wetu twende Mbeya mkatuonyeshe mahali, kijiji na mkulima huyu ambaye *red bowl warm* alipatikana katika shamba hilo vinginevyo mnatuweka katika nafasi mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mbeya sasa hivi ume-*paralyze* kabisa, mmeshusha kabisa *economy* ya Mbeya, mzunguko wa pesa umekwisha. Nilikuwa na viwanda zaidi ya vitano ambavyo vilikuwa vinaitegemea pamba, nilikuwa na *Mbeya Industry* ime-*collapse*, nilikuwa na *Southern Highlands Ginnery* hakuna kitu, nilikuwa na *Mbeya Textile Mills* naye ameniambia anaondoa mashine zake, anafunga hawezi kuendelea kuagiza pamba kutoka Cameroun na Nigeria na viwanda vingine vidogo vidogo vyote vimefungwa. Sasa mnashangaa nini mnapoona ujambazi unazidi, mnashangaa nini sasa mnapoona watu wanataka mioyo ya watu wanaona ndio biashara nzuri kuliko pamba ambayo tumeifunga...

**MBUNGE FULANI:** Ngozi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Na ngozi vile vile. *(Kicheko)*

Nataka niwaambie wananchi wanaofanya mambo haya wengi ni *retrenchees* ndio wanafanya vitendo kama hivi lakini kama Serikali nafikiri lazima tuvikemee, tutafute utaratibu mwingine isiwe ni kisingizio au sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu haya yatolewe kwa ufasaha ili tuweze kuelewana. Hoja yangu ya msingi ni kwamba, ukiimarisha viwanda na kilimo, umewaondolea watu umaskini, umewapa ajira yao ya kudumu. Sisi Mbeya huwezi kumkuta mtu mzima, hata mama yangu mzazi inapita wiki, wiki mbili, hujamwona nyumbani kwangu anajitegemea, ndio taratibu zetu kule. Sasa nataka nijue mji hauendi, ninajua inawezekana kabisa pamba haina faida sana, faida yake ni ndogo kama alivyosema Mheshimiwa Raphael Chegeni Masunga, lakini mnasemaje juu ya viwanda vilivyokuwa vimeajiri watu zaidi ya 10,000, mnasemaje juu ya watu hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja yangu kwa nini nazungumza hivi? Mimi nilichukua *initiative* ya kwenda Zambia, Malawi, Msumbiji na *South Africa.* Nataka

nione huyu *red bowl warm* mnayemzungumzia ninyi Wataalam wa Tanzania yuko wapi kwa sababu Zambia wanalima pamba ya asili, Malawi pamba ya asili, *red bowl worm* yupo Kusini kule *Makatini Flats* mpakani na Ihambanle Mozambique, ndiyo yupo tena kidogo, lakini huku Kaskazini tuna tatizo la *White Flies Jassids*. Sasa kama mnataka kuitumia Mbeya kama *buffer zone,* mnaitumia kwa kumzuia mdudu yupi, maana Zambia hawana, Malawi hawana? Naomba tuzungumze kitaalam, tusiwe tunazungumza kwa kutaka kuumizana tu. Wote tunataka kurudi Bungeni hapa, tuoneane huruma jamani. Kwanza, wengine ni vijana, tutafanya kazi gani mkituangusha? Tunahitaji kurudi, lakini haturudi kwa sababu ya maslahi, tunataka turudi tuijenge nchi hii maana tuna nguvu, ujana ni chumvi tunataka tulisukume gurudumu hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niwaombe Wataalam mniambie ninyi *buffer zone* mnayoiweka ni ya mdudu yupi? *After all* ukienda *South Africa* wanasema sisi tatizo letu siyo funza mwekundu, tatizo letu ni funza wa Kimarekani *(American Bowl Worm).* Huyu funza mwekundu anatibika kwa madawa, kuna *das burn* hii ya kawaida ambayo ipo kwenye maduka yetu na *endosulfan* zinatibu zinamaliza kabisa na hata katika kufuata *process* ya kawaida tu ya kuvuna, kuchoma, unamaliza kabisa matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kama kweli kwa upendo, kwa dhamira ya dhati ya kuiendeleza Mbeya na wananchi wake, mmeona kwamba kilimo hiki cha pamba cha namna hii kitashindikana kwa nini msi-*introduce BT-cotton* ambayo pato lake ni kubwa lakini *red bowl worm* na *American worm* akigusa tu ile pamba anakufa. Hii ndiyo *think tank* tuliyonayo mnafanya nini? Kama mnaogopa hii nyingine isizidi kusambaza, kwa nini ham-*introduce* hiyo. Mimi sio *researcher* lakini kwa muda mfupi nime-*gather* haya maana *BT-cotton* ni nzuri, pato lake ni kubwa lakini vile vile yenyewe ni dawa, mdudu ikimgusa tu basi amekwisha. Sasa mnasemaje juu ya hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, atuandalie safari twende kwenye Vijiji hivyo na wakulima, maana mimi wakati ule nilikuwa Meya wa Manispaa ya Mbeya. Tulichofanya kwenye *RCC* mlituletea mdudu kwenye *Test Tube*, mkasema huyu ndiye *red bowl worm,* ndiyo *research* inavyofanyika? Tunaomba maelezo ya uhakika kwa sababu mimi nilikuwepo wakati tunaonyeshwa na *RCC* na baadhi ya wafanyakazi wenu wa Kilimo wanaruka, wanasema sisi hatukuhusishwa, hao kama walikuja kufanya *research* walikwenda moja kwa moja bila kuja kwetu. Sasa kwa nini tunawaumiza wananchi? Nataka nijue kwa nini mnakipiga marufuku kilimo cha pamba Mbeya, kwa misingi ipi? Kwa sababu *red bowl worm* hayupo Mbeya, Zambia wala Malawi, lengo ni nini? Naomba Serikali isikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Lakini kabla sijaanza kuchangia na mimi nitoe mkono wa pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kufiwa na Mbunge wao, Marehemu Yete Mwalyego, aliyefariki tarehe 24 Juni, 2004. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo mimi sina matatizo na sina mushkeli kabisa na hoja hii kwa sababu kupitia hoja hii naweza nikapata mambo ya kuzungumzia ili kuboresha hoja hii iweze kufanya vizuri zaidi katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda mimi nijikite katika kuikumbusha Serikali tulichosema katika ripoti ya Mpango Kamambe wa umwagiliaji maji mashamba katika semina ya Wabunge ya tarehe 28 Juni, 2003. Katika semina ile yapo mambo kama manne hivi tuliyazingatia sana na mimi nilijua kwamba haya ndiyo Serikali kwa ujumla inakwenda kuyafanyia kazi na nimeona nilipokuwa nasoma mengi yamefanyiwa kazi lakini nitasisitiza ili yaweze kutekelezwa katika hali ya kuwezesha mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ambalo tulikubaliana ni kwamba, eneo tunaloweza kulishughulikia kwa kiwango cha juu kabisa katika umwagiliaji ni zile hekta 2.3 milioni, hizi tuna uwezo kabisa, tunaweza kufanya kazi na kazi ikaonekana. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye kazi kweli hili eneo lionekane kwa sababu bado hatujaona kazi kama imefanywa. Ili eneo hili liweze kuonekana vizuri, naomba sana fedha ambazo tutawapa ziweze kuonyesha dalili za kufanya kazi vizuri katika eneo la umwagiliaji. Mimi nazungumzia umwagiliaji tu, nakwenda katika eneo la kumwagilia maana katika bajeti ya Mipango na Fedha, nilizungumzia sana suala la kilimo kwa ujumla, lakini sasa nalenga eneo hili la umwagiliaji. Hilo ndilo eneo ambalo tulikubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunaweza kulishughulikia angalau kwa wastani ni hekta 4.8 milioni. Sasa mimi sitaki hili suala la wastani, tunaweza kabisa kwa mujibu wa sasa hivi tukaunganisha na lile ambalo tunaweza kulishughulikia kwa kiwango cha juu ili eneo hili lihame liende kule tuunganishe tuwe na hekta nyingi zaidi za kushughulikia katika kilimo cha umwagiliaji, hicho ndiyo pekee kinachoweza kuondoa njaa, umaskini, kitapandisha uchumi wetu katika hali ya sasa ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tulizungumza sana hapa na ambalo linaweza kushughulikiwa kwa uwezo mdogo ni zile hekta 22.3 milioni. Sasa hili ndilo mimi nataka tulishughulikie kwa wastani. Tukifanya tutapunguza hata kulaumiana humu, tutafanya kazi vizuri kabisa, tutaondoa umaskini, njaa na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, semina ilisema kwa mujibu wa utafiti kwamba kwa jumla Taifa lina jumla ya hekari milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Sasa eneo hili ndio la kushughulikia. Tukope kwa ajili ya kupeleka hapo, mbona tunakopa tunapeleka kwenye shule, barabara, sasa basi tukope tupeleke katika umwagiliaji, ndiyo tutajiondoa katika hali hii ya umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia basi *master plan* hii Serikali ikitekeleza kwa vitendo nina uhakika na imani kubwa kabisa tutaondoa umaskini kwa haraka sana, tutaondoa njaa kwa haraka sana, uchumi utapata kasi ya kukua kwa haraka sana, lakini vile vile nchi yetu itakuwa tajiri na hiyo ndiyo shabaha yetu, shabaha yetu sisi ni kuwa matajiri ili wananchi wetu wasitusumbue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo sasa nataka nieleze niliyotumwa na wananchi hasa katika masuala yanayohusu mabonde. Nimetumwa na wananchi wa Jimbo langu kuwa yapo mabonde ya mito makubwa, madogo na madogo zaidi ambayo ni muhimu sana yashughulikiwe. Wananchi wanajitahidi kwa uwezo wao lakini wanahitaji msaada mkubwa wa Serikali ili tuwatoe katika hali ya unyonge wa njaa. Tuanze na bonde kubwa linaloitwa Bonde la Mto Bubu, bahati nzuri Naibu Waziri alifika, aliliona. Hilo ni bonde zuri sana likishughulikiwa, likiwekewa miundombinu litatoa manufaa kwa baadhi ya Vijiji: Nitataja Kata na idadi ya Vijiji vitakavyonufaika na Vijiji hivi vikinufaika ndiyo nchi inanufaika. Kwa hiyo, bonde hilo likijengewa miundombinu ambayo bahati nzuri Naibu Waziri alipofika waliiona, lakini hawakurudi tena kulishughulikia. Sasa safari hii naomba, baada ya hapa Waziri kwa kupitia fedha hizi ambazo tutazipitisha hapa, likashughulikiwe kwa manufaa ya umma. Kwa mfano, Kata ya Kindale, Vijiji vitakavyonufaika ni vinne na hizi ndio habari muhimu hata Waandishi wa Habari wajue, hizi ndio habari ambazo wananchi wanazitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Kindale Vijiji vinne, Kata ya Suruke Vijiji vitakavyonufaika ni vitatu. Halafu vijana takriban asilimia 65 wanaokaa Mjini pale watanufaika, watakwenda pale katika kilimo cha umwagiliaji. Kata ya Changaa, Vijiji vitatu, Kata ya Sawi Vijiji vinne, Kata ya Kitilo Vijiji vinne na Kata ya Bereko Vijiji viwili. Bonde hili linalotoka Kondoa mpaka Farkwa mpaka Bahi huku, likishughulikiwa hata njaa katika Mkoa wa Dodoma itaondoka, maana najua hotuba nyingi sana zinashambulia sana watu wa Dodoma, tutanyamaza hata kuomba omba. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ilizingatie hilo. Hilo ndilo Bonde la Mto Bubu, Naibu Waziri analijua na wataalam walifika, lakini hawajarudi. Sasa sijui kwa nini hawakurudi, sijui waliogopa kwa sababu ya daraja, lakini sasa hivi tunajenga daraja vizuri sana, tumepeleka lile daraja juu kabisa ili kutoa nafasi ya kujenga bwawa kwa ajili ya umwagiliaji, lile daraja lipo karibu asilimia hamsini kukamilika. Kwa hiyo, Waziri anaweza kwenda kuona ili kutoa maelekezo kazi hii ifanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde lingine ni Bonde la Mto Kisese. Kule Kisese tulipata mradi mpya, unaendelea kutekelezwa lakini fedha haziji kwa mtiririko unaotakiwa. Fedha zije kwa mtiririko mzuri na zije za kutosha ili mradi ule uweze kukamilishwa haraka. Huo ndiyo ukombozi wa wananchi na Vijiji vinavyofaidika hapo ni Vijiji vya Mapinduzi, Kisese Disa, Kisese Sauna, Kisese Madisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni Bonde la Mto Kisese lakini vilevile kuna bonde lingine la Urui, yapo mabonde mazuri lakini sasa tunashindwa kwa sababu miundombinu ni mibaya. Katika bonde hili kuna *scheme* inayoendelea lakini tunaikarabati kupitia *TASAF*, lakini sasa *TASAF* ni chache. Serikali ikiongeza pale tunaweza kupanua sana eneo hilo, tukapata kilimo kizuri sana cha umwagiliaji na Vijiji vya Hurui, Mitati, Mkurumusi na maeneo mengine yakafaidika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde lingine vile vile ni Bonde la Mto Kikore. Katika bonde hili vile vile tuna *scheme* ya zamani ambayo imechakaa, inahitaji kukarabatiwa, kwa hiyo, fedha zinahitajika. Bonde hili litavinufaisha Vijiji vya Kikore, Madege, Mkurumusi, Hurui yenyewe na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mimi nitalenga hasa umwagiliaji kwa sababu suala la umwagiliaji hatulitilii maanani katika kilimo. Hata hapa katika Kitabu mmeeleza, lakini hamkuweka mikakati. *(Makofi)*

Baada ya hapo, katika maeneo yangu ya mwisho naomba nizungumzie habari ya mwaka 2003. Wakulima kutoka Kondoa waliomba mikopo kwa ajili ya kukarabati au kufufua matrekta, lakini hakuna hata mmoja aliyekubaliwa, sababu masharti magumu. Wakulima wanatoka Vijijini, kule wanatakiwa wawe na hati ya nyumba na vitu vingine, sasa kule hakuna. Kwa kweli hai ni geresha kabisa hawatapata, watapata wa Mijini, watanunua matrekta yatahamia Mjini, kule kilimo kitakuwa hakuna. Naomba sana mbadilishe hili, mtafute njia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mwaka huu wa 2004/2005, wananchi wameomba na nitawataja hapa ,wamenifuata mpaka hapa kwamba tunasisitiza safari hii tupewe, sisi tunataka kufufua matrekta tulime kilimo cha biashara ili kilete matunda zaidi. Nao ni Bwana Masare, Bwana Mkamile, Bwana Nkya, Bwana Kisaki, Bwana Kisomba, Bwana Sachi, Bwana Ichachi na Bwana Dia. Wamejiandaa lakini najua Serikali itawakwamisha. Sasa naomba Waziri asimame imara ili wasikwamishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nizungumzie habari ya mwaka 2001/2002 na 2002/2003, Serikali ilikuwa imetuahidi kutupa pikipiki mbili kwa ajili ya kufuatilia masuala ya umwagiliaji kule Kondoa na barua zipo kule Kondoa. Lakini miaka yote mitatu pikipiki hazijafika, sasa kupitia hapa, naomba pikipiki hizo ziende ili zisaidie kufuatilia na kusimamia shughuli za umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nashukuru sana, mimi sina nongwa kabisa na hoja hii, nasema ipite ili Waziri aweze kufanya kazi maana ukiizuia tena atashindwa kufanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii nami nichangie kwa kifupi sana kwenye Hotuba ya Wizara ya Kilimo. Lakini nianze kwa kusema tu kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, kile ambacho mwenzetu Mheshimiwa Waziri ameomba basi sisi Wabunge turuhusu ili aweze kwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia eneo moja tu na la pili ni dogo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo, kila mtu anajua na ukiulizwa uti wa mgongo ni nini. Uti wa mgongo ukiharibika au kuvunjika kile kifupa kimoja tu kidogo unakufa. Sasa sijui ni jinsi gani sisi tulivyojiandaa kuhusu kuimarisha na kuendeleza kilimo chetu. Mheshimiwa Waziri, nafikiri amesikia *concern* ya Waheshimiwa Wabunge wote tangu bajeti, hotuba ya Waziri Mkuu na hii hotuba yake mwenyewe. Lakini ukitazama kwa mapana zaidi leo Mtanzania, mkulima huyu, ambapo tunasema ni asilimia themanini wanategemea kilimo analima kwa jembe la mkono. Asilimia themanini! Mheshimiwa Waziri, kama hatutaweza kununua matrekta angalau kwa kila Mkoa au kila Wilaya hapa

kilimo tunajidanganya, ni bure, maana sisi tunapozungumzia huu umwagiliaji si sawa na kumwagilia bustani. Tunazungumzia kumwagilia mashamba makubwa yenye kuweza kuleta tija, huna trekta utalima na mkono au na wanyama kazi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimrudishe Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake ukurasa ule wa 37, unasema hivi: "Aidha, makampuni mawili yamepatiwa mikopo ya kununua jumla ya matrekta tisa". Kichekesho! Matrketa tisa kwa nchi ya Tanzania yenye watu zaidi ya milioni 34. Jamani hata wenzetu wataalam hapa tumsaidieni basi Waziri, kweli kabisa. Lakini ukitoka hapo wenzetu waliokuwa na matrekta yao mwanzo, bahati nzuri Mheshimiwa Waziri mwaka 2003 alitamka vizuri tu na Wabunge wakashangilia kweli kweli. Tazama pale ukurasa wa 36, unasema: "Aidha, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo moja kwa moja yenye thamani ya shilingi milioni 452.2 kwa ajili ya kukarabati matrekta mabovu".

Akaendelea kusema: "Jumla ya waombaji 340 wanaopitishwa na Bodi ya Mfuko wa Pembejeo kupewa mikopo ya kukarabati matrekta, waombaji 103 tayari wamepata mikopo yao kama ifuatavyo: Kichekesho kingine, Mwanza na ukubwa wake, ile Mwanza ya wakulima na wafugaji, watu saba. Saba tu, moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, mwisho. Morogoro ishirini na tisa, Dar es Salaam mmoja, Shinyanga watano pamoja na ukubwa wake, Iringa tisa na kadhalika na kadhalika. Wapo Watanzania wanataka kulima kabisa kwa dhati kilimo kikubwa lakini Serikali yetu imekuwa haiwasaidii. Pale Kongwa, ukipita utakuta mahindi mengi sana. Ukimwuliza ndugu yangu, Mheshimiwa Job Ndugai pale atakwambia yale mahindi yanakuwa mengi siyo kwa sababu wananchi wale wanalima kwa jembe la mkono, hapana, wanalima kwa trekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yale watu bado wana matrekta yao, ili tulime zaidi na tupate chakula kingi zaidi tujitosheleze ndani na tuweze kuuza, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, hebu ikiwezekana mwaka 2005, ninajua atakuwepo tu *Inshallah,* tufanye makusudi, Serikali angalau iseme mwaka huu wa fedha tunanunua matrekta angalau 1,000 kwa kuanzia. Kama siyo 1,000 basi 500. Rais Mugabe ametangaza, iliandikwa kwenye gazeti ili walime zaidi wana utaratibu wa kununua matrekta 5,000 kufidia yale yaliyochukuliwa na Wazungu. Sisi tuna mikakati gani?

Kwa kulima kwa jembe la mkono hata tukilima mpaka jioni wananchi wetu wataumia. Lazima Serikali ifanye jitihada iagize matrekta, ifanye utaratibu inunue matrekta. Ni suala la uamuzi tu, lakini kama hatuwezi kuamua basi tutang'ang'ania kulima kwa jembe la mkono ambayo ni asilimia sabini. Tanzania na ukubwa wake matrekta yaliyopo Tanzania nzima ni asilimia kumi, inasikitisha kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa dhati kabisa zile pesa ambazo tulikubaliana kwamba hizi zitakwenda kukarabati matrekta hebu ule urasimu ujaribu kupunguzwa kwa faida ya wananchi hao wenye matrekta. Wapo watu wangu kama ndugu yangu alivyowataja wa kwake na mimi si vibaya nikawataja wa kwangu waliokuja kunilalamikia na kuomba msaada.

Yupo Mzee Mwananhurukuru, Mzee Charles Nung'hwa, Mzee Kabipi, Mzee Shauri, Mzee Yonas Shineneko, Mzee Charles Makune na wengine. Kwa dhati kabisa tunaomba Mheshimiwa Waziri wala siyo utani, tuwasaidie kama tunataka kilimo chetu kiwe bora na tuweze kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ombi tu. Wengine wamezungumzia suala la mbolea na sisi kama wafugaji Mkoa wa Mwanza tunayo mbolea ya samadi wakati mwingine ukitaka kufanya mambo mazuri lazima utumie nguvu. Serikali itoe agizo kwa *DCs,* Makatibu Tarafa na kwa *RCs* katika maeneo yenye mifugo kila kaya ile mbolea isichomwe moto, ipelekwe mashambani. Nina uhakika Waziri Mkuu yupo pale ananisikia vizuri na bahati nzuri yeye ni mkulima mzuri na analima kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie kidogo suala la pamba. Wameshaanza kuuza pamba yao kwa bei ya Sh. 300/= mpaka Sh. 350/=, lakini niwaombe kupitia Bunge lako wananchi wa maeneo ya Kwimba na Mwanza kwa ujumla, kwa maana ya Jimbo la Kwimba na Jimbo la Sumve.

Kwa sababu bei inawezekana kushuka, niwaombe pamba yao waiuze hivi sasa, wasiifungie ndani vinginevyo bei itakaposhuka watafika mahali watauza hata kwa shilingi 200/= au 180/=. Nawaomba sana ndugu zangu wakulima wangu wa Jimbo la Sumve na Kwimba, pamba yao waiuze sasa hivi, wasiifungie ndani kwa kusubiri labda kwamba bei itapanda, bei haitapanda bali itashuka. Nina hakika watakuwa wamesikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, wakati ninachangia katika Hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumzia sana kilimo, lakini mimi kama Mbunge, nilikuwa ninawakilisha mawazo ya Wananchi wa Jimbo langu la Sumve. Bahati nzuri mimi sina ugomvi kabisa kabisa na Waziri wa Kilimo na Chakula, hata kidogo kwa sababu sijawahi kukwaruzana naye hata siku moja ila suala la matrekta kama hataleta, tutagombana.

Kwa sisi ambao tunakwenda Kanisani kuna ile sala ya kuungama, unasema nakuungamia Mungu Mwenyezi, nanyi ndugu zangu nimekosa mno kwa mawazo, maneno, kwa vitendo na kwa kutotimiza wajibu. Kama hutatimiza wajibu wako kwa yale uliyoyaainisha humu ndani itabidi uje uungame. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili na la mwisho niwaombe kweli kabisa na kwa dhati, Wataalam wa Mheshimiwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula wamsaidie. Hizi hoja zinazosemwa na Waheshimiwa Wabunge si za Mheshimiwa Waziri, hapana, ni ninyi wataalam mnaotutazama saa hizi mnajifanya kama vile hamtuoni wala hamtusikii, Waziri wenu hamumsaidii vizuri. Kama mngekuwa mnamsaidia vizuri haya makombora anayopata humu ndani yasingepatikana lakini hamumsaidii kwa dhati na ninyi itabidi tuwatafutie muda wenu tuwashughulikie kwa sababu ninyi ndiyo mnaoangusha kilimo chetu Tanzania.

Haiwezekani kila siku tunazungumzia umwagiliaji, umwagiliaji na bwana umwagiliaji yupo. Hivi kuna sababu gani wananchi wa Mkoa kwa mfano wa Morogoro, ukienda pale Mvomero unaambiwa kuna njaa, ukipita kila barabara kuna mito

inaotiririka. Kuna mito 84 inayotiririka maji kila siku, kiangazi na masika lakini unaambiwa kuna njaa. Kwa nini bwana umwagiliaji asiende pale Morogoro akasema naweka kambi hapa. Lazima Morogoro liwe eneo maalum la umwagiliaji, amekaa tu ofisini na magari na nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vizuri sana kuwasema wataalam, tunawaheshimu sana kwa kazi zao lakini wanatulazimisha sisi Waheshimiwa Wabunge tuseme. Nawaomba sana mumsaidie Waziri wenu. Hii si sifa nzuri wala siyo sura nzuri kwa Wizara, mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu, anasimama anasema jamani Mheshimiwa Waziri, hana makosa ni kwa sababu ya ukosefu wa mvua.

Lakini katika timu ya watu 11 ya mpira, ukiingia kucheza mpira, utakuwa unapewa pasi, wanataka kufunga wewe unatoa nje au unanyang'anywa, Kocha atasema pumzika ili aingizwe mwingine. Sasa wataalam msaidieni Waziri wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, naona shughuli iliyopangwa kwa leo imekwisha lakini nina tangazo moja kwamba, tulishapitisha fomu tukawaomba Wenyeviti wa Kamati za Mikoa za Wabunge watujazie Ofisi za Wabunge, tujue nani ana ofisi na nani hana. Mpaka sasa ofisi yetu imepokea fomu kama tano, sita hivi, tunaomba sasa wale Waheshimiwa Wenyeviti ndiyo washughulikie wazipeleke pale ofisini kwetu au wampe Ndugu Nenelwa Mwihambi.

Basi baada ya hapo naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. Bunge linaahirishwa.

*(Saa 1.31 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne tarehe 29 Juni, 2004 saa tatu asubuhi)*